NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 29 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Saba, Kikao cha Thelathini na Sita. Ningependa nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru sana, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao wamefanya kazi nzuri sana, katika kipindi ambacho mimi mwenyewe sikuwepo na Mheshimiwa Naibu Spika hakuwepo, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Azzan Zungu na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. Ahsanteni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Pia natambua Waheshimiwa Wabunge tuliokuwepo *weekend*, hapa Dodoma palikuwa na shughuli kubwa, kwa hiyo tunawapongeza sana *Mbao FC,* watani zangu Wasukuma kwa kujitahidi, lakini pia tunawapongeza sana Simba kwa kuchukua Kombe la *FA*. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara wa Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. JULIANA D. SHONZA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juliana Shonza, sasa ni wakati wa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI (K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 288

**Mahakama zote nchini Kutumia Lugha ya Kiswahili**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Mahakama zote nchini zitaanza kuendesha kesi kwa lugha ya Kiswahili?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Mahakama Sura ya 11 yaani *(Magistrates' Courts Act CAP 11; S.12),* lugha inayotumika kuendesha kesi katika Mahakama zote za Mwanzo ni Kiswahili. Aidha, kifungu hiki kinatamka kwamba kesi katika Mahakama za Wilaya na za Hakimu Mkazi zitaendeshwa kwa Kiswahili ama Kiingereza, isipokuwa hukumu inaandikwa kwa Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama Kuu, Kanuni za Lugha za Mahakana ukisoma Kanuni ya (2) inasema kuwa Lugha ya Mahakama Kuu itakuwa Kiswahili au Kiingereza, isipokuwa kumbukumbu za maamuzi, ama hukumu itakuwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Rufani ya mwaka 2009, ukisoma Kanuni ya (5) lugha inayotumika katika kuendesha mashauri itakuwa ni Kiswahili au Kiingereza kulingana na maelekezo ya Jaji Mkuu au Jaji anayesikiliza shauri husika, isipokuwa hukumu inaandikwa kwa Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, hivyo ninapenda kulihakikishia

Bunge lako Tukufu kwamba uendeshaji wa mashauri katika Mahakama zote nchini kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo unaruhusu kutumia lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza na tumekuwa tukizingatia lugha hizo katika uendeshaji wa mashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, karibu.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, naomba kuuliza maswali tu madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa jibu katika swali langu la msingi linakiri kuwa kumbukumbu na hukumu katika Mahakama za Wilaya hadi Mahakama ya Rufani ni kwa Kiingereza. Je, Serikali haioni kuwa kumbukumbu na hukumu katika lugha ya kigeni yaani Kiingereza ni kikwazo kikubwa kwa mwananchi anayetaka kukata rufaa kwa kupata haki yake?

Swali la pili, kwa kuwa kauli mbiu ya Serikali ni haki sawa kwa wote na kwa wakati, lakini tumekuwa tukishuhudia Mahakama zikijitahidi kumaliza kesi zake, lakini hukumu zinakuwa zinapatikana kwa kuchelewa sana, hali inayopelekea wengine kutokukata rufaa kwa wakati na walioko gerezani kuendelea kuteseka gerezani.

Je, Serikali inatoa kauli gani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukubaliana na Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba ana hoja ya msingi, lakini nikumbushe tu Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tuliamua mwaka 1964 kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya Taifa, vilevile Kiingereza kuwa lugha ambayo tunaitumia katika shughuli za Serikali. Ni kama Mheshimiwa Baba wa Taifa alivyosema kwamba Kiingereza ndiyo Kiswahili cha dunia.

Kutoka 1964 mpaka sasa tumeweza kufanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha kwamba tunakiingiza Kiswahili katika mfumo wa Mahakama bila kupotosha utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la utumiaji wa Kiswahili kwa kumbukumbu, kwa hukumu, kwa uendeshaji katika Mahakama za Mwanzo ambao umefanikiwa sana. Hatujaona kabisa *miscarriage of justice* pale.

Mheshimiwa Spika, pili Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ambayo mwanzoni ilikuwa inaitwa TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) chini ya Profesa Mlacha, iliweza kushirikisha Baraza la Kiswahili la Tanzania pamoja na Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa Sheria, nilikuwepo mimi pamoja na Marehemu Profesa Joan Mwaikyusa, Mungu aiweke roho yake pema, peponi, tukaweza kutoa Kamusi ya kwanza ya Kiswahili ya Kisheria, yote haya ni maandalizi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kila Muswada wa Sheria leo hii ukiletwa hapa Bungeni na sheria zenyewe, lazima ije kwa Kiingereza na Kiswahili na hilo wewe mwenyewe umekuwa ukisisitiza sana.

Mwisho BAKITA imeshakusanya sasa hivi Istilahi zaidi ya 200 za kisheria ambazo zinasubiri tu kusanifishwa *(standardize).* Kwa msingi huo, Mahakama yetu ambayo ni chombo huru katika Katiba yetu ni Muhimili unaojitegemea, una msingi sawa wa kutosha tuweze kupanua wigo wa matumizi ya Kiswahili katika kumbukumbu na hata kutoa hukumu hata kwenda Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Kabati kwamba tunachoepusha hapa ni kukurupuka tu kuingia na kutumia Kiswahili ilikuwa tu ni kuepusha utata katika nyaraka zetu, *ambiguities* na kuwa *equivocal,* kuwa na utata katika utafsiri nyaraka za Kimahakama, ndiyo maana tumekwenda polepole sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nakubaliana naye kwa kweli haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa, lakini ni kweli vilevile kuwa haki iliyowahishwa sana mara nyingi hukosa umakini. Kesi nyingi zinachelewa hasa za jinai kumalizika si kwa sababu ya Mahakama lakini kutokana na mchakato mzima wa utoaji haki. Kwa mfano, suala la upelelezi huchukua muda mrefu sana, na inachukua muda mrefu si kwa sababu vyombo vyetu vya dola havifanyi kazi, lakini kuna tatizo la kutopata ushirikiano mzuri kwa mashahidi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Iringa anakotoka Mheshimiwa Kabati, tuna kesi nyingi sana, sana za makosa ya kujamiiana na yanatokea ndani ya familia, kupata ushahidi mle ndani ni kazi kubwa kweli na ndiyo maana tunatoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na vyombo vya dola pale inapotokea kosa, kusaidia katika ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kwamba, uthibitisho wa makosa mengine unahitaji Mkemia Mkuu achunguze na atoe jibu, inachukua muda mrefu, Mkemia Mkuu anaweza kuwa na mafaili 3000 ya uchunguzi na yote yanahitaji kwenda Mahakamani, kwa hiyo kazi ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la mwisho ni uhitaji wa kisheria kwamba kila kosa lazima lithibitishwe *beyond reasonable doubt* yaani pasipo na wasiwasi wowote. Sasa hiyo hatuwezi kulikwepa ili kuweza kulinda haki za kila mtu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati haya mambo ya kufanya fanya kwenye familia huko Iringa. Swali la nyongeza Mheshimiwa Nape. *(Kicheko)*

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kijiji cha Mnara, Kata ya Mnara, Tarafa ya Rondo Jimboni Mtama kwa kupindi cha miaka mitatu sasa imepita tumekamilisha jengo zuri la kisasa la Mahakama, lakini kwa kipindi chote hicho Serikali imekuwa

kwa namna moja ama nyingine pengine inapiga chenga kufungua na kuruhusu jengo hili litumike.

Mheshimiwa Spika, Mbunge aliyepita alisaidia ujenzi, ameomba Serikali tulifungue, lakini mpaka leo Serikali haijafungua. Sasa ni lini Mheshimiwa Waziri Serikali itaruhusu jengo hili litumike ili haki itendeke kwa watu wangu hawa kupata huduma karibu na maeneo yao.

**SPIKA:** Majibu kwa swali hilo fupi la nyongeza Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana yeye pamoja na wananchi wa Jimbo lake kwa kupata jengo la Mahakama zuri, lakini mimi mwenyewe nasikitika kwamba mpaka sasa halijaweza kuzinduliwa.

Naomba nitoe ahadi kwamba tutakapotoka tu hapa, tena nataka niwe mbele yake, nitampigia Mtendaji Mkuu wa Mahakama, tuhakikishe kweli hili jengo linaanza kutumika. Kwa sababu huko ndiko kusogeza huduma za Mahakama kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali linalofuata linaulizwa kuelekea Wizara ya Maji na Umwagiliaji la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini.

Na. 289

**Ahadi ya Serikali ya Ujenzi wa Mradi wa Maji**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kupeleka maji katika vijiji vya Nkata, Ntemba, Kitosi, Ntuchi, Isale hadi Msilihofu kupitia mradi uliokuwa na thamani ya shilingi bilioni 2.8 na vilevile ahadi hiyo imetolewa na Serikali ya Awamu ya Tano.

(a) Je, mradi huo umefikia hatua gani?

(b) Je, ni lini hasa wananchi wategemee kutatuliwa kwa kero yao ya ukosefu wa maji safi kupitia mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Isale ulisanifiwa mwaka 2013 katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kupitia mpango wa vijiji kumi kwa kila Halmashauri. Mradi huu ulilenga kukipatia maji Kijiji cha Isale kutoka Mto Nzuma. Mwaka 2014 utekelezaji wa mradi huu ulisimama kwa muda ili kufanya mapitio ya usanifu wa mradi utakaojumuisha pia mahitaji ya huduma ya maji kwa wananchi wa vijiji vya Ntuchi, Nkata, Mtemba na Msilihofu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya awali ya usanifu iliwaislishwa na Mtaalam Mshauri na kujadiliwa kwa pamoja na Halmashauri na Mkoa ambapo Mtaalam Mshauri ameelekezwa kufanya marekebisho ili kukidhi mahitaji halisi ya vijiji vyote. Mapitio ya usanifu yatakamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2017 na mradi utatekelezwa katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyoanza kutekelezwa mwezi Julai, 2016 na utakapokamilika utatatua kero ya ukosefu wa maji safi kwa wananchi wa Nkasi Kusini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba wafanye kama walivyosema. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, mapema mwaka huu Waziri wa Maji alitembelea Mkoa wa Rukwa na akatembea Wilaya ya Nkasi, pia alipata nafasi ya kutembelea Mradi wa Kawa. Mradi wa Kawa una umri wa miaka sita na umetumia zaidi/karibu

shilingi bilioni tatu, lakini wananchi wa vijiji vya Shengelesha, Kundi na Kalundi hawajaanza kupata maji, licha ya miundombinu yote kuwa imeshajengwa ya kupeleka maji.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi hawa juu ya kupata maji mapema iwezekanavyo?

Swali la pili, hivi karibuni Serikali iliifunga shule ya sekondari ya Milundikwa na kuihamishia Kasu. Kijiji cha Kasu hakina maji ya uhakika ya kuweza kusaidia wananchi pamoja na shule.

Je, Serikali ipo tayari kufanya utafiti ili kipatikane chanzo kizuri kitakachowezesha kusaidia shule na kijiji cha Kasu, Katani, Milundikwa na Kantawa kwa ajili ya huduma ya maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer* Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mipata ...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga makofi na vigelegele kushangilia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona mnapiga makofi kuna nini?

**MBUNGE FULANI:** Ubingwa wa mchangani. *(Makofi/ Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Wameingia wachovu.

*(Hapa Wachezaji wa Klabu ya Simba na Viongozi waliingia ndani ya Bunge na kukaa sehemu ya wageni)*

**SPIKA:** Karibuni sana wachezaji wa Simba na viongozi

karibuni sana nitawatambulisha hapo baadae nitawapa nafasi, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niipongeze Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Mipata kwamba utekelezaji wa mradi wa bwawa la Kawa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Waziri kutembelea pale Mheshimiwa Mipata ulimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba mradi ule sivyema uendeshwe kwa kutumia jenereta inayotumia mafuta ya *diesel*, ukamshauri kwamba ni vyema tutumie umeme wa jua. Kutokana na huo ushauri wako nikufahamishe kwamba sasa tumekamilisha usanifu na wakati wowote tutanunua umeme wa *solar* na kufunga pale ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, ninaahidi ya kuwa ni muda mfupi tu unaokuja wananchi watapata huduma ya maji, kwa sababau maji yapo na miundombinu yote imeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ni kweli baada ya Serikali kuhamisha shule ya Milundikwa na kuipeleka Kasu kumejitokeza tatizo la maji pale, ikiwemo vijiji vya Kantamwa, Milundikwa na Katani.

Mheshimiwa Spika, ninamuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri husika ashirikiane na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa sasa mtaalam tunaye kule tayari ili tuweze kufanya usanifu tupate chanzo kitakachohudumia hii shule ya Kasu pamoja na vijiji vinavyozunguka ili wananchi wa maeneo hayo wasipate tatizo la huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata la Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini.

Na. 290

**Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Nne ilianza ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini katika eneo la Mitengo Mikindani – Mtwara.

(a) Je, kuna mikakati gani ya kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa hospitali hiyo?

(b) Je, ni lini wananchi wategemee kuanza kutumia hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ipo kwenye hatua ya kuandaa awamu nyingine ya kumalizia sehemu iliyokwishaanzishwa ya jengo la mapokezi ya wagonjwa wa nje yaani *Out Partient Department (OPD)* pamoja na kukamilisha majengo mengine kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, ambapo kiwango cha kazi kilichoingiwa mkataba kwa awamu ya kwanza kimekamilika na kukabidhiwa kwa Wizara. Mwaka 2011 Wizara ilijenga uzio wa ukuta wenye kilometa 2.7 kwa ajili ya usalama na uhifadhi wa eneo la hospitali. Sanjari na hilo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wamekubali kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la Wagonjwa wa nje *OPD* na ujenzi huo utaanza mapema pindi taratibu za ndani zitakapokamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, matarajio ya Wizara kwamba kipindi cha mwaka mmoja baada ya kumpata mkandarasi wa awamu ya pili sambamba na upatikanaji wa fedha za

kuendelea na ujenzi, jengo la wagonjwa wa nje litakamilika na kuweza kuanza kutumika wakati majengo mengine yanaendelea kukamilishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali mengine ya nyongeza kwa sababu swali la msingi kwa kweli Mheshimiwa limejibiwa kwa ujumla zaidi kiasi kwamba linaninyima matumaini.

Mheshimiwa Spika, swali langu niliuliza kuna mkakati gani wa kuharakisha, sasa suala la uzio wa mwaka 2011 nadhani hilo si sehemu ya kuharakisha ujenzi wa hiyo hospitali. Suala la kama Bima ya Afya pia wamekubali kusaidia katika ujenzi huo tumelisikia zaidi ya miaka miwili sasa.

Je, ni lini taratibu za ndani zitakapokamilika ambazo zilichukua zaidi ya miaka miwili?

Swali la pili, hivi majengo ya *OPD* peke yake yanatosha kuifanya kuwa ni Hospitali ya Rufaa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dada yangu Hawa Abdulrahman Ghasia kwa ufuatiliaji wa karibu sana wa suala hili. Ninadhani wananchi wa Mtwara Vijiji wananisikia kwamba suala hili amekuwa akilifuatilia kwa ukaribu na hii ni mara yake ya zaidi ya tatu kuuliza suala hili.

Majibu ya swali lake la kwanza kwamba ni lini mchakato wa ndani utakamilika naomba nisitoe *time frame*

mahsusi kwa sababu sina uhakika ni lini mchakato huu utakamilika lakini nimuahidi tu kwamba nitalifuatilia mimi mwenyewe kwa ukaribu na nitamjulisha pindi nitakapokuwa nimepata jibu la uhakika kwamba ni lini haswa mchakato wa ndani utakamilika kabla *NHIF* hawajatoa pesa kwa ajili ya kwenda kumalizia jengo la *OPD.*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linalohusu mchakato wa kuanzisha hospitali yenyewe kwamba je, inatosheleza tu kwa kuwa na *OPD* ili iwe hospitali ya Kanda, hapana. Tunachokifanya ndicho alichokiuliza kwenye swali la msingi kwamba, tunataka hospitali walau ianze kutoa huduma sasa katika kuanza kutoa huduma ili ikamilike zinahitajika pesa nyingi sana. Kwa kuwa pesa zote hazipatikani siku moja na mahitaji ya hospitali hii ni makubwa na sote tunakubaliana kwamba kuna umuhimu wa kuwepo na hospitali hii na huduma hizi kuanza kwa haraka, ndiyo maana tumeona kuliko kusubiria mpaka hospitali yote ikamilike wakati tuna majengo ya awali yameshakaribia kukamilika kabisa na tunaweza tukaanza kutoa baadhi ya huduma, tumeona tuanze kutoa huduma kwa awali, lakini zitatoka katika kiwango hicho hicho cha ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda haupo upande wetu mnivumilie, tuendelee na Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete.

Na. 291

**Idadi ya Ng'ombe na Mbuzi wa Maziwa Nchini**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN (K.n.y. MHE. MBAROUK SALIM ALI)** aliuliza:-

Tanzania pamoja na kuwa na mifugo mingi bado kuna uhaba mkubwa wa maziwa.

Je, Tanzania ina ng'ombe na mbuzi wangapi wa maziwa?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubailiana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tanzania ina idadi kubwa ya mifugo lakini bado kuna upungufu wa maziwa ambapo takwimu za makadirio za mwaka 2016 zinaonyesha kuwa kuna jumla ya ng'ombe milioni 28.4, mbuzi milioni 16.7, kondoo milioni tano, nguruwe milioni 1.9, kuku wa asili milioni 37.4 na kuku wa kisasa milioni 34.5. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya lita bilioni 2.09 za maziwa zilizalishwa na unywaji wa maziwa kwa mtu kwa mwaka ulifikia lita 47, ikilinganishwa lita 200 zinazopendekezwa na Shirika la Chakula Dunian *(FAO)*.

Mheshimiwa Spika, kati ya ng'ombe milioni 28.4, ng'ombe rasmi wa maziwa ni 782,995 tu sawa na asilimia tatu ya ng'ombe wote. Aidha, kati ya mbuzi milioni 16.7 ni mbuzi rasmi takribani 50,000 ndiyo wa maziwa ambao ni asilimia 0.3 ya mbuzi wote.

Mheshimiwa Spika, zipo jitihada mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali ili kukabiliana na upungufu wa maziwa hapa nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kuimarisha mashamba ya kuzalisha mifugo ya Serikali *(Livestock Multiplication Units)* ili kuongeza idadi ya ng'ombe wenye uwezo wa kuzalisha maziwa kwa wingi.

Aidha, Serikali imeanzisha vituo vya uhimilishaji katika Kanda Sita hapa nchini ambazo ni Kanda ya Ziwa - Mwanza, Kanda ya Magharibi - Katavi, Kanda ya Kati - Dodoma, Kanda ya Mashariki - Kibaha, Kanda ya Kusini - Lindi, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya, kwa lengo la kutoa huduma ya uhimilishaji wa ng'ombe wa maziwa walioko kwenye maeneo hayo pamoja na ng'ombe wa asili ili kuzalisha idadi kubwa ya ng'ombe wa maziwa. Jitihada hizi zitawezesha idadi ya ng'ombe wa maziwa kufikia milioni 2.9 ifikapo

mwaka 2021/2022 ambao pamoja na ng'ombe wa asili wataweza kuzalisha lita bilioni 3. 8 za maziwa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo kuwekeza katika uzalishaji wa mitamba ya maziwa na mashamba ya ng'ombe wa maziwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa maziwa hapa nchini.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Yussuf swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri aliyoyajibu hata asiyoulizwa, maana yake kaulizwa ng'ombe wa maziwa tu kuku hatoi maziwa. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza kuna viwanda vingi vinavyozalisha maziwa hapa nchini, na kwa idadi ya maziwa ya pakiti tuliyonayo ndani ya nchi hii yanazidi mara tano au sita ya lita hizi alizozitaja. Je Mheshimiwa Waziri anataka kutuaminisha kwamba maziwa haya ya pakiti yanayozalishwa nchini ni zile tetesi kwamba ni unga unaotoka India unakuja kuzalisha maziwa hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili amesema wanategemea kuzalisha lita bilioni 3.8 ifikapo mwaka 2021/2022 ni kati ya miaka sita kuanzia leo. Mheshimiwa Waziri kuna miujiza gani ambayo mtaifanya kama Wizara muweze kuzalisha lita bilioni 1.7 katika kipindi hiki cha miaka sita? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Dkt. Tizeba tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yako maziwa yanayozalishwa hapa nchini yanayotokana na unga wa maziwa na pia ni ukweli kwamba siyo maziwa yote yaliyo kwenye paketi ni yanatokana na huo unga wa maziwa. Wako wazalishaji

wanaotumia unga wa maziwa kuzalisha maziwa ya paketi lakini pia wako wazalishaji wanaotumia maziwa ya paketi wanaotumia maziwa ya asili ya moja kwa moja. Viko viwanda vyetu wasindikaji wa maziwa huko Iringa na Tanga hawa hawatumii unga katika kuzalisha maziwa ya paketi ambayo yanauzwa hapa nchini. Lakini viwanda kama vya Bakhresa yeye anatumia unga katika kuzalisha baadhi ya maziwa anayotoa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili tutatumia muujiza gani kufikia hizo lita bilioni 3.8 muujiza ni ule tuliousema katika jibu letu la msingi kwamba *combination* ya hizo *measures* ya uzalishaji wa mbari safi, koo safi za mifugo uhimilishaji na uongezaji wa huduma katika mashamba yaliyopo na urasimishaji wa wavunaji wa maziwa katika vijiji vyetu huko, utatufikisha kwenye hili lengo letu la lita bilioni 3.8.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Goodluck Mlinga swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, katika ngo'mbe milioni 28 ni ng'ombe 700,000 tu wanaozalisha maziwa, hii inatokana na wafugaji kutokuwa na watetezi katika nchi wakiwemo wafugaji wa Iragua. Je, Wizara sasa iko tayari kuhakikisha wafugaji hawanyanyaswi na watu wa maliasili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali zuri sana hilo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Dkt. Tizeba majibu tafadhali. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kwamba wafugaji nchini hawanyanyaswi na mtendaji yeyote wa Serikali na inapotokea tukapata ushahidi kwamba mtendaji yeyote wa Serikali amekiuka maadili ya kazi, basi Serikali haitasita kuchukua hatua mara moja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda naomba tuendelee na swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota kutoka Nanyamba kwa Wizara hiyo hiyo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Chikota.

Na. 292

**Ongezeko Kubwa la Gharama za Kuzalisha Korosho**

**MHE. ABBDALAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la gharama za kuzalisha korosho zinazosababishwa na pembejeo kuuzwa kwa bei ya juu.

Je Serikali ina mpango wa kutoa mikopo midogo midogo kwa wakulima wa korosho ili waweze kumudu gharama hizo?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima ikiwemo ruzuku ya kununua viuatilifu vya zao la korosho. Lengo la kutoa ruzuku hizo ni pamoja na kuwapunguzia wakulima gharama ya bei ya soko ya pembejeo hizo ambazo zinachangia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa ruzuku ya pembejeo, Serikali pia imeanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani unaotumiwa kuuzia korosho, utaratibu ambao umesaidia kupata soko la uhakika na kuongeza bei ya korosho kutoka shilingi 2,900 kwa kilo moja msimu wa mwaka 2015/2016 hadi kufikia shilingi 4,000 kwa kilo moja msimu wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kupitia Tume ya Ushirika, Serikali imeandelea kuwahimiza wakulima kujiunga kwenye vyama vya ushirika na vikundi vya wakulima ili kurahisisha kupata mikopo itakayo wawezesha kumudu gharama za uzalishaji. Aidha, mwaka 2015 Serikali imeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ambayo inatoa mikopo ya muda mfupi miaka miwili, muda wa kati miaka miwili hadi mitano na muda mrefu miaka mitano hadi miaka 15 kwa wakulima, kwa riba nafuu ya kati ya asilimia nane hadi asilimia 12. Benki hii imeendelea kutoa elimu ya mikopo kwa wakulima, kwa hali hiyo napenda kuwashauri wakulima kote nchini kupitia vyama vya ushirika na vikundi kutumia fursa hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa pembejeo za ruzuku hazitoshelezi mahitaji yote ya zao la korosho, Serikali inampango gani sasa zile pembejeo zingine ambazo mkulima atahitaji azipate sokoni kuagiza kwa pamoja *(bulk purchase)* kama itakavyofanya mbolea katika msimu huu kwa mwaka 2017/2018?

Swali la pili, ni ukweli usiopingika kwamba korosho mwaka huu imeingiza fedha nyingi sana za kigeni ni zao ambalo linaongoza, je, Benki ya Maendeleo ya Wakulima Tanzania ni lini itafungua tawi Mkoani Mtwara ili iweze kuwahudumia wakulima wa korosho wa Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota nilidhani utaanzia kwa kuishukuru Serikali kwa kutoa *sulphur* ya bure. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, pembejeo hasa ya korosho ambayo inatumika zaidi ni hiyo *sulphur* na *sulphur dust* imekuwa ikiagizwa kutegemea na fedha ambayo imekuwa inapatikana katika ule Mfuko wa *WAKFU* wakati ule wa uendelezaji wa zao la korosho, pamoja na ile iliyokuwa inaagizwa kwa ruzuku na kuuzwa kwa wakulima kwa asilimia 50 bado wafanyabiashara binafsi walikuwa wanaagiza hii *sulphur* na kuiuza kwa wakulima ambao walikuwa hawapati fursa ya kununua ile inayoletwa kwa ruzuku ya Serikali. Kwa hivyo, sasa hivi tulichokifanya kwanza tumeongeza *volume* ya kuagiza kutoka tani 13,000 zilizoagizwa katika msimu uliopita mpaka tani 18,000 mwaka huu na lengo letu ni kwamba kwa msimu ujao wa korosho tutaongeza kutoka tani 18,000 mpaka tani 25,000 ambazo zinahitajika kwa ajili ya wakulima maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao umekuwa unatumika ni uleule ambao tunau–*introduce* sasa kwenye mbolea ni wa *bulk importation*, umetusaidia sana katika kushusha bei ya *sulphur dust* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini *TADB* itafungua tawi huko Mtwara, nadhani mipango ipo na tulisema katika hotuba yetu ya bajeti kwamba, kwa kuanzia *TADB* wanataka wafungue matawi katika Kanda Saba hapa nchini, tulizitaja na jinsi kadri mtaji wao unavyoongezeka wataendelea kufungua matawi katika maeneo mengine nchini.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Omary Mgumba swali la nyongeza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa gharamba za uzalishaji wa korosho za wabanguaji wa ndani wadogo na wakubwa ni kubwa pamoja na korosho yenyewe kuzalisha, na kwa kuwa wabanguaji wadogo na wakubwa wanashindanishwa kupata korosho kama malighafi katika mnada wa

stakabadhi ghalani pamoja na wabanguaji kutoka nchi za nje kutoka India na Vietinam ambao wanapata ruzuku.

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwawezesha wabanguaji wadogo na wakubwa waliowekeza nchini, kupata korosho kama malighafi katika minada hapa nchini ili kutoa ajira na kuongeza thamani korosho zetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Tizeba, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge ndilo eneo mojawapo ambalo Serikali inalifanyia kazi kwa umakini sana, kwa sababu ni katika eneo hili ambako au tutaendelea kusafirisha korosho ghafi kwenda nje au tutatengeneza utaratibu ambao korosho itabanguliwa nchini na kusafirishwa ikiwa imebanguliwa.

Mheshimiwa Spika, suala la soko, ndio msingi wa kwanza wa kujua, mbangue muuze iliyobanguliwa au muuze ambayo haijabanguliwa. Kwa sababu soko la korosho liko *sensitive* sana na ubora wa korosho yenyewe, mnaweza mkatumbukia kwenye ubanguaji, halafu mkaishia kukaa na korosho yenu mkakosa mnunuzi na wakulima wataathirika zaidi ama mkabangua nchini kwa utaratibu ambao unawezekana mkashindana kwenye soko, kwa hivyo mkatengeneza hizo ajira anazozisema hapa nchini na mkauza korosho mkapata soko kuuza korosho nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ziko nchi ambazo wameweka utaratibu wa upendeleo, kwanza, kwa kuwaruhusu wabanguaji wa ndani wanunue katika masoko na baada ya kununua ndio wanaruhusu wanunuzi kutoka nje waingie na wao kununua, yote haya tunayatafakari na tutakuja na jawabu ambalo litakuwa kwa vyovyote haliwaweki katika uwezekano wa kukosa soko wakulima, pia tuwe na uwezo wa kubangua korosho wenyewe hapa nchini ili twende na yote mawili bila kuathiri jambo moja au lingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Washeshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, ina maswali matatu, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini.

Na. 293

**Milipuko Mikubwa kutoka kwenye Mgodi wa Dhahabu wa GGM na Madhara yake kwa Wananchi**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Mgodi wa *GGM* - Geita umekuwa ukitumia milipuko mikubwa wakati wa kulipua miamba ya dhahabu na kusababisha madhara makubwa kwa wananchi jirani na maeneo hayo, kama wale wa eneo la Katoma.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba nyumba za wananchi zinapasuka na baadhi ya watu huzimia kutokana na mshtuko?

(b) Je, Serikali inalitatua vipi tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu shughuli za ulipuaji zianze katika eneo la Katoma tarehe 23 Septemba, 2014 kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi wa kijiji hicho kuwa milipuko inayofanywa na Kampuni ya *GGM* imekuwa ikisababisha sauti na mitetemo mikubwa na hivyo kuleta usumbufu na athari mbalimbali kwa wananchi na majengo yao.

Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko hayo, mwaka 2014 Serikali kupitia Idara ya Madini na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kushirikiana na wananchi wa Mtaa

wa Katoma pamoja Geita *GGM*, waliunda Kamati shirikishi ya kushughulikia malalamiko ya wananchi hao, ijulikanayo kama *Blast Monitoring Committee (BMC)*. Kazi kubwa ya Kamati hiyo ilikuwa ni kukutana kila siku ya ulipuaji na kupokea malalamiko wakati wa mlipuko.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2016 Wizara ilituma timu ya wataalam kutoka Wakala wa Jiolojia Tanzania – *GST* kwa ajili ya kufanya tathmini ya kina ya nyufa za nyumba ambazo zimesababishwa na *GGM*. Timu hiyo ilibaini uwezekano wa milipuko ya mgodi huo katika shimo la Katoma kuchangia nyufa katika nyumba na maeneo mengine ya Katoma pamoja na *Nyamalembo Compound*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hiyo ya *GST,* Wizara iliunda timu ya wataalam iliyojumuisha wawakilishi wa wananchi wa maeneo hayo ili kufanya utambuzi wa nyuma zenye nyufa. Kutokana na utambuzi huo, takribani nyumba 890 katika maeneo hayo zilibainika kuwa na nyufa. Hivi sasa uchambuzi wa kina unafanywa kuhusiana na hatua stahiki za kuchukua uchambuzi huo utatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017 na taarifa yake itatolewa kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nilitaka kumtaarifu kwamba hiyo *Blast Monitoring Committee* ilivunjwa na haipo tena, na ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, mgodi huu unaendelea na mfumo huu wa ku-*blast* ambapo kutokana na *blasting* hii watu wameendelea kupata madhara na tarehe 30 Machi watu nane walizimia, mama mmoja ambaye alikuwa ni mama lishe alizimia karibu siku tatu na kulazwa hospitali, lakini juhudi za Mkuu wa Wilaya za kuwataka watu wa mgodi kwanza walipie matibabu, lakini walipe gharama za mama lishe huyu ziligonga mwamba baada ya watu wa mgodi kukataa.

Je, ni utaratibu gani utumike ili wanaoathirika kiafya waweze kulipwa fidia?

Swali la pili, kupitia Bunge na kupitia mikutano kadhaa Mheshimiwa Naibu Waziri na Nishati, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Waziri wa Nishati aliyeondoka walitoa maagizo mengi ya kuhakikisha kwamba waathirika, wa milipuko hii wanalipwa fidia katika eneo la Katoma, lakini mpaka sasa tunapozungumza ni mwaka mmoja umepita.

Je, ni lini ahadi hii ya Serikali itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini majibu kwa ufupi, ni lini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Constantine anavyohangaika na matatizo ya wananchi hasa wa Katoma na *Nyamalembo Compound* na ninaamini wananchi wanaona juhudi zako Mheshimiwa Constantine.

Mgodi wa *GGM* kweli umekuwa ukifanya shughuli za ulipuaji na tarehe 30 mwezi Machi mwaka huu, ulifanya ulipuaji na kama alivyosema Mheshimiwa Constantine kuna mtu mmoja ambaye alipata madhara, kampuni tumeendelea kujadiliana nao na wanaangalia namna ya kufanya fidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Constantine huyo mwananchi pamoja na wananchi wengine watafidiwa fidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini, tuliunda timu kama ambavyo nimeeleza na kwa kweli tumetuma timu zaidi ya mara mbili na sasa hivi timu itakayokwenda sasa kutathmini yale wananchi wenye nyumba 890 ambao nyumba zao zimeathirika, tarehe 05 Juni watakwenda sasa kujadiliana pamoja na wenye nyumba zilizoathirika ili hatima yao ya kulipwa fidia iweze kufanyika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Constantine wewe pamoja na uongozi wa Halmashauri pamoja na mgodi na timu itakayoundwa mtashirikishwa ili wananchi hao sasa waanze kulipwa fidia zao.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela na swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo.

Na. 294

**Mradi wa *REA III* Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Jimbo la Kalambo lina kata 23 na vijiji 111; katika awamu ya kwanza na ya pili ya mradi wa *REA* ni vijiji vichache tu vilipata umeme.

Je, katika utekelezaji wa *REA III* ni vijiji vingapi vinategemea kupata umeme ili wananchi wa maeneo hayo waweze kujiandaa kujiendeleza kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi kabambe wa usambazaji umeme vijijini awamu ya tatu umeanza rasmi tangu mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele mradi vitatu vya *densification, grid extension* pamoja na *off-grid renewable* vinavyolenga kuongeza wigo wa usambazaji katika vijiji vyote vilivyobaki nchi nzima, vitongoji vyote, taasisi za umma, na maeneo ya pembezoni ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme. Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu katika jimbo la Kalambo utajumuisha vijiji 89 kupitia vipengele - mradi vya *densification grid extension,* utaokamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya vijiji hivyo itajumuisha ujenzi wa njia ya msongo umeme wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 413.49; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa

kilometa 745; pamoja na ufungaji wa transfoma 149. Kazi nyingine itakuwa ni kuwaunganishia umeme wateja wa awali 9,816 kazi ya gharama hii ni shilingi bilioni 36.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika awamu iliyotangulia Wilaya ya Kalambo ilipatia umeme vijiji vichache sana kutokana na *scope* ya kazi iliyokuwa imetolewa. Je, Serikali ipo tayari kuhakikisha kwamba vile vijiji ambavyo vilikuwa viwe kwenye *REA* Awamu ya Pili vinaanza kuwekewa umeme haraka iwezekanavyo, ikiwepo kijiji cha Mwazi ambacho tayari transfoma iko pale ni suala la kushusha umeme pamoja na kijiji cha Kazila? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ni shuhuda, tulienda naye, akaenda kijiji cha Samazi na Ukanda wa Ziwa Tanganyika, miundombinu ya kule alikiri jinsi ambavyo iko haja kubwa ya kuhakikisha kwamba umeme unafika maeneo yale.

Je, yupo tayari kuhakikisha kwamba vijiji hivi vinapatiwa umeme haraka iwezekanavyo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini, Dkt. Kalemani tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kandege tumetembea naye kwenye Jimbo lake, hakika wananchi wa Jimbo lako Mheshimiwa wanafarijika sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maswali yake mawili ya nyongeza, kweli katika Jimbo la Kalambo ni vijiji 12 tu

vilipitiwa na vyenyewe tulipeleka kwenye vituo tu vya umeme, sasa nikuhakikishie Mheshimiwa Kandege, vijiji 89 vyote vilivyobaki, ikiwemo kijiji cha Jengeni, Nondo, Santa Maria, Legeza Mwendo na vingine vyote ninakuhakikishia kwamba vitapelekewa umeme sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili ninahakikisha vipi. Hatua ya kwanza kabisa tumempelekea mkandarasi, hivi sasa Mkandarasi Nakroi ameishaonana na Mheshimiwa Mbunge na ataanza sasa jitihada za kuendelea katika Jimbo lako la Kalambo. Nikuhakikishie kwamba ataanza na maeneo ambayo tayari kuna transfoma kazi iliyobaki sasa ni kuwasha na ataanza na kuwasha. Katika eneo la Santa Maria pamoja na kwamba msishindane na lenyewe itapelekwa transfoma ili umeme uanze kuwaka mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, swali lako.

Na. 295

**Utafiti wa Madini Kata za Nyakafuru na Bukandwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Leseni ya utafiti wa uchimbaji wa dhahabu ya Mabangu imechukua muda mrefu sana katika Kata za Nyakafuru na Bukandwe.

Je, ni lini mgodi wa uchimbaji dhahabu baina ya Mabangu na Resolute utaanza uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Nyakafuru *(Nyakafuru*

*Gold Mining Project)* unahusisha leseni 22 za utafutaji wa Madini zinazomilikiwa na Kampuni ya Mabangu *Mining Limited* ambayo ni Kampuni tanzu ya *Resolute Tanzania Limited.* Mashapo *(deposit)* katika mradi huu yamesambaa katika leseni hizi ambazo maeneo yake yana ukubwa ya kilometa 1.4 hadi 25.17. Mashapo yaliyogunduliwa katika leseni hizi kwa pamoja ndiyo yanaweza kuchimbwa kibiashara. Hata hivyo kati ya leseni 22, leseni tisa kampuni imeamua kuziachia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kampuni ya *Mabangu Limited* ni Kampuni tanzu ya *Resolute Tanzania Limited*, na kwa kuwa Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* iliyokuwa inamilikiwa na *Golden Pride* ya Nzega inadaiwa kodi na *TRA,* Kampuni ya Mabangu sasa inahusishwa na deni hilo la shilingi bilioni 147.007. Kutokana na Kampuni hiyo kuhusishwa na deni hilo, anayetarajiwa sasa kuwa mbia wa Kampuni ya *Manas Resources* mwenye jukumu la kufadhili mgodi ameamua sasa kupeleka mbele ufadhali wake.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mradi wa Nyakafuru sasa utaanza kuzalishaji dhahabu mwezi Juni, 2019 baada ya masuala ya kodi kukamilika na kupata leseni ya uchimbaji pamoja na mazingira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Masele swali.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwanza, kwa sababu Kampuni ya Resolute imeamua kuachia leseni zake tisa, je, Serikali itakuwa tayari sasa kuzigawa hizo sasa leseni kwa wachimbaji wadogo Wilayani Mbogwe ili waweze kunufaika na dhahabu iliyopo katika eneo hilo? *(Makofi)*

Swali la pili, dawa ya deni ni kulipa. Kampuni hii ya Resolute inadaiwa sasa shilingi bilioni 143 na Serikali. Je, Serikali

ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba deni hili linalipwa kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali hayo mawili mazuri, majibu yake kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini, Dkt. Kalemani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Masele nakupongeza sana, najua juhudi zako na wananchi wako wanatambua jinsi unavyoshughulikia maslahi ya wananchi hasa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kweli kabisa tumejadiliana sana na kampuni hii, kampuni hii ina leseni 22 na maeneo mengi haiyafanyii kazi, kwa hiyo tumekubaliana na Kampuni hiyo sasa imeamua kuya-*surrender* maeneo tisa na maeneo hayo tunagawa sasa kwa wananchi wa Mbogwe, Mheshimiwa Mbunge ninakushauri sana sasa wananchi wako waanze kuunda vikundi ili sasa waweze kurasimishwa, mpango wa kuwagawia ifikapo mwezi wa Julai na Agosti, tutawamilikisha rasmi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na deni, ni kweli kabisa dawa ya deni ni kulipa. Kampuni hii imekuwa ikidaiwa shilingi bilioni 143.007 na kwa sababu ilitaka kuhamisha umiliki wake sisi Serikali tulikataa mpaka deni litakapolipwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hatua inayofanyika wamekubaliana na *TRA* na Kampuni imekubali kulipa, kwa hiyo kuja kufika mwezi wa Julai, kampuni imeahidi kulipa deni hilo. Baada ya kulipa sasa taratibu za umilikishaji zitaendelea rasmi.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 296

## Mgogoro wa Ardhi kati ya Kampuni ya Highland na Wananchi wa Mbarali

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Kampuni ya *Highland Estate* Mbarali na wananchi wanaolizunguka shamba hilo kwa kuwa mwekezaji amekuwa akipora ardhi kwa wananchi na kusababisha uvunjifu wa amani kwa muda mrefu sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shamba linalomilikiwa na Kampuni ya *Highland Estate* awali lilikuwa likimilikiwa na Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula kuanzia mwaka 1978. Baada ya upimaji kukamilika 1981, shamba hilo liliendelea kumilikuwa na *NAFCO* kwa Hati Na. 327–DLR. Tarehe 18 Agosti, 2008 shamba hili liliuzwa na Serikali kwa Kampuni ya *Highland Estate Ltd.*

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa shamba la *Highland Estate* unahusu tafsiri ya mipaka baina ya shamba hilo na vijiji vya Mwanavala, Ibumila, Imalilo, Songwe, Urunda, Ubaruku, Utyego, Mbarali, Mpakani, Mkombwe, Mwakaganga, Ibohola na Nyelegete.

Mheshimiwa Spika, hatua za awali za utatuzi wa mgogoro huu zinahitaji kupata tafsiri sahihi ya mpaka wa shamba kulingana na ramani ya upimaji iliyoidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na vijiji vinavyozunguka

shamba hilo. Zoezi la kutafsiri mipaka baina ya shamba na vijiji husika limeshaanza kufanyiwa kazi na wataalam wa Ofisi ya Mkuu wa wa Mkoa wa Mbeya, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbarali pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa kushirikiana na wanakijiji husika isipokuwa wanakijiji wa kijiji cha Nyelegete ambao wamesusia zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kutatua mgogoro huu bado zinaendelea kufanywa na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa kuwahimiza kijiji cha Nyalegete kutoa ushirikiano kwenye utatuzi wa mgogoro huu ili uweze kumalizika.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kutoa ushirikiano kwa wataalam wa sekta ya ardhi katika maeneo yao ili kuharakisha utatuzi wa migogoro ya ardhi hususan inayohusiana na mipaka ya mashamba. Aidha, napongeza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa utaratibu wake wa kusikiliza kero za wananchi ikiwemo kutatua migogoro ya ardhi mara mbili kwa kila mwezi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Swali la kwanza, kwa kuwa jibu la msingi la Serikali inakiri kwamba shamba hili lilipata hati kuanzia mwaka 1978 mpaka mwaka 1981.

Je, ni kwa nini Serikali haikuwa na hati ambayo leo hii mwekezaji huyu amekuwa akiwaonea wananchi wa vijiji hivyo tajwa alivyovitaja Mheshimiwa Waziri?

Swali la pili, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbarali akiwemo na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali binafsi siwaamini katika utekelezaji wao wa kazi zao. Je, Mheshimwa Waziri huoni umuhimu wa mimi na wewe kuongozana na kwenda

kuwasikilisha wananchi na wanakijiji wa Nyelegete waliokataa kusikiliza mahusiano yao, mimi na wewe tukaenda kwa pamoja. Ni lini na utakuwa tayari tukaongozana kwenda kusimamia hili?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anasema ni kwa nini Serikali haikuwa na hati. Si kweli kwamba Serikali haikuwa na hati kama anavyosema, maeneo yote yanayomilikiwa na Serikali yanafahamika toka awali, na wanakijiji wanaozunguka eneo lile walitambua kwamba lile lilikuwa ni eneo la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la kumuuzia mmiliki mwingine tofauti na Serikali ili aweze kuishi vizuri na wanakijiji wanaomzunguka ni lazima ule uhakiki wa mipaka ufanyike kwa kuhusisha pande zote ambazo zinahusika katika mgogoro huo, kwa sababu huwezi ukampa tu wakati huo huo na wananchi pia nao walikuwa wanalitazama shamba lile.

Mheshimiwa Spika, lazima kufanya ule uhakiki wa mipaka ili kumfanya huyu mwekezaji ambaye yupo aweze kutambua mipaka yake vizuri. Kwa vyovyote unavyouza kwa mtu lazima umkabidhi eneo lako na kuhusisha kwamba ni wapi ambapo mipaka yako inaishia. Kwa hiyo, suala hilo nadhani linaeleweka kwa staili hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema habari ya kwenda Mbarali, nakumbuka mwezi Machi nilikwenda katika Mkoa wa Mbeya na Mbarali nilifika na suala hili lilizungumzwa, lakini kama bado halijatatuliwa na mgogoro bado upo, nadhani tutaangalia ratiba itakavyokuwa imekaa ili tuweze kuongozana na kusikiliza wale wananchi jinsi wanavyolalamika lakini najua chini ya mikono salama ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi masuala hayo yatatatuliwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano litaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, kwa niaba yake Mheshimiwa Waitara.

Na. 297

**Mgogoro wa Ardhi baina ya Wananchi wa Kipunguni na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege - Dar es Salaam**

**MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y. MHE. ANATROPIA L. THEONEST)** aliuliza:-

Kuna mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa Kipunguni 'A' na Kipunguni Mashariki dhidi ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Jijini Dar es Salaam. Wananchi hao wanapinga uthamini uliofanywa na fidia kidogo kwa kikundi cha watu wachache huku wengine wakizuiwa kuendeleza maeneo yao.

(a) Je, ni lini Serikali itaenda kumaliza mgogoro huo uliodumu tangu mwaka 2007?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwapa fidia ya kiwango cha soko wananchi waliozuiwa kuendeleza maeneo yao na kuendelea kubaki maskini kwa muda wote huo?

**NAIBU WAZIRI WA WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, aah samahani naona Mzee Waitara ameniroga hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a ) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya uthamini wa ardhi katika maeneo ya Kipunguni 'A' na Kipunguni Mashariki ikiwa

ni pamoja na maeneo ya Kigilagila na Kipawa mwaka 1997 kwa kuwashirikisha wakazi wa maeneo husika kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji Ardhi *(Land Acquisition Act)* ya mwaka 1967 ambayo inaainisha mambo ya kuzingatia ikiwa ni thamani ya mazao na majengo yaliyopo kwenye maeneo husika, kumpatia mkazi wa eneo linalotwaliwa kiwanja na vilevile kulipa riba ya asilimia sita kwa mwaka pale ambapo malipo yanacheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali haikuwa na fedha za kutosha kuwalipa wakazi wote kwa pamoja, malipo yalifanyika kwa awamu tatu kadri fedha zilivyokuwa zinapatikana. Awamu ya kwanza na ya pili ya mwaka 2009 - 2011 ilihusu malipo ya wakazi wa Kipawa na Kigilagila na katika awamu ya tatu ambayo ilitolewa mwaka 2014 ililipa baadhi ya wakazi wa Kipunguni ambao idadi yao ilikuwa 59.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sasa Serikali imekusudia kumaliza kulipa fidia wananchi waliobaki katika maeneo hayo kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba viwango vya ulipaji fidia huzingatia sheria iliyotumika kufanya uthamini husika. Hivyo kwa kuwa uthamini wa maeneo ya Kipunguni ‘A’ na Kipunguni Mashariki ulifanyika mwaka 1997 kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji Ardhi ya mwaka 1967 malipo au fidia kwa wakazi wa maeneo husika yatazingatia matakwa ya sheria hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, huu ni mgogoro wa eneo ambalo limetathminiwa tangu mwaka 1997, huu ni mwaka 2017 miaka ishirini baadae.

Swali la kwanza, ni kwa nini Serikali inakataa kufanya tathmini upya katika maeneo haya hasa ukizingatia hali ya maisha ya sasa, kwamba hawa watu hata wakilipwa fidia leo hawawezi kufanya chochote kulingana na ugumu wa maisha ulivyo, kwa nini Serikali haipo tayari kufanya tathmini ya fidia ili walipwe kulingana na hali halisi ya maisha ya sasa?

Swali la pili, mgogoro huu pia umeathiri wananchi waliohamishwa kutoka Kipunguni 'A' kwenda Kipunguni 'B' Jimbo la Ukonga, Kipawa wakapelekwa Kata ya Buyuni Ukonga. Tunapozungumza hawa watu hawajalipwa fedha na walihamishwa kutoka Kipawa Kipunguni wakapelekwa Mbuyuni ambako hawakupewa tena maeneo. Sasa kuna mgogoro kati ya wananchi waliotoka Kipawa Kipunguni na wakazi wenyeji wa kule Buyuni.

Mheshimiwa Waziri yupo tayari baada ya Bunge hili au hata *weekend* yoyote tuambatane twende akawasikilize wananchi wenyewe awaone wanavyolalamika na kulia aone kama kuna sababu ya msingi sana ya kuchukua hatua mapema kwa kulipa fidia na kuondoa mgogoro uliopo katika eneo hilo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Injinia Ngonyani tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, sasa tumedhamiria kulipa fidia yote katika mwaka huu wa fedha unaoanza mwezi Julai, kwa sababu tumedhamiria tukisema tuanze kufanya uthamini upya itatuchelewesha kwa sababu kazi ya fidia nayo ni kazi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba sana ndugu zangu tulimalize hili suala na kwa kweli kwa namna fidia tulivyolipa ni kama tumekuja kulipa mara tatu zaidi ya ile thamani iliyokadiriwa mwanzo kwa sababu ya hiyo *interest* na *interest* ni kwa mujibu wa sheria, sehemu zote mbili kulipa kwa kufuata *interest* ya kila mwaka ama kuamua kufanya fidia upya zote ni njia sahihi na zote zinafuata sheria za nchi yetu.

Ninakuomba tulipe fidia kwa kufuata *interest* ambayo imekadiriwa kuanzia mwaka huo walipofanyiwa tathmini, najua Serikali tutaingia hasara kwa sababu tutalipa zaidi kuliko kama tungeweza kufanya *evaluation* upya, lakini Serikali imekubali ili tusipoteze muda tena tulimalize hilo *once and for all*.

Pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge niko tayari baada ya kumaliza Bunge hili tupange twende tukalishughulikie suala hilo huko. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona muda wetu umeisha na maswali yameisha wale ambao hamkupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza tusameheane kama mnavyoona muda ni mdogo sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuko kwenye matangazo, kwanza lazima twende kwa vipaumbele hapa. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu anao wageni wake ambao ni wageni wa Bunge hili pia, nao si wengine bali ni wachezaji 23 na viongozi wao na benchi la ufundi la timu ya *Simba Sports Club.(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbeleko.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo ni timu ya Simba na wale vijana wa mjini wanasema *this is Simba bwana! (Makofi)*

Mambo waliyoyafanya siku Jumamosi wote ni mashahidi, pia kipekee tunamshukuru sana Mheshimiwa Juma Nkamia ambaye juzi alitangaza mpira huo kupitia *TBC* tunakushukuru sana. Simba tunawatakia kila la kheri tunawategemea kwenye mashindano haya ya Kimataifa mtatuwakilisha vizuri sana na mtachukua Kombe la Afrika. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wengine walioko katika Jukwaa la Spika ni pamoja na wageni 92 wa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Balozi Dkt.

Augustine Mahiga ambao ni Katibu Mkuu Balozi Dkt. Aziz Mlima karibu sana, Naibu Katibu Mkuu Balozi Ramadhani Mwinyi, Mwenyekiti wa Bodi ya *AICC* Balozi Dkt. Ladislaus Komba, Mkuu wa Itifaki Balozi Grace Martin, Mkurugenzi wa Idara ya Diaspora Balozi Anisa Mbega, Mkurugenzi Ushirikiano wa Kikanda Balozi Innocent Shiyo na Mkurugenzi Ushirikiano wa Kimataifa Balozi Selestine Mushi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao Mabalozi kutoka nchi mbalimbali ambazo ni kama zifuatazo:

Balozi *Republic of* Saharawi Mheshimiwa Brahim El Mami Buseif, tunaye Balozi wa Democratic *Republic of* Korea Mheshimiwa Kim Yong Su, karibu. Balozi *Republic of* Burundi Mheshimiwa Gervais Abayeho, karibu sana Balozi kutoka *fasi* ya Bujumbura, na tuna mchezaji fulani pale anatoka huko. Balozi wa *Republic of Sudan* Mheshimiwa Ahmed Abdallah Sharfi. Balozi wa *Republic of Zambia* Mheshimiwa Benson Keith Chali, Balozi *Republic of Kenya* Bonifance Muhia, karibu sana jirani. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Balozi mdogo wa Algeria Mheshimiwa Mohamed Nabil, Balozi wa Syria Mheshimiwa Abdulmonem Annan, Balozi wa Nigeria Mheshimiwa Salisu Umaru, Mwakilishi wa Balozi wa China Ndugu Dai Xu, Mwakilishi wa Balozi wa Russia Ndugu Pavel Alferov, Balozi wa nchi jirani ya Rwanda Mheshimiwa Issa Mugabutsinze, Mwakilishi kutoka *IMF* Ndugu Chelaus Rutachururwa na wameambatana na wageni wengine wengi kutoka Wizarani na Kurugenzi mbalimbali, Wakuu wa Taasisi, Vitengo na Maofisa mbalimbali chini ya Wizara hiyo ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Pia wako wanafunzi 32 kutoka Chuo cha Diplomasia Jijini Dar es Salaam naomba msimame pale mlipo wanadiplomasia, karibuni sana hapa Bungeni mjifunze mambo yanavyokwenda hapa, karibuni sana. Wako pia wageni 41 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM)*, karibuni sana na wageni wote mliopo pia mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club,* ambaye anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mechi ya mpira wa miguu iliyochezwa siku ya Jumamosi kati ya *Bunge Sports Club* na wafanyakazi wa Kampuni ya *AZAM* ikiwa ni mechi ya utangulizi wa mchezo wa fainali kati ya Simba na Mbao, *Bunge Sports Club* walipata bao mbili *AZAM* bao moja. Wafungaji kwa upande wa Bunge alikuwa ni Mheshimwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King naomba Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Ali Hassan King msimame, ninawashukuru sana kwa heshima kubwa mliyotupatia siku hiyo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mgeni rasmi katika mchezo huo alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Michezo hiyo pia ilihudhuriwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. Pia *Bunge Sports Club* inaipongeza sana timu ya *Simba Sports Club* kwa kutwaa Ubingwa wa Kombe la Shirikisho. Aidha, *Bunge Sports Club* wanawapa pole timu ya *Mbao FC* waendelee kujiandaa vizuri kwa ajili ya mwakani. *(Makofi)*

*Bunge Sports Club* inawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na kuwashukuru wananchi wa Dodoma kwa ujumla kwa jinsi mnavyojitokeza kwa wingi katika kushuhudia mitanange mbalimbali ambayo inachezwa na *Bunge Sports Club. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia *Bunge Sports Club* inatoa pole kwa familia ya Marehemu Shose mpenzi wa Simba aliyefariki dunia kwa ajali ya gari jana wakati akitokea Dodoma kurejea Dar es Salaam. Tunawaombea majeruhi wote wa ajali hiyo wapone haraka.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo sasa naomba nimuite Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu aweze kuendelea na shughuli zilizo mbele yetu. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hivi Klabu ya Simba ime......*(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Walibebwa, Mheshimiwa Mwenyekiti. Ushindi wa mezani.

**MWENYEKITI:** Hongereni mabingwa wa Tanzania.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti umeshindwa hata kusema. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI - KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, likubali kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa fadhila na rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Bunge lako Tukufu, kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja

waliozungumza kabla yangu wakiongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango ambao kwa hakika hotuba zao zimekuwa dira na msingi wa kuainisha masuala muhimu ya kitaifa na kimataifa ambayo baadhi yake yanagusa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu imefanywa kuwa nyepesi zaidi kutokana na ushirikiano mzuri na ushauri tunaoupata mara kwa mara kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Hivyo napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab na Makamu wake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Miongozo na ushauri wao imekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama mbele yenu kusoma hotuba hii, nyuma yangu kuna kundi kubwa la Watendaji na Watumishi wanaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwao kwa kuwa kwa kiasi kikubwa ndio wameniwezesha nisimame mbele yenu leo kuwasilisha hotuba hii. Kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Susan Alphonce Kolimba - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Dkt. Aziz Ponary Mlima - Katibu Mkuu, Mheshimiwa Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi - Naibu Katibu Mkuu, Mabalozi, Wakurugenzi na wafanyakazi wengine wote kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa pongezi kwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kulitumikia Taifa katika Bunge lako Tukufu. Kati ya hao ni pamoja na mimi, ninatoa tena shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa hii ya pekee kuwa Mbunge ninayewezesha

kuhutubia Bunge lako Tukufu leo. Aidha, sina budi kutoa pongezi maalum kwa Wabunge wateule wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, ni dhahiri kuwa kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na Taifa letu. Ni matarajio yetu kuwa wataendelea kutetea na kusimamia maslahi ya nchi yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kutunza misingi ya mshikamano uliopo baina ya Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru kwa dhati mke wangu mpendwa Mama Elizabeth Mahiga, watoto na familia yangu yote kwa ujumla kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kunipa utulivu wa kutosha kuniwezesha kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga Taifa na kutetea maslahi ya Taifa letu nje na ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, naungana na wabunge wenzangu kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia za Wabunge wenzetu wawili, Marehemu Hafidh Ali Tahir na Marehemu Dkt. Elly Marco Macha waliotangulia mbele ya haki wakati wakiendelea kulitumikia Taifa katika Bunge lako Tukufu.

Aidha, natumia fursa hii kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia za wafanyakazi wenzangu Wizarani, Marehemu Hadija Mwichande na Marehemu Dkt. Cuthbert Leonard Ngalepeka waliotutoka katika kipindi hiki. Tuendelee kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awapumzishe mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Mei, 2017 Taifa lilizizima kwa majonzi makubwa baada ya kupoteza watoto 32, walimu wawili na dereva mmoja wa shule ya Lucky Vincent ya Arusha kwa ajali mbaya ya gari lililokuwa limebeba wanafunzi hao katika Wilaya ya Karatu wakitokea Mkoani Arusha kwenda kufanya mitihani ya majaribio. Kwa majonzi makubwa mno naomba nichukue fursa hii kutoa salamu za pekee kwa wazazi, walimu, Mkoa wa Arusha na Watanzania wote kwa ujumla.

Aidha, ninaomba nifikishe salamu za rambirambi kutoka Balozi mbalimbali za nchi za nje zilizopo hapa nchini na mashirika mbalimbali ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuwashukuru wasamaria wema Dkt. Steeve Mayor, Dkt. Jennifer Milby, Dkt. Maanda Volker na Ndugu Kelvin Negaard, raia wa Marekani kwa moyo wao wa upendo waliouonesha kwa kuwahudumia marehemu na majeruhi wa ajali hiyo. Ninawashukuru sana kwa msaada wao ambao haukuishia kwenye eneo la ajali bali pia walitafuta usafiri wa kuwapeleka majeruhi nchini Marekani kwa matibabu zaidi kwa gharama zao. Shukrani za dhati ziende pia kwa Taasisi ya Bill Graham kwa kukubali kutoa usafiri wa ndege kuwasafirisha majeruhi, wazazi, na wataalam wa afya wa Tanzania hadi North Carolina na baadae kuchukuliwa na ndege maalum ya wagonjwa wa dharura hadi Hospitali ya Mercy iliyopo Sioux *City*, Iowa, Marekani wanapotibiwa hadi sasa na hali za wagonjwa zinaendelea kuwa nzuri. Hakika ukarimu na upendo mkubwa waliouonesha kwa watoto hawa hautasahaulika katika mioyo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaishukuru pia Serikali ya Jamhuri ya Kenya kwa kututia moyo wakati wa tukio hili la kuhuzunisha. Aidha, ninawashukuru Watanzania wote waliojitolea kwa namna moja ama nyingine katika mazishi na matibabu ya wahanga wa ajali hiyo. Tuendelee kuwaombea majeruhi wapone haraka ili waweze kuendelea na masomo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ina sehemu kuu nane kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba yangu. Hivyo nitasoma muhtasari wake na ninaomba hotuba hii iingizwe weye Kumbukumbu za Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mweyekiti, tahthimi ya hali ya dunia; kabla sijatoa tathmini ya hali na mwelekeo wa siasa duniani na jinsi Tanzania ilivyojipanga kushiriki, ningependa kulikumbusha Bunge lako Tukufu juu ya misingi ya Sera yetu ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Tanzania kupata uhuru na kusaidia nchi nyingine za Afrika kujikomboa kutokana na ukoloni na ubaguzi wa rangi, Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania inaendelea kujikita katika misingi ifuatayo:-

(a) Kulinda uhuru, umoja na heshima ya nchi yetu;

(b) Kuendeleza ujirani mwema katika kanda yetu na kukuza umoja na ushirikiano barani Afrika;

(c) Kuheshimu kanuni ya kutoingilia masuala ya ndani ya nchi nyingine;

(d) Kutofungamana na upande wowote na kuchagua kwa hiari bila masharti marafiki katika Jumuiya ya Kimataifa;

(e) Kushirikiana kikamilifu Kimataifa na nchi, mashirika na taasisi mbalimbali katika nyanja za diplomasia, siasa, uchumi, utaalam na teknolojia; na

(f) Kukuza na kutekeleza diplomasia ya uchumi, hususan uchumi wa viwanda katika Awamu hii ya Tano. Na hii ni sura mpya ya siasa yetu na Sera yetu ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu diplomasia ya uchumi wa viwanda. Katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kama ilivyoainishwa hapa, Serikali ya Awamu ya Tano itazingatia mikakati na vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuanzisha mahusiano mapya ya kidiplomasia ambayo yataongeza tija kwa maslahi ya nchi hususan maendeleo ya uchumi, viwanda na teknolojia na nchi hizo mpya ni kama vile Israel, Morocco, Algeria, Qatar na nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha mkakati wa diplomasia ya uchumi wa viwanda, tutaendelea na mikakati ifuatayo katika Sekta ya Viwanda:-

(1) Utafutaji wa mitaji kutoka vyanzo vya fedha vya Kimataifa kama vile mabenki ili kuwezesha na kuyaleta hapa nchini.

(2) Kutambua na kuchukua utaalam na ufundi kutoka nje utakaosaidia kujenga na kuendesha viwanda hapa nchini.

(3) Kutafuta na kushawishi wawekezaji katika sekta muhimu za kuendeleza Viwanda kama vile Miundombinu, Nishati na Uchukuzi.

(4) Kuunganisha wawekezaji kutoka Sekta ya Kilimo na Viwanda *agro processing industries* ili kuongeza thamani ya bidhaa na kukidhi mahitaji ya chakula katika Taifa letu.

(5) Kuainisha fursa za ubia kati ya wawekezaji kutoka Sekta Binafsi na Sekta ya Umma yaani *Public Private Partnership* katika viwanda.

(6) Kuwekeza katika vyuo vya ufundi na uendeshaji wa viwanda, ufundi unaolenga kuhudumia viwanda.

(7) Kuunganisha soko la ndani kwa kutafuta soko la nje kwa bidhaa zinazotokana na viwanda hapa nchini; na

(8) Kupeleka wanadiplomasia nje wenye ujuzi wa kidiplomasia ya uchumi kulingana na vipaumbele vya nchi na huko wanakowakilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunda kitengo cha intelijensia ya uchumi na uchambuzi ndani ya Idara ya Sera ya Wizara yangu. Kufuatia mkakati huo, tumeweza kuvutia uwekezaji wa takribani viwanda 224 vyenye mtaji wa zaidi ya trilioni 4.2 katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro na mingineyo na haya yametokea ndani ya miezi 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kufungua fursa za uwekezaji, kuratibu na kutathmini

mafanikio katika uwekezaji. Kushiriki kikamilifu katika kutafuta suluhu ya migogoro kwa njia ya amani kwa kuzungumza moja kwa moja na wadau husika na kushiriki kikamilifu katika majukwaa ya kimataifa au kikanda katika kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi Tanzania itaendelea na mkakati wake endelevu wa kutetea uhuru na haki kimataifa huku ikizingatia vipaumbele vyake vya maendeleo mapana na siasa yake ya kutofungamana na upande wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya kisera naomba kutoa tathmini ya hali ya siasa na mwelekeo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 tathmini ya hali ya dunia kwa ujumla inaonesha kuwa dunia imeshuhudia ongezeko dogo katika kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika Mataifa ya Magharibi yenye uchumi mkubwa hali inayochangia kuendelea kudorora kwa biashara ya kimataifa. Ongezeko la machafuko ya kisiasa, migogoro ya kivita na vitendo vya kigaidi katika baadhi ya mataifa vimechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la wakimbizi na wahamaji wasio na hati za kusafiria. Mabadiliko ya tabianchi yanayozidi kuleta athari kubwa katika ikolojia na kutishia uhai wa viumbe na shughuli za kibinadamu. Hususan kwa Mataifa yanayoendelea kutokana na uwezo mdogo wa Mataifa hayo kukabiliana nayo hivyo kurudisha nyuma juhudi za kujikwamua na umaskini. Matukio hayo ya kidunia yameibua hisia kuwa ipo haja kwa Jumuiya ya Kimataifa kufanya jitihada mahsusi kukabiliana nayo ili kuimarisha ustawi wa dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa tathmini hiyo ya jumla, aya ya 18 hadi ya 22 ya kitabu cha hotuba yangu inafafanua kwa kina tathmini ya maeneo machache kuhusu hali ya ulinzi na usalama duniani katika Mabara ya Afrika, Asia, Ulaya pamoja na Bara la Amerika ya Kusini na Kaskazini. Aidha, aya ya 23 hadi ya 25 inaeleza tathmini ya

kina ya haki na hali ya uchumi duniani kwa Mabara hayo kwa kipindi cha mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika medani za siasa, kumekuwa na chaguzi katika nchi kadhaa kama vile Marekani, Ufaransa na Uholanzi, ambapo katika chaguzi zote hizo dunia imeshuhudia ongezeko kubwa la wafuasi wa siasa zenye mrengo wa kulia na wa kibaguzi. Serikali mpya zilizoingia madarakani hasa huko Ulaya zina mrengo wa wastani na ushirikiano Kimataifa, pia zitajikita zaidi katika kuhamasisha maendeleo ya ndani na kupunguza kasi ya ukuaji wa biashara za uchumi wa dunia kwa ujumla. Serikali hizo zitapunguza makali ya vyama vyenye mrengo wa kulia. Aidha, uamuzi wa kujitoa kwa Taifa la Uingereza katika Jumuiya ya Umoja wa Ulaya pia ni kielelezo cha tofauti zinazojitokeza katika mataifa ya Ulaya na ni vizuri tukaelewa matokeo yake kwa nchi zinazoendelea kama vile Tanzania ili tujipange iwezekanavyo katika kushirikiana na nchi hizo.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali mpya ya Marekani haijafafanua siasa yake ya uhusiano na Afrika. Matamshi ya Rais wa sasa wa Marekani kuhusu Afrika yamekuwa yakitofautiana na tawala zilizopita na yanaashiria mwelekeo mpya huko Marekani. Hata hivyo, Serikali ya Marekani imeendeleza msaada kwa Tanzania katika kupambana na maambukizi ya UKIMWI. Tunashukuru kwa msaada huo wa dola za Kimarekani milioni 526.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya kuyumba kwa hali ya uchumi duniani, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga pamoja na mambo mengine kuendelea kuwashawishi wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuwekeza katika sekta mbalimbali hapa nchini, kuboresha mazingira ya vituo vivutio vya uwekezaji, kuendelea kutafuta fursa za masoko ya bidhaa zetu nje ya nchi na kushawishi watalii kutoka mataifa mengine kutembelea nchi yetu ili kupanua wigo wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha

2016/2017; kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 Wizara yangu ilitekeleza majukumu mbalimbali kama inavyoenekana katika aya 28 ya kitabu cha hotuba yangu. Katika kutekeleza majukumu hayo kwa mwaka 2016/2017 Wizara yangu ilitengewa kiasi cha shilingi 162,109,416,709; kati ya fedha hizo, shilingi 158,109,516,709 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 8,000,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida, shilingi 143,768,662,709 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 10,340,754,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara ilitarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 24,001,150,000. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2017 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 19,773,333,502 sawa na asilimia 83 ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2017 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 95,037,516,058, sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge, kati ya fedha hizo shilingi 83,039,138,698 ni kwa ajili ya bajeti ya matumizi mengineyo, shilingi 8,509,062,360 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 3,489,315,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa licha ya changamoto mbalimbali za kibajeti. Katika kipindi hiki Wizara imeendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya fedha za umma katika kudhibiti matumizi na mapato ambapo kwa kudhihirisha hilo, Wizara yangu na Balozi zote isipokuwa Ubalozi mmoja tu zimepata hati safi ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Nachukua nafasi hii kuwashukuru watendaji wa Wizara na kuwahimiza waendelee kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za umma wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi jinsi Wizara ilivyotekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 na

kwanza kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje ikiwa ni pamoja na Sera ya Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi inaendelea kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje yenye lengo la kukuza uchumi kupitia Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda kwa kuratibu na kufanikisha ziara za viongozi wanaokuja nchini, Mikutano ya Tume za Pamoja na Tume za Kudumu za Ushirikiano, masuala ya ushirikiano kati ya Tanzania na nchi rafiki, Mikutano ya Bara la Afrika na nchi nyingine pamoja na makongamano ya biashara yaliyofanyika ndani na nje ya nchi. Tunatumia kila jukwaa na kila fursa ya kuendeleza diplomasia ya uchumi katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara yangu iliratibu ziara ya viongozi, Mikutano ya Tume ya Kudumu na Ushirikiano, *Mission* na wataalamu mbalimbali kutoka mataifa ya Vietnam, India, China, Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu, Qatar, Iran, Israel, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Morocco, Zambia, Kenya, Uganda, Ethiopia, Afrika ya Kusini, Cuba, Czech, Finland, Uswisi, Canada, Uturuki, Japan na Jamhuri ya Korea. Kati ya ziara zilizofanyika nchini, nchi yetu ilijadiliana na viongozi hao na kufikia kusaini mikataba mbalimbali katika sekta za afya, maji, utalii, elimu, biashara, uchumi na ufundi, miundombinu na barabara, bandari, reli na viwanja vya ndege. Maelezo ya kina kuhusu makubaliano yaliyofikiwa kutokana na ziara hizo hapa nchini pamoja na mikataba iliyoainishwa yanapatikana kuanzia aya 34 hadi 87 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kutekeleza jukumu hili, Wizara inaendelea kufanya kazi kwa karibu na sekta za umma na binafsi katika kuratibu maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika majukwaa na makongamano ya kibiashara na uwekezaji kimataifa. Faida za majukwaa hayo ni kufungua fursa za kiuchumi kwa wafanyabiashara wa

Kitanzania na kuimarisha mahusiano ya kibiashara na kuvutia uwekezaji nchini hususan katika sekta ya viwanda. Maelezo ya kuhusu majukwaa yaliyofanyika na nchi tulizoshirikiana nazo yanapatikana kuanzia aya ya 88 hadi 89 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusimamia Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliratibu na kusimamia, kusainiwa kwa mikataba 12 na hati za makubaliano 28 baina ya Tanzania na nchi mbalimbali katika sekta za viwanda, anga, nishati, kilimo, afya, elimu na masuala ya usalama na diplomasia kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba na makubaliano hayo ni kiashiria kikubwa katika kuimarisha uhusianao wa Kidiplomasia baina ya nchi zetu na nchi nyingine na hasa diplomasia ya uchumi uliojikita kwenye viwanda. Mashiriki ya Kikanda na Kimataifa katika kuongeza kasi ya kuvutia wawekezaji kukuza biashara na kutangaza utalii, Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo ili kulinda maslahi mapana ya nchi yetu ikishirikiana na Wizara na sekta zote mbalimbali ambapo makubaliano hayo yanasimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusimama masuala yanayohusu kinga za haki za wanadiplosia waliopo nchini; Wizara inaendelea kushirikiana na mamlaka mbalimbali nchi ili kuhakikisha kuwa jamii za kibalozi zinazowakilisha nchini hapa na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini, zinapata haki zao kama ilivyoainishwa katika sheria ya kimataifa hususan mkataba wa Vienna, kuhusu mahusiano ya kidiplomasia ya mwaka 1961.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa wito kwa Mabalozi, Wanadiplomasia, Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa na wafanyakazi wote wenye kinga kuendelea kuheshimu sheria na taratibu za nchi pamoja Mkataba huo wa Vienna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusimamia na

kuratibu masuala ua Itifaki na Uwakilishi; Wizara inaendelea kuratibu ziara za viongozi mbalimbali wa kitaifa kwenda nje. Ziara hizo ni za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Baadhi ya ziara za viongozi hao zilizofanywa katika nchi za nje ni zifuatazo; Ethiopia, Kenya, Mauritius, Indonesia, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, China na Swaziland.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizi zimeendelea kuwa na mafanikio makubwa sio tu katika kukuza na kuimarisha mahusianao baina yetu na nchi hizo pamoja na Mashirika ya Kimataifa, bali pia zimeendelea kuitangaza Tanzania kama kitovu cha fursa za kiuchumi pamoja na kuisaidia kupata ufadhili katika miradi mikubwa ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine Wizara imeendelea kuandaa na kuratibu sherehe za kuwasilisha hati za utambulisho za mabalozi wa nchi mbalimbali wanaowakilisha nchi zao hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwao Mabalozi waliowakilisha hati zao hapa ni kutoka wa nchi za Italy, Saudi Arabia, Morocco, Zambia, Cuba, Iran, Burundi, Jamhuri ya Korea, Somalia, Ireland, Canada, Thailand, Austria, Uingereza, Sudan, Slovakia, Ukraine, Ghana, Hungary, Belarus, Guinea, Botswana, Niger, Mauritius, Cyprus, Bangladesh, Nepal, Gabon, Ecuador, New Zealand na Congo Brazaville. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli; Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kwenye Balozi zetu nje na kutoa viza kwa raia wa kigeni wanaotembelea nchini, kurahisisha upatikanaji wa viza kwa maafisa na watendaji wa Serikali, vyama vya siasa na taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo; pia kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania waishio

nje ya nchi na kutatua matatizo na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa nje za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuratibu masuala ya ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa; katika kipindi hiki Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika masuala ya ushirikiano wa kikanda ikiwemo Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi na Jumuiya ya Afrika Masharikikama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki Barani Afrika. Ili kuimarisha ushirikiano na Bara la Afrika, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 28 wa Umoja wa Afrika ambao ulipitisha maazimio yaliyobainisha katika aya ya 100 ya kitabu changu cha hotuba yangu.

Aidha, pembezoni mwa mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikabidhi zawadi ya kinyago chenye kuashiria umoja kilichowekwa katika Jengo la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika lililopewa jina la *Julius Nyerere Peace and Security Building* huko Addis Ababa. Jengo hili lilipewa jina hilo kutokana na mchango mkubwa wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika masuala ya ukombozi, umoja na amani katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ushirikiano na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano na majukwaa mbalimbali ya Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliratibu ushiriki wa nchi yetu katika masuala ya siasa, ulinzi, usalama na utangamano wa Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika uundaji wa mkakati wa jumuiya ya kuendeleza viwanda ya mwaka 2016 ndani ya *SADC* inayoendelea mpaka mwaka 2063 na Mpango Kazi wa utekelezaji wake hasa katika sekta za viwanda katika Kanda ya *SADC*. Maelezo ya kina kuhusu masuala hayo yanapatikana kuanzia aya ya 103 hadi 117 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano na nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa jumuiya ya nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi uliofanyika mjini Jakarta, Indonesia mwezi Machi 2017. Maelezo ya kina kuhusu maazimio ya mkutano huo yanapatikana kuanzia aya ya 118 hadi 119 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye kutekeleza kikamilifu majukumu mbalimbali kwa lengo la kuendeleza maslahi mapana ya kitaifa katika Mtangamano wa Jumuiya hiyo. Aidha, Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji wa mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki ya Umoja wa Forodha, Itifaki ya Soko la Pamoja, Itifaki ya Umoja wa Fedha na ushirikiano baina ya Jumuiya ya Afrika na kanda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara inaendelea kuratibu sekta za uzalishaji, sekta za huduma za jamii na utekelezaji wa programu ni miradi ya miundombinu ya jumuiya. Maelezo ya kina kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itifaki zake ni kama ilivyoainishwa kuanza aya ya 119 hadi 159 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa baada ya Tanzania kushika nafasi ya Uwenyekiti kwa miaka miwili mfululizo wa jumuiya yetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Mei, 2017 katika Mkutano wa Kumi na Nane wa Wakuu wa Nchi alikabidhi Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda katika kipindi cha Uenyekiti wa Tanzania. Jumuiya ya Afrika Mashariki imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa programu na miradi yake mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha uenyekiti wa nchi yetu pamoja na utekeleaji wa masuala ya siasa, ulinzi na usalama yamefafanuliwa katika aya ya 160 hadi 177 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki. Katika mikutano hiyo, Bunge letu la Tatu la Afrika Mashariki lilipitisha miswada minne ya sheria iliyoorodheshwa katika aya ya 178 ya kitabu cha hotuba yangu. Miswada hiyo inawasilishwa kwa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kusainiwa na kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimaisha ushirikiano wa Kimataifa, katika kipindi hiki Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Umoja wa Mataifa hapa nchini inaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali, ndani na nje ya Serikali kuhusu malengo ya maendeleo endelevu. Lengo ni kuhakikisha kwamba umma na makundi yote kwenye jamii yanafahamu nafasi yao kwenye utekelezaji wa malengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara iliratibu na kushiriki katika masuala mengine ya ushirikiano wa Kimataifa ikiwemo Mkutano wa 71 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa; Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi; Mkutano wa Tano na Mfuko wa Dunia kwa Masuala ya Afya ijulikanayo kama *Global Fund* na Mkutano wa Shirika la Posta duniani. Aidha, Wizara iliratibu na kufuatilia ushiriki wa Tanzania katika *Mission* za Umoja wa Mataifa za kulinda amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwasilishaji wa taarifa na hali ya haki za binadamu; masuala ya wakimbizi pamoja na ujenzi wa eneo la kuhifadhi masalia ya kumbukumbu za kesi za mauaji ya Kimbari. Maelezo ya kina kuhusu malengo, maazimio na mafanikio ya mikutano hiyo ikiwa na pamoja na mafanikio na hatua zilizofikiwa katika operesheni za kulinda amani yanapatikana kuanzia aya ya 179 hadi aya ya 209 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haitaendelea kushirikiana na mashirika ya Kimataifa katika kulinda matumizi endelevu ya mito iliyo ndani ya mipaka ya nchi yetu, kama vile Mto Ruaha na iliyopo Tanzania lakini inaanzia nchi jirani kama vile Mto Mara. Matumizi ya maji hayo ni muhimu sana katika kuendeleza utalii na uhifadhi wa mazingira ambayo ni urithi wa nchi husika na ulimwengu wote kwa ujumla. Maelezo zaidi kuhusu jukumu hili la kulinda matumizi ya maji ya mito hii yanapatikana katika aya ya 207.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuwahamasisha na kuwashirikisha Watanzania waishio Ughaibuni katika kuchangia maendeleo nchini. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliandaa Kongamano la Tatu la Diaspora lililofanyika Zanzibar mwezi Agosti, 2016 ambapo Diaspora kutoka zaidi ya nchi 20 duniani walishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara iliratibu ushiriki wa taasisi za Umma na binafsi wenye kongamano la kuadhimisha siku ya Tanzania yenye lengo la kutangaza fursa za uwekezaji kwenye Sekta ya Maliasili na Utalii lililofanyika Texas, Marekani mwezi Mei, 2017 yaani mapema mwezi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu uratibu wa masuala ya Watanzania waishio Ughaibuni pamoja na faida za makongamano haya yanapatikana kuanzia aya ya 210 hadi aya ya 213 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimamia utawala na maendeleo ya utumishi, Wizarani na kwenye balozi zetu. Wizara kwa kushirikiana na wafadhili imeendelea kugharamia mafunzo ya Watumishi ya muda mrefu na muda mfupi ndani ya nje ya nchi katika Diplomasia ya Uchumi na hasa wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki watumishi 77 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 14 waliendelea mafunzo ya muda mrefu katika shahada ya umahiri. Katika kipindi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa Mabalozi kujaza nafasi zilizokuwa wazi katika vituo vifuatavyo; Beijing, Paris, Brussels, Muscat, Rome, New Delhi, Pretoria, Nairobi, Brazilia, Maputo, Kinshasa, Kampala, Abuja na Geneva. Aidha, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi wa Mabalozi kwa ajili ya balozi mpya katika nchi za Algeria, Israel, Korea Kusini, Sudan, Qatar na Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo na taasisi zilizo chini ya Wizara; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya maendeleo kiasi cha shillingi bilioni nane. Hadi kufikia mwezi Mei, 2017 Wizara imepokea shilingi bilioni 3.4 za bajeti ya maendeleo sawa na asilimia 44. Miradi iliyotekelezwa na fedha zilizotumika vimeorodheshwa kuanzia aya ya 217 hadi aya ya 218 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara yangu inasimamia taasisi tatu ambazo ni Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Jijini Dar es Salaam, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa ikiwa ni pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa taasisi hizo yameainishwa kuanzia aya 219 hadi aya ya 227 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 zipo changamoto mbalimbali ambazo Wizara imekabiliana nazo wakati wa kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na njia ya kukabiliana nazo vimefafanuliwa kwa undani, kwa kina zaidi katika aya ya 228 hadi 232 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na mambo mengine, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na majukumu yake kama yalivyoainishwa katika aya ya 233 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mabalozi, Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi zao katika kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na washirika wa maendeleo kutoka nchi na Taasisi mbalimbali za Kimataifa, Kikanda, pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wote wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini, Algeria, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Finland, Hungary, India, Italia, Ireland, Israel, Iran, Japan, Korea Kusini, Korea Kaskazini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Malta, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Uswisi na Uturuki na Vietnam. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri omba pesa muda wako imekwisha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu iliyobakia iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge na hapa nilipofika, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa soma tu hiyo pesa unayoiomba. Soma hiyo *amount* iingie kwenye *Hansard.*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu kwa mwaka 2017/2018 Wizara imetengewa shilingi 150,845,419,000; kati ya fedha hizo shilingi 142,845,419,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 8,000,000,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. AUGUSTINE PHILIP MAHIGA (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuweka mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/ 2017. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/ 2018.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa fadhila na rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Bunge lako Tukufu kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** niungane na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja waliozungumza kabla yangu wakiongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango ambao kwa hakika hotuba zao zimekuwa dira na msingi wa kuainisha masuala muhimu ya Kitaifa na Kimataifa ambayo baadhi yake yanagusa majukumu ya Wizara yangu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mhe. Balozi Adadi Mohammed Rajab (Mb) na Makamu wake Mhe.

Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis (Mb) pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali imekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaposimama mbele yenu kusoma hotuba hii nyuma yangu kuna kundi kubwa la watendaji na watumishi wanaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwao kwa kuwa kwa kiasi kikubwa ndio wamewezesha nisimame mbele yenu leo kuwasilisha hotuba hii.

Kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mhe. Dkt. Susan Alphonce Kolimba (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mhe. Balozi Dkt. Aziz Ponary Mlima, Katibu Mkuu; Mhe. Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu; Mabalozi; Wakurugenzi; na Wafanyakazi wengine wote kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutoa pongezi kwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kulitumikia Taifa katika Bunge lako Tukufu. Aidha, sina budi kutoa pongezi maalum kwa Wabunge Wateule wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Ni dhahiri kuwa kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na Taifa letu. Ni matarajio yetu kuwa watakuwa wazalendo, watatetea na kusimamia maslahi ya nchi yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kutunza misingi ya mshikamano uliopo baina ya Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki na Dunia kwa ujumla.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kumshukuru kwa dhati mke wangu mpendwa Mama Elizabeth Mahiga, Watoto na familia yangu yote kwa ujumla kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kunipa utulivu wa kutosha kuniwezesha kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga taifa na kutetea maslahi ya taifa letu nje na ndani ya nchi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa, naungana na wabunge wenzangu kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia za wabunge wenzetu wawili, Marehemu Hafidh Ally Tahir na Marehemu Dkt. Elly Marko Macha waliotangulia mbele ya haki wakati wakiendelea kulitumikia Taifa katika Bunge lako Tukufu. Aidha, natumia fursa hii kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia za wafanyakazi wenzangu Wizarani, marehemu Hadija Mwichande na Marehemu Dkt. Cuthbert Leonard Ngalepeka waliotutoka katika kipindi hiki. Tuendelee kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awapumzishe mahala pema peponi. Amina.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 6 Mei, 2017 Taifa lilizizima kwa majonzi makubwa baada ya kupoteza watoto 32, walimu wawili na dereva mmoja wa Shule ya Lucky Vincent ya Arusha kwa ajali mbaya ya gari iliyotokea Wilayani Karatu. Kwa majonzi makubwa mno naomba nichukue fursa hii kutoa salamu za pole kwa wazazi, walimu, Mkoa wa Arusha na Watanzania wote kwa ujumla. Aidha, ninaomba nifikishe salamu za rambirambi kwa Bunge lako Tukufu kutoka Balozi mbalimbali za nchi za Nje zilizopo hapa nchini na mashirika mbalimbali ya kimataifa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuwashukuru wasamaria wema Dkt. Steeve Mayor, Dkt. Jennifer Milby, Dkt. Maanda Volker na Bw. Kelvin Negaard, raia wa Marekani kwa moyo wao wa upendo waliouonesha kwa kuwahudumia marehemu na majeruhi wa ajali hiyo. Ninawashukuru sana kwa msaada wao ambao haukuishia kwenye eneo la ajali bali pia walitafuta usafiri wa kuwapeleka majeruhi nchini Marekani kwa matibabu zaidi kwa gharama zao.

Shukrani za dhati ziende pia kwa taasisi ya Bill Graham kwa kukubali kutoa usafiri wa ndege kuwasafirisha majeruhi, wazazi, na wataalam wa afya wa Tanzania hadi North Carolina na baadae kuchukuliwa na ndege maalum ya wagonjwa wa dharura hadi Hospitali ya Mercy iliyopo Sioux City, Iowa, Marekani wanapotibiwa hadi hivi sasa na hali zao

zinaendelea vizuri. Hakika ukarimu na upendo mkubwa waliouonesha kwa watoto hawa hautasahaulika katika mioyo ya Watanzania.

**11.** ***Mheshimiwa Spika*** naishukuru pia Serikali ya Jamhuri ya Kenya kwa kututia moyo wakati wa tukio hili la kuhuzunisha. Aidha, ninawashukuru watanzania wote waliojitolea kwa namna moja ama nyingine katika mazishi na matibabu ya wahanga wa ajali hiyo. Tuendelee kuwaombea majeruhi wapone haraka ili waweze kuendelea na masomo yao.

## TATHMINI YA HALI YA DUNIA

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijatoa tathmini ya hali na mwelekeo wa siasa duniani na jinsi Tanzania ilivyojipanga kushiriki, ningependa kulikumbusha Bunge lako Tukufu juu ya misingi ya Sera yetu ya Mambo ya Nje.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Tanzania pamoja na nchi nyingine za Afrika kujikomboa kutokana na ukoloni na ubaguzi wa rangi, Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania inaendelea kujikita katika misingi ifuatayo;

1. Kulinda uhuru, umoja na heshima ya nchi yetu;
2. Kuendeleza ujirani mwema katika kanda yetu na kukuza umoja na ushirikiano barani Afrika;
3. Kuheshimu kanuni ya kutoingilia masuala ya ndani ya nchi nyingine;
4. Kutofungamana na upande wowote na kuchagua kwa hiari bila masharti marafiki katika Jumuiya ya Kimataifa;
5. Kushirikiana kikamilifu kimataifa na nchi, mashirika na taasisi mbalimbali katika nyanja za diplomasia, siasa, uchumi, utaalam na teknolojia; na

6. Kukuza na kutekeleza diplomasia ya uchumi, hususan uchumi wa viwanda katika Awamu hii ya Tano.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kama ilivyoainishwa hapa, Serikali ya Awamu ya Tano itazingatia mikakati na vipaumbele vifuatavyo:

1. Kuanzisha mahusiano mapya ya kidiplomasia ambayo yataongeza tija kwa maslahi ya nchi hususan maendeleo ya kiuchumi na teknolojia;

2. Kushiriki kikamilifu katika kutafuta suluhu ya migogoro kwa njia ya amani kwa kuzungumza moja kwa moja na wadau husika na kushiriki kikamilifu katika majukwaa ya kimataifa au kitaifa katika kutatua migogoro hiyo.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kifupi Tanzania itaendelea na mkakati wake endelevu wa kutetea uhuru na haki kimataifa huku ikizingatia vipaumbele vyake vya maendeleo na siasa yake ya kutofungamana na upande wowote.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya kisera naomba kutoa tathmini ya hali ya dunia.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2016/2017 dunia imeshuhudia ongezeko dogo katika kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika mataifa ya magharibi yenye uchumi mkubwa hali inayochangia kuendelea kudorora kwa biashara ya kimataifa. Aidha, Dunia imeendelea kushuhudia ongezeko la machafuko ya kisiasa, migogoro ya kivita na vitendo vya kigaidi katika baadhi ya mataifa. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la wakimbizi na wahamaji haramu. Kwa upande mwingine, mabadiliko ya tabianchi yamezidi kuleta athari kubwa katika ikolojia na kutishia uhai wa viumbe na shughuli za kibinadamu. Athari hii ni kubwa zaidi kwenye mataifa yanayoendelea kutokana na uwezo mdogo wa mataifa hayo kukabiliana na changamoto hizo, hivyo kurudisha nyuma juhudi za kujikwamua na umaskini. Matukio hayo ya kidunia yameibua hisia kuwa ipo

haja kwa Jumuiya ya Kimataifa kufanya jitihada mahsusi kukabiliana nayo ili kuimarisha ustawi wa Dunia kwa ujumla. Baada ya kutoa tathmini hiyo ya jumla, sasa naomba uniruhusu nitoe tathmini ya maeneo machache kama ifuatavyo:-

**Hali ya Ulinzi na Usalama Duniani**

**(i) Barani Afrika**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya Ulinzi na Usalama barani Afrika imeendelea kuimarika kutokana na juhudi mbalimbali za usuluhishi na upatanishi zinazoendelea kufanywa na Jumuiya ya Kimataifa. Ndani ya kipindi cha mwaka mmoja dunia imeshuhudia kupungua kwa mashambulizi yanayotekelezwa na makundi ya waasi, upinzani na magaidi katika nchi za Somalia, Afrika ya Kati na Nigeria. Vilevile, hatua za upatanishi katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lesotho na Sudan Kusini zinaelekea kuzaa matunda kutokana na maendeleo mazuri ya majadiliano baina ya pande zinazohasimiana. Kama Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Asasi ya SADC ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama, Tanzania imepewa jukumu la kusimamia utatuzi wa migogoro ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Lesotho. Aidha, kupitia Chama Tawala cha CCM kwa kushirikiana na Chama cha ANC cha Afrika Kusini, Tanzania imechangia katika kutafuta suluhu kwenye mgogoro wa Sudan Kusini.

**(ii) Barani Asia**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika Rasi ya Korea imeendelea kutetereka kutokana na vitendo vya pande mbili hasimu ambazo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea kwa upande mmoja na Jamhuri ya Korea na Marekani kwa upande mwingine. Hali ya kushutumiana kwa pande hizi inatokana na kila upande kuhofia juu ya uwezekano wa uvamizi kutoka upande mwingine. Mpango wa kutengeneza silaha za nyuklia pamoja na majaribio ya makombora ya masafa marefu yanayofanywa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea kwa upande mmoja na

mazoezi ya kijeshi ya pamoja yanayofanywa na Jamhuri ya Korea na Marekani kwa upande mwingine, vimezidisha hofu katika rasi hiyo na ukanda mzima. Endapo vita itatokea baina ya pande hizi mbili italeta madhara makubwa si tu katika ukanda huo bali pia eneo lote la Asia, Pasifiki na dunia kwa ujumla.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na mshirika wa Mkataba wa Kuzuia Kuenea kwa Silaha za Nyuklia na kuhimiza matumizi salama ya teknolojia hiyo. Hivyo, tutaendelea kuunga mkono juhudi za Jumuiya ya Kimataifa katika kusuluhisha mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo ili kuhakikisha hali ya amani na usalama inaendelea kudumishwa duniani.

**(iii) Barani Ulaya**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama katika eneo la Umoja wa Ulaya imekumbwa na changamoto ya vitendo vyenye viashiria vya ugaidi pamoja na wimbi kubwa la wakimbizi na wahamaji haramu. Mashambulio ya kutumia milipuko ya mabomu katika miji ya London, Manchester, Paris, Brussels, Berlin na Stockholm yamezua hofu na taharuki kubwa miongoni mwa wananchi wa nchi hizo. Mataifa hayo ya Umoja wa Ulaya pia, yameendelea kushuhudia ongezeko kubwa la Wakimbizi kutokana na migogoro ya kivita inayoendelea katika eneo la Mashariki ya Kati hususan nchi za Syria na Iraq. Vilevile, idadi ya Wahamaji haramu wengi wao wakitokea mataifa ya Afrika Magharibi na kuingia mataifa ya Umoja wa Ulaya nayo imeendelea kuongezeka. Hali hiyo ya wasiwasi imesababisha kuibuka kwa vyama na vikundi vyenye siasa kali ya ubaguzi katika Bara la Ulaya. Chaguzi za hivi karibuni huko Ufaransa na Uholanzi zimefanikiwa kuleta ushirikiano kwa vyama vya wastani lakini tatizo bado lipo.

**(iv) Amerika ya Kusini na Kaskazini**

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama katika eneo la Amerika ya Kusini na Kaskazini imeendelea

kuwa shwari ikishuhudiwa kupungua kwa mapambano baina ya majeshi ya Serikali na makundi yanayojihusisha na biashara ya dawa za kulevya katika nchi kama vile Mexico. Aidha, jitihada za upatanishi katika nchi ya Colombia zimechangia kwa kiasi kikubwa kusitisha mapambano ya kivita kati ya Serikali ya nchi hiyo na kundi la uasi lijulikanalo kama *FARC*. Vilevile, katika nchi ya Venezuela, Serikali yenye mrengo wa kushoto inakabiliwa na upinzani mkubwa na kusababisha hali nchini humo kuendelea kuwa tete. Katika kunusuru hali hiyo, Papa Francis anajaribu kupatanisha.

**Hali ya Uchumi Duniani**

**i). Barani Afrika**

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Benki ya Dunia, uchumi wa Bara la Afrika kwa mwaka 2016 ulishuka kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na mwaka 2015. Sababu za kushuka kwa ukuaji wa uchumi ni pamoja na kuporomoka kwa bei ya mafuta katika mataifa yanayozalisha na kuuza bidhaa hiyo kama vile Angola na Nigeria. Halikadhalika, kushuka kwa bei ya bidhaa zinazozalishwa barani Afrika kwenye Soko la Dunia hususan malighafi pia kumechangia kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa Bara hili. Hata hivyo, kwa mwaka 2017 uchumi wa Bara hili unatarajiwa kukua japo kwa kiasi kidogo kutokana na kuimarika kwa bei ya mafuta na bei ya bidhaa katika soko la Dunia.

**ii). Barani Asia**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Uchumi wa Bara la Asia ambao katika miaka ya hivi karibuni umekuwa ukikua kwa kasi kubwa kwa wastani ukilinganishwa na ukuaji wa uchumi katika maeneo mengine duniani, ulidorora kwa kiasi hasa kutokana na kupungua kwa ukuaji wa uchumi wa nchi kama vile China uliosababishwa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za nchi hiyo duniani. Hali hii, inafanya nchi kama China, Japan, India na Korea Kusini kurekebisha kwa kiwango fulani cha misaada ya uwekezaji na biashara na nchi zinazoendelea kama za Afrika.

### iii). Barani Ulaya na Amerika

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Ulaya na Amerika uchumi umedorora hata hivyo kuna dalili za kuanza kuimarika japo kwa kasi ndogo huku kukiwa na ongezeko kubwa la ukosefu wa ajira kutokana na kupungua kwa biashara na uwekezaji pamoja na mzigo wa madeni unaoendelea kuathiri uchumi wa baadhi ya nchi katika Umoja wa Ulaya. Kudorora kwa uchumi wa nchi hizi kubwa kumeathiri kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika medani za siasa, kumekuwa na chaguzi katika nchi kadhaa kama vile Marekani, Ufaransa, Uholanzi na Austria ambapo katika chaguzi zote hizo dunia imeshuhudia ongezeko kubwa la wafuasi wa siasa zenye mrengo wa kulia. Inatazamiwa kuwa Serikali mpya zilizoingia madarakani na zinazofuata mrengo huo zitajikita zaidi katika kuhamasisha maendeleo ya ndani na kupunguza kasi ya ukuaji wa biashara na uchumi wa dunia kwa ujumla. Aidha, uamuzi wa kujitoa kwa Taifa la Uingereza katika Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ni kielelezo cha siasa zenye mrengo huo. Serikali mpya ya Marekani haijafafanua siasa yake ya uhusiano na Afrika. Matamshi ya Rais wa Marekani kuhusu Afrika yamekuwa yakitofautiana na tawala zilizopita. Hata hivyo, Serikali ya Marekani imeendeleza msaada kwa Tanzania katika kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

### Mikakati ya kukabiliana na athari za kuyumba kwa uchumi

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya kuyumba kwa hali ya uchumi duniani, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za umma ili kuendelea kupunguza utegemezi kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;

b) Kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia Sera ya Ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi ya mwaka 2009 na Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi ya mwaka 2010. Mkakati huu unasaidia kuongeza wigo wa vyanzo vya fedha za kugharamia miradi ya maendeleo;

c) Kuendelea kuwashawishi wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuwekeza zaidi hapa nchini. Jitihada hizi zinaenda sambamba na uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara nchini na kupunguza gharama za kufanya biashara na uwekezaji;

d) Kuendelea kutafuta fursa za masoko ya bidhaa zetu, kukuza utalii wa ndani na kushawishi watalii kutoka mataifa mengine kutembelea nchi yetu ili kupanua wigo wa mapato na kupunguza athari inayoweza kusababishwa na kuyumba kwa biashara baina ya Tanzania na nchi nyingine; na

e) Kuendelea kuhamasisha ukuaji wa sekta ya viwanda ambayo itazalisha bidhaa na ajira kwa wingi na kuongeza mapato yatokanayo na kodi.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kueleza utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2016/2017, naomba uniruhusu niainishe kwa ufupi majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

i. Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje;

ii. Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Uhusiano baina ya Tanzania na nchi mbalimbali;

iii. Kusimamia Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa;

iv. Kusimamia masuala yanayohusu Kinga na Haki za wanadiplomasia waliopo nchini;

v. Kusimamia na kuratibu masuala ya Itifaki na Uwakilishi;

vi. Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli;

vii. Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa;

viii. Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Watanzania Waishio Ughaibuni;

ix. Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

x. Kuratibu na Kusimamia Miradi ya Maendeleo na Taasisi zilizo chini ya Wizara; na

xi. Kusimamia utawala na Maendeleo ya Utumishi Wizarani na kwenye Balozi zetu.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu hayo kwa mwaka 2016/2017, Wizara yangu ilitengewa kiasi cha **Shilingi 162,109,416,709.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 154,109,416,709.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 8,000,000,000.00** ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 143,768,662,709.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 10,340,754,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara ilitarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 24,001,150,000.00**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2017, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 19,773,333,502.00** sawa na asilimia **83** ya makusanyo yote ya maduhuli. Ni

matarajio ya Wizara kuwa itafikia malengo yake ya kukusanya maduhuli yaliyokadiriwa.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2017 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 95,037,516,058.00** sawa na asilimia **59** ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo **Shilingi 83,039,138,698.00** ni kwa ajili ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; **Shilingi 8,509,062,360.00** ni kwa ajili ya mishahara; na **Shilingi 3,489,315,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa licha ya changamoto mbalimbali za kibajeti. Katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya fedha za umma katika kudhibiti matumizi na mapato ambapo kwa kudhihirisha hilo, Wizara pamoja na Balozi zote isipokuwa Ubalozi mmoja zimepata Hati Safi ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/16. Nachukua fursa hii kuwashukuru Watendaji wa Wizara na kuwahimiza waendelee kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za umma wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi jinsi Wizara ilivyotekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017:-

**KUBUNI NA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA SERA YA NCHI YA MAMBO YA NJE**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara, Taasisi za Serikali na Sekta binafsi iliratibu na kufanikisha ziara za viongozi wanaokuja nchini, mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano, masuala ya ushirikiano kati ya Tanzania na nchi rafiki, mikutano ya Bara la Afrika na nchi nyingine pamoja na makongamano ya biashara yaliyofanyika ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo:

## India

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya kitaifa ya Mhe. Nerendra Modi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya India iliyofanyika nchini mwezi Julai 2016. Pamoja na mambo mengine, Serikali za Tanzania na India zilisaini Mkataba wa Mkopo wa Dola za Marekani milioni 92 kwa ajili ya mradi wa maji wa Zanzibar ambao umeanza kutekelezwa. Aidha, utekelezaji wa makubaliano ya kuondoa hitajio la viza kwa raia wa India na Tanzania wenye Pasi za Kidiplomasia na Pasi za Huduma umeanza tangu mwezi Desemba 2016.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali ya India iliahidi kutoa mkopo wenye riba nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kusambaza maji katika miji 17 ya Kasulu, Ludewa, Manyoni, Mugumu, Chunya, Sikonge, Makonde, Handeni, Makambako, Wanging'ombe, Kayanga, Songea, Zanzibar, Geita, Kilwa Masoko na Njombe. Mnamo mwezi Machi 2017, Serikali hiyo iliwasilisha rasmi uamuzi wake wa kutoa mkopo huo ambao utatolewa na Benki ya Exim ya India kwa riba ya asilimia 1.5 na utalipwa kwa kipindi cha miaka 25. Tayari benki hiyo imewasilisha nyaraka za masharti ya mkopo huo na Serikali inaendelea na taratibu za uchambuzi.

## China

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Waratibu wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika uliofanyika Beijing, China mwezi Julai 2016. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kazi uliopitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi za China na Afrika uliofanyika Johannesburg, Afrika Kusini mwezi Desemba 2015. Miradi inayopewa kipaumbele katika mpango kazi huo inajumuisha ujenzi wa miundombinu ya reli, bandari, nishati, viwanja vya ndege, barabara, maji, mawasiliano, maeneo ya viwanda pamoja na vyuo vya ufundi. Katika kufanikisha azma hiyo, China imeelekeza majimbo yake tajiri kuhamishia viwanda vyake barani Afrika katika nchi zilizochaguliwa. Kwa upande wa

Tanzania, jimbo la *Jiangsu* limeshaanza uwekezaji kwenye viwanda vya nguo vilivyopo Dar es Salaam na Shinyanga na kutoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 1,630. Aidha, kampuni ya *Tianhe Shiye* kutoka jimbo hilo inatarajia kufanya uwekezaji katika ujenzi wa maeneo maalum ya viwanda utakaogharimu Dola za Marekani bilioni mbili.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ushawishi wetu wa kidiplomasia, China iliichagua Tanzania kuwa nchi ya kuzindulia mpango wake wa Diplomasia ya Umma kati yake na Bara la Afrika. Wizara iliratibu uzinduzi wa Kongamano la kwanza chini ya mpango huo, lililofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Agosti 2016. Manufaa yaliyopatikana katika kongamano hilo ni pamoja na kukuza mahusiano na mawasiliano kati ya China na Tanzania kuanzia ngazi za Viongozi wa Serikali, wataalam, wafanyabiashara, wawekezaji, wanamichezo na baina ya watu na watu. Aidha, wasemaji wa Serikali na Taasisi zake walijengewa uwezo wa kutoa habari za nchi kwa wakati bila kuingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine na kusimamia vyombo vya habari kutopotosha umma kwa kutoa taarifa zinazopinga maendeleo ya nchi au kupotosha utendaji wa Serikali.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano wa Tano wa Kamati ya Pamoja ya Ushirikiano katika masuala ya Uchumi, Ufundi na Biashara kati ya Tanzania na China ulifanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Oktoba 2016. Mafanikio ya mkutano huo ni kuimarika kwa mahusiano kati ya nchi hizi mbili katika sekta za biashara, uchumi na ufundi ambapo Serikali ya China ilikubali kuipa Serikali ya Tanzania msaada wa kiasi cha RMB Yuan milioni 300 sawa na Shilingi bilioni 97. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo itakayokubaliwa na pande zote mbili ikiwemo mradi wa vifaa vya ukaguzi na usalama kwa ajili ya viwanja vya ndege.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mhe. Wang Yi, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Tanzania iliyofanyika mwezi Januari 2017. Kufuatia ziara hiyo, Serikali zote mbili zilikubaliana kuimarisha na kukuza uhusiano wa kiuchumi, kibiashara,

kiutamaduni na kijeshi pamoja na kuimarisha ushirikiano uliopo katika masuala ya kimataifa kwa manufaa ya nchi zote mbili. Aidha, Wizara imesaini Mkataba wa msaada wa fedha za China Yuan 2,000,000, sawa na Shilingi milioni 633 kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya wageni mashuhuri Chamwino, Dodoma. Kukamilika kwa ujenzi wa makazi hayo kutatoa fursa kwa Wageni hao mashuhuri kupata mahali pa kufikia panapoendana na hadhi ya nyadhifa zao. Aidha, kutokana na hatua ya Serikali kuhamishia makao yake Dodoma, ujenzi huo utapunguza gharama ya malazi ya viongozi kutoka mataifa mbalimbali wanaokuja nchini kwa ziara rasmi au za kikazi.

**Kuwait**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** uhusiano kati ya nchi yetu na Kuwait unazidi kuwa mzuri. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya ujumbe wa Wataalam wa Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait uliokuja nchini mwezi Desemba 2016, kwa lengo la kufanya tathmini ya miradi inayotekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko huo pamoja na kupokea maombi ya miradi mipya iliyowasilishwa na Serikali ya Tanzania. Miradi mipya iliyojadiliwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Chaya-Nyahua, mkoani Tabora na mradi wa ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ziara hiyo pamoja na majadiliano ya wataalam, Bodi ya Mfuko wa Kuwait kwenye kikao chake cha mwezi Februari 2017, imeidhinisha fedha za Kuwait kiasi cha *Dinar* 15,000,000 sawa na Shilingi bilioni 110 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Barabara ya Chaya-Nyahua yenye urefu wa kilometa 85.4. Mkataba wa mkopo huo ulisainiwa mwezi Machi 2017, Jijini Dar es Salaam ambapo Mhe. Dkt. Philip Isidory Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango alisaini kwa niaba ya Serikali ya Tanzania.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ubalozi wa Kuwait kwa kushirikiana na Wizara yangu umeanzisha kampeni ijulikanayo kama "Maabara kwa Shule za Sekondari na Kisima

kwa shule za Msingi". Miradi hii inalenga kusaidia kuwepo kwa maabara kwa shule za Sekondari na Kisima kwa shule za msingi ambapo Ubalozi huo kupitia Taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali za nchini Kuwait zitakuwa zinafadhili miradi hiyo. Hadi sasa shule 27 zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga zimenufaika na programu hiyo ambayo ni endelevu.

**Umoja wa Falme za Kiarabu**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushawishi wadau mbalimbali wa maendeleo hususan nchi marafiki kuchangia utoaji wa huduma za kijamii. Kufuatia mazungumzo ya Wizara yangu na Waziri wa Nchi anayeshughulikia Ushirikiano wa Kimataifa wa Umoja wa Falme za Kiarabu mwezi Desemba 2016, Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia Programu ijulikanayo kama *Zayed Giving Initiative* imetoa Zahanati mbili zinazotembea ambazo zitatoa huduma bure ya kupima na kutibu magonjwa yasiyoambukiza katika mikoa yote nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Zahanati hizo zilitoa huduma katika Jiji la Dar es Salaam mwezi Februari na Machi 2017 na sasa zipo Zanzibar tangu mwezi Aprili 2017 kabla ya kwenda mikoa mingine.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara iliratibu ziara ya Ujumbe Maalum wa Kiuchumi wa Mrithi wa Mfalme wa Abu Dhabi ambaye ni Kaimu Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu iliyofanyika mwezi Oktoba 2016. Pamoja na mambo mengine, Ujumbe huo ulipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa Serikali.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa ziara hiyo, Tanzania iliwasilisha miradi mikubwa ya sekta ya Miundombinu ya barabara, bandari, reli na viwanja vya ndege inayohitaji ufadhili kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi ambao upo chini ya Mrithi huyo wa Mfalme. Mfuko huo tayari umeidhinisha kuipatia Tanzania mkopo nafuu wa Dola za

Marekani milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Malagarasi hadi Uvinza mkoani Kigoma yenye urefu wa kilometa 51. Aidha, Mheshimiwa Rais amemualika Mrithi wa Mfalme wa Abu Dhabi kufanya ziara rasmi nchini mwaka huu ikiwa ni njia mojawapo ya kuimarisha mahusiano ya nchi hizi mbili.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa kwanza wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu uliofanyika Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu mwezi Desemba 2016. Katika mkutano huo, masuala yaliyojadiliwa na kuwekewa maazimio ni pamoja na kuboresha uwekezaji na biashara, nishati, ulinzi na usalama, usafiri wa anga, kuendeleza miundombinu, elimu (kupatiwa nafasi za mafunzo) pamoja na kilimo na mazingira. Wakati wa Mkutano huo,Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu zilisaini mikataba miwili ya Ushirikiano katika Sekta ya Anga; na Ushirikiano katika Sekta ya Utalii.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Umoja wa Falme za Kiarabu ni moja kati ya nchi muhimu za kimkakati katika biashara. Ili kuboresha zaidi mazingira ya biashara na uwekezaji baina ya nchi hizi mbili, Wizara yangu inaendelea kuratibu majadiliano ya Mkataba wa Kutotoza Kodi mara Mbili na Kukwepa kulipa Kodi (*Avoidance of Double Taxation and Tax Avoidance Agreement*) na Mkataba wa Kuendeleza na Kulinda Uwekezaji baina ya nchi hizi mbili (*Agreement on Promotion and Protection of Investments*).

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha biashara baina ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu, Tanzania imealikwa kushiriki kwenye maonesho makubwa ya kibiashara yatakayofanyika Dubai mwaka 2020 (Dubai Expo 2020). Naomba kutumia fursa hii, kuwashauri wafanyabiashara wa Tanzania kutumia fursa hiyo kwa kushiriki kikamilifu kwenye maonesho hayo.

**Qatar**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** uhusiano kati ya Tanzania na Qatar umeendelea kuwa mzuri. Kupitia uhusiano huo, Wizara imefanikiwa kupata msaada wa magari 10 ya wagonjwa kutoka Ubalozi wa Qatar uliopo nchini. Magari hayo yalikabidhiwa kwa Mhe. Ummy Mwalimu (Mb), Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto mwezi Desemba 2016. Magari hayo yamekuwa ya msaada mkubwa katika kutoa huduma za afya.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Qatar ni miongoni mwa nchi zenye uzoefu mkubwa katika sekta ya gesi na mafuta. Kwa kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na gesi na mafuta, tumeona ni vyema tukafungua ubalozi Doha ili kuimarisha zaidi ushirikiano baina ya nchi hizi hususan diplomasia yetu ya uchumi.

**Iran**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2016, Wizara iliratibu ziara ya Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran anayeshughulikia masuala ya Afrika. Kufuatia ziara hiyo, pamoja na mambo mengine, Serikali ya Iran ilikabidhi msaada wa vifaa kwa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkokotoni, Zanzibar wenye thamani ya Dola za Marekani 500,000. Aidha, Serikali ya Iran ilitoa ahadi ya kujenga vyuo vya ufundi stadi vingine zaidi Unguja na Pemba pamoja na kutoa fursa za Mafunzo kwa Watanzania katika sekta za Nishati ya Mafuta na Gesi.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Iran imeonesha utayari wa kuifutia nchi yetu madeni yaliyolimbikizwa tangu miaka ya 1970 na kuwekeza hapa nchini katika viwanda vikubwa na vidogo.

**Israel**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** uhusiano kati ya Tanzania na Israel umeendelea kuimarika. Kufuatia kuimarika kwa

uhusiano huo, Serikali ya Israel imeahidi kutoa msaada wa kujenga chumba cha wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyopo Dodoma ambacho ujenzi wake unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi wa *Save the Child Heart* unaotekelezwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali ya Israel imejitolea kufadhili mafunzo ya tiba ya moyo kwa madaktari wa Taasisi hiyo ili kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa wa moyo kutibiwa nje ya nchi. Hivi sasa, Taasisi hiyo inatoa huduma kwa Watanzania na vilevile inapokea wagonjwa kutoka nchi za nje zilizo jirani. Kadhalika, Serikali ya Israel imetoa msaada wa mchoro wa kituo cha maafa kinachotegemewa kujengwa eneo la Msalato hapa Dodoma. Wataalam kutoka Israel wanategemewa kuja nchini mnamo mwezi Juni 2017 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utakaowezesha kuchora mchoro huo. Kujengwa kwa kituo hicho kinachotarajiwa kuwa na kiwango cha kimataifa kitaongeza uwezo wa Dodoma kukabiliana na maafa ikizingatiwa kuwa Dodoma inatarajia kupokea wageni wengi kutokana na azma ya Serikali kuhamia Dodoma.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara ya kwanza tangu Taifa letu lipate uhuru, Tanzania inafungua ubalozi Tel Aviv mwaka huu. Kwa kufungua Ubalozi huo, Tanzania itanufaika kwa kushirikiana na Israel katika kupata utaalam wa kilimo cha umwagiliaji, TEHAMA, ulinzi na utalii.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania itaendelea kushiriki katika mijadala ya kimataifa kuhusu suala la haki za Wapalestina.

**Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Joseph Kabange Kabila, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo alifanya ziara ya Kitaifa nchini mwezi Oktoba 2016. Kufuatia ziara hiyo, nchi hizi mbili zilisaini Makubaliano ya Ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi ambayo yatawezesha kushirikiana katika

kufanya utafiti wa mafuta na gesi katika Ziwa Tanganyika. Aidha, makubaliano yamefikiwa juu ya wafanyabiashara wa nchi hiyo kuendelea kutumia Bandari ya Dar es Salaam kusafirisha mizigo yao. Hatua hii itaongeza mapato katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha mizigo.

**Morocco**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 2016, Mfalme Mohamed VI wa Morocco alifanya ziara ya Kitaifa nchini. Morocco ni nchi ya tano barani Afrika yenye uchumi mkubwa. Hivyo, katika kutekeleza diplomasia yetu ya uchumi, hatuna budi kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara na nchi hiyo.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa, wakati wa ziara ya Mfalme wa Morocco, wafanyabiashara wapatao elfu moja waliambatana na kiongozi huyo hatua ambayo ilitoa fursa kwa wafanyabiashara wetu hapa nchini kukutana na wafanyabiashara hao kwa lengo la kuanzisha mahusiano ya kibiashara. Kutokana na ziara hiyo, nchi hizi mbili zilisaini jumla ya Mikataba 23 ya Ushirikiano katika sekta za kilimo, uvuvi, usafiri wa anga, nishati, utalii, viwanda, fedha na bima. Pia, wakati wa ziara hiyo, Mfalme wa Morocco alitoa ahadi ya kujenga uwanja mkubwa wa kisasa wa mpira wa miguu hapa mjini Dodoma. Hadi hivi sasa eneo utakapojengwa uwanja huo limeshapatikana na timu ya wataalam kutoka nchini Morocco imeshafika kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa uwanja huo.

**Zambia**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia iliyofanyika hapa nchini mwezi Novemba 2016. Wakati wa ziara hiyo, nchi hizi zilikubaliana kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na uchumi hususan kuongeza ufanisi wa utendaji wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na

Zambia na bomba la mafuta kutoka Tanzania kwenda Zambia. Kufuatia ziara hiyo, Wakuu wa Nchi hizi mbili waliagiza sheria inayounda Mamlaka ya TAZARA ifanyiwe mapitio na pande zote kwa ajili ya kuboresha utendaji wa mamlaka hiyo. Kufuatia agizo hilo, ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Mheshimiwa George Mcheche Masatu, Mwansheria Mkuu wa Serikali ulifanya ziara nchini Zambia na kufanya mazungumzo na wenzao nchini humo. Katika muendelezo wa mazungumzo hayo, mnamo Mwezi Februari 2017 ujumbe wa Zambia ulifanya ziara nchini kama sehemu ya kuendeleza majadiliano ya namna ya kuboresha Sheria ya Mamlaka ya TAZARA na hivi sasa majadiliano bado yanaendelea kwa kuwahusisha wadau wengine. Aidha, Mheshimiwa Lungu alipata fursa ya kujionea maboresho yaliyofanywa katika Bandari ya Dar es Salaam na hivyo kuahidi kushawishi wafanyabiashara nchini mwake kuendelea kutumia Bandari hiyo.

**Kenya**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Kenya uliofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Desemba 2016. Katika mkutano huo, masuala mbalimbali ya ushirikiano katika nyanja za uchumi, siasa, usalama na biashara yalijadiliwa. Mkutano huo ulizidi kuimarisha mahusiano yaliyopo kati ya Tanzania na Kenya.

**Malawi**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Malawi ulifanyika Lilongwe, Malawi mwezi Februari 2017. Katika mkutano huo masuala mbalimbali ya ushirikiano katika nyanja za uchumi, siasa, usalama, usafirishaji, nishati, uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe na biashara yalijadiliwa na makubaliano kufikiwa. Tanzania na Malawi zilifanikiwa kutia saini mikataba miwili ya Huduma za Anga na Mashauriano ya Kidiplomasia. Mkutano huu ulizidi kuimarisha mahusiano yaliyopo kati ya Tanzania na Malawi. Aidha, napenda

kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba, mazungumzo ya kutafuta suluhu ya mgogoro wa mpaka katika ziwa Nyasa kati ya Tanzania na Malawi chini ya usuluhishi wa Mhe. Joaquim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji na Mwenyekiti wa Jukwaa la Viongozi na Wakuu wa Nchi Wastaafu wa Umoja wa Afrika, akisaidiwa na Mhe. Festus Mogae, Rais Mstaafu wa Botswana na Mhe. Thabo Mbeki, Rais Mstaafu wa Afrika Kusini yanatarajiwa kuanza tena wakati wowote hivi karibuni. Wizara inasubiri kupata tarehe rasmi ya kuanza kwa mazungumzo hayo kutoka Ofisi ya Rais Mstaafu Mhe. Chissano.

**Uganda**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda alifanya ziara ya Kitaifa nchini mwezi Februari 2017. Kufuatia ziara hiyo, nchi hizi mbili zilitia saini hati ya kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kisiasa. Halikadhalika, zilikubaliana kuimarisha mahusiano katika sekta ya biashara na uwekezaji; uchukuzi; mafuta na nishati. Viongozi wa nchi hizi mbili waliagiza kufanyika kwa Mkutano wa Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano ifikapo mwezi Aprili 2017.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda ulifanyika Jijini Arusha mwezi Aprili 2017. Katika mkutano huo, masuala mbalimbali ya ushirikiano katika nyanja za uchumi, siasa, usalama, usafirishaji, nishati na biashara yalijadiliwa na makubaliano kufikiwa. Aidha, Mkataba wa Ubia wa Mradi wa Umeme wa Murongo - Kikagati ulisainiwa na Mawaziri wa Nishati wa pande zote mbili kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa mitambo ya kufua umeme. Vilevile, Tanzania na Uganda zilitia saini Mkataba wa Ushirikiano katika Sekta ya Anga.

**Ethiopia**

**66.** ***Mheshishimiwa Spika,*** ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Hailemariam Dessalegn, Waziri Mkuu wa Shirikisho la Kidemokrasia la Jamhuri ya Ethiopia ilifanyika

nchini mwezi Machi 2017. Ziara hiyo imeimarisha mahusiano mazuri yaliyopo kati ya nchi zetu mbili katika nyanja za kidiplomasia, kiuchumi na kijamii. Tanzania na Ethiopia zilikubaliana kushirikiana katika maeneo 15 ambayo ni kufungua kituo kikubwa cha kuhifadhi mizigo cha bandari kavu; Ushirikiano katika Sekta ya Anga; Ushirikiano wa Kijeshi; Matumizi ya maji ya Mto Nile; Ushirikano katika Sekta ya Nishati; na Ushirikiano katika Sekta ya Mifugo na bidhaa za Ngozi. Maeneo mengine ni Kuondolewa kwa hitajio la Visa Rejea kwa raia wa Ethiopia; Ethiopia kufungua Ubalozi wake Tanzania; Ushirikiano katika sekta ya madini; Kuendeleza lugha ya Kiswahili; Ushirikiano katika Sekta ya Utalii; Ushirikiano katika Sekta ya Michezo; Ushirikiano kwenye Sekta ya Fedha; na Ushirikiano katika Sekta ya Mawasiliano.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu itashirikiana na Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali pamoja na sekta binafsi katika kufuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo.

**Afrika Kusini**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Jacob Gedleyihlekisa Zuma, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini alifanya Ziara ya Kitaifa nchini mwezi Mei 2017. Ziara hiyo imetoa fursa kwa viongozi wetu kujadili masuala mbalimbali yanayohusu nchi hizi mbili pamoja na masuala ya kikanda na kimataifa. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Zuma aliambatana na ujumbe wa wafanyabiashara zaidi ya 80 hatua ambayo ilitoa fursa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kubadilishana nao uzoefu. Kwa kipindi kirefu, Tanzania na Afrika Kusini zimekuwa zikishirikiana katika sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kupitia ziara hiyo, mikataba ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, sayansi, teknolojia, uwekezaji, utamaduni na kilimo ilisainiwa.

**Cuba**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 2016, Mheshimiwa Salvador Antonio Valdés Mesa, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Cuba alifanya ziara nchini. Mheshimiwa Mesa

akiwa nchini alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na viongozi wengine wa Serikali. Kufuatia mazungumzo hayo, Serikali ya Cuba iliahidi kuendelea kuleta madaktari wa binadamu hapa nchini ili kuwajengea uwezo wataalam wetu wa Sekta ya Afya. Kwa sasa kuna madaktari 24 kutoka Cuba ambao wanatoa huduma za kitabibu na mafunzo katika hospitali na vyuo vya afya vilivyopo nchini. Madaktari hao wamesambazwa Zanzibar na katika Mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma, Pwani na Mbeya.

## Czech

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya Mhe. Ivan Jancarek, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Czech hapa nchini mwezi Septemba 2016. Wakati wa ziara hiyo Tanzania na Czech zilikubaliana kuimarisha ushirikiano uliopo na kuongeza maeneo mapya ya ushirikiano, katika sekta za elimu, biashara na uwekezaji. Aidha, Serikali ya Czech iliahidi kufadhili wanafunzi wa Kitanzania kusoma katika vyuo vikuu vya nchi hiyo na kujenga kiwanda cha kuzalisha viuatilifu vya wadudu wanaoshambulia mazao ya mihogo na migomba. Vilevile, Serikali hiyo iliahidi kujenga kiwanda cha kutengeneza viatu na samani ambacho kitaendeshwa kwa ubia kati yake na Jeshi la Magereza.

## Finland

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya Mhe. Kai Mykkänen, Waziri wa Biashara za Kimataifa na Maendeleo wa Jamhuri ya Finland iliyofanyika nchini mwezi Novemba 2016. Pamoja na mambo mengine, Mhe. Mykkänen alishiriki katika uzinduzi wa Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Umeme jijini Dar es salaam. Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland kwa gharama ya Shilingi bilioni 74.6. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 63.56 zimetolewa na Serikali ya Finland na Shilingi bilioni 11.03 zimetolewa na Serikali ya Tanzania.

**Uswisi**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ziara ya Balozi Manuel Sager, Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Uswisi iliyofanyika mwezi Februari, 2017. Balozi huyo, alitembelea hospitali ya Rufaa ya Mtakatifu Francis iliyopo Ifakara na kuzindua Jengo la Wagonjwa wa Nje ambalo limejengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Uswisi. Ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kuongeza ubora wa huduma za afya na kuhudumia wagonjwa wengi zaidi.

**Canada**

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha uliopita, majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Canada kuhusu uhuishwaji wa msaada wa Serikali ya Canada katika Mfuko wa Afya yalikamilika. Serikali ya Canada iliridhia kuendelea kuisaidia Tanzania kupitia Mfuko huo ambapo itachangia kiasi cha Dola za Canada milioni 87.3 sawa na Shilingi bilioni 141.9 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2020. Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, Serikali hiyo ilikuwa imetoa kiasi cha Dola za Canada milioni 19, sawa na Shilingi bilioni 30.9 kuchangia mfuko huo.

**Uturuki**

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Racep Tayyip Erdogan, Rais wa Jamhuri ya Uturuki alifanya ziara ya kitaifa nchini mwezi Januari 2017. Kufuatia ziara hiyo, masuala mbalimbali yalijadiliwa kati ya Tanzania na Uturuki. Miongoni mwa masuala hayo ni mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa uliozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili 2017. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu itahusisha ujenzi wa kipande cha reli kuanzia Dar-es-Salaam hadi Morogoro kwa kutumia fedha za ndani. Mradi huo unatekelezwa kwa ubia kati ya Kampuni ya YAPI Merkez ya Uturuki na MOTA-ENGEL AFRIKA ya Ureno. Kwa kutambua kuwa gharama za kutekeleza mradi huo ni

kubwa, Wizara inaendelea kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka kwenye mashirika ya kimataifa, taasisi za fedha na nchi rafiki kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa awamu nyingine za mradi huo. Awamu hizo zitajumuisha kipande cha kutoka Morogoro kwenda Dodoma na baadae Mwanza na Kigoma na hatimaye kuunganisha na nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kukamilika kwa mradi huu kutakuza biashara, uwekezaji, ajira na kuongeza pato la taifa.

**Japan**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa Ushirikiano kati ya Tanzania na Japan uliofanyika Jijini Dar es salaam mwezi Agosti 2016. Lengo la mkutano huo lilikuwa kupitisha miradi itakayofadhiliwa na Serikali ya Japan katika mwaka 2016 hadi 2017. Jumla ya miradi 18 kutoka sekta za nishati, ujenzi wa barabara na maboresho ya bandari iliwasilishwa kwa Serikali ya Japan ili kuombewa ufadhili. Hadi kufikia mwezi Mei 2017, jumla ya miradi mitano (5) ilikuwa imekubaliwa wakati miradi 13 majadiliano bado yanaendelea. Miradi iliyokubaliwa ni: Mradi wa kuimarisha uwezo katika upangaji na utekelezaji wa programu ya kuendeleza kilimo wilayani; Mradi wa kutoa ushauri elekezi kuhusu uendelezaji wa sekta ya viwanda; Mradi wa kutoa ushauri elekezi kuhusu uendelezaji wa kongani za viwanda; Mradi wa usimamizi wa rasilimali ya maji yaliyo chini ya ardhi Zanzibar; na Mradi wa kutoa ushauri elekezi kuhusu maji kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Zanzibar.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa Sita wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika uliofanyika kwa mara ya kwanza barani Afrika nchini Kenya mwezi Agosti 2016. Nchi 48 za Afrika zilishiriki katika Mkutano huo. Matokeo ya mkutano huo ni pamoja na azma ya Serikali ya Japan:

i. Kutoa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 30 kwa Bara la Afrika ambazo zitatolewa kwa njia ya misaada,

mikopo na uwekezaji katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Kati ya kiasi kilichoahidiwa, Dola za Marekani bilioni 10 zitatolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika. Miundombinu hii ni pamoja na barabara, umeme na mipango miji;

ii. Kutoa mafunzo kwa vijana takribani 30,000 katika fani mbalimbali kama vile uendeshaji na usimamizi wa viwanda, ufundi, shughuli za kiuchumi na elimu ya biashara;

iii. Kutoa walimu wa kujitolea wapatao 20,000 kwa ajili ya kufundisha masomo ya hisabati na sayansi ili kuwajengea uwezo wanafunzi katika masomo hayo;

iv. Kuongeza Dola za Marekani bilioni 2 kwenye Mfuko wa Kukuza Biashara na Uwekezaji; na

v. Kuanzisha *Japan - Africa Public-Private Economic Forum* ili kukuza majadiliano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kati ya Afrika na Japan.

**Jamhuri ya Korea**

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2016 Wizara iliratibu mkutano kati ya Ujumbe kutoka Jamhuri ya Korea ulioongozwa na Mkurugenzi wa Benki ya Exim ya Korea na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkutano huo, Serikali ya Jamhuri ya Korea iliahidi kuipatia Tanzania msaada wa Dola za Marekani milioni 300 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020. Aidha, nchi hiyo iliichagua Tanzania kuwa moja ya nchi za kipaumbele katika ushirikiano wake na nchi za Afrika.Vilevile, kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea, Wizara iliratibu programu maalum ya upatikanaji wa walimu wa kujitolea wa masomo ya Sayansi na Hisabati kutoka nchi hiyo kwa ajili ya kuja kufundisha nchini. Mwezi Agosti 2016 Wizara iliwapokea walimu 10 ambao wamepangwa kufundisha katika shule za Sekondari za Zanaki, Benjamin William Mkapa na Jangwani zilizopo Dar es Salaam.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2016 Wizara iliratibu ziara ya Wabunge kutoka Jamhuri ya Korea waliofika nchini kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Madhumuni ya ziara hii yalikuwa ni kukuza na kuendeleza ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge la Jamhuri ya Korea.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa uhusiano wa kidiplomasia, Serikali ya Jamhuri ya Korea imeifahamisha Wizara yangu kuwa inawasiliana na Bunge la nchi yao ili kuikaribisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kutembelea Bunge la nchi hiyo kwa ajili ya kubadilishana uzoefu.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika mwezi Septemba 2016, Wizara iliratibu ziara ya ujumbe kutoka Taasisi ya Ushirikiano katika masuala ya Kilimo kati ya Jamhuri ya Korea na Afrika iliyoanzishwa mwaka 2010. Taasisi hiyo inajishughulisha na utafiti wa mazao ya kilimo na dawa za kuua wadudu wanaoshambulia mazao. Tafiti za Taasisi hiyo hufanyika kwa kushirikiana na maafisa ugani wa nchi husika kwenye mazao mbalimbali kama vile mpunga, mihogo, nyanya na mengineyo. Nchi wanachama hupata fursa za kupata mafunzo, kubadilishana uzoefu na utafiti kupitia mikutano na makongamano mbalimbali yanayoandaliwa kila mwaka na taasisi hiyo kwa lengo la kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa miradi inayotekelezwa na taasisi hiyo ni *Africa Rice* ambao ni mradi mkubwa wa utafiti katika zao la mpunga wenye lengo la kukuza teknolojia katika uzalishaji wa zao hilo ili kupunguza umaskini na kuhakikisha usalama wa chakula. Kutokana na ziara hiyo Tanzania kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imeanza hatua za awali za kujiunga na Taasisi hiyo ili kupata utaalam zaidi utakaowezesha kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile,Wizara iliratibu ziara ya wajumbe kutoka Jamhuri ya Korea kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam mwezi Septemba 2016. Wajumbe hao walikutana na kufanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam. Mradi huu ni miongoni mwa miradi inayotarajiwa kufadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Korea kwa Dola za Marekani milioni 9.9. Kukamilika kwa mradi huo kutapunguza adha ya maji taka na kuhakikisha usalama wa afya kwa wakazi katika Jiji la Dar es Salaam.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili 2017 nilifanya ziara ya kikazi ya kwanza Barani Asia kwa kutembelea Jamhuri ya Korea nikiwa kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Wakati wa ziara yangu nilifanya mkutano na mwenyeji wangu Mhe. Yun Byung-se, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo na tulizungumzia masuala mbalimbali yenye maslahi kwa nchi zetu, ikiwemo hali ya sasa ya ushirikiano wa kiuchumi na miradi ya maendeleo. Aidha, tulijadili kuhusu hali ya Rasi ya Korea ambapo Tanzania tuliendelea kusisitiza msimamo wetu wa kuunga mkono juhudi za Jumuiya ya Kimataifa katika kuhakikisha amani na usalama katika Rasi hiyo inapatikana. Nilifanya ziara hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa mahusiano ya kidiplomasia kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea mwaka 1992.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha miaka 25, Serikali ya Korea imeisaidia Tanzania kufanikisha utekelezaji wa miradi mikubwa ikiwemo Ujenzi wa Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi unaojumuisha madaraja matatu yenye jumla ya urefu wa mita 275 pamoja na barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 48; na Ujenzi wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Mloganzila yenye uwezo wa kulaza wagonjwa 600. Vilevile, Serikali ya Korea imefadhili ujenzi wa Hospitali ya mama na mtoto iliyopo Chanika, Dar es Salaam yenye uwezo wa kulaza wagonjwa 160 ambayo inatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni. Aidha, Watanzania zaidi ya 1,000

wamenufaika kwa kupata ufadhili wa kusoma katika vyuo mbalimbali nchini Korea.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Zanzibar, Jamhuri ya Korea imefadhili ujenzi wa shule ya Sekondari ya Tumaini iliyopo Kwarara, Unguja. Aidha, Jamhuri ya Korea imekubali kuisaidia Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar vitendea kazi kwa lengo la kuijengea uwezo mamlaka hiyo. Vilevile, Serikali ya nchi hiyo kupitia shirika lake la Maendeleo la KOICA inatarajia kutekeleza mradi wa kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji Pemba na Unguja wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 50.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ziara yangu nilipata pia fursa ya kukutana na Uongozi wa Shirika la Maendeleo la Korea kwa lengo la kuwasilisha ombi la kujengewa uwezo Serikali yetu katika masuala mbalimbali ya kiutendaji. Aidha, nilitumia nafasi hiyo kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo hapa nchini kwa baadhi ya Wanachama wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Jamhuri ya Korea. Vilevile, nilitembelea Chuo cha Taifa cha Diplomasia cha Jamhuri ya Korea kwa ajili ya kujifunza uendeshaji wa Chuo hicho pamoja na kuimarisha ushirikiano wakidiplomasia kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mambo mengine Jamhuri ya Korea imeahidi kuendelea kuisadia nchi yetu katika maeneo mbalimbali itakayohitaji kujengewa uwezo, kuhamasisha wafanyabiashara kuwekeza nchini na kuimarisha ushirikiano wa vyuo vyetu vya diplomasia.

**Ushiriki wa Tanzania katika Makongamano ya Biashara**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya kazi kwa karibu na Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Taasisi ya Sekta Binafsi katika kuratibu maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika majukwaa ya kibiashara na uwekezaji ya kimataifa. Faida za majukwaa hayo ni kufungua fursa za

kiuchumi kwa wafanyabiashara wa kitanzania na kuimarisha mahusiano ya kibiashara na kuvutia uwekezaji nchini hususan katika sekta ya viwanda.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi sasa, majukwaa ambayo Wizara imeyafanikisha kwa kushirikiana na wadau hao ni Jukwaa la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na India lililofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Julai 2016; Jukwaa la Biashara kati ya Tanzania na Rwanda lililofanyika Kigali mwezi Septemba 2016; Kongamano la Pili la Biashara kati ya Tanzania na Misri lililofanyika Cairo mwezi Septemba 2016; Jukwaa la Biashara kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo lililofanyika Lubumbashi mwezi Septemba 2016; Kongamano la Pili la Biashara kati ya Tanzania na Comoro lililofanyika Zanzibar mwezi Oktoba 2016; Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Israel lililofanyika Tel Aviv mwezi Novemba 2016; Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Zambia lililofanyika Lusaka mwezi Machi 2017; Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Mauritius lililofanyika Port Louis mwezi Machi 2017; Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Czech lililofanyika Prague mwezi Mei 2017; na Kongamano la Biashata kati ya Tanzania na Italia lililofanyika Rome mwezi Mei 2017.

## Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeanza zoezi la kupitia Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 ili iweze kuendana na mabadiliko makubwa ya kisiasa na kiuchumi ambayo yametokea ndani na nje ya nchi. Ili kuwa na Sera inayokidhi mahitaji ya sasa na baadae, Wizara imeunda Timu ya Wataalam inayojumuisha Wanazuoni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Chuo cha Diplomasia; Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali; pamoja na Sekta Binafsi. Timu hiyo imeanza kufanya tathmini ya Sera hiyo kwa lengo la kupima mafanikio yaliyopatikana; kubaini mapungufu; changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake; na kuainisha namna ya kuzitatua.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Sera nzuri na inayotekelezeka kwa kiasi kikubwa inategemea ushiriki wa wadau mbalimbali wakati wa uandaaji wake. Kwa kutambua umuhimu huo, Timu hiyo imekusanya maoni kutoka pande zote za Muungano kwa kuzingatia uwakilishi wa makundi mbalimbali katika jamii wakiwemo Viongozi Wakuu Wastaafu; Mawaziri; wanadiplomasia; wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; wafanyabiashara mashuhuri; wajasiriamali wadogo; watoa huduma; Asasi Zisizo za Kiserikali na wananchi kwa ujumla. Maoni hayo yalipatikana kutoka Zanzibar na mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha, Ruvuma, Mbeya, Kigoma na Kagera.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa tathmini hiyo kutawezesha kuandaliwa kwa rasimu ya Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje ambayo itazingatia maoni ya wadau. Naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine kutoa ushirikiano kila wakati Timu ya Wataalam itakapohitaji kuwaona kwa ajili ya kupata maoni yenu katika hatua inayofuata ya kuandaa rasimu ya Sera hiyo.

**KUSIMAMIA MIKATABA NA MAKUBALIANO YA KIMATAIFA**

93. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliratibu na kusimamia kusainiwa kwa Mikataba 12 na Hati za Makubaliano 28 baina ya Tanzania na nchi mbalimbali. Mikataba na Makubaliano hayo ni kiashiria kikubwa katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine, mashirika ya Kikanda na Kimataifa katika kuongeza kasi ya kuvutia uwekezaji, kukuza biashara na kutangaza utalii. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo kwa kuzingatia maslahi ya nchi yetu.

94. ***Mheshimiwa Spika***, orodha ya Mikataba na hati za Makubaliano zilizosainiwa katika kipindi hicho ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 1**.

## KUSIMAMIA MASUALA YANAYOHUSU KINGA NA HAKI ZA WANADIPLOMASIA WALIOPO NCHINI

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na mamlaka mbalimbali nchini ili kuhakikisha kuwa jamii za kibalozi zinazowakilisha nchi zao na mashirika ya kimataifa hapa nchini, zinapata haki zao kama ilivyoainishwa katika Sheria za Kimataifa hususan Mkataba wa Vienna kuhusu Mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961. Aidha, Serikali inaendelea kutoa wito kwa Mabalozi, Wanadiplomasia, Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa na wafanyakazi wote wenye kinga kuendelea kuheshimu sheria, kanuni na taratibu za nchi pamoja na Mkataba wa Vienna.

## KUSIMAMIA NA KURATIBU MASUALA YA ITIFAKI NA UWAKILISHI

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu ziara za viongozi mbalimbali wa kitaifa kwenda nje na masuala ya itifaki na uwakilishi kwa mabalozi na wanadiplomasia wanaowakilisha nchi zao hapa nchini.

**97.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeratibu ziara za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Baadhi ya ziara za viongozi hao zilifanywa katika nchi za China, Djibout, Ethiopia, Indonesia, India, Jordan, Kenya, Mauritius, Swaziland na Umoja wa Falme za Kiarabu. Ziara hizi zimeendelea kuwa na mafanikio makubwa siyo tu katika kukuza na kuimarisha mahusiano baina yetu na nchi hizo pamoja na mashirika ya kimataifa bali zimeendelea kuitangaza Tanzania kama kitovu cha fursa za kiuchumi pamoja na kuisaidia kupata ufadhili katika miradi mikubwa ya maendeleo.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kuandaa na kuratibu sherehe za kuwasilisha hati za utambulisho za Mabalozi wa nchi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini. Miongoni mwao ni

Mabalozi wa nchi za Italy, Saudi Arabia, Morocco, Zambia, Cuba, Iran, Burundi, Jamhuri ya Korea, Somalia, Ireland, Canada, Thailand, Austria, Uingereza, Sudan, Slovakia, Ukraine, Ghana, Hungary, Belarus, Guinea, Botswana, Niger, Mauritius, Cyprus, Bangladesh, Nepal, Gabon, Ecuador, New Zealand na Congo Brazaville.

## KUANZISHA NA KUSIMAMIA HUDUMA ZA KIKONSELI

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kwenye balozi zetu nje na kutoa viza kwa raia wa kigeni wanaotembelea nchini; kurahisisha upatikanaji wa viza kwa maafisa na watendaji wa Serikali, Vyama vya Siasa na Taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo; Kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania waishio nje ya nchi; na kutatua matatizo na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini.

## KURATIBU MASUALA YA USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

### A. Ushirikiano wa Kikanda
### Umoja wa Afrika

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 28 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Januari 2017. Katika Mkutano huo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi na Serikali walijadili na kupitisha maazimio kadhaa. Miongoni mwa maazimio yaliyopitishwa ni:-

i. Umoja wa Afrika kuendelea kufuatilia kwa karibu hali ya amani na usalama katika nchi mbalimbali zenye migogoro barani Afrika zikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Libya, Burundi na Sudan Kusini;

ii. Nchi ambazo hazijaanza kutekeleza Makubaliano ya kutumia asilimia 0.2 ya ushuru wa forodha kwa bidhaa zote zinazoingizwa kutoka nje ya Afrika kwa ajili ya Kuchangia Umoja wa Afrika, zilipewa muda wa kujipanga hadi mwaka 2018;

iii. Nchi wanachama zitafute fedha kwa ajili ya kutekeleza uondoshwaji wa vikwazo visivyo vya kibiashara barani Afrika; na

iv. Ombi la nchi ya Morocco kujiunga na Umoja huo.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** pembezoni mwa Mkutano huo, Mheshimiwa Rais alikabidhi zawadi ya kinyago chenye kuashiria Umoja kilichowekwa katika Jengo la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika lililopewa jina la *Julius Nyerere Peace and Security Building*. Jengo hilo lilizinduliwa mwezi Oktoba 2016 na kupewa jina hilo kutokana na mchango mkubwa wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika masuala ya amani na usalama barani Afrika.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo, Mheshimiwa Rais pia alipata fursa ya kukutana na viongozi mbalimbali na kujadili masuala yanayohusu mahusiano ya nchi yetu na ya Kimataifa. Viongozi aliokutana nao ni pamoja na Mheshimiwa Hailemariam Desalegn, Waziri Mkuu wa Ethiopia; Mheshimiwa Prof. Arthur Peter Mutharika, Rais wa Malawi; Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda; Mhe. Abdel Fattah el-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri; Mheshimiwa Danny Antoine Rollen Faure, Rais wa Jamhuri ya Shelisheli; na Mheshimiwa Antonio Gutteres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Mazungumzo yake na viongozi hao yalilenga katika kuimarisha mahusiano ya kisiasa na kufungua fursa katika nyanja za uwekezaji, biashara na utalii.

**Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano na majukwaa mbalimbali ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliratibu ushiriki wa nchi yetu katika masuala ya siasa, ulinzi, usalama na utangamano wa Jumuiya hiyo kama ifuatavyo:-

**Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama katika Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika mwezi Agosti 2016 Mbabane, Swaziland, Tanzania ilikabidhiwa nafasi ya Uenyekiti wa Asasi ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama ijulikanayo kama *Organ Troika* kwa kipindi cha Agosti 2016 hadi Agosti 2017. Hii ni mara ya tatu kwa nchi yetu kupewa jukumu hilo adhimu kutokana na imani waliyonayo nchi wanachama kwa nchi yetu na uzoefu wetu katika utatuzi wa changamoto za kisiasa, kiulinzi na kiusalama katika Ukanda huo. Kutokana na nafasi ya Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Asasi hiyo, Wizara imeratibu na kuongoza ushiriki wa Viongozi na Wajumbe mbalimbali kwenye utatuzi wa migogoro ndani ya Ukanda huu ikiwemo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Falme ya Lesotho na Madagascar kama ifuatavyo:-

**i. Ujumbe wa Mawaziri wa Asasi ya Utatu ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kutetereka kwa hali ya usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mwezi Septemba 2016 na kutokana na Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama, nilipewa jukumu na Mheshimiwa Rais, kuongoza Ujumbe Maalum wa Mawaziri wa Utatu wa Asasi hiyo nchini DRC. Ziara ya kwanza ya Ujumbe wa Mawaziri ilifanyika mwezi Oktoba 2016, ambapo

ujumbe ulikutana na wadau mbalimbali wa kisiasa nchini humo na kusisitiza umuhimu wa kutafuta makubaliano kwa njia ya majadiliano. Aidha, ujumbe huo uliunga mkono Majadiliano ya Kitaifa yaliyokuwa yakiendelea nchini humo, yaliyosimamiwa na Umoja wa Afrika chini ya uwezeshaji wa Mhe. Edem Kodjo, Waziri Mkuu Mstaafu wa Togo. Majadiliano haya ndiyo yaliyofanikisha kufikiwa Makubaliano ya wadau wa siasa nchini DRC ya mwezi Oktoba 2016.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa makubaliano ya mwezi Oktoba 2016 hayakuhusisha vyama vyote vya upinzani nchini humo, juhudi za kushirikisha wadau wengine ambao hawakutia saini makubaliano hayo ziliendelea chini ya usimamizi wa Kanisa Katoliki ambapo mwezi Desemba 2016 wadau wa siasa nchini humo walitia saini Makubaliano mapya. Makubaliano hayo yanatoa mwongozo wa kuundwa kwa Serikali shirikishi ya Mpito ambayo itaongoza nchini humo hadi Uchaguzi Mkuu utakapofanyika mwezi Desemba 2017. Katika kutekeleza makubaliano hayo, mwezi Aprili 2017, Mheshimiwa Rais Kabila alimteua Bw. Bruno Tshibala, kutoka chama cha Upinzani cha *Union for Democracy and Social Progress (UDPS)* kuwa Waziri Mkuu na mwanzoni mwa mwezi Mei 2017, Baraza Jipya la Mawaziri lilitangazwa.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia maendeleo haya chanya, niliongoza ziara ya pili ya Ujumbe wa Mawaziri wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama nchini DRC mwezi Aprili 2017. Katika ziara hiyo, tumeweza kuona jitihada anazozifanya Mheshimiwa Rais Kabila katika kipindi hiki cha kuelekea maandalizi ya Uchaguzi Mkuu nchini humo. Hivi sasa, zoezi la uandikishaji wapiga kura linaendelea na jumla ya wananchi milioni 23 wamekwishaandikishwa kati ya milioni 40 wanaotarajiwa kuandikishwa.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nafasi yetu ya Uenyekiti wa SADC tuna wajibu wa kuendelea kuunga mkono juhudi hizi ili kuhakikisha amani na usalama vinatawala nchini DRC.

### ii. Kamati ya Uangalizi ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika nchini Lesotho

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwenyekiti wa Asasi ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alimteua Mhe. Jaji Mstaafu Frederick Werema, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uangalizi ya SADC nchini Lesotho. Kamati hiyo inayoundwa na wajumbe kutoka nchi za *Double Troika* ambazo ni Afrika Kusini, Angola, Botswana, Msumbiji, Swaziland na Tanzania, ilipewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya Wakuu wa Nchi na Serikali yanayolenga kurejesha amani ya kudumu nchini humo.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Kamati imefanya ziara tatu nchini Lesotho, ambapo pamoja na mambo mengine, imebaini kwamba maagizo yanayotolewa na Wakuu wa Nchi na Serikali kwa Serikali ya Lesotho hayajatekelezwa ipasavyo huku hali ya kisiasa nchini humo ikiendelea kutetereka. Itakumbukwa kuwa, Mfalme wa Lesotho alifikia uamuzi wa kuvunja Bunge la nchi hiyo baada ya Wabunge kupiga kura ya kutokuwa na imani na Serikali. Kwa muktadha huo, Kamati ya Uangalizi ya SADC nchini Lesotho imetoa pendekezo la kupeleka Waangalizi nchini Lesotho ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mageuzi na hatua za kuiwezesha nchi hiyo kurudi katika hali ya utulivu na amani huku ikijiandaa kufanya Uchaguzi Mkuu mwezi Juni 2017.

### iii. Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Zambia na Jamhuri ya Shelisheli

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kudumisha misingi ya demokrasia na amani katika Kanda, Wizara iliratibu na kuongoza Timu ya SADC ya Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu katika nchi za Zambia na Shelisheli.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Uchaguzi Mkuu nchini Zambia uliofanyika mwezi Agosti 2016, ulihusisha vyama tisa

vilivyotoa wagombea wa Urais. Uchaguzi huo uliendeshwa kulingana na Katiba ya Zambia ya mwaka 2016 ambapo Mheshimiwa Edgar Lungu alitangazwa mshindi na kuapishwa kuwa Rais wa nchi hiyo tarehe 16 Agosti 2016. Timu ya waangalizi ilielezea kuridhika kwake na uchaguzi huo na kuwa ulikidhi vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika vya kuwa na uchaguzi huru na wa haki.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** nilipewa heshima ya kuongoza Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi kutoka Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika Uchaguzi Mkuu wa Wabunge wa Jamhuri ya Shelisheli uliofanyika mwezi Septemba 2016. Katika uchaguzi huo wagombea kutoka vyama vitatu vya siasa na wagombea huru watatu walishiriki kugombea majimbo 25 ya uchaguzi katika nchi hiyo. Chama Tawala cha *Parti Lepep* kilipata majimbo 10 na muungano wa vyama vya upinzani wa *LDS* ulipata majimbo 15. Uchaguzi huo uliokuwa huru na wa haki, ulifanyika kwa amani na utulivu na ulikidhi vigezo vilivyowekwa na Jumuiya. Kutokana na chama tawala kupata ushindi mdogo katika uchaguzi huo, mwezi Oktoba 2016 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Shelisheli Mheshimiwa James Alix Mitchel, alitangaza kujiuzulu wadhifa wake na nafasi yake kuchukuliwa na aliyekuwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Danny Faure. Mheshimiwa Faure aliapishwa tarehe 16 Oktoba 2016 kuwa Rais wa nchi hiyo.

### iv. Mkutano wa Kamati Ndogo ya Mawaziri wa Siasa na Diplomasia

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Kamati Ndogo ya Mawaziri wa Siasa na Diplomasia uliofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Februari 2017. Katika Mkutano huo, Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Mambo ya Nje, Diplomasia na Siasa walipokea na kujadili taarifa za masuala ya siasa, ulinzi na usalama katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Falme ya Lesotho. Vilevile, Mawaziri walipokea na kujadili taarifa za tathmini za maombi ya Burundi na Comoro kujiunga katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambapo Mawaziri walikubaliana kwamba kwa kuwa Comoro imekidhi vigezo

karibu vyote vilivyowekwa na SADC, inaweza kujiunga isipokuwa kwa Burundi inayohitaji kufanyiwa uchambuzi na mjadala wa kina.

### v. Mafunzo ya Raia kuhusu Usuluhishi wa Migogoro

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa maazimio ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ni kuanzisha program za kuwajengea uwezo watumishi katika masuala ya usuluhishi na upatanishi wa migogoro. Kutokana na azimio hilo, Wizara iliratibu na kushiriki katika mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi katika masuala ya utatuzi na usuluhishi wa migogoro yaliyoandaliwa na SADC. Jumla ya watumishi 30 kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali walishiriki mafunzo hayo. Hatua hiyo imewezesha nchi yetu kuongeza idadi ya wataalam wa masuala ya usuluhishi na upatanishi wa migogoro kwa njia ya amani.

### vi. Kuendeleza Viwanda katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na uchumi wa viwanda, Wizara imeratibu ushiriki wa Tanzania katika uandaaji wa Mkakati wa Jumuiya wa Kuendeleza Viwanda 2016 – 2063 na Mpango Kazi wa utekelezaji wake. Mkakati huo unalenga kuziwezesha nchi wanachama ikiwemo Tanzania, kuweka nguvu ya pamoja katika kukuza viwanda hivyo na kuziwezesha nchi kushiriki zaidi katika mnyororo wa thamani kikanda na kimataifa. Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mkakati huo uliidhinishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali katika Mkutano wa Dharura uliofanyika Mbabane Swaziland mwezi Machi 2017 ambapo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### vii. Ajira kwa Watanzania katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Watanzania wanapata nafasi za ajira katika Sekretariati ya SADC, Wizara ilifanikiwa kuzishawishi nchi Wanachama kuongeza muda wa mkataba wa Dkt. Stergomena Laurent Tax, mtanzania ambaye kwa sasa ndiye Katibu Mtendaji wa Jumuiya. Wakuu wa Nchi na Serikali waliridhia nyongeza ya mkataba wake kwa kipindi cha pili na cha mwisho katika mkutano wao uliofanyika Mbabane, Swaziland mwezi Machi 2017. Aidha, katika mkutano huo, Mhe. Jaji Mstaafu Regina Rweyemamu aliteuliwa kuwa kati ya Majaji saba wanaounda timu ya Majaji wa kuhudumia Mahakama ya Masuala ya Kiutumishi ya Jumuiya kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Agosti 2017. Kufuatia ajira ya Mheshimiwa Jaji Mstaafu Rweyemamu, idadi ya Watanzania walioajiriwa katika Sekretariati ya Jumuiya imefikia 18.

### Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi zinazopakana na bahari ya Hindi uliofanyika mjini Jakarta, Indonesia mwezi Machi 2017. Mkutano huo umefanyika wakati Jumuiya ikiadhimisha miaka 20 ya kuanzishwa kwake. Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi na Serikali walisaini Makubaliano ya Jakarta ambayo yamebainisha mikakati, mipango na maazimio yanayolenga kuongeza kasi ya maendeleo kwa nchi wanachama kwa kuanisha mafanikio na changamoto za Jumuiya. Mkutano huo pia uliidhinisha Mpango Kazi wa utekelezaji wa Makubaliano hayo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2017 hadi 2021.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango Kazi huo umejumuisha maeneo ya vipaumbele vya Jumuiya ambavyo

ni Biashara na Uwekezaji, Usafiri wa Bahari, Uvuvi, Menejimenti ya Udhibiti wa Majanga, Taaluma, Sayansi na Teknolojia, Utalii na Utamaduni, Uchumi Bahari na masuala ya Jinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Kila Nchi mwanachama inatakiwa kuchagua eneo moja au zaidi ambalo itatoa uongozi katika utekelezaji wake. Wakati wa Mkutano huo, Tanzania ilionesha nia ya kutoa uongozi katika eneo la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Hata hivyo, taarifa rasmi za uchaguzi wa maeneo hayo zitawasilishwa na kujadiliwa katika Mkutano wa Maafisa Waandamizi utakaofanyika nchini Indonesia, mwezi Julai 2017.

**Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu ina dhamana ya kuratibu na kusimamia shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Ibara ya 8 Ibara ndogo ya 3 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999. Kwa mantiki hiyo, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania kwa kutekeleza kikamilifu majukumu mbalimbali kwa lengo la kusimamia maslahi mapana ya kitaifa katika Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

**a. Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha**

**i. Biashara na Uwekezaji katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika kuandaa Taarifa ya Mwenendo wa Biashara na Uwekezaji katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2015 ikiwa na lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Ripoti hiyo inabainisha kuwa, utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umekuwa na mafanikio katika kukuza biashara ya bidhaa na uwekezaji miongoni mwa Nchi wanachama.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama imeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 4,483.6 mwaka 2011 hadi kufika Dola za

Marekani milioni 5,069.7 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 13. Kwa upande wa Tanzania biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki imeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 787.1 mwaka 2011 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,203.6 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 53.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** mauzo ya Tanzania kwenye Soko la Afrika Mashariki yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka Dola za Marekani milioni 409.0 mwaka 2011 hadi Dola za Marekani milioni 924.9 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 126 wakati manunuzi yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 378.1 mwaka 2011 hadi Dola za Marekani milioni 278.1 mwaka 2015 sawa na punguzo la asilimia 26.5. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na visimbuzi, kamba za katani, mbogamboga, matunda, tangawizi, chai, karatasi, vyakula vya mifugo na sabuni.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Umoja wa Forodha ni pamoja na kukuza biashara ya bidhaa na kuchochea uwekezaji miongoni mwa Nchi Wanachama, na ndio maana tuna kampuni kutoka nchi wanachama zilizowekeza Tanzania na kampuni za Tanzania zilizowekeza kwenye Nchi nyingine Wanachama. Baadhi ya kampuni kutoka Tanzania ni Bakhresa, Mount Meru, Benki ya CRDB na Bank M. Aidha, kampuni zilizowekeza hapa kwetu ni pamoja na Benki ya KCB na NAKUMAT. Uwekezaji unaovuka mipaka unachangia kukuza biashara na ajira miongoni mwa nchi wanachama. Katika mwaka 2016, Tanzania iliandikisha Jumla ya miradi 6 kutoka nchi za Kenya, Uganda na Rwanda yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2.5.

### ii. Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha kwa lengo la kukuza biashara baina ya Nchi Wanachama na kupunguza gharama za kufanya biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika barabara Kuu ya Kati, Tanzania imeendelea kutumia vituo vitatu katika kupima uzito wa malori

yanayotumia barabara hiyo vilivyopo Vigwaza, Nyuki na Nyakahura.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, jumla ya Vikwazo Visivyokuwa vya Kiforodha 116 katika Jumuiya viliondolewa. Kati ya hivyo, vikwazo vinavyoihusu Tanzania vilivyoondolewa ni:- Kodi ya asilimia 1.5 kwa ajili ya maendeleo ya reli kwa bidhaa zinazoingia nchini kutoka Nchi Wanachama; kushindwa kutoa taarifa ya mabadiliko ya taratibu za uingizaji na uuzaji wa bidhaa; kodi kwa bidhaa za maonesho ya 40 ya Sabasaba kutoka kwenye Nchi Wanachama; na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kufunga ofisi mapema (saa 9 Alasiri) na hivyo kukwamisha ukaguzi wa mizigo katika bandari kavu.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyofikiwa kwa upande wa Tanzania pekee ni pamoja na kuimarisha uwezo wa Kamati ya Kitaifa ya Uondoaji Vikwazo visivyo vya forodha na kuiwezesha kufanya vikao kila mwezi badala ya kila robo ya mwaka kama ilivyokuwa awali hivyo kupunguza malalamiko ya vikwazo hivyo kukaa muda mrefu bila kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

### iii. Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha na Sheria ya Uasilia wa Bidhaa

**127.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeratibu na kusimamia mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha na Sheria ya Uasilia wa Bidhaa. Katika kukamilisha azma hiyo, Nchi Wanachama zimekamilisha Hadidu za Rejea, kupendekeza vigezo vitakavyotumika katika kuweka kiwango cha ushuru wa forodha katika bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya na kuandaa Mpango Kazi wa kukamilisha kazi hiyo.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wajumbe wa Tanzania wanaoshiriki katika zoezi hilo wanatoka Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania. Zoezi hili ni muhimu na linagusa

mustakabali wa nchi yetu katika kuendeleza viwanda, uwekezaji na kukuza biashara. Hivyo, natoa wito kwa sekta binafsi kushirikiana kikamilifu na kikosi kazi hiki, ili kutoa taarifa zitakazowezesha mapitio yatakayofanyika kuwa na tija kwa ustawi wa taifa letu.

### b. Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki kwenye utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Mafanikio ya utekelezaji wa Itifaki hiyo kwa upande wa Tanzania ni pamoja na kuandaa na kuanza kutumia Kanuni Mpya za Uhamiaji za mwaka 2016; utaratibu wa ushirikiano kati ya taasisi zinazotoa huduma mipakani na Sheria ya Ajira za Kigeni ya mwaka 2015 ambayo imezingatia matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja.

### c. Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Nchi Wanachama zimekamilisha Sera ya Mikataba ya Kodi ambayo itatumika kuandaa Modeli ya Mikataba ya Kodi itakayotumiwa na kila nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika majadiliano yanayohusu kodi na nchi nyingine. Hii itawezesha kuleta uwiano wa viwango vya kodi vinavyotozwa na nchi wanachama kwa wawekezaji kutoka nje ya Jumuiya.

### d. Ushirikiano Baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kanda Nyingine

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano 17 wa Dharura wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Jijini Dar es Salaam mwezi Septemba 2016 ulipokea na kujadili suala la Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya *(EAC-EU Economic Partnership Agreement –EPA)*. Baada ya majadiliano ya kina, Viongozi Wakuu wa Nchi walikubaliana kuendelea na mashauriano ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto za EPA zilizokuwa zimebainishwa. Katika kutekeleza makubaliano ya Viongozi Wakuu wa Nchi za

Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu EPA, Wizara ilishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kufanya uchambuzi wa ndani wa kina na kuandaa mapendekezo ya msimamo wa nchi. Uchambuzi uliofanyika ulionesha kuwa Mkataba huo siyo rafiki kwa ustawi wa Taifa letu hasa katika utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Viwanda.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia maombi ya Bunge lako Tukufu, Serikali iliwasilisha Mkataba huo Bungeni. Baada ya majadiliano, Bunge lilitoa Azimio la kuishauri Serikali isisaini Mkataba huo.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa 18 wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Dar es salaam mwezi Mei 2017, suala la Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki lilijadiliwa. Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekubaliana kuwa Rais wa Jamhuri ya Uganda ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya kuongoza ujumbe kwenda Umoja wa Ulaya kwa lengo la kutafuta muafaka wa namna ya kuondoa changamoto zilizopo katika Mkataba huo. Aidha, ujumbe huo unalenga kushawishi Umoja wa Ulaya kutoiadhibu Kenya wakati majadiliano ya kutafuta muafaka yakiendelea.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Viongozi hao pia walikubaliana kuwa, endapo Juhudi za kupata muafaka kuhusu changamoto za Mkataba wa EPA kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya hazitazaa matunda ndani ya kipindi cha miezi sita, utaangaliwa uwezekano wa nchi zitakazokuwa tayari kuendelea na Mkataba wa EPA kwa mujibu wa ibara 7(e) ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohusu kanuni ya ‘‘*Variable Geometry*’’.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tano wa Baraza la Mawaziri wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC uliofanyika Nairobi, Kenya mwezi Oktoba 2016. Mkutano huo ulipokea na kujadili taarifa ya maeneo yaliyosalia katika majadiliano ya awamu

ya kwanza ambayo ni Uondoaji wa Ushuru wa Forodha; Uasilia wa Bidhaa; na Usuluhishi wa Migogoro ya Biashara. Vilevile, Mkutano ulipokea na kuridhia baadhi ya viambatisho vya Mkataba huo vinavyohusu Vikwazo Visivyo vya Kiforodha; Ushirikiano katika Masuala ya Forodha; Uwezeshaji Biashara; Biashara ya Bidhaa zinazopita kwenda nchi nyingine; Vikwazo vya Kiufundi vya Kibiashara na Afya ya Wanyama na Mimea. Baraza la Mawaziri pia lilipokea taarifa ya utiaji saini Mkataba huo ambapo jumla ya nchi 18 tayari zilikuwa zimesaini. Kufuatia hatua hiyo, Baraza la Mawaziri liliagiza nchi ambazo hazijasaini kufanya hivyo na zile ambazo zimesaini ziendelee na taratibu za kuridhia. Tanzania imeshasaini Mkataba huo na taratibu za kuridhiwa zinaendelea.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki Kongamano la 14 la AGOA lililofanyika Washington DC, Marekani mwezi Septemba 2016. Kaulimbiu ya Kongamano hilo ilikuwa ni "Kuimarisha Ushirikiano wa Kibiashara na Uwekezaji kati ya Marekani na Afrika". Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na: Biashara na masuala ya wafanyakazi; Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa AGOA; Namna ya kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu; Kuvutia uwekezaji ili kuhakikisha Mpango wa AGOA unatumika ipasavyo; Uwiano wa usalama na biashara kimataifa; Mkataba wa urahisishaji biashara; Uwezeshwaji wa upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; na Mikakati ya kunufaika na mpango wa AGOA.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Afrika. Hadi sasa nchi za Umoja wa Afrika zimepitisha kanuni za kuendesha majadiliano, hadidu za rejea za vikundi kazi vitakavyoshiriki katika majadiliano ya maeneo yenye utaalam mahsusi, pamoja na kupitisha mpango kazi wa namna ya kukamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika.

**e. Sekta za Uzalishaji**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Afya

ya Wanyama na Mimea wa Jumuiya yaliyofanyika Nairobi, Kenya mwezi Novemba 2016. Muswada huo unalenga kuwa na sheria itakayoziwezesha nchi wanachama kutekeleza sera, taratibu na mikakati iliyobainishwa kwenye Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea ya Jumuiya, kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa chakula cha Binadamu na Wanyama.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya Rasimu ya Mkataba wa kukuza na kuinua Viwanda Vidogo na vya Kati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkataba huo utatoa fursa kwa nchi wanachama kutatua changamoto na kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya viwanda vidogo na vya kati katika Jumuiya. Miongoni mwa masuala ambayo yamepewa kipaumbele katika kuinua Sekta hii muhimu ni:- mazingira rafiki ya ulipaji kodi; uwezeshaji wa wafanyabiashara wadogo kwa kurasimisha biashara zisizo rasmi; utoaji wa mikopo kwa riba nafuu; na kuanzisha vituo vya kuwajengea uwezo wajasiriamali. Aidha, katika hatua ya utekelezaji wa Sera na Mkakati wa kuendeleza Viwanda wa Afrika Mashariki, nchi wanachama zinaendelea na majadiliano ya Rasimu ya muswada wa Uendelezaji wa Viwanda katika Jumuiya.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia iliratibu na kushiriki katika Maonesho ya 17 ya Juakali/Nguvukazi kwa mwaka 2016 yaliyofanyika Kampala, Uganda mwezi Desemba 2016. Maonesho haya yalijumuisha wajasiriamali zaidi ya mia saba kutoka nchi wanachama na yalikuwa na kaulimbiu isemayo "**Nunua bidhaa za Afrika Mashariki, Jenga Uchumi wa Afrika Mashariki"**.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jumla ya Wajasiriamali 138 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walishiriki maonesho hayo ambapo Tanzania ilifanikiwa kutoa washindi watatu ambao ni Bi. Margareth Kiondo katika bidhaa za vinyago; Tegoe's *Honey Group* katika bidhaa za asali; na katika bidhaa za nguo mshindi alikuwa Bi. Fridah Tarimo. Washindi hao wote walitunukiwa vyeti vya ubora wa bidhaa katika maonesho hayo.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wajasiriamali wengi walitumia fursa hiyo kutangaza, na kuuza bidhaa zao, kubadilishana ujuzi, teknolojia na uzoefu katika fani mbalimbali za uzalishaji wa bidhaa pamoja na utafutaji wa masoko na pia kujenga mahusiano ya kibiashara baina yao.

### f. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Miundombinu ya Uchumi na Huduma za Jamii

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika utekelezaji wa miradi na programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Uendelezaji wa Miundombinu ya Uchumi na Huduma za Jamii kama ifuatavyo:

#### i. Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika ujenzi na uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani. Katika Kituo cha Rusumo kilichopo mpakani mwa Tanzania na Rwanda limefunguliwa Tawi la Benki ya NMB ndani ya jengo la Kituo hicho lililoanza kutoa huduma mwezi Julai 2016. Kufunguliwa kwa Tawi hilo kumeongeza ufanisi katika kutoa huduma kituoni hapo. Aidha, mnamo mwezi Februari 2017 ulifanyika utafiti wa kuangalia matokeo ya kuanzisha Mfumo wa Pamoja wa Utoaji Huduma kwenye Kituo hicho. Matokeo ya awali ya Utafiti huo uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan yanaonesha kuwa muda wa kukamilisha taratibu kwa malori ya mizigo yanayovuka mpaka kupitia Kituo hicho umepungua kutoka wastani wa siku moja hadi saa moja na nusu. Kwa sasa malori zaidi ya 200 yanavuka mpaka kupitia Kituo hicho kwa siku ikilinganishwa na wastani wa malori 90 kabla ya utaratibu wa Mfumo huo kuanza kutumika mwezi Machi 2016.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Benki ya Maendeleo ya Afrika imetoa msaada wa Dola za Marekani 525,120 kwa lengo la kuwezesha uendeshaji wa Kituo cha Namanga kilichopo mpakani mwa Tanzania na Kenya. Fedha hizo ni kwa ajili ya ununuzi wa samani na vifaa vya TEHAMA; kuwajengea uwezo

wa utekelezaji wa Mfumo huo Watalaam wa Taasisi zinazotoa huduma mpakani; na kutoa elimu kwa wananchi na watumiaji wa Kituo hicho. Mwezi Novemba 2016, Wizara iliratibu makabidhiano ya vifaa vya TEHAMA vilivyonunuliwa kupitia msaada huo. Vifaa hivyo ni pamoja na komputa 80, swichi 8, printa 32 na *scanner* 20.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kuhusu Kituo cha Tunduma kilichopo mpakani mwa Tanzania na Zambia, Mkataba wa Ujenzi kati ya Mkandarasi Kampuni ya *Nadhra Engineering Construction Company Limited* na taasisi ya *Trade Mark East Africa* (TMEA), ambayo ni mfadhili wa ujenzi wa Kituo hicho ulisainiwa mwezi Oktoba 2016. Ujenzi wa Kituo hicho ulianza mwezi Novemba 2016 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2018.

### ii. Uendelezaji wa Mtandao wa Barabara

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kamati ya Makatibu Wakuu ya Usimamizi wa Miradi ya Barabara za Afrika Mashariki uliofanyika Mombasa, Kenya mwezi Desemba 2016. Pamoja na mambo mengine, nchi wanachama zilionesha kuridhishwa na hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi wa barabara ya Arusha – Holili/ Taveta – Voi, ikiwemo sehemu ya Sakina - Tengeru yenye urefu wa kilometa 14.1 ambayo ujenzi wake utakuwa wa kipindi cha miaka miwili na nusu kuanzia mwezi Februari 2016.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa Kamati ya Pamoja ya Wataalam wa Kikanda inayosimamia utekelezaji wa Mradi wa kuwezesha Sekta ya Uchukuzi na Biashara kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Oktoba 2016. Katika Mkutano huo, Tanzania iliwasilisha miradi ya kipaumbele katika sekta za Bandari, Nishati, Reli, Barabara na Anga ili ijumuishwe katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo. Aidha, nchi wanachama zinaendelea na majadiliano ya Rasimu ya Mfumo wa Sheria wa Matumizi ya Mtaala wa Mafunzo ya Madereva wa Magari ya Biashara katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kushiriki majadiliano ya Mpango wa Miaka 5 wa Kuwezesha Sekta ya Uchukuzi na Biashara kwa Njia ya Barabara kwenye eneo huru la biashara la utatu wa COMESA – EAC – SADC uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Novemba 2016. Mpango huo unalenga kuwianisha sera, sheria, kanuni na mifumo ya kitaasisi kwenye sekta ya uchukuzi kwa njia ya barabara kwenye nchi zote 19 Wanachama wa Utatu huo.

**iii. Sekta ya Mawasiliano**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kushiriki katika kuandaa Rasimu ya Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Posta kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkakati huo una lengo la kuboresha Huduma za Mawasiliano zinazotolewa kwa njia ya Posta kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia kwenye sekta hiyo. Majadiliano kuhusiana na mkakati huo yanaendelea kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.

**151.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara iliratibu na kushiriki katika Ziara ya Kamati ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji ya Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Februari 2017. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kufuatilia hatua zilizofikiwa kuhusiana na uwianishaji wa gharama za maunganisho ya simu za mkononi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati hiyo ilikutana na Wataalam wa Sekta ya Mawasiliano hapa nchini. Aidha, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mpango huo, wadau wa mawasiliano walipendekeza Nchi Wanachama kuweka Mitambo ya kufuatilia na kupambana na uhalifu wa kimtandao na Jumuiya ya Afrika Mashariki kufanya utafiti wa kubainisha faida na changamoto za mfumo huo.

**iv. Sekta ya Elimu**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 18 uliofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Mei 2017 walitoa Tamko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa Eneo Moja la Elimu ya

Juu (*Declaration on the Establishment of the East African Community Common Higher Education Area*).Tamko hilo lina lengo la kuhakikisha mafanikio ambayo hadi sasa yamepatikana katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye elimu ya juu yanawianishwa ili kuwa na mfumo mmoja wenye kuwezesha utolewaji wa elimu na mafunzo yenye viwango bora vitakavyotambulika baina ya Nchi Wanachama. Wakuu wa Nchi wameliagiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kufanya mageuzi yanayohitajika katika Elimu na Mafunzo ili kufikia lengo hili.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** kila mwaka Wanafunzi wa Sekondari wa Jumuiya ya Afrika Mashariki huandaliwa shindano la kuandika Insha na washindi watano hutunukiwa vyeti pamoja na zawadi na Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mada ambayo wanafunzi huandikia Insha hulenga kuwajengea uelewa wa Mtangamano wa Afrika Mashariki. Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 18 uliofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Mei 2017 walitoa vyeti pamoja na zawadi kwa washindi wa Shindano la Insha la Jumuiya la mwaka 2016. Kwa upande wa Tanzania mshindi alikuwa ni Alex Mbogo kutoka Shule ya Sekondari Kibaha, Mkoa wa Pwani.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 13 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Elimu, Sayansi na Teknolojia, Utamaduni na Michezo uliofanyika Nairobi, Kenya mwezi Oktoba 2016. Katika Mkutano huo Nchi Wanachama ziliidhinisha Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la Mpango Mkakati huo ni kuratibu na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuzijengea uwezo taasisi zinazojihusisha na utafiti wa Kiswahili.

### v. Sekta ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Pili la Watoto la Jumuiya ya Afrika

Mashariki lililofanyika Nairobi, Kenya mwezi Agosti 2016**.** Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kuwakutanisha pamoja Watoto wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuwapa fursa ya kushiriki katika shughuli zinazowahusu na kuwajengea uwezo wa kutambua haki zao. Katika Kongamano hilo, Sera ya Mtoto ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inalenga kulinda haki za watoto ilizinduliwa rasmi. Katika Kongamano hilo, watoto wawili na mwangalizi wao mmoja kutoka Tanzania walishiriki.

### vi. Sekta ya Kazi na Ajira

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu Mkutano wa kuandaa Mpango wa Pamoja wa Kubadilishana Wafanyakazi Vijana miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Nairobi, Kenya mwezi Novemba 2016. Mpango huo unalenga kutekeleza Ibara ya 10 ibara ndogo ya 8 ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mpango huo, nchi Wanachama zinajadili mpango wa kubadilishana vijana waajiriwa katika nchi za Jumuiya hiyo. Kukamilika kwa Mpango huo kutatoa fursa kwa vijana wetu kujijengea uwezo na kupata uzoefu katika fani mbalimbali.

### vii. Sekta ya Afya

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea na uratibu wa ukamilishwaji wa Sera ya Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera hii iliidhinishwa na Mkutano wa 35 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya uliofanyika Arusha mwezi Aprili 2017. Msingi Mkuu wa Sera hii ni kutoa mwongozo katika kukabiliana na changamoto katika sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa hasa katika upatikanaji wa dawa zenye ubora, kuhimiza utoaji huduma za afya kwa kuzingatia misingi ya maadili, sheria na kujali utu. Aidha, Sera hii inatoa mwongozo wa kuandaa mikakati ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ya binadamu na wanyama. Vilevile, itachochea ukuaji wa ubunifu na tafiti za kisayansi na pia kuzalisha wataalam wenye uwezo na weledi katika masuala ya Afya.

### viii. Miradi na Programu za Mazingira

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 17 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Bonde la Ziwa Victoria pamoja na Maadhimisho ya Miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria yaliyofanyika Kisumu, Kenya mwezi Novemba 2016. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama zilizindua Mpango Mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Dhana ya Idadi ya Watu, Afya, na Mazingira wa mwaka 2016 – 2021. Mpango Mkakati huo utaongoza Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo na Sekta binafsi katika kuhuisha na kuratibu utekelezaji wa dhana hiyo wakati wa utekelezaji wa miradi yao.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Kongamano la Utafiti wa Kisayansi na Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria lililofanyika Jijini Mwanza mwezi Februari 2017. Kongamano hilo lilifunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na maazimio mengine, Kongamano hilo liliazimia Jumuiya ya Afrika Mashariki iendelee na maandalizi ya awamu ya tatu ya Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria kwa kuanza kutafuta rasilimali fedha.

## g. Utekelezaji wa Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mkutano wa 18 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Mei 2017, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikabidhi Uenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda. Hii ni kufuatia Tanzania kushika nafasi hiyo kwa vipindi viwili mfululizo. Katika kipindi cha Uenyekiti wa Tanzania, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipiga hatua kubwa katika utekelezaji wa programu na miradi yake mbalimbali.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanza kwa utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha ikiwa ni utekelezaji wa Itifaki ya Jumuiya ya Umoja wa Forodha. Utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha umewezesha kupunguza muda wa kusafirisha mizigo na abiria baada ya vituo 11 kati ya 15 vya kutoa huduma kwa pamoja kujengwa. Kwa upande wa utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya barabara na reli zinazounganisha mataifa ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ujenzi wa barabara ya Arusha – Holili – Taveta - Voi kati ya Tanzania na Kenya unaendelea ambapo kipande cha kutoka Sakina hadi Tengeru ujenzi wake unaendelea. Ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam – Tabora – Mwanza na Tabora – Kigoma – Keza – Msongati itakayounganisha Tanzania na nchi za Burundi na Rwanda umeanza. Aidha, katika kipindi hicho Jamhuri ya Sudan Kusini ilikamilisha taratibu za kisheria zilizoiwezesha kuwa Mwanachama kamili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya kuwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya Hati za Kuridhia Mkataba wa Kujiunga na Jumuiya hiyo mwezi Septemba 2016.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha Shirikisho la Kisiasa kuwa ni hatua ya mwisho ya mtangamno wa Afrika Mashariki na unatekelezwa hatua kwa hatua kuanzia Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja kisha Umoja wa Fedha na hatimaye Shirikisho la Kisiasa. Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya katika Mkutano wao wa Kawaida wa 18 wameidhinisha Jumuiya kuanza na mfumo wa *Confederation* kama hatua ya kipindi cha Mpito cha kuelekea kwenye Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Aidha, wameagiza Baraza la Mawaziri kuunda timu ya wataalam wa masuala ya katiba ili kuandaa Rasimu ya Katiba itakayoiwezesha Jumuiya kuanza kutekeleza mfumo huo.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kukamilika kwa kipindi cha utumishi cha Dkt. Enos Steven Bukuku, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Mipango na Miundombinu, Mkutano wa 18 wa Wakuu wa Nchi Wanachama ulimteua

na kumuapisha Injinia Stephen Daud Malekela Mlote kutoka Tanzania kushika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. Vilevile, mkutano huo ulimteua Jaji Dkt. Charles Oyo Nyawello kutoka Jamhuri ya Sudan Kusini kuwa jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki katika Mahakama ya Awali.

**164.** ***Mheshimiwa* Spika,** jitihada za usuluhishi wa Mgogoro wa Kisiasa Nchini Burundi zinaendelea chini ya Mwezeshaji Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya kukamilika awamu ya mashauriano na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Burundi, Mwezeshaji ameainisha maeneo kadhaa ya msingi ambayo yatakuwa sehemu ya majadiliano.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo hayo ni usalama na kumaliza vitendo vya uvunjifu wa amani; utawala wa sheria na kumaliza ukiukwaji wa haki za binadamu; hali ya utekelezaji wa Mkataba wa Amani wa Arusha wa Mwaka 2000; masuala ya demokrasia; masuala ya kijamii na binadamu, madhara ya uchumi yaliyosababishwa na mgogoro huo; uhusiano wa nchi hiyo na majirani zake pamoja na Jumuiya za Kimataifa; na utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Maalum kuhusu Burundi wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya Kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Maeneo hayo yatawasilishwa katika awamu ya kwanza ya majadiliano ambayo inahusisha viongozi na wadau muhimu kisiasa nchini Burundi ili kuainisha yale ambayo wanakubaliana. Wadau wengine kama asasi za kijamii, viongozi wa kidini, makundi ya wanawake na vijana watashirikishwa katika awamu ya pili ya usuluhishi ili kujadili maeneno ambayo yatakosa muafaka katika awamu ya kwanza.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 7 wa Dunia wa Masuala ya Uchaguzi sanjari na Programu ya Uangalizi wa Uchaguzi wa Marekani wa mwaka 2016 uliofanyika katika majimbo ya Washington DC, Maryland na Virginia mwezi Novemba 2016. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kujenga uelewa na kuimarisha

usimamizi/uendeshaji na uangalizi wa uchaguzi kwenye Kanda mbalimbali ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Mkutano huo ulikuwa ni fursa kwa wajumbe na Jumuiya ya Afrika Mashariki kujifunza na kubadilishana uzoefu na Kanda nyingine kuhusu namna ya kuendesha chaguzi za kidemokrasia na kuimarisha amani na usalama wakati wa uchaguzi.

**h. Uwianishaji wa Vibali vya Kazi na Ukaazi katika Nchi Wanachama**

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya uwianishwaji wa madaraja ya vibali vya kazi/ ukaazi na ada ya vibali kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia kuwa suala la vibali vya kazi Tanzania Bara na Zanzibar linashughulikiwa na Wizara tofauti, Tanzania imepewa muda hadi kufikia mwezi Septemba 2017 kuwianisha Sheria na Kanuni zinazohusiana na utoaji wa vibali vya kazi na tozo za ada kati ya Tanzania Bara na Zanzibar kabla ya kukamilisha majadiliano hayo katika ngazi ya Jumuiya. Wizara inaendelea kuratibu majadiliano ya ndani kuhusu suala hili.

**i. Maandalizi ya Pasi Mpya ya Kusafiria ya Kimataifa ya Afrika Mashariki**

**168.** ***Mheshimiwa Spika*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Uhamiaji kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mjini Moshi mwezi Novemba 2016. Mkutano huo ulifanya tathmini ya hatua iliyofikiwa na Nchi Wanachama katika kukamilisha maandalizi ya kuanza matumizi ya Pasi Mpya ya Kusafiria ya Kimataifa ya Afrika Mashariki ifikapo mwezi Aprili 2017.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo ilibainika kuwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zipo katika hatua tofauti za maandalizi ya kutoa Pasi hizo. Nchi za Burundi na Kenya zimekamilisha maandalizi ya kutoa pasi hizo, wakati Tanzania, Uganda na Rwanda zinaendelea kukamilisha taratibu za utekelezaji. Hivyo, ilipendekezwa

muda wa kuanza kutoa Pasi hizo usogezwe mbele kutoka mwezi Aprili 2017 hadi mwezi Desemba 2017.

### j. Mapambano Dhidi ya Ugaidi, Uharamia, Biashara Haramu ya Binadamu na Dawa za Kulevya

**170.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Taasisi za Kupambana na Ugaidi uliofanyika Entebbe, Uganda mwezi Novemba 2016. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama zilibadilishana uzoefu kuhusiana na mapambano dhidi ya ugaidi, kuweka mfumo mmoja wa kurekodi na kubadilishana taarifa na mienendo ya ugaidi. Aidha, nchi wanachama zilikubaliana kuhuisha sheria za kupambana na ugaidi katika Jumuiya kwa lengo la kuwa na tafsiri moja na kiwango sawa cha adhabu.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa kupambana na uharamia katika Bahari ya Hindi ambao unahusisha pia Kanda za SADC, COMESA na IGAD. Majukumu ya utekelezaji wa Mkakati huo yamegawanywa kikanda ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki imepangiwa jukumu la kuhifadhi watuhumiwa wa uharamia watakaokamatwa, kuendesha mashtaka dhidi yao na kuwafunga watakaopatikana na hatia na kisha kuwarejesha nchini mwao mara baada ya kumaliza vifungo.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu hilo, Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa mafunzo mwezi Aprili 2017 kwa ajili ya kuwajengea uwezo Waendesha Mashtaka na Wanasheria kuhusu namna ya kushughulikia kesi za uharamia na kuendesha mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa uharamia.

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa Kupambana na Biashara haramu ya Binadamu. Nchi Wanachama zimebaini kuwa tatizo la biashara haramu ya binadamu katika Jumuiya limekuwa likiongezeka kila mwaka na kwamba wahanga wakubwa wa biashara hiyo ni wanawake na watoto huku chanzo kikuu

kikitajwa kuwa ni umaskini. Nchi Wanachama zimekubaliana kuhuisha sheria za kupambana na biashara hiyo na kuimarisha mawasiliano kuhusiana na mienendo ya wahusika katika biashara hiyo.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa Kupambana na dawa za kulevya katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Nchi Wanachama zilibadilishana uzoefu kwenye maeneo mbalimbali. Maeneo hayo ni pamoja na njia na mbinu mpya za usafirishaji na uzalishaji wa dawa za kulevya; kubainisha maeneo ambayo ni kitovu cha uzalishaji wa dawa za kulevya hasa bangi; na kuainisha malighafi za viwanda zinazotumika kuzalisha dawa za kulevya. Aidha, Nchi Wanachama zimekubaliana kuhuisha sheria za kupambana na dawa za kulevya, kuanzisha kanzidata ya kutunza taarifa za watuhumiwa na kuandaa Mkakati wa kuelimisha umma juu ya madhara ya dawa hizo.

### k. Mafunzo kwa Maafisa Kadeti

**175.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Wakufunzi wa Vyuo vya Maafisa Kadeti wa Majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Kigali, Rwanda mwezi Machi 2017. Mkutano huo, uliandaa na kuwianisha baadhi ya masomo ambayo yatatumika kama rejea kwa vyuo vyote vya Maafisa Kadeti kwenye Nchi Wanachama wa Jumuiya. Aidha, Wakuu wa Vyuo hivyo walikubaliana masuala yatakayofundishwa kwenye masomo ili kuleta ulinganifu katika mafunzo hayo.

### l. Zoezi la Pamoja la Kijeshi la Afrika Mashariki

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu na kushiriki katika maandalizi ya zoezi la Pamoja la Kijeshi la Afrika Mashariki la Kamandi ya pamoja ya kijeshi lililofanyika Bujumbura, Burundi mwezi Februari 2017. Zoezi hili pia limepangwa kufanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Desemba 2017. Lengo la zoezi hilo ni kujenga uwezo wa majeshi yetu katika Operesheni za kulinda

Amani, kupambana na Ugaidi, kukabiliana na Majanga na Uharamia.

**177. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kushiriki katika maandalizi ya Rasimu ya awali ya majadiliano ya Uundaji wa Mkataba wa Pamoja wa Ulinzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hiyo ni utekelezaji wa matakwa ya Itifaki ya Ushirikiano katika Ulinzi ya Jumuiya ambapo Nchi Wanachama zinatakiwa kukamilisha majadiliano hayo ndani ya mwaka mmoja tangu kuanza kutumika kwa Itifaki hiyo. Tayari, Baraza la Mawaziri la Jumuiya limeidhinisha Rasimu hiyo kama Mwongozo wa Majadiliano ya Mkataba huo.

**Bunge la Afrika Mashariki**

**178. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika Mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki. Katika Mikutano hiyo, Bunge la Tatu la Afrika Mashariki lilipitisha Miswada minne ya Sheria. Miswada hiyo itawasilishwa kwa Wakuu wa Nchi Wanachama kwa hatua stahiki. Miswada hiyo ni:-

i. Muswada wa Sheria wa Afrika Mashariki wa Kukabiliana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu katika Jumuiya wa mwaka 2016;

ii. Muswada wa Sheria wa Afrika Mashariki wa Malipo/ Maslahi kwa Viongozi Maalum wa Viungo/Taasisi za Jumuiya wa mwaka 2015;

iii. Muswada wa Sheria wa Afrika Mashariki wa Utawala wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2016; na

iv. Muswada wa Sheria wa Afrika Mashariki wa Usawa wa Kijinsia wa mwaka 2016.

## B. Ushirikiano wa Kimataifa

### Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu Umoja wa Mataifa kupitisha Ajenda ya mwaka 2030 iliyobeba Malengo ya Maendeleo Endelevu. Utekelezaji wa malengo hayo Kimataifa ulianza rasmi mwezi Januari 2016 na yatafanyiwa tathmini kila baada ya miaka mitano na hatimaye tathmini ya mwisho mwaka 2030.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017,Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Umoja wa Mataifa hapa nchini imeendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya Serikali kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo ni kuhakikisha kuwa umma na makundi yote kwenye jamii yanafahamu nafasi yao kwenye utekelezaji wa Malengo hayo. Hadi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa hapa nchini tumeweza kutoa elimu kwa wananchi kwenye mikoa ya Mbeya, Kagera, Kilimanjaro, Kigoma, Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, elimu hiyo pia ilitolewa Zanzibar katika visiwa vya Pemba na Unguja. Zoezi hili ni endelevu kwa nchi nzima, hivyo litaendelea kufanyika ili kuhakikisha kila mdau anashiriki ipasavyo katika kutimiza malengo ya ajenda hii. Kwa upande wa Bunge, kama ambavyo tuliwahi kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge wakati wa mchakato wa kuundwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu mwezi Machi 2015, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine muhimu tutaendelea kutoa elimu kwa Wabunge kadri itakavyohitajika ili kufanikisha utekelezaji wake.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali imeendelea kuratibu na kushiriki katika Mikutano mbalimbali ya Kimataifa kwa lengo la kujifunza, kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja na nchi na wadau wengine juu ya namna bora ya kushirikiana katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo

Endelevu. Baadhi ya Mikutano hiyo ni:- Jukwaa la Kisiasa la Ngazi za Juu kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu lililofanyika New York, Marekani mwezi Julai 2016; Mkutano wa Ngazi ya Juu wa "*Global Partnership for Effective Development Cooperation – GPEDC*" uliofanyika Nairobi, Kenya mwezi Novemba hadi Desemba 2016; Mkutano wa Kimataifa kuhusu Usafiri Endelevu uliofanyika Ashgabat, Turkmenistan mwezi Novemba, 2016.

Mikutano mingine ni Mkutano wa Shirika la Posta Duniani uliofanyika Istanbul, Uturuki mwezi Septemba hadi Oktoba 2016; Mkutano wa Tatu wa Shirika la Makazi Duniani uliofanyika Quito, Equador mwezi Oktoba 2016; Mkutano wa Baraza la Kiuchumi na Kijamii la Umoja wa Mataifa kuhusu Uendeshaji wa Shughuli za Kimaendeleo uliofanyika New York, Marekani mwezi Februari hadi Machi 2017; na Mkutano wa 61 wa Umoja wa Mataifa wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani uliofanyika New York, Marekani mwezi Machi 2017.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imenufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na mikutano hiyo ambayo imetoa fursa kwetu kusimamia kikamilifu maslahi mapana ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa ambao unatekelezwa kuanzia mwezi Julai 2016 hadi mwezi Juni 2021. Katika kipindi cha utekelezaji wa mpango huo, Tanzania itafaidika na miradi yenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.3 ambapo asilimia 8 ya fedha hizo zitatumika kwa miradi ya Zanzibar. Utekelezaji wa mpango huo unawiana na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016 - 2021); na Mpango wa Pili wa Kupunguza Umaskini Zanzibar wa mwaka 2016 – 2021; Ajenda ya Afrika ya 2063; na Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030.

**Kikao cha 71 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Kikao cha 71 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika New York, Marekani kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 2016. Tanzania ilitumia Kikao hicho kueleza misimamo yake kwenye masuala mbalimbali ikiwemo mgogoro wa Saharawi Magharibi; kuwa na Taifa la Palestina sambamba na Israel salama; na kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, kupitia kikao hicho tuliijulisha Jumuiya ya Kimataifa juu ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kutatua migogoro ya kisiasa inayozikabili nchi jirani; kupambana na ugaidi pamoja na dawa za kulevya. Vilevile, tulitoa taarifa kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa katika kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili nchi, Bara la Afrika na dunia kwa ujumla katika kutokomeza umaskini; kupambana na rushwa; na dawa za kulevya. Aidha, Tanzania ilisisitiza kuendelea kusimamia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kama sehemu ya mkakati endelevu wa kuheshimu na kulinda haki za binadamu kwa ujumla pamoja na haki za watoto na walemavu.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa Kikao hicho, pia ulifanyika Mkutano maalum kuhusu masuala ya Wakimbizi na Wahamaji uliolenga kutafuta namna bora ya kukabiliana na tatizo hilo. Tanzania ilitumia fursa hiyo kuieleza dunia changamoto zinazolikabili Taifa katika kuhifadhi wakimbizi na kuzishukuru nchi marafiki na mashirika ya kimataifa kwa ushirikiano katika kusaidia kutunza wakimbizi waliopo nchini. Pamoja na kwamba Tanzania inao wajibu wa kutunza wakimbizi kama mshirika wa mikataba ya kimataifa na sera za wakimbizi, tulitumia Mkutano huo kuitaka Jumuiya ya Kimataifa nayo kuwajibika zaidi katika suala hili kwa kuendelea kushirikiana na nchi yetu pamoja na nchi nyingine za Afrika katika kuhudumia wakimbizi na jamii za Watanzania zinazozunguka kambi za wakimbizi. Kwa mara nyingine, Tanzania iliihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa itaendelea kuheshimu mikataba ya kimataifa na kikanda inayoipa nchi yetu wajibu wa kupokea na kuhifadhi wakimbizi.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kutumia fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi marafiki na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa kwa kuendelea kutuunga mkono katika kuhifadhi wakimbizi. Nchi kama Marekani, Canada, Australia na Norway zimekuwa zikipokea wakimbizi wanaohifadhiwa nchini kwa ajili ya kuwapa uraia kwenye nchi zao kama njia mojawapo ya kuwasaidia wakimbizi, hivyo kusaidia kupunguza gharama za kuwahifadhi wakimbizi hao. Kwa sasa programu ya kuhamisha wakimbizi 50,000 wenye uraia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwenda nchini Marekani kwa ajili ya kupatiwa uraia wa nchi hiyo kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2015 hadi 2025 inaendelea vizuri.

**Ushiriki kwenye Operesheni za Kulinda Amani Duniani**

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kufuatilia ushiriki wa Tanzania kwenye Operesheni za Kulinda Amani. Hadi sasa, Tanzania ina jumla ya walinda amani 2,279 kwenye Misheni sita za Umoja wa Mataifa ambazo ni: MONUSCO, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; UNAMID, Darfur; UNIFIL, Lebanon; UNMISS, Sudan Kusini; UNISFA, Abyei; na MINUSCA, Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ushiriki wetu kwenye operesheni hizi, Tanzania imeendelea kuaminika na kuheshimika katika Jumuiya ya Kimataifa. Kutokana na sifa hii, Watanzania wenye ujuzi waliteuliwa kwenye Kamandi za juu kwenye Misheni mbalimbali zikiwemo MONUSCO – FIB katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na UNAMID ya Darfur, Sudan. Ushiriki huo umezidi kuwajengea Wanajeshi wetu uzoefu katika medani za kimataifa na kuongeza maarifa na mbinu mbalimbali za kijeshi ikiwemo kujifunza matumizi ya vifaa vya kisasa vya kijeshi.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii kuuhakikishia uongozi wa Umoja wa Mataifa kuwa, Tanzania itaendelea kuhakikisha kuwa askari wetu wanaheshimu sheria, kanuni, taratibu na maadili ya kulinda amani katika misheni hizo.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara iliratibu na kufuatilia ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya kuhifadhi masalia na kumbukumbu za kesi za mauaji ya kimbari ya Rwanda katika eneo la Laki Laki, Arusha. Kwa kutambua umuhimu wa suala hili, Serikali imechangia eneo lenye ukubwa wa ekari 16 kwa ajili ya shughuli za ujenzi na eneo la ekari tano kati ya hizo tayari limejengwa majengo matatu ambayo ni Jengo la Mahakama; Jengo la Kuhifadhi Kumbukumbu, Maktaba, Kantini; na Jengo la Utawala.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** Umoja wa Mataifa umechangia kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.8 ambazo zimetumika kugharamia ujenzi wa majengo hayo ambayo mojawapo linaongoza Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa na Maktaba kubwa na ya kisasa kuhusu masuala ya sheria hususan sheria za kimataifa kuhusu uhalifu. Napenda kutumia nafasi hii kuwakaribisha Wanazuoni kutoka ndani na nje ya nchi kutumia rasilimali zinazopatikana kwenye Maktaba hiyo ili kujijengea uwezo na kuelimisha umma juu ya athari za matukio ya uhalifu kupitia tasnia hii ya sheria. Idara za Sheria, Mahakama na Vitivo vya Sheria Vyuo Vikuu mnakaribishwa kutumia maktaba hii kwa shughuli mbalimbali hasa tafiti.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, majengo hayo ambayo yalizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba 2016, yalijengwa na Wakandarasi wa Tanzania baada ya kushindanishwa na Kampuni nyingine za Kimataifa.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Tanzania ikiwa Mwenyekiti wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano wa Kisiasa, Ulinzi na Usalama ilipewa jukumu la kuwasilisha ombi maalum kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu kuiongezea muda Misheni ya Kulinda Amani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ijulikanayo kama MONUSCO - FIB. Maamuzi haya yalifikiwa kwa kuzingatia umuhimu wa vikosi hivyo katika kulinda amani na usalama nchini humo na kwa kuzingatia hali ya kisiasa iliyopo hivi sasa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, inayochangiwa

na kuongezeka kwa vikundi vya uasi pamoja na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Desemba 2017.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** nilipewa jukumu na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza Ujumbe Maalum wa Tanzania kuwasilisha ombi hilo kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Hivyo, tarehe 28 Machi 2017, niliwasilisha ombi hilo kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, New York, Marekani.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tarehe 31 Machi 2017, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, lilipitisha kwa kauli moja Azimio la kukiongezea muda kikosi cha kulinda Amani cha MONUSCO-FIB. Kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi wanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika na nchi wanachama wa SADC kwa ujumla wake kwa imani walioionesha kwa Tanzania kwa kuipa jukumu la kusimamia suala hili na kusaidia kulifanikisha.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufanikiwa kwa suala hili, sio tu Tanzania inakuwa imetekeleza majukumu yake kama Mwenyekiti wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano wa Kisiasa, Ulinzi na Usalama, bali pia inatekeleza moja ya nguzo za Sera yake ya Mambo ya Nje inayosisitiza ujirani mwema

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuongezewa muda kwa vikosi vya MONUSCO-FIB ni hatua muhimu kwa kuwa inatoa nafasi ya kutafuta suluhu ya hali ya kisiasa ili kurejesha amani na usalama katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, kuwepo kwa amani na usalama katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutaongeza fursa za biashara na faida nyingine za kiuchumi na kijamii baina ya nchi hiyo na nchi za SADC na Maziwa Makuu, hivyo kuinua uchumi wa ukanda huu na ule wa nchi moja moja.

**Misaada na Mikopo kutoka Mashirika ya Kimataifa**

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha uhusiano kati ya nchi yetu na mashirika ya fedha ya kimataifa kwa lengo la kuendelea kunufaika na ushauri wao na mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, kipaumbele kikiwa katika miradi mikubwa ya miundombinu ya barabara, reli, nishati na maji.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka huu wa fedha,Viongozi mbalimbali wa mashirika ya fedha walifanya ziara za kikazi hapa nchini. Viongozi hao ni Mhe. Dkt. Frannie Léautier, aliyekuwa Makamu wa Rais Mwandamizi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika; na Bw. Amadou Hott, Makamu wa Rais wa Benki hiyo anayeshughulikia masuala ya nishati. Viongozi hao walifanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na viongozi wengine wa Serikali kuhusu namna ya kusaidia kuendeleza Miundombinu ya barabara, reli na nishati. Ziara hizo zilifuatiwa na ziara ya Wakurugenzi nane (8) wa Idara mbalimbali za Benki hiyo waliyoifanya hapa nchini mwezi Februari hadi Machi 2017 kwa lengo la kujadiliana kwa kina na Serikali namna bora ya kutekeleza maboresho ya sekta ya miundombinu na nishati. Miongoni mwa miradi ambayo ilijadiliwa ni ujenzi wa vituo vya kuzalisha umeme Malagarasi na Kakonko huko Kigoma; pamoja na njia ya kusafirisha umeme kuunganisha Ukanda wa Kaskazini Magharibi kwenye Gridi ya Taifa.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakurugenzi hao pia, walifanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kufanya tathmini ya miradi ya ujenzi wa barabara za Mahonda – Mkokotoni (Kilomita 31); Fuoni-Kombeni (Kilomita 8.6); Pale – Kiongele (Kilomita 4.6); na Matemwe – Muyuni (Kilomita 7.6) zinazofadhiliwa na benki hiyo.

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2017, Mhe. Dkt. Jim Yong Kim, Rais wa Benki ya Dunia alifanya ziara ya kikazi nchini, ambapo pamoja na mambo mengine, alifanya

mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kushiriki katika kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya barabara ya Morogoro na Sam Nujoma katika eneo la Ubungo. Wakati wa uzinduzi wa mradi huo, mikataba mikubwa mitatu (3) yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 780 ilisainiwa kati ya Benki ya Dunia na Serikali. Kiongozi huyo pia, aliahidi kuendelea kuisaidia Tanzania kupata mikopo ya riba nafuu kwenye sekta mbalimbali. Mikopo hiyo inatarajiwa kufikia kiasi cha Dola za Marekani kati ya bilioni tatu (3) na nne (4) katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Ujio wa viongozi hao wa ngazi za juu wa mashirika ya fedha ni ishara ya ushirikiano madhubuti kati ya Tanzania na Mashirika hayo na pia ni ishara ya kukubalika kwa sera za kiuchumi zinazosimamiwa na Serikali ya Awamu ya Tano. Hivyo, kuimarika kwa ushirikiano huo kunatuhakikishia kuendelea kupata fedha za kuendeleza miundombinu ambayo ni kichocheo kikubwa cha ustawi wa sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo na biashara na hatimaye kusukuma azma ya kukuza viwanda na kuongeza ajira.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kudumisha ushirikiano na mashirika ya fedha, Wizara yangu imeendelea pia kushirikiana na Umoja wa Mataifa na mashirika mengine ya kimataifa yanayolenga kuboresha huduma za kijamii. Katika mwaka huu wa fedha, Viongozi Wakuu wa Umoja wa Mataifa na Mashirika yake walitembelea Tanzania. Viongozi hao ni kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu; Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira; na Shirika la Umoja wa Mataifa la Wahamaji. Kwa ujumla ziara hizo zilitoa nafasi kwa Tanzania kujadiliana na Viongozi hao namna wanavyoweza kuisaidia nchi kuendeleza na kuboresha utoaji wa huduma katika sekta za Afya, Mazingira na Uhamaji. Mfano, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu limeipatia Tanzania msaada wenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani 831,000 unaojumuisha magari manne (4) ya wagonjwa, magari mawili (2) ya huduma na vifaa tiba.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kufuatia ombi la Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Antonio Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa akiwa njiani kuelekea New York, Marekani, alipita kwa muda mfupi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam tarehe 9 Machi 2017 na nilifanya naye mazungumzo kwa niaba ya Mheshimiwa Rais.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katibu huyo Mkuu wa Umoja wa Mataifa, aliipongeza Tanzania kwa uwezo wake wa kutekeleza kanuni za utawala bora ndani ya nchi na pia kudumisha amani Barani Afrika hususan katika Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Mheshimiwa Guterres alimpongeza Mheshimiwa Rais Magufuli na Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin Mkapa kwa jitihada zao katika kutatua migogoro ya kisiasa katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, alipongeza juhudi za Tanzania za kuendelea kuhifadhi wakimbizi kutoka nchi hizo. Tanzania ingependa kuona hali ya amani na utulivu inaendelea kuwepo katika nchi zinazotuzunguka ili kuzuia kuongezeka kwa wakimbizi.

**Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Paris**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 22 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 22) uliofanyika Marrakech, Morocco, mwezi Novemba 2016. Mkutano huo ulikuwa ni wa kwanza tangu kupitishwa kwa Makubaliano ya Paris mwezi Desemba 2015 na ulijikita katika kujadili utekelezaji wa Makubaliano hayo yaliyoanza kutekelezwa mwezi Novemba 2016. Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi zinazoathirika na mabadiliko ya tabianchi, imesaini Makubaliano hayo yanayoweka mikakati ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kuzijengea nchi uwezo wa kukabiliana na athari hizo. Kwa sasa, Tanzania ipo katika hatua za maandalizi ya kuridhia Makubaliano hayo.

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na masuala mengine, Mkutano wa COP 22 ulijadili umuhimu wa mifuko ya kimataifa inayofadhili miradi ya uhifadhi wa mazingira na

ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi katika kutekeleza Makubaliano ya Paris. Mifuko hiyo ambayo Tanzania imekuwa ikinufaika nayo ni pamoja na *Green Climate Fund (GCF), Global Environment Facility (GEF), Adaptation Fund (AF)* na *Least Developed Countries Fund (LDCF)*. Tunaishukuru Mifuko hii kwa misaada inayotoa kwa Tanzania, na tunazishukuru nchi zinazochangia fedha kwenye Mifuko hii. Tunaendelea kutoa wito kwa nchi zilizoendelea kuendelea kuongeza michango kwenye mifuko hiyo ili nchi maskini ambazo hazijasababisha tatizo hili ziweze kutekeleza mipango na miradi ya kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko hayo.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, inaendelea kuhamasisha sekta ya umma na sekta binafsi kufuatilia kwa karibu ufadhili unaotolewa na mifuko hiyo kwenye miradi ya kupambana na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na uhifadhi wa mazingira ili kuiokoa nchi na rasilimali zake na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania itaendelea kushirikiana na vyombo vya kimataifa hususan vile vya Umoja wa Mataifa katika kulinda mazingira ya wanyamapori na misitu kwa ajili ya utalii hususan matumizi endelevu ya maji ya Mto Ruaha na Mto Mara.

## Mfuko wa Dunia wa Masuala ya Afya

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu ilishiriki kwenye Mkutano wa Tano wa Mfuko wa Dunia wa Masuala ya Afya ujulikanao kama *Global Fund* uliofanyika Montreal, Canada mwezi Septemba 2016. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kuhamasisha nchi zilizoendelea na mashirika mbalimbali ya kimataifa kuchangia kiasi cha Dola za Marekani bilioni 13 kwa ajili ya kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu katika nchi zinazoendelea. Mkutano huo, ulifanikiwa kuchangisha kiasi cha Dola za Marekani bilioni 12.9, fedha ambazo zitatumika kusaidia nchi nyingi zinazoendelea

ikiwemo Tanzania, kupambana na magonjwa hayo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2018 hadi 2020.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa kwa kuchangia mfuko huo ili kuzisaidia nchi zinazoendelea kupambana na magonjwa hayo. Aidha, napenda kutoa wito kwa nchi na mashirika mengine kuiga mfano huo. Nichukue nafasi hii tena kuishukuru Serikali na watu wa Marekani kwa msaada wa hivi karibuni kwa Tanzania wa Dola za Marekani milioni 526 kwa ajili ya kuendelea kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

**KURATIBU NA KUSIMAMIA MASUALA YA WATANZANIA WAISHIO UGHAIBUNI**

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuwahamasisha na kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni katika kuchangia maendeleo nchini. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliandaa Kongamano la Tatu la Diaspora lililofanyika Zanzibar mwezi Agosti 2016, ambapo Diaspora kutoka zaidi ya nchi 20 duniani walishiriki. Makongamano hayo yamekuwa yakileta hamasa kubwa kwa Diaspora kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo nchini kupitia uwekezaji katika sekta za elimu, afya, miundombinu, uchukuzi, utalii, nishati na madini. Vilevile, Wizara iliratibu ushiriki wa Taasisi za Umma na Binafsi kwenye Kongamano la kuadhimisha Siku ya Tanzania yenye lengo la kutangaza fursa za uwekezaji kwenye sekta ya maliasili na utalii, lililofanyika Texas, Marekani mwezi Mei 2017.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kukusanya na kutunza kumbukumbu za Watanzania wanaoishi ughaibuni na kuwahimiza kusajili Jumuiya zao katika Ofisi za Balozi zilizo karibu nao. Usajili huo utaiwezesha Serikali kukamilisha kanzidata itakayopatikana katika Tovuti maalum ya Diaspora, ili taarifa za Diaspora zenye kuonesha takwimu sahihi za idadi yao, elimu, ujuzi na maarifa

waliyonayo zisaidie Serikali kuwashirikisha kikamilifu katika kuleta maendeleo nchini.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kutoa elimu kwa Watanzania waishio ughaibuni ili kuhakikisha wanazitambua haki na fursa zilizopo. Tunawakumbusha kila mara kuendelea kuijengea taswira nzuri nchi yetu kwa kuishi na kufuata sheria za nchi husika, tunawapa taarifa za fursa zilizopo kwa sasa ndani ya nchi yetu, changamoto na mafanikio pamoja na kuhamasisha uwekezaji. Halikadhalika, tunasikiliza changamoto zao na kuzitatua kwa kushirikiana na Serikali za nchi walizopo pamoja na Wizara za sekta husika.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** mathalan katika eneo la umiliki ardhi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilitoa ufafanuzi kupitia Ofisi za Balozi zetu na maeneo ya uwakilishi kuhusiana na umiliki wa ardhi. Walifahamishwa kuwa, kulingana na Sheria ya uraia namba 6 ya mwaka 1995 na Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, Mtanzania ambaye ameukana uraia wake anapoteza hadhi ya kuwa raia wa Tanzania na hivyo hataruhusiwa kumiliki ardhi nchini. Hata hivyo, kupitia Taasisi ya Uwekezaji, Watanzania hao bado wana fursa ya kuwekeza nchini kulingana na sheria na miongozo ya uwekezaji iliyopo nchini.

## KUSIMAMIA UTAWALA NA MAENDELEO YA UTUMISHI WIZARANI NA KWENYE BALOZI ZETU

### Uwezo uliopo katika Wizara

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jumla ya watumishi 487ambapo watumishi 107 wapo kwenye Balozi zetu na watumishi 380 wapo Makao Makuu.

### Mafunzo

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuwajengea uwezo watumishi waliopo, Wizara kwa kushirikiana na wafadhili imeendelea kugharamia mafunzo

ya muda mrefu na ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Katika kipindi hiki, watumishi 77 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 14 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika shahada ya Umahiri.

**Uteuzi**

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa na uwakilishi nje, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa Mabalozi ili kujaza nafasi zilizo wazi katika vituo vya Beijing, Paris, Brussels, Muscat, Rome, New Delhi, Pretoria, Nairobi, Brasilia, Maputo, Kinshasa, Kampala, Abuja, Moroni na Geneva. Aidha, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi wa Mabalozi wa vituo vipya katika nchi za Algeria, Israel, Korea Kusini, Sudan, Qatar na Uturuki.

**KURATIBU NA KUSIMAMIA MIRADI YA MAENDELEO NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**Miradi ya Maendeleo ya Wizara**

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya maendeleo kiasi cha Shillingi bilioni 8. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ambalo ni sehemu ya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kiasi cha Shilingi bilioni 2.3; kukamilisha ukarabati jengo la ghorofa tisa litakalotumika kwa ajili ya ofisi na makazi katika Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji kiasi cha Shilingi bilioni 1.3; kukarabati makazi ya Balozi na watumishi yaliyopo Stockholm, Sweden kiasi cha Shilingi bilioni 2.2; kukarabati majengo mawili yanayomilikiwa na Serikali yaliyopo Khartoum, Sudan kiasi cha Shilingi bilioni 1.8; na kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na Balozi za Tanzania nje kiasi cha Shilingi milioni 321.5.

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Mei 2017, Wizara imepokea Shilingi bilioni 3.4 za bajeti ya maendeleo sawa na asilimia 43.6. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi bilioni 2.1 ni kwa ajili ya kukarabati makazi ya Balozi na watumishi

yaliyopo Stockholm, Sweden na Shilingi bilioni 1.3 zimetumika kwa ajili ya kumlipa mkandarasi anayekamilisha kazi ya ukarabati wa jengo la Ofisi na makazi lililopo Maputo, Msumbiji. Wizara inaendelea kufuatilia fedha za maendeleo ziliozosalia ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa.

### Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuna taasisi tatu ambazo Wizara yangu ina jukumu la kuzisimamia ambazo ni Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Jijini Dar es Salaam, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha, ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam. Naomba nichukue fursa hii kutoa taarifa ya taasisi hizo kama ifuatavyo:-

### Chuo cha Diplomasia

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupata ithibati na kutambuliwa rasmi na Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi, Chuo sasa kimejikita katika kutoa Programu za Diplomasia ya Uchumi ili kwenda sambamba na Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda. Aidha, Chuo kimeanza kutoa kozi za muda mfupi na muda mrefu za utatuzi wa migogoro.

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mipango na malengo yake ya kujiimarisha na kujitanua ili kukipa uwezo na kujitegemea, Chuo kilijikita katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2012/2013 – 2016/2017. Kipaumbele cha Mpango Mkakati huo ni kuboresha miundombinu ya Chuo ili kwenda sambamba na utekelezaji wa matakwa ya Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Chuo hakikupewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo lakini Wizara kwa kutambua hilo ilitumia mahusiano mazuri yaliyopo kati yake na wadau mbalimbali kukiwezesha Chuo hicho kupata misaada ya vitendea kazi. Kupitia juhudi hizo, nchi ya Jamhuri ya Korea ilikipatia Chuo hicho msaada wa kompyuta 150. Vilevile, Ubalozi wa Kuwait

nchini ulisaidia kufanya ukarabati wa Maktaba ya Chuo hicho.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mazingira ya Chuo yanaboreshwa, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu imetenga fedha za bajeti ya maendeleo kwa ajili ya Chuo ili kuboresha miundombinu yake. Hatua hiyo itawezesha Chuo kuongeza program, udahili na uwezo wa kujitegemea.

**Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha**

**223.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Machi 2017 Kituo kimeweza kuwa mwenyeji wa Mikutano **274** ambayo **54** ni ya kimataifa na **220** ya kitaifa. Aidha, katika kipindi hicho, Kituo kimefanikiwa kupata mapato kiasi cha **Shilingi 10,155,779,694.00** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Vilevile, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Kituo kimeendelea kupata hati safi ya ukaguzi.

**224.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Kituo kimepanga kuingiza mapato kiasi cha **Shilingi 16,920,100,686.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kinategemewa kuingiza kiasi cha **Shilingi 4,047,100,000.00**.

**225.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza wigo wa utoaji huduma, AICC inategemea kukopa kiasi cha **Shilingi bilioni 2.12** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa upanuzi wa Hospitali ya AICC baada ya kupata kibali cha Wizara ya Fedha na Mipango. Kituo pia kinaendelea kufanya taratibu za kuwezesha kujengwa Kituo mahsusi cha mikutano kitakachoitwa *Mt. Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC).* Kituo hicho ndicho kitakuwa suluhisho sahihi la mahitaji ya mikutano ya kimataifa na maonesho hapa nchini. Vilevile, Kituo kinaendelea na mchakato wa kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha mikutano Dodoma.

**226.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya Mahakama ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda *(UN-ICTR)* kufunga shughuli zake na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuhamishia baadhi ya shughuli zake katika jengo lao jipya, kwa sasa Kituo cha AICC kina nafasi ya kutosha kuweza kupokea taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa. Hivyo, ninatumia nafasi hii kukaribisha taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi zitakazopenda kuweka makao yao Jijini Arusha kutumia nafasi hizo za ofisi zilizo wazi.

**Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika**

**227.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania (APRM Tanzania) kwa mujibu wa miongozo ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kama ifuatavyo:

i. Kushiriki katika Mkutano wa Bunge la Afrika uliojadili Ripoti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika uliofanyika Sharm el Sheikh, Misri mwezi Oktoba 2016. Katika Mkutano huo, Wajumbe walieleza kuridhishwa kwao na hatua zilizofikiwa na Tanzania katika kudumisha amani na utulivu, kulinda haki za binadamu, kudumisha Muungano, maendeleo ya kiuchumi, matumizi ya lugha moja ya Kiswahili na utoaji wa huduma muhimu za kijamii. APRM Tanzania pia ilipata fursa ya kueleza hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kutatua changamoto mbalimbali zilizobainishwa kwenye ripoti hiyo;

ii. Kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuondoa changamoto za utawala bora zinazoihusu nchi yetu zilizobainishwa kwenye Ripoti ya APRM. Mkazo umewekwa katika kukamilisha ripoti ya utekelezaji wa mpango huo kwa upande wa Zanzibar ili kupata ripoti moja ya nchi itakayowasilishwa kwenye Kikao kijacho cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika;

iii. Kushiriki katika Mkutano wa kutafuta Wajumbe Wapya wa Jopo la Watu Mashuhuri la Mpango wa Afrika wa

Kujitathmini katika Utawala Bora uliofanyika Cape Town, Afrika Kusini mwezi Novemba 2016. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu alichaguliwa kuwa miongoni mwa wajumbe wa Jopo hilo. Wajumbe wengine waliochaguliwa wanatoka katika nchi za Algeria, Misri, Nigeria na Msumbiji;

iv. Kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu matokeo ya tathmini ya utawala bora kwa nchi yetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari na pia kwa kutumia majukwaa mengineyo; na

v. Kuisaidia Serikali kuimarisha Mfumo wa Kujitathmini Kiutawala Bora.

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA NAMNA YA KUZIPATIA UFUMBUZI**

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwepo kwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17, zipo changamoto mbalimbali ambazo Wizara imekabiliana nazo wakati wa kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kutumia fedha nyingi za bajeti kugharamia pango kwa ajili ya ofisi na makazi balozini; Kasi ndogo ya ubadilishaji wa Sheria za nchi ili kuendana na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki; Kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa; na uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu masuala ya Mtangamano.

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara inaendelea kutekeleza mpango wake wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi Balozini kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo zinazotolewa na Serikali na kwa kushirikisha Mifuko ya Uwekezaji iliyopo nchini katika kutekeleza baadhi ya miradi yake ya maendeleo; kuruhusu kasi ya ubadilishaji sheria za nchi ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la

Pamoja; na kuzihimiza Taasisi za Serikali kutoa kipaumbele na kuongeza kasi ya ubadilishaji wa sheria zilizoainishwa ili kuwawezesha Watanzania kunufaika ipasavyo na fursa za Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda.

**230.** ***Mheshimiwa Spika,***kwa kutambua umuhimu wa kipekee wa kutoa elimu kwa Umma wa Watanzania juu ya fursa zinazotokana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama, Wizara imekuwa ikitoa taarifa mbalimbali za fursa zinazopatikana nje ya mipaka ya Tanzania. Kwa muktadha huu,Wizara imeendelea kutumia vyombo vya habari vya umma, binafsi na vya kimataifa kama vile TBC1, Capital, Clouds, Radio One, BBC, CGTN, VoA, RFI, DW na Bloomberg kutoa Elimu kwa Umma kuhusu fursa zinazotokana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Aidha, Wizara imeendelea pia kutumia machapisho, Tovuti yake na Mitandao ya kijamii kama vile Tweeter na Blog ili kuweza kuwafikia wadau wengi zaidi.

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mawasiliano baina ya Wizara na wadau wake, Wizara ilianzisha utaratibu wa kuzungumza na Waandishi wa Habari kila wiki. Malengo ya mikutano hii ni kuueleza umma masuala mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara ikiwemo maazimio yanayofikiwa kwenye mikutano mbalimbali ya kimataifa na kikanda, ziara za viongozi wanaotembelea nchini na pia kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu Wizara. Jumla ya mikutano 70 kati ya Wizara na Waandishi wa Habari kutoka vyombo vyote vya habari ilifanyika ndani ya mwaka huu wa fedha.

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni matumaini yangu kuwa juhudi hizi zitapanua uelewa wa Wananchi kuhusu utendaji wa Wizara kwa ujumla pamoja na kuwahamasisha kutumia fursa zilizopo katika Jumuiya mbalimbali za kikanda na Kimataifa.

## MALENGO YA WIZARA KWA MWAKAWA FEDHA 2017/2018

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na mambo mengine, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na majukumu yake kama ifuatavyo:

i. Kutangaza mazingira mazuri ya nchi yetu kwa ajili ya uwekezaji kutokana na historia yake ya miaka mingi ya amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa;

ii. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi mbalimbali zilizotolewa kwa nchi yetu na nchi wahisani, mashirika ya kikanda na ya kimataifa katika kusaidia utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo;

iii. Kuendelea kuratibu Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali katika kuvutia wawekezaji na watalii, kutafuta nafasi za masomo, ajira na nafasi za kubadilishana uzoefu na kutafuta masoko;

iv. Kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine na ile ya mashirika ya kikanda na kimataifa;

v. Kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya viongozi mbalimbali wa kitaifa;

vi. Kuendelea kusimamia balozi zetu katika kutekeleza majukumu ya uratibu hasa kutafuta wawekezaji, fursa za ajira, nafasi za masomo na masoko kwa bidhaa zetu;

vii. Kuendelea kufuatilia kwa karibu mageuzi kwenye taasisi za Umoja wa Mataifa kama vile Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Baraza la Kiuchumi na Kijamii, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Maendeleo;

viii. Kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na Konseli Kuu na kuendelea kununua, kujenga na kukarabati majengo kwa ajili ya makazi na ofisi za Balozi kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu;

ix. Kujenga mahusiano ya kirafiki na ushirikiano wa kiuchumi kati yetu na vyombo mbalimbali vya Kikanda na Kimataifa, unaozingatia maslahi ya Taifa letu;

x. Kuendelea kutetea na kusimamia maslahi ya nchi maskini kwenye mikutano yote mikubwa na hasa ile ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake. Vilevile, tutaendelea kufanya mazungumzo na nchi tajiri duniani ili kuhakikisha zinatekeleza ahadi mbalimbali zilizotoa ili kuharakisha maendeleo ya nchi maskini. Kwa mfano, ahadi za G8 na ile ahadi ya kila nchi tajiri kutoa asilimia 0.7 ya pato lake la Taifa kwa nchi zinazoendelea na kutoa asilimia 0.2 ya pato lake kwa nchi maskini sana duniani kama msaada;

xi. Kuendelea kutambua jumuiya za watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya taifa;

xii. Kuratibu maandalizi na kushiriki kwenye majadiliano katika mikutano ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mabaraza ya Kisekta ya Mawaziri ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na mikutano ya Vikundi Kazi na Wataalam;

xiii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mabaraza ya Kisekta ya Mawaziri ya Afrika Mashariki, miradi na programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xiv. Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa miaka kumi wa Umoja wa Fedha katika kuelekea kwenye eneo la Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xv. Kuratibu zoezi la mapitio ya Sheria za Tanzania ili kuwezesha Watanzania kunufaika na utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xvi. Kuratibu majadiliano na kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na COMESA na SADC pamoja na Eneo Huru la Biashara la Afrika;

xvii. Kuratibu majadiliano kuhusu maeneo ya ushirikiano katika uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi (reli, barabara, bandari, nishati, viwanja vya ndege na hali ya hewa) na kijamii (elimu, afya, mazingira, jinsia na watoto) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xviii. Kuratibu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha katika biashara baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xix. Kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki;

xx. Kuratibu na kushiriki katika maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia mfumo wa *Confederation*;

xxi. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuanzisha Baraza la Usalama la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxii. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Afrika Mashariki;

xxiii. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuanzisha Itifaki ya Utawala Bora ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxiv. Kutoa Elimu kwa Umma juu ya fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxv. Kuratibu mapitio, utafiti, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxvi. Kuratibu na kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Taasisi ya *TradeMark East Africa* Wizarani, Wizara nyingine, Idara, Taasisi za Serikali na sekta binafsi; na

xxvii. Kukamilisha kuandaa Sera Mpya ya Mambo ya Nje.

**SHUKRANI**

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mabalozi, Wawakilishi wa taasisi za Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi zao katika kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wote wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini, Algeria, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Finland, Hungary, India, Italia, Ireland, Israel, Iran, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Malta, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Uswisi na Uturuki.

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, shukrani ziwaendee Umoja wa Ulaya, AfDB, *African Capacity Building Facility*, Benki ya Dunia, IAEA, IMF, *Investment Climate Facility for Africa,* UNDP na Mashirika mengine yote ya Umoja wa Mataifa, *TradeMark East Africa*, *The Association of European*

*Parliamentarians with Africa* na WWF pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Diplomasia ya uchumi.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, tunapenda kutoa shukrani zetu kwa wadau mbalimbali ambao wameendelea kutujengea uwezo Wizarani ikiwemo kufanikisha uamuzi wa Serikali wa kuhamia Dodoma. Tunazishukuru Serikali za Kuwait na Oman kwa msaada wa magari; UNDP kwa vifaa vya mawasiliano; na Jamhuri ya Korea na Kuwait kwa msaada wa Kompyuta. Vilevile, Wizara inamshukuru Mheshimiwa Jasem Al-Najem Balozi wa Kuwait nchini, kwa utayari wake wa kuendelea kutusaidia katika maeneo mengine na Mheshimiwa Dkt. Lu Younqing Balozi wa China nchini kwa kuahidi kutoa fedha zitakazojenga nyumba ya Wageni Mashuhuri eneo la Chamwino hapa Dodoma.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu, kwa mwaka 2017/2018 Wizara imepangiwa bajeti ya kiasi cha **Shilingi 150,845,419,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 142,845,419,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 8,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018, **Shilingi 133,424,290,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 9,421,129,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Kati ya fedha za Matumizi Mengineyo **Shilingi 410,000,000.00** ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Tanzania, **Shilingi 3,341,148,909.00** ni kwa ajili ya fedha za Mishahara na Matumizi Mengineyo ya Chuo cha Diplomasia na **Shilingi 513,060,356.00** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika fedha za bajeti ya Maendeleo kiasi cha **Shillingi 8,000,000,000.00** zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, **Shilingi 1,815,527,215.00** zitatumika kukarabati jengo la ofisi na makazi ya watumishi, Ubalozi wa Tanzania Kampala; **Shilingi 315,425,000.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi yaliyopo Kinshasa, DRC; **Shilingi 477,293,775.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa ofisi ya Ubalozi na makazi ya watumishi, Ubalozi wa Tanzania Harare; **Shilingi 373,320,000.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya Balozi, ubalozi wa Tanzania Beijing; **Shilingi 534,682,500** ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya watumishi, Ubalozi wa Tanzania Pretoria; **Shilingi 593,300,000.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za ubalozi zilizopo Ubalozi wa Tanzania Lilongwe; **Shilingi 508,420,000.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya watumishi Ubalozi wa Tanzania Cairo; **Shilingi 865,300,200.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini; **Shilingi 257,006,310.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la zamani la ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Washington DC, **Shilingi 259,725,000.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Balozi, ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, **Shilingi 195,943,440.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi, Ubalozi wa Tanzania Brussels; na **Shilingi 1,804,056,560.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya ubalozi, Ubalozi wa Tanzania Muscat.

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 25,773,882,820.00** ikiwa ni maduhuli ya Serikali.

## HITIMISHO

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 150,845,419,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 142,845,419,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 8,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati, ajiandae Msemaji wa Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa taarifa. Niungane na Watanzania wenzangu kuwapa pole wananchi wote waliokumbwa na mafuriko nchini kote Tanzania, likiwemo Jimbo la Mfenesini kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaainisha kuwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na mambo mengine itasimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinaainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine zina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe

Joseph Magufuli kwa kufungua ofisi mpya za Ubalozi mbalimbali duniani hivi karibuni. Vilevile tunampongeza kwa kazi nzuri ya kuendeleza heshima ya Tanzania katika diplomasia, uhusiano wa kikanda na Kimataifa katika kipindi hiki cha uongozi wake ambacho diplomasia ya kiuchumi inahitajika zaidi kuliko wakati mwingine wowote wa vipindi vilivyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi ya kuchambua bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki – Fungu 34 ilifanyika tarehe 2 Aprili, 2017 Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Maendeleo;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitengewa shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa maendeleo katika Kasma 6391 iliyohusika na ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo balozini na Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati yangu ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara hii iliyotengewa fedha kwa mwaka 2016/2017 inayohusu ujenzi na ukarabati wa

majengo katika Balozi za huko Maputo, Msumbiji na Stockholm, Sweden.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kutembelea na kufanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati pia ilitembelea na kufanya ukaguzi wa majengo ya Ubalozi wa Tanzania ulioko Pretoria na Johannersburg nchini Afrika Kusini kutokana na umuhimu wa ubalozi huo katika mahusiano ya kiuchumi na kidiplomasia kati ya nchi hiyo na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu yatokanayo na Ukaguzi; sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, gharama za miradi hiyo na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza miradi hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilijigawa katika makundi matatu; kundi la kwanza lilikwenda nchini Msumbiji, kundi la pili lilikwenda Sweden na kundi la tatu lilikwenda Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi lililokwenda Maputo, Msumbiji lilikagua mradi wa ukarabati wa jengo la ghorofa tisa lililopo Mtaa wa Martires lililoko Mjini Maputo, Msumbiji. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 1,316,435,000 wakati fedha zilizopelekwa hadi ukaguzi huu unafanyika ni shilingi 900,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ukaguzi wa mradi huu Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

(i) Mkataba wa utekelezaji wa USD 2,107,000 ulisainiwa tangu tarehe 20/02/2012;

(ii) Bwana Socrates aliteuliwa kuwa Mhandisi Mshauri kwa gharama ya 11% ya mradi ambayo ni USD 231,773;

(iii) Kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu, gharama yake ilipanda hadi kufikia USD 3,056,839 kutoka gharama za awali zilizopo kifungu namba (i) hapo juu, hivyo gharama za Mradi zimeongezeka kwa USD 949,810;

(iv) Kutokana na kuongezeka kwa gharama za mradi, gharama za Mhandisi Mshauri pia zimeongezeka kutoka USD 231,773 hadi USD 336,252;

(v) Hadi tarehe 31Machi, 2017 mkandarasi anadai USD 888,073 wakati Mhandisi Mshauri anadai USD 150,534;

(vi) Kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi huo, mkandarasi anadai riba ambayo kiwango chake bado kipo kwenye mazungumzo kati ya mkandarasi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(vii) Kwa mujibu wa mazungumzo yanayoendelea, imeelezwa kuwa kama Mkandarasi atalipwa fedha zilizobaki kutokana na mkataba USD 888,073 kabla ya kumalizika mwezi Mei, 2017, ameahidi kuwa atamaliza kazi zilizobakia na atalikabidhi jengo hilo kwa matumizi katikati ya mwezi Julai, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kuchelewa kupelekwa kwa fedha za utekelezaji wa mradi, ili malipo yafanyike kwa mujibu wa mkataba. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 Mradi huu ulikuwa umepelekewa shilingi 900,000,000 na shilingi 416,435,000 bado zilikuwa hazijapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ukarabati unaendelea imegunduliwa kuwa zimejitokeza kazi za ziada ambazo hazikufanyiwa tathmini kwenye usanifu wa jengo *(BOQ)*, kazi hizo zimepandisha gharama ya mradi wote. Mradi huu ulitegemewa kumalizika mwezi Februari, 2014 kama fedha zingetolewa kwa mujibu wa mkataba, lakini hadi muda huu bado haujamalizika na haijulikani utamalizika lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meneja mradi huo kutoka Tanzania *(TBA)* kushindwa kwenda kukagua hatua kwa hatua kumesababisha ucheleweshaji wa malipo kwa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna suala la Ubalozi kuendelea kukodi nyumba kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya wafanyakazi wake, kutokana na mradi huo kutomalizika kwa wakati. Hivi sasa Serikali inatumia USD 20,190 kwa mwezi kwa ajili ya kulipia pango la ofisi na makazi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mradi huo ungekamilika kwa wakati, hivi sasa jengo hilo lingekuwa linaiingizia Serikali fedha zisizopungua USD 280,000 kwa mwaka kutokana na kupangisha sehemu mbali mbali za jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi uliokaguliwa nchini Sweden unahusu ukarabati wa makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi. Taarifa iliyotolewa na Ubalozi ilieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 2,172,880,000. Vilevile taarifa hiyo ilieleza kuwa, Hazina ilishatoa fedha hizo na zimekwishapokelewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, fedha hizo bado hazijapelekwa Ubalozini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi huu ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017 hazikuwahi kupelekwa ubalozini;

(ii) Majengo na makazi ya Balozi na nyumba za Watumishi hayajafanyiwa ukarabati kwa takribani miaka tisa sasa na yapo katika hali mbaya; na

(iii) Gharama za kukarabati nyumba hizo ni kubwa kuliko fedha zinazotengwa kila mwaka kwa ajili ya ukarabati huo.

Mheshimwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na kutokutekelezwa kwa mradi huo kwa muda mrefu, Kamati ilibaini athari mbalimbali ikiwa ni pamoja:-

(i) Kuliondolea Taifa heshima na kuharibu taswira ya nchi yetu nje ya nchi;

(ii) Serikali kulipa gharama ya shilingi 420,000,000 kwa ajili ya kodi ya pango kwa kuwa nyumba hizo hazifai kutumika kama makazi ya binadamu;

(iii) Kwa kuhamwa nyumba hizo kumesababisha kushusha thamani ya bei ya nyumba za mtaa huo, kitu ambacho kimesababisha kuathiri ujirani mwema; na

(iv) Kinga ya Ubalozi tayari imeshaondolewa kwenye nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi lililokwenda Afrika Kusini lilielezwa kwamba Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliopo Mjini Pretoria una majengo nane ambayo ni mali ya Serikali zetu mbili. Kati ya majengo hayo, majengo saba ni mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na jengo moja ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha fedha kilichoombwa ili kufanya ukarabati wa nyumba sita chakavu ili angalau ziweze kukalika ni kiasi cha *Rand* 1,800,000 sawa na takriban shilingi milioni 279. Hata hivyo, hadi Machi, 2016 kiasi cha *Rand* 763,218 sawa na shilingi 118,298,000 zilitolewa kwa ajili ya matengenezo madogo madogo kwa nyumba tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kwamba katika bajeti ijayo Ubalozi uliomba katika maoteo ya bajeti, kiasi cha *Rand* 5,480,000 sawa na shilingi za Tanzania 936,038,000. Kiasi kilichoweza kuingizwa katika bajeti ni shilingi 534,682,000 kutokana na ukomo wa bajeti ambao Wizara imewekewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ziara ya Kamati, imebainika kwamba iwapo ukarabati wa majengo hayo ya Ubalozi hautafanyika athari zifuatazo zitatokea:-

(i) Serikali itakuwa na gharama kubwa za kodi ya pango kutokana na Watumishi wengi kukaa kwenye nyumba za kupanga;

(ii) Viwanja na nyumba zetu zitaendelea kushuka thamani yake hadi kupelekea nyumba za jirani kushuka thamani, nyumba hizo kufanywa magofu na Serikali ya Afrika Kusini kuziondoa katika nyumba zinazostahili kuwa makazi ya binadamu;

(iii) Kulazimika kuzivunja kabisa na kuzijenga upya, jambo ambalo Serikali itaingia gharama kubwa ya ujenzi wa nyumba mpya kadri itakavyoelekezwa na Wataalam wa Mipango Miji wa Afrika Kusini; na

(iv) Kushusha thamani ya nyumba zilizo jirani na nyumba zetu, pia nyumba za jirani watashindwa kupata wapangaji wa nyumba zao pale wanapohitajika kupangisha nyumba hizo kwa kuhofia usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na mambo mengine ni kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo na matumizi sawia ya fedha zinazoidhinishwa na Bunge katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inapojiridhisha na uwepo wa miradi na baada ya kulinganisha miradi hiyo na fedha iliyotumika katika kuitekeleza, inaweza kuishauri Serikali ipasavyo katika jukumu lake la kusimamia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa kutimiza azma ya Wizara kwenye eneo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 ni jambo muhimu. Hata hivyo, ili kufanikisha azma hiyo, upo umuhimu mkubwa kwa Serikali kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinatolewa zote kabla ya tarehe 30 Juni, 2017

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji imebainisha kuwa hali ya majengo yetu bado siyo ya kuridhisha. Bado jengo la

ghorofa tisa lililotolewa na Serikali ya Msumbiji kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama zawadi ikiwemo nyumba ya makazi ya Balozi tokea mwaka 1975, ukarabati wake haujakamilika kuanzia mwaka 2012/2013 hadi mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo karibu kila mwaka linatengewa fedha katika miradi ya maendeleo. Hivyo Serikali ichukue jukumu la makusudi kuhakikisha mradi huo unamalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mradi wa Makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi zilizopo Stockholm, Sweden, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutoa kibali haraka kwa ajili ya kuruhusu uuzwaji wa nyumba ya makazi ya Balozi na kujenga upya nyumba ya makazi ya watumishi Jijini Stockholm. Hii itaepusha Serikali kuingia gharama kubwa ya kulipa kodi ya pango ya shilingi milioni 420 kwa mwaka, vilevile itarudisha heshima ya Tanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini yaliyopo Pretoria, inaonesha kuwa pamoja na kukarabatiwa majengo matatu katika mwaka wa fedha 2016/2017 bado yapo majengo mengine matatu yanayohitaji kufanyiwa ukarabati wa haraka, vinginevyo gharama zake zitakuwa kubwa sana kadri tunavyochelewa. Aidha, kupitia Wizara hii, Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* kuyafanyia ukarabati majengo yao wanayoyamiliki huko Johannesburg na Pretoria, Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipeleke fedha kwa wakati ili kuepusha matatizo mengi yanayojitokeza zikiwemo tozo za ucheleweshaji wa malipo ambazo kila siku zinapandisha gharama za miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meneja wa Miradi kutoka Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* apewe umuhimu wa kutembelea miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ilinde heshima iliyopewa na nchi ya Msumbiji ya kuwa nchi ya kwanza kupeleka Balozi katika nchi ya Msumbiji huru.

Pia Serikali ilifanye jengo la ghorofa tisa huko Maputo, Msumbiji kama kitega uchumi, ambalo likikodishwa Ubalozi unaweza kujiendesha wenyewe na kiziendesha baadhi ya ofisi nyingine za Ubalozi zilizoko Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa jengo la Msumbiji kutaondoa tatizo la Serikali kukodi nyumba kwa Watumishi wa Ofisi ya Ubalozi huo ambazo nyingine zimeonekana kuwa hazina hata usalama wa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi inayoheshimika sana katika nchi za *SADC*, hivyo ni aibu kuwa na jengo la Msumbuji ililopewa zawadi inashindwa kulitengeneza tangu mwaka 1975. Serikali ipeleke fedha ili kunusuru kutumia fedha nyingi kwa kukodi majengo ya ofisi za Ubalozi na makazi ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha matatizo mengi katika mikataba ya miradi ya ujenzi, inashauriwa Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* wahusishwe na kushirikishwa wakati wa kuandaa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzingatia mantiki ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati imepokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa kipindi cha tarehe 01 Julai, 2016 hadi 28 Februari, 2017. Vigezo vilivyotumika katika uchambuzi huo vilijumuisha mambo yafuatayo:-

(i) Malengo ya bajeti yanayopaswa kutekelezwa na Wizara;

(ii) Majukumu ya msingi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(iii) Dhamira ya Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017;

(iv) Hali halisi ya mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017; na

(v) Jinsi Wizara ilivyotumia fedha zilizopatikana na kukabiliana na hali ya mabadiliko ya kidiplomasia na kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, sehemu hii ya taarifa inaeleza kuhusu mambo makuu matatu yafuatayo:-

(i) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli;

(ii) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia Mwezi Machi, 2017; na

(iii) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 24,001,150,000 kupitia Balozi 35 zilizopewa Kasma 2001 hadi 2035.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha tarehe 2 Aprili, 2017 Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia tarehe 28 Febuari, 2017 jumla ya shilingi 14,560,449,174 zilikusanywa na Ofisi za Balozi zetu mbalimbali. Kiasi hicho ni asilimia 60.67 ya makadirio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, makusanyo yangelitakiwa kufikia kiwango kisichopungua asilimia 66 yaani kisichopungua shilingi 16,001,566,705. Hii ni kwa kuwa wakati Wizara inaripoti makusanyo ilikuwa imemaliza mwezi wa nane wa utekelezaji wa bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa uchambuzi huo, ni dhahiri kwamba kiwango kilichokusanywa kilikuwa nyuma kwa lengo kwa asilimia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa kulinganisha

fedha zilizopatikana hadi kufikia mwisho wa mwezi Febuari, 2017 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 na kiasi cha fedha iliyokadiriwa kwa matumizi ya Wizara hii. Njia kuu iliyotumika kufanya uchambuzi na ulinganisho ilihusisha ukokotoaji wa asilimia ya bajeti iliyoidhishwa na matumizi ya kawaida, matumizi ya uendeshaji, matumizi ya mishahara na matumizi ya maendeleo. Ulinganisho huo unaonekena katika Jedwali Na. 1 la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuchambua mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha, matarajio ya kasma mbalimbali za Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo, Kamati ililinganisha fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara, matumizi ya uendeshaji na matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo kama inavyoonekana katika *graph* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi huo yanabainisha mambo sita yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ilipokea asilimia 56 ya bajeti ya matumizi ambayo ni sawa na shilingi 87,202,012,000 kati ya shilingi 151,396,775,000 zilizoidhinishwa na Bunge. Ni dhahiri kuwa asilimia 44 ya bajeti ya Wizara hii haikupatikana hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/2017.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 43 ya bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na shilingi 3,489,315,000 kati ya shilingi 8,000,000,000 zilizoidhinishwa. Asilimia 56 ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo haikupatikana hadi katikati ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/2017.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya bajeti ya uendeshaji (mishahara), ulikuwa asilimia 58 ambayo ni shilingi 83,711,697,000 badala ya asilimia 66.67 ambayo ni sawa na shilingi 95,662,632,000 zilizotarajiwa kutolewa. Upatikanaji huo ni pungufu kwa asilimia 8.33. Kwa kuwa mishahara ililipwa kwa kiwango cha asilimia 100 ya

mahitaji kwa kipindi chote, ni wazi kwamba, upungufu mkubwa ulijitokeza katika upatikanaji wa fedha za uendeshaji.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yaliyoongoza kwa upatikanaji wa fedha ni ulipaji wa mishahara ambapo asilimia 81 ya bajeti iliyoidhinishwa ilipatikana hadi kufikia katikati ya robo ya tatu ya mwaka.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yaliyofuatia kwa upatikanaji wa fedha ni gharama za uendeshaji ambapo kiasi cha asilimia 56 kilipatikana hadi katikati ya robo ya tatu. Ni wazi kuwa upatikanaji huo wa fedha siyo mbaya sana ingawa uliathiri utekelezaji wa majukumu kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yaliyoathirika zaidi na upatikanaji wa fedha ni miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha asilimia 43 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo kilipatikana. Kwa hali hiyo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo haujakamilika kwa kiasi cha asilimia 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matokeo hayo ya uchambuzi, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa umuhimu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho cha mwaka wa fedha wa 2016/2017 ikilinganishwa na utekelezaji wa miradi hiyo katika kipindi kama hicho cha mwaka 2015/2016 ambapo pesa hazikuwa zimetolewa hadi mwezi Machi, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu kuzingatiwa kwa maoni wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo 24 kuhusu mafunzo ya diplomasia, utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa namna Wizara ilivyozingatia maoni na ushauri wa Kamati katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Taarifa hiyo ilionesha kuwa upo ushauri wa Kamati uliozingatiwa

kikamilifu na pia upo unaoendelea kuzingatiwa na au usiozingatiwa kabisa. Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu suala la Wizara kuwapokea watu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia, yatie kwenye *Hansard* yote.

**MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YABUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yetu hii yote iingizwe katika *Hansard*.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YABUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hitimisho, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mahiga, kwa ushirikiano alioutoa wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza kazi zake.

Aidha, namshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba na Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Aziz Mlima na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan Muombwa pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii walioshiriki kutoa ufafanuzi uliotakiwa na Kamati wakati wa vikao.

**MWENYEKITI:** Ahsante, wanatosha. Nakushukuru Mheshimiwa umesoma vizuri na kwa muda unaotakiwa. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaainisha kuwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na mambo mengine itasimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine, zina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza, kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kufungua Ofisi mpya za Balozi mbalimbali Duniani hivi karibuni. Vilevile tunampongeza kwa kazi nzuri ya kuendeleza heshima ya Tanzania katika Diplomasia, Uhusiano wa Kikanda na Kimataifa katika kipindi hiki cha Uongozi wake ambacho Diplomasia ya Kiuchumi inahitajika zaidi kuliko wakati mwingine wowote wa vipindi vilivyopita.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya pongezi hizo naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi ya kuchambua bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Fungu 34 ilifanyika tarehe 2 Aprili, 2017 Mjini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne (4) yafuatayo:-

i) Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 ilitengewa Shs. 8,000,000,000/= kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Kasma 6391 inayohusika na Ununuzi, Ujenzi na Ukarabati wa Majengo Balozini na Makao Makuu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati yangu ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2016/2017 inayohusu Ujenzi na Ukarabati wa Majengo katika Balozi za Tanzania huko Maputo – Msumbiji na Stockholm –Sweden.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na kutembelea na kufanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa

Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati pia ilitembelea na kufanya ukaguzi wa Majengo ya Ubalozi wa Tanzania yaliyoko Pretoria na Johannersburg nchini Afrika Kusini kutokana na umuhimu wa Ubalozi huo katika mahusiano ya Kiuchumi na Kidiplomasia kati ya nchi hiyo na nchi yetu.

### 2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa, gharama za miradi hiyo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilijigawa katika makundi Matatu. Kundi la Kwanza lilikwenda nchini Msumbiji, kundi la Pili Sweden na kundi la Tatu lilikwenda Afrika Kusini.

#### 2.2.1 Mradi wa ukarabati wa Jengo la ghorofa Tisa lililopo Maputo nchini Msumbiji

**Mheshimiwa Spika,** kundi lililokwenda Maputo Msumbiji lilikagua Mradi wa ukarabati wa Jengo la ghorofa Tisa lililopo Mtaa wa Martires Das Machava Namba 85 Maputo nchini Msumbiji, lilitengewa **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Kumi na Sita, Laki Nne na Thalathini na Tano Elfu (1,316,435,000/=)** katika kifungu kidogo namba 411000 kinachosomeka "*Rehabilitation and Other Civil Works*", wakati fedha zilizopelekwa hadi ukaguzi huu unafanyika ni **Shs Milioni Mia Tisa tu (900,000,000/=).**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ukaguzi wa mradi huu Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

i) Mkataba wa utekelezaji wa **USD 2,107,028.89** ulisainiwa tangu tarehe 20/02/2012;

ii) Bwana Socrates Natividade aliteuliwa kuwa Mhandisi Mshauri kwa gharama ya 11% ya mradi ambayo ni USD **231,773.17;**

iii) Kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mradi huu gharama yake imepanda hadi kufikia **USD 3,056,839.15** kutoka gharama za awali zilizopo kifungu namba moja (1) hapo juu , hivyo, gharama za Mradi zimeongezeka kwa **USD 949,810.26;**

iv) Kutokana na kuongezeka kwa gharama za Mradi, gharama za Mhandisi Mshauri pia zimeongezeka kutoka **USD 231,773.17** hadi **USD 336,252.31;**

v) Hadi tarehe 31Machi, 2017 Mkandarasi anadai **USD 888,073.02** wakati Mhandisi Mshauri anadai **USD 150.534.08;**

vi) Kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa mujibu wa Mkataba wa Ujenzi huo, Mkandarasi anadai riba ambayo kiwango chake bado kipo kwenye mazungumzo kati ya Mkandarasi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

vii) Kwa mujibu wa mazungumzo yanayoendelea imeelezwa kuwa kama Mkandarasi atalipwa fedha zilizobakia kutokana na Mkataba **USD 888,073.02** kabla ya kumalizika Mwezi Mei 2017 ameahidi kuwa atamaliza kazi zilizobakia na atalikabidhi jengo hilo kwa matumizi katikati ya Mwezi Julai 2017.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mradi huu ni pamoja na:-

i) Kuchelewa kupelekwa kwa fedha za Utekelezaji wa Mradi ili malipo yafanyike kwa mujibu wa Mkataba;

ii) Hadi tarehe 15 Mei, 2017 Mradi huu ulikuwa umepelekewa **Shs. Milioni Mia Tisa (900,000,000/=)** na **Shs. Milioni Mia Nne Kumi na Sita laki Nne na Thalathini na Tano Elfu (416,435,000/=)** bado zilikuwa hazijapelekwa;

iii) Wakati ukarabati unaendelea imegundulika kuwa zimejitokeza kazi za ziada ambazo hazikufanyiwa tathmini kwenye Usanifu wa jengo (Bill Of Quantity – BOQ), kazi hizo zimepandisha gharama ya Mradi wote;

iv) Mradi huu ulitegemewa kumalizika **Mwezi Febuari, 2014** kama fedha zingetolewa kwa mujibu wa Mkataba lakini hadi muda huu bado haujamalizika na haijulikani utamalizika lini;

v) Meneja Mradi huo kutoka **Tanzania Building Agency (TBA)** kushindwa kwenda kukagua hatua kwa hatua, na kumesababisha ucheleweshaji wa malipo kwa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri;

vi) Ubalozi kuendelea kukodi nyumba kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya Wafanyakazi wake, kutokana na mradi huo kutomalizika kwa wakati. Hivi sasa Serikali inatumia **USD 20,190.00** kwa Mwezi kwa ajili ya kulipia pango la Ofisi na Makazi ya Wafanyakazi; na

vii) Kama Mradi huo ungekamilika kwa wakati hivi sasa jengo hilo lingekuwa linaiingizia Serikali fedha zisizopungua **USD 280,000.00** kwa Mwaka kutokana na kupangisha sehemu mbali mbali za jengo hilo.

### 2.2.2 Mradi wa Ukarabati wa Makazi ya Balozi na Nyumba za watumishi Stockholm nchini Sweden

**Mheshimiwa Spika**, mradi uliokaguliwa Stockholm-Sweden unahusu ukarabati wa makazi ya Balozi na nyumba za watumishi. Taarifa iliyotolewa na Ubalozi ilieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu ulitengewa jumla ya **shilingi 2,172,880,000**. Vilevile, Taarifa hiyo ilieleza kuwa, Hazina ilishatoa fedha hizo na zimekwishapokelewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, fedha hizo bado hazijapelekwa Ubalozini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo**.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi huu ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na 2016/2017 hazikuwahi kupelekwa Ubalozini;

ii) Majengo ya Makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi hayajafanyiwa ukarabati kwa takribani miaka tisa sasa na yapo katika hali mbaya; na

iii) Gharama za kukarabati nyumba hizo ni kubwa kuliko fedha zinazotengwa kila mwaka kwa ajili ya ukarabati huo.

**Mheshimwa Spika**, Aidha, kutokana na kutokutekelezwa kwa mradi huu kwa muda mrefu, Kamati ilibaini athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

i) Kuliondolea Taifa heshima na kuharibu taswira ya nchi yetu nje ya nchi;

ii) Serikali kulipa gharama ya **shilingi milioni mia nne na ishirini (420,000,000/=)** kwa ajili ya kodi ya pango kwa kuwa nyumba hizo hazifai kutumika kama makazi ya binadamu;

iii) Kwa kuhamwa nyumba hizo kumesababisha kushusha thamani ya bei za nyumba ya mtaa huo, kitu ambacho kimepelekea kuathiri ujirani mwema; na

iv) Kinga ya Ubalozi tayari imeondolewa kwenye nyumba hizo.

### 2.2.3 Ukaguzi wa Majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini

**Mheshimiwa Spika,** kundi lililokwenda Afrika Kusini lilielezwa kwamba Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliopo mjini Pretoria una majengo Nane (8) ambayo

ni mali za Serikali zetu Mbili. Kati ya majengo hayo, majengo Saba (7) ni mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na jengo Moja (1) ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 kiasi cha fedha kilichoombwa ili kufanya ukarabati wa nyumba 6 chakavu ili angalau ziweze kukalika ni kiasi cha **Rand 1,800,000.00** sawa na takribani **Tsh. 279 Millioni.** Hata hivyo, hadi Machi 2016 kiasi cha **Rand 763,218.96 sawa na Tsh. 118,298,938.80** zilitolewa kwa ajili ya matengenezo madogo madogo kwa nyumba tatu (3) tu. Kamati ilifahamishwa kwamba Katika Bajeti ijayo Ubalozi uliomba katika maoteo ya bajeti kiasi cha Rand 5,480,000 sawa na Tsh. 936,038,800. Kiasi kilichoweza kuingizwa katika bajeti ni Tsh. 534,682,500. kutokana na ukomo wa bajeti ***(budget ceiling)*** ambayo Wizara imewekewa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara ya Kamati imebainika kwamba iwapo ukarabati wa majengo hayo ya Ubalozi hautafanyika athari zifuatazo zinaweza kujitokeza:-

i. Serikali itakuwa na gharama kubwa za kodi ya pango kutokana na Watumishi wengi kukaa kwenye nyumba za kupanga;

ii. Viwanja na nyumba zetu zitaendelea kushuka thamani yake pia kupelekea nyumba za jirani kushuka thamani, Nyumba hizo kufanywa magofu na Serikali ya Afrika Kusini kuziondoa katika nyumba zinazostahili kuwa makazi ya Binadamu;

iii. Kulazimika kuzivunja kabisa na kuzijenga upya. Jambo ambalo Serikali itaingia gharama kubwa ya ujenzi wa nyumba mpya kadri itakavyo elekezwa na wataalam wa Mipango Miji wa Serikali ya Afrika Kusini; na

iv. Kushusha thamani ya nyumba zilizojirani na nyumba zetu, pia nyumba za jirani watashindwa kupata

wapangaji wa nyumba zao pale wanapohitajika kupangisha nyumba hizo kwa kuhofia usalama.

## 2.3 Maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo pamoja na mambo mengine ni kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo na matumizi sawia ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapojiridhisha na uwepo wa miradi na baada ya kulinganisha miradi hiyo na fedha iliyotumika katika kuitekeleza, inaweza kuishauri Serikali ipasavyo katika jukumu lake la kusimamia maendeleo katika nchi.

### 2.3.1 Maoni na Mapendekezo ya jumla kuhusu Miradi ya Maendeleo

i. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa kutimiza azma ya Wizara kwenye eneo la utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni jambo muhimu. Hata hivyo, ili kufanikisha azma hiyo upo umuhimu mkubwa kwa Serikali kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zinatolewa zote kabla ya tarehe 30 Juni, 2017;

ii. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji umebainisha kuwa hali ya Majengo yetu bado si ya kuridhisha. Bado jengo la ghorofa Tisa (9) lililotolewa na Serikali ya Msumbiji kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama zawadi ikiwemo nyumba ya makazi ya Balozi tokea Mwaka 1975, ukarabati wake haujakamilika kuanzia Mwaka wa Fedha 2012/2013 hadi Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo karibu kila mwaka linatengewa fedha katika Miradi ya Maendeleo. Hivyo Serikali

ichukue juhudi za makusudi kuhakikisha Mradi huo unamalizika kabisa;

i). **Mheshimiwa Spika**, kwa mradi wa makazi ya Balozi na nyumba za watumishi zilizopo Stockholm- Sweden, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutoa kibali haraka kwa ajili ya kuruhusu uuzwaji wa nyumba ya makazi ya Balozi na kujenga upya nyumba ya makazi ya watumishi jijini Stockholm. Hii itaepusha Serikali kuingia gharama kubwa ya kulipa kodi ya pango ya shilingi milioni 420 kwa mwaka vilevile itarudisha heshima ya Tanzania nje ya nchi.

iii. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini yaliyopo Pretoria inaonyesha kuwa pamoja na kukarabatiwa Majengo matatu (3) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, bado yapo Majengo mengine matatu(3) yanayohitaji kufanyiwa ukarabati wa haraka, vinginevyo gharama zake zitakuwa kubwa sana kadri tunavyochelewa. Aidha kupitia Wizara hii, Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kuyafanyia ukarabati wa haraka Majengo yao wanayoyamiliki huko Joharnnesburg na Pretoria nchini Afrika Kusini;

iv. Serikali ipeleke fedha kwa wakati, ili kuepusha matatizo mengi yanayojitokeza zikiwemo tozo “penalties” za ucheleweshaji wa malipo ambazo kila siku zinapandisha gharama za Miradi;

v. Meneja wa Miradi kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) apewe umuhimu wa kutembelea miradi kwa wakati;

vi. Serikali ilinde heshima iliyopewa na nchi ya Msumbiji ya kuwa nchi ya kwanza kupeleka Balozi katika nchi ya Msumbiji Huru; na

vii. Serikali ilifanye jengo la Ghorofa tisa (9) huko Maputo - Msumbiji kama kitega uchumi, ambalo likikodishwa

Ubalozi unaweza kujiendesha wenyewe na kiziendesha baadhi ya Ofisi nyingine za Ubalozi zilizoko Kusini mwa Afrika;

viii. Kukamilika kwa jengo la Msumbiji kutaondoa tatizo la Serikali kukodi nyumba kwa watumishi wa Ofisi ya Ubalozi huo ambazo nyingine zimeonekana kuwa hazina hata usalama wa kuishi;

ix. Tanzania ni nchi inayoheshimika sana katika nchi za SADC, hivyo ni aibu kuwa jengo la Msumbuji ililopewa zawadi inashindwa kulitengeneza tangu mwaka 1975 mpaka sasa;

x. Serikali ipeleke fedha ili kunusuru kutumia fedha nyingi kwa kukodi majengo ya Ofisi za Ubalozi na Makazi ya Watumishi; na

xi. Ili kuepusha matatizo mengi katika Mikataba ya miradi ya ujenzi inashauriwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wakahusishwa na kushirikishwa wakati wa kuandaa mikataba hiyo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 3.1 Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia mantiki ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa kipindi cha tarehe 01 Julai, 2016 hadi tarehe 28 Februari, 2017. Vigezo vilivyotumika katika Uchambuzi huo vilijumuisha mambo yafuatayo:-

i) Malengo ya bejeti yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara;

ii) Majukumu ya msingi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Dhamira ya Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iv) Hali halisi ya mwenendo wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

v) Jinsi Wizara ilivyotumia fedha zilizopatikana na kukabiliana na hali ya mabadiliko ya Kidiplomasia na Kiuchumi Duniani;

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo hayo, sehemu hii ya Taarifa inaeleza kuhusu mambo makuu matatu ambayo ni:-

i) Hali ya ukusanyaji wa Maduhuli;

ii) Hali ya Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia Mwezi Machi, 2017;

iii) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

### 3.1.1 Hali ya Ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **24,001,150,000.00** kupitia Balozi Thelathini na Tano (35) zilizopewa Kasma 2001 hadi 2035. Katika kikao cha tarehe 2 Aprili, 2017 Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia tarehe 28 Febuari, 2017, jumla ya **Shs. 14,560,449,174.67** zilikusanywa na Ofisi za Balozi zetu mbalimbali. Kiasi hicho ni asilimia 60.67 ya makadirio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** katika hali ya kawaida, makusanyo yangelitakiwa kufikia kiwango kisichopungua asilimia 66.67, yaani kiasi kisichopungua Shilingi

**16,001,566,705.00**. Hii ni kwa kuwa wakati Wizara inaripoti makusanyo ilikuwa imemaliza Mwezi wa Nane wa utekelezaji wa bajeti yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kwa uchambuzi huo, ni dhahiri kwamba kiwango kilichokusanywa kilikuwa nyuma ya lengo kwa asilimia 6.00.

### 3.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Mipango ya Bajeti kwa kulinganisha fedha zilizopatikana hadi kufikia mwisho wa Mwezi Febuari, 2017 kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 na kiasi cha fedha iliyokadiriwa kwa matumizi ya Wizara. Njia kuu iliyotumika kufanya uchambuzi na ulinganisho ilihusisha ukokotoaji wa asilimia ya bajeti iliyoidhishwa kwa matumizi ya kawaida (Recurrent), Matumizi ya Uendeshaji (OC), Matumizi ya Mishahara (PE) pamoja na Matumizi ya Maendeleo (Development). Ulinganisho huo unaonekena katika Jedwali Na. 01 la Taarifa hii.


**Jedwali Na. 01: Ulinganisho wa Bajeti na Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2016/2017 | | FEDHA ZILIZOPATIKANA KUTOKA HAZINA HADI 28 FEBRUARI, 2017 | |
|---|---|---|---|
| **MGAWANYO** | **BAJETI** | **MGAWANYO** | **% BAJETI ILIYOIDHINISHWA** |
| Matumizi ya Kawaida (OC +PE) | 143,486,775,000 | 83,711,697,183 | 58.34 |
| Mishahara (PE) | 10,430,754,000 | 8,509,062,360 | 81.58 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 133,056,021,000 | 75,202,634,823 | 56.52 |
| Maendeleo | 8,000,000,000 | 3,489,315,000 | 43.62 |
| **Jumla** | **151,396,775,000** | **87,201,012,183** | **57.60** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, ili kuchambua mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha na matarajio kwa kasma mbalimbali za Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo, Kamati ililinganisha fedha zilizopatikana kwa ajili ya Mishahara, Matumizi ya Uendeshaji na Matumizi ya

kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika grafu Namba 01 ya Taarifa hii;




**Chanzo**: *Jedwali Na. 01 kuhusu Ulinganisho wa Bajeti na Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina*

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi huo yanabainisha mambo sita yafuatayo:-

i) Wizara hii ilikuwa imepokea asilimia 56.0 ya bajeti yake ya matumizi ambayo ni sawa na **Shs. 87,202,012,103/=** kati ya **shs 151,396,775,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge. Ni dhahiri kuwa asilimia 44 ya bajeti ya Wizara hii haikupatikana hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2016/2017;

ii) Wizara ilikuwa imepokea asilimia 43.62 ya Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na **Sh. 3,489,315,000/=** kati ya **Sh. 8,000,000,000/=** zilizoidhinishwa 56.39 ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo haikupatikana hadi katikati ya robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Bajeti ya Uendeshaji (OC) na Mishahara (PE) ulikuwa asilimia 58.34 ambayo ni Shilingi **83,711,697,183.00** badala ya asilimia 66.67 ambayo ni sh. **95,662,632,892.50** zilizotarajiwa kutolewa. Upatikanaji huo ni pungufu ya asilimia 8.33. Kwa kuwa Mishahara ililipwa kwa kiwango cha asilimia 100 ya mahitaji kwa kipindi chote ni wazi kwamba upungufu mkubwa ulijitokeza katika upatikanaji wa fedha za uendeshaji;

iv) Matumizi yaliyoongoza kwa upatikanaji wa fedha ni Ulipaji wa Mishahara ambapo asilimia 81.58 ya bajeti iliyoidhinishwa ilipatikana hadi kufikia katikati ya robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha;

v) Matumizi yaliyofuatia kwa upatikanaji wa fedha ni gharama za uendeshaji ambapo kiasi cha asilima 56.52 kilipatikana hadi katikati ya robo ya tatu. Ni wazi kuwa upatikanaji huo wa fedha si mbaya sana ingawa uliathiri utekelezaji wa majukumu kwa kiasi Fulani;

vi) Matumizi yaliyoathirika zaidi na upatikanaji wa fedha ni Miradi ya Maendeleo ambapo kiasi cha asilimia 43.62 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo kilipatikana. Kwa hali hiyo ni Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo haujakamilika kwa kiasi cha asilimia 56.38.

**Mheshimiwa Spika,** kwa matokeo hayo ya Uchambuzi, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa umuhimu wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi hicho kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 ikilinganishwa na utekelezaji wa miradi hiyo katika kipindi kama hicho kwa Mwakawa Fedha 2015/2016 ambapo pesa hazikuwa zimetolewa hadi Mwezi Machi, 2016.

### 3.2 Taarifa kuhusu kuzingatiwa kwa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwakawa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo

ishirini na nne (24) kuhusu Mafunzo ya Diplomasia, Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa namna Wizara ilivyozingatia Maoni na Ushauri wa Kamati katika utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2016/2017. Taarifa hiyo ilionesha kuwa upo ushauri wa Kamati uliozingatiwa kikamilifu na pia upo unaoendelea kuzingatiwa na au usiozingatiwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu suala la Wizara kuwapeleka watumishi wenye fani zinazohitajika katika Ofisi za Kibalozi na kuwarejesha waliomaliza muda wao pamoja na wasio na tija ya utumishi wao balozini. Taarifa ilionesha kuwa Serikali kwa kiwango kikubwa imetekeleza jambo hili.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa Ushauri ambao utekelezaji wake upo kwenye mchakato ni kuhusu Serikali kuweka mkakati wa kuhakikisha kwamba Diplomasia ya Kiuchumi inatekelezwa katika mfumo wa kuinufaisha na kuimarisha uchumi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taarifa ilionesha kuwa Wizara inaendelea na mikakati ya kufanikisha jambo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuzingatia ushauri kwa sehemu kubwa bado kuna sehemu ya ushauri ambayo haijazingatiwa kabisa. Sehemu hiyo inajumuisha ushauri kuhusu mambo manne yafuatayo:-

i) Serikali kupitia Sheria za Tanzania ambazo zinatakiwa kufanyiwa marekebisho ili ziendane na utekelezaji wa mambo ya Mtangamano wa Afrika Mashariki;

ii) Serikali kupeleka fedha za matumizi ya Ofisi za Ubalozi moja kwa moja kama vile inavyofanya kwa Halmashauri za Wilaya na Miji;

iii) Watumishi wa Balozi zetu nje ya nchi kuwekewa utaratibu bora zaidi utakaowawezesha kupata

malipo yao kwa wakati na kuwaondolea adha na aibu katika utekelezaji wa majukumu yao; na

iv) Serikali kuifanyia marekebisho Sera ya Mambo ya Nje ili iendane na mabadiliko ya Diplomasia ya Kiuchumi Duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza kuwa Serikali itoe uzito stahiki kwa ushauri huo muhimu katika kufanikisha ipasavyo majukumu ya Wizara hii yaliyoainishwa katika Hati Idhini (*The Ministers Assignment of Ministerial Functions Notice* 2016) iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Toleo Namba 16.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea Hati idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara za Serikali, Toleo la tarehe 22 Aprili, 2016 na kuoanisha na Malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Rejea nyingine zilizozingatiwa ni pamoja na:-

i) Maelezo ya Serikali kuhusu Ukomo wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 yaliyotolewa tarehe 28 Machi, 2017 na Waziri wa fedha na Mipango kwa mujibu wa Kanuni ya 97 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ;

ii) Maelezo ya Serikali kuhusu Mwelekeo wa Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Majukumu ya msingi ya Wizara kama hizi (Wizara za Mambo ya Nje) katika nchi nyingine; na

iv) Hali ya Diplomasia ya Kiuchumi Duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kuchambua kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara hii, Kamati iliridhika kuwa Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi kulingana na Dira, Dhima, Dhamira na Kaulimbiu yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Lengo hili limepangwa kufikiwa kwa utekelezaji wa mambo ishirini na sita (26) ikiwemo kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu kuundwa kwa Baraza la Usalama la Afrika Mashariki. ***Hata hivyo, Kamati imebaini hakukuwa na taarifa juu ya shughuli zilizopangwa kuhusiana na Uandaaji wa Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki.***

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri na inaeleweka duniani kote kuwa katika uendeshaji wa mambo mbalimbali ya Taifa, Sera ni Mwongozo muhimu sana. Kamati kwa muda mrefu imekuwa ikiishauri Serikali kuandaa Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki sambamba na sera ya Mambo ya Nje ili kutoa mwongozo mahsusi kuhusu masuala ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hata hivyo utekelezaji wa jambo hili haujawa wa kuridhisha.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Balozi zake inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 25,773,882,820/=.** Kiasi hiki ni asilimia 17.08 ya bajeti ya Wizara inayokadiriwa kutumika kwa Mwaka ujao wa Fedha 2017/2018 ikilinganishwa na Makusanyo ya asilimia 15.85 ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujiridhisha na mwenendo wa ukadiriaji, Kamati ililinganisha makadirio hayo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uchambuzi wa makadirio hayo ulibainisha yafuatayo:-

i) Maduhuli ya kiasi cha Shilingi **Sh 25,773,882,820/=** zinazolengwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni asilimia 17.08 ya bajeti ya Wizara;

ii) Uwiano wa Lengo la Makusanyo kwa bajeti ya matumizi umeongezeka kutoka asilimia 15.85 ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi asilimia 17.08 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Makadirio ya Maduhuli ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti hayakujumuishwa kama sehemu ya Bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Utaratibu huu unatofautiana kidogo na ule wa miaka iliyopita ya 2014/2015 na 2015/2016. Kwa utaratibu huu, fedha zote zinazotarajiwa kuidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Wizara hii zinatakiwa zipatikane moja kwa moja kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhika na lengo lililowekwa kuhusu maduhuli yatakayokusanywa na Wizara hii kupitia Balozi zetu zilizopo nchi mbalimbali. Muhimu katika jambo hili ni kusisitiza ufanisi katika makusanyo ili kufikia lengo lililowekwa.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kutekeleza malengo ishirini na sita (26) yaliyoelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shs 150,845,419,000.00**. Katika kuchambua makadirio hayo, Kamati ililinganisha kiasi cha matumizi kinachoombwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha, Uwiano wa matumizi yanayopangwa kwa Miradi ya Maendeleo, Mishahara na Uendeshaji ulichambuliwa kwa kuzingatia mantiki ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, matumizi ya Jedwali na Grafu yametumika kubainisha mambo muhimu ya kiuchambuzi. Kwa mfano Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo na Bajeti ya kawaida kwa Bajeti ya Wizara unaonyeshwa katika Jedwali Na. 02 na Grafu Na. 02.

**Jedwali Na. 02**: Uwiano wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Bajeti ya Wizara kwa miaka miwili ya fedha.

| MWAKA | | 2016/2017 | | 2017/2018 | |
|---|---|---|---|---|---|
| MGAWANYO | | Bajeti | % ya bajeti | Bajeti | % ya bajeti |
| Maendeleo | | 8,000,000,000 | 5.3 | 8,000,000,000 | 5.3 |
| Matumizi ya Kawida | OC | 133,056,021,000 | 87.8 | 133,424,290,000 | 88.5 |
| | PE | 10,430,754,000 | 6.9 | 9,421,129,000 | 6.2 |
| | Jumla | 143,486,775,000 | 94.7 | 142,845,419,000 | 94.7 |
| **JUMLA YA BAJETI** | | **151,486,775,000** | **100** | **150,845,419,000** | **100** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 207/018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mradi Na. 6391 chini ya Fungu 34 la Wizara hii. Katika uchambuzi huo, Kamati ilichanganua Kasma Nne za Wizara hii kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 03 na Grafu Na. 3 ya Taarifa hii. Kasma hizo zinahusu mambo yafuatayo:-

i) Gharama za Usafiri nje ya nchi – Kasma 221100;

ii) Gharama za Ushauri elekezi – Kasma 410700;


iii) Gharama za Ukarabati wa Majengo, Kampala; Kinshasa; Harare; Beijing; Pretoria; Lilongwe; Cairo; Washington D.C; Brussels na Chuo cha Diplomasia Kurasini – Kasma 411000

iv) Gharama za Ujenzi wa jengo la Ubalozi wa Addis Ababa na Ubalozi wa Kuwait – Kasma 411100

**Jedwali Na 03: Uwiano wa Makadirio ya Kasma za Utekelezaji wa Mradi Na. 6391**

| MAELEZO YA KASMA | MAKADIRIO | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Usafiri nje ya nchi | 352,057,100.00 | 4.40 |
| Ushauri elekezi | 245,090,000.00 | 3.06 |
| Ukarabati | 5,399,071,340.00 | 67.49 |
| Ujenzi | 2,003,781,560.00 | 25.05 |
| **JUMLA** | **8,000,000,000.00** | 100 |

**Chanzo: RANDAMA UK 191 - 192**




**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii unaonesha mambo saba (7) yafuatayo:-

i) Bajeti ya Wizara hii itapungua kutoka sh. **151,486,775,000/-** hadi sh. **150,845,419,000/-** ikiwa ni punguzo la kiasi cha sh. **641,356,000/-** sawa na asilimia 0.4. Bajeti ya wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni karibu sawa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017;

ii) Bajeti ya kugharamia Miradi ya Maendeleo imeendelea kuwa kwa kiasi kile kile kama ilivyokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Bajeti hiyo ni kwa ajili ya kugharamia ununuzi, Ujenzi na Ukarabati wa Majengo Balozini na Makao Makuu ya Wizara chini ya Mradi Namba 6391 ambao katika Kitabu cha Nne cha Bajeti (*Supply Votes, Volume IV*) unasomeka "*Acquisition, Expansion and Rehabilitation of Mission's buildings*". Kiasi hicho ni sawasawa na Kiasi kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Bajeti ya Mishahara imepungua kwa asilimia 9.7 kutoka sh. **10,430,754,000/-** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi Sh. **9,421,129,000/-** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iv) Bajeti kwa ajili ya Uendeshaji (OC) imeongezeka kidogo kwa kiasi cha asilimia 0.3 kutoka Sh. **133,056,021,000/-** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi sh. **133,424,290,000/-** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

v) Bajeti kwa ajili ya Utekelezaji wa majukumu ya Balozi zetu Arobaini na Moja (41) katika nchi mbalimbali zenye Vifungu (Subvotes) 2001 hadi 2041Balozi ni Sh **Shs 111,281,063,000/=** sawa na asilimia 73.8 ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

vi) Asilimia 67.49 ya Bajeti ya Maendeleo imetengwa kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa majengo katika Balozi za Tanzani huko Kampala, Kinshasa, Harare, Beijing, Pretoria, Lilongwe, Cairo, Washington DC, Brussels na Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es salaam;

iv) Asilimia 25.05 ya Bajeti ya Maendeleo itatumika kugharamia ujenzi wa jengo kwa ajili ya Makazi ya Balozi katika Ubalozi wa Tanzania ulioko Addis Ababa na Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania ulioko Muscat nchini Oman; na

v) Asilimia 4.4 imetengwa kwa ajili ya Usafiri nje ya nchi na asilimia 3.06 imetengwa kwa ajili ya kugharamia ushauri elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo Kamati imeridhika kuwa kwa mipango iliyopangwa kutekelezwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imezingatia ushauri iliyoutoa katika vikao mbali mbali.

## 5.0 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huo, Kamati ilirejea Sera na Miongozo mbalimbali inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pamoja na matarajio ya Wananchi kwa Bunge lao katika kuisimamia na kuishauri Wizara hii na kushauri kama ifuatavyo:-

i) kuendelea kutekeleza mambo yote yaliyotolewa ushauri na Kamati wakati ikijadili utekelezaji wa kazi za Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na kuagiza kuwa yatekelezwe Mwaka huu wa 2016/2017 lakini kutokana na changamoto mbali mbali hayakuwahi kutekelezwa;

ii) Kuendelea kutoa ufafanuzi kuhusu mambo na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara hii ili Wananchi waweze kuelewa na kutumia fursa zinazopatikana Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na nchi nyingine Duniani kote;

iii) Kwa kuwa suala la umiliki wa Chuo Cha Diplomasia kilichopo Kurasini baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Msumbiji bado linaleta utata ni vyema sasa jambo hilo likafikia mwisho katika kipindi cha 2017/2018. Katika kutafuta suluhu hiyo Serikali iitumie Tume ya Pamoja ya Tanzania na Msumbiji " Tanzania – Mozambique Joint Permanent Commission (JPC) " ambayo haijakutana kwa muda mrefu sasa ;

iv) Kwa kuwa kipo Chuo cha Diplomasia Kurasini na vile vile upo Mpango wa kutanua Chuo hicho katika jiji la Arusha; ikitokea fursa nyingine ya kujenga Chuo au kituo cha Kimataifa basi kijengwe Makao Makuu ya nchi Mjini Dodoma;

v) Serikali itoe kipaumbele katika kulipa michango ya nchi yetu kwenye Taasisi za Kimataifa ili kuepusha kukwamisha uendeshaji wa Taasisi hizo pamoja na kuendelea kujenga heshima ya muda mrefu ya nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa;

vi) Serikali itoe umuhimu wa kwanza kushirikiana na zile nchi ambazo kwa kushirikiana nazo uchumi wa nchi yetu utaimarika kwa kiwango kikubwa hususan katika nyanja za kibiashara na uimarishaji wa miundo mbinu;

vii) Pamoja na elimu inayotolewa kuhusu faida zinazopatikana katika Ushirikiano wa Kimataifa, Serikali iweke umuhimu na uzito maalum kuhusu faida zinazopatikana katika Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC);

viii) Serikali ifungue Ofisi za Ubalozi au kuweka Balozi za heshima katika nchi na maeneo ambayo nchi yetu ina mahusiano makubwa ya kibiashara kama vile Bostwana, Guangzhou – China, Lubumbashi – DRC, Cuba na kwingineko;

ix) Serikali ilifanyie matengenezo makubwa au kujenga jengo jipya la Kurugenzi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki lililopo Zanzibar;

x) Serikali ihakikishe inazipatia fedha, Watumishi na vitendea kazi vingine Ofisi zote za Balozi mpya zilizofunguliwa katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017;

xi) Kamati imebaini kuwepo ongezeko la kunyanyaswa kwa wafanyakazi wa majumbani huko nchi za nje, hivyo Serikali iweke utaratibu madhubuti utakaohakikisha kunakuwepo na usalama kwa Watanzania wanaofanya kazi mbalimbali nje ya nchi;

xii) Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kutekeleza ushauri wake uliotolewa katika miaka iliyopita kuhusu kuongeza juhudi za uboreshaji wa majengo ya Ofisi na Makazi

ya Watumishi Balozini pamoja na kuwapatia vitendea kazi vya kisasa; na

xiii) Serikali kulipa uzito unaostahiki suala la kukamilisha upatikanaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ili kuwa na Dira na mwelekeo unaoendana na hali ya kisasa ya Diplomasia ya Kiuchumi Duniani;

xiv) Serikali ione umuhimu wa kuwa na Maafisa wenye taaluma ya masuala ya Mambo ya Nje (Foreign Service Officers) katika Balozi zetu ili kuwa na ufanisi katika Utekelezaji wa majukumu ya Balozi. Aidha, Balozi ziwe na waambata wa uchumi ili kuboresha dhana ya Diplomasia ya Uchumi katika Balozi zetu;

xv) Serikali itekeleze utaratibu wa "Rotation" ya watumishi katika balozi zetu ili kuondoa hali ya baadhi ya maafisa kukaa katika Ubalozi mmoja kwa muda mrefu na kupunguza ufanisi wa kazi kutokana na mazoea; na

xvi) Serikali ithamini umuhimu wa Diaspora katika kuchangia na kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kuwapa fursa mbali mbali za kiuchumi kisheria.

## 6.0HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Namshukuru pia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mahiga, (Mb) kwa ushirikiano alioutoa wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza kazi zake.

Aidha, Namshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba, (Mb) na Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Aziz Mlima na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan Muombwa Mwinyi pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii walioshiriki kutoa ufafanuzi uliotakiwa na Kamati wakati wa vikao.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, Kujadili na Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini michango yao, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb, "
5. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb "
6. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb, "
7. Mhe. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb, "
8. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb, "
9. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb, "
10. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb, "
11. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb, "
12. Mhe. Machano Othman Said, Mb, "
13. Mhe. Cosato David Chumi, Mb, "
14. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb, "
15. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb, "
16. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb, "
17. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb, "
18. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb, "
19. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb, "
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb, "
21. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb, "
22. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb "
23. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb "
24. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb, "
25. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb "
26. Mhe. Yahaya Omari Masare, Mb "
27. Mhe. Stephen J. Masele, Mb, "
28. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb "

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile nawashukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndugu Angelina Sanga pamoja na

wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuhakikisha kuwa Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mwisho, lakini si kwa umuhimu nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Issa Abdallah na Ndugu Grace Bidya wakisaidiwa na Ndugu Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii pamoja na kuyajadili na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii **Fungu 34** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja kabla yangu.

**Mheshmiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hii ni hotuba yangu ya pili nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Leo tunajadili bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ya Wizara hii, nikiwa sijaridhishwa hata kidogo kwa kiwango cha usikivu ulioonesha na Serikali hii katika kutekeleza masuala mengi ya msingi, ambayo Kambi ya Upinzani iliyashauri mwaka 2016 tukiwa na nia njema kabisa ya kulinyanyua Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taifa letu liweze kupiga hatua kubwa sana kimaendeleo, ni muhimu sana viongozi

wa Serikali na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wakazingatia ushauri huu aliowahi kuutoa mwanazuoni wa Korea ya Kusini na kwa sasa ni Rais wa Benki ya dunia, Jim Yong Kim; alisema: ***"**No matter how good you think you are, as a leader, my goodness, the people around you will have all kinds of ideas for how you can get better. So for me, the most fundamental thing about leadership is to have the humility to continue to get feedback and to try to get better because your job is to try to help everybody else to get better." (Makofi)*

"Haijalishi unajiona bora kiasi gani kama kiongozi ndugu yangu, watu walio karibu nawe bado watakuwa na kila aina ya mawazo ya jinsi ya kukufanya uwe bora. Kwa hiyo, kwangu mimi, jambo la msingi kabisa kuliko yote katika uongozi ni kuwa na ustahimilivu wa kuendelea kupokea maoni na kujaribu kuwa bora zaidi kwa sababu kazi yako ni kujaribu kumsaidia kila mtu awe bora." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufike wakati sasa tutoke kwenye *hangover* yaani mawenge ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ili tuweze kuunganisha fikra zetu kwa faida ya nchi yetu. Haki na upendo huinua Taifa. Tuna Tanzania ya kujenga, tuna vizazi vya kurithi, wakati wa kuendekeza ujuaji, ubaguzi, dharau na vijembe visivyo na msingi sasa ni heri ukafikia kikomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kujali itikadi za vyama vyetu, namwomba sana Mwenyezi Mungu Baba aliye juu atujalie busara za kusikilizana zaidi, kuheshimiana zaidi na kukubali kuunganisha fikra zetu kwa manufaa ya Taifa letu. Kama alivyotujalia pumzi hata tukaifikia siku hii ya leo, basi na atujalie pia baraka za Kitaifa ili tuweze kuyaona machweo ya ndoto njema za Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru watu wangu wa nguvu wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kuendelea kuniamini na kunipa jeuri ya kufanya kila lililo jema kwa ajili yao na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzito wa kipekee, namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe; Mheshimiwa Riziki Shahari, Naibu Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote wa Kambi nzima ya Upinzani; Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Umoja wa UKAWA kwa imani kubwa wanayoendelea kuwa nayo kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbuke Kissa Msigwa, Mama Mchungaji huyu, mke na rafiki yangu kipenzi; ndiye aliye nyuma ya mbwembwe zangu, ari na kasi kubwa niliyonayo katika kuutumikia umma wa Wana-Iringa na Watanzania wote bila kuchoka. Namshukuru sana mama huyu na watoto wangu wote kwa kuendelea kuwa nami bega kwa bega bila kujali muda mwingi wanaonikosa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa hotuba hii imebeba maono na mwelekeo mpya juu ya namna bora zaidi ya kutimiza dira na dhima ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa maendeleo ya haraka ya Taifa letu. Kauli mbiu ya hotuba hii ni Tufikiri Tofauti, Tupange Tofauti na Tutende Tofauti; Tanzania ya Tofauti Inakuja." Ni imani yangu kuwa nitapewa usikivu wa kutosha kutoka kwa Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na dira kuu ya Sera mpya ya Mambo ya Nje. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kwa mujibu wa dira hii, ndiyo inayopaswa kuwa mshawishi mkuu wa maslahi ya kiuchumi na maslahi mengine ya Tanzania kupitia ushirikiano na utengamano wetu na nchi, makampuni, taasisi na jumuiya mbalimbali za Kimataifa na Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuifikia dira hii, Wizara inapaswa, pamoja na mambo mengine, kutumia mikakati ya diplomasia ya uchumi katika kuvutia fursa za kiuchumi

kwa maslahi ya nchi yetu. Kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka 2016, hizi ni zama mpya. Kama diplomasia ya kizamani ililenga zaidi kutafuta ukombozi, kulinda uhuru, mamlaka na amani ya nchi, basi diplomasia ya uchumi inalenga zaidi ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, diplomasia ya uchumi, pamoja na mambo mengine, inahusu kuvutia fursa za uwekezaji wa kigeni *(foreign investments),* utalii na biashara huria *(free trade)* kwa kufanya ushawishi wenye kufungua masoko mapya ya kuuzia bidhaa za Kitanzania; kupunguza au kuondoa masharti ya kikodi; na kusaidia wafanyabiashara na wawekezaji wa Kitanzania kuzitumia kikamilifu fursa za kiuchumi zinazopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hotuba yangu ya mwaka 2016 ilizungumzia jinsi Serikali ya CCM ilivyoshindwa kabisa kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita, mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu Tano madarakani nao uliendelea kudumisha udhaifu ule ule wa Serikali za CCM ambao umekuwepo siku zote. Hakuna jitihada zozote za msingi zilizofanyika ili kujenga uwezo na ushawishi wa Serikali katika diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Kambi ya Upinzani hivi karibuni, umebaini kuwa kuna sababu kuu mbili zinazoifanya Serikali ya Tanzania ifanye vibaya kwenye diplomasia ya uchumi.

Kwanza, ukiondoa Sera ya Mambo ya Nje inayotoa tamko la jumla tu kwamba diplomasia ya uchumi ndiyo kipaumbele kikuu cha Sera ya Mambo ya Nje, Tanzania haina ajenda ya Taifa juu ya Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, Tanzania haina ajenda ya Taifa juu ya Diplomasia ya Uchumi wala mipango mikakati inayopimika *(strategic plans)* ambayo ingebeba vipaumbele mahsusi *(specific priorities)* juu ya nini hasa tunakitafuta kwenye kila Taifa tunaloshirikiana nalo kwa maslahi yetu ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuendelee ni lazima Serikali hii ikubali kufikiri tofauti, kupanga tofauti na kutenda tofauti. Ni lazima Serikali hii ikubali kusikia na kujifunza kutoka kwenye akili kubwa, kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani na kutoka kwenye Mataifa yaliyofanikiwa sana kwenye medani za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nawapeleka kidogo Australia. Australia ni moja ya Mataifa yenye uchumi mkubwa sana duniani. Sababu kuu ya kufanikiwa kwa Taifa hili ni kutekeleza kwa umahiri na weledi mkubwa diplomasia ya uchumi. Mathalani, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2016 thamani ya biashara ya nje ambayo Australia inafanya na nchi mbalimbali duniani ilikuwa ni sawa na asilimia 41 ya Pato lote la Taifa *(GDP)* la nchi hiyo na hii ni takwimu ambayo haijawahi kuporomoka tangu mwaka 1900. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akizungumzia mafanikio ya nchi yake kwenye diplomasia ya uchumi, Mwanadiplomasia mbobezi, mahiri na Waziri wa 38 wa Mambo ya Nje wa Australia, Julie Bishop alisema kuwa nchi yake imefanikiwa katika diplomasia ya uchumi kwa sababu ya kuwa na mipango mikakati inayotekelezeka na yenye malengo na vipaumbele mahsusi juu ya diplomasia gani ifanyike kwenye kila nchi kati ya nchi zote 95 zenye Ubalozi wa Australia duniani. Mpango mkakati wa kila ubalozi unatoa mwongozo wa jinsi gani wanadiplomasia wa Australia watachochea ushirikiano wa kibiashara, kiuchumi na kiuwekezaji kwa niaba ya Taifa lao kwenye nchi walizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya Australia, jirani zetu wa Kenya nao wana mipango mikakati iliyo bora ya kutekeleza diplomasia ya uchumi kwenye balozi zao. Mfano mzuri ni mpango mkakati wa Ubalozi wa Kenya mjini Cairo Misri ambao umeainisha vipaumbele mahsusi na kueleza kinagaubaga nini hasa Kenya inalenga kukipata kwa ushirikiano wake na Misri? Hapa ndipo udhaifu wa kwanza wa Tanzania ulipo. Serikali ya CCM haina mipango bora inayoweza kutekelezeka wala kupimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ya nchi yetu kutopata mafanikio ya kuridhisha, ni uhaba wa wanadiplomasia wenye weledi na umahiri kwenye diplomasia ya uchumi. Hatua ya Serikali kuteua Mabalozi wa nchi za nje kwa kuzingatia zaidi u-CCM wao badala ya utalaam, uzoefu na umahiri wao kwenye diplomasia ya uchumi utaendelea kuikwamisha nchi kwa miaka mingi zaidi ikiwemo Serikali kutokubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 Kambi ya Upinzani tulieleza jinsi Wizara ilivyoshindwa kwa muda mrefu kutoa mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa idadi ya kutosha ya maofisa wake. Tulisema, wakati Tanzania ikiwa na Ofisi za Ubalozi kwenye nchi 35 duniani, hadi kufikia mwezi Mei, 2015 ni watumishi 32 tu ndio waliokuwa wamehitimu mafunzo ya muda mfupi ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kuwa hata baada ya Kambi ya Upinzani kueleza upungufu huo, bado Wizara haikuchukua hatua madhubuti za kumaliza tatizo hili. Sehemu ya Taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tarehe 17 Januari, 2017, pamoja na mambo mengine, ilisema, nami nanukuu:

“Wizara imejiwekea mikakati mbalimbali katika kuhakikisha inatekeleza ipasavyo diplomasia ya uchumi. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutafuta fursa mbalimbali za mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa watumishi wa Wizara katika nchi marafiki; kutafuta fursa za ufadhili wa masomo za muda mfupi na muda mrefu kutoka nchi mbalimbali; kushirikisha Maafisa katika makongamano na mikutano mbalimbali ya biashara na uwekezaji ili kuwajengea uwezo.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ya Wizara inathibitisha jinsi Serikali isivyokuwa na umakini na inavyofanya mzaha na diplomasia ya uchumi hasa ukitilia maanani ufafanuzi ufuatao:-

Moja, maelezo ya Wizara yanathibitisha kuwa Serikali haijajipanga kabisa kufundisha watumishi yake yenyewe na badala yake inategemea kuokoteza fursa za kupeleka watumishi wake wakafundishwe diplomasia ya uchumi kwenye nchi rafiki kwa kadri zitakavyopatikana.

Pili, maelezo ya Wizara yanathibitisha kuwa Serikali haioni hata umuhimu wa kupanga bajeti ya kugharamia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ya diplomasia ya uchumi na badala yake inategemea kutafuta ufadhili. Kama ufadhili usipopatikana, basi hii nchi itaendelea kupoteza fursa nyingi za kiuchumi zilizopo duniani kwa sababu tu ya kuchelewa kuwa na wataalam wenye ujuzi wa diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo hayo ya Wizara yanathibitisha kuwa kumbe Wizara inafanya mzaha kazini, maana hupeleka watumishi mbumbumbu kwenye makongamano na mikutano nyeti ya biashara na uwekezaji, eti tu wakajifunze nini maana ya diplomasia ya uchumi. Wakati Serikali yetu inafanya hivyo, Mataifa mengine hupeleka wanadiplomasia waliobobea kwenda kunadi fursa za kiuchumi na kuvutia uwekezaji wa biashara katika nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kutokana na maelezo hayo, Wizara nzima sasa inatutia mashaka makubwa juu ya weledi ilionao kwenye diplomasia ya uchumi. Ni hatari kutegemea elimu ya nje pekee katika kuwapa mafunzo watumishi wa Wizara kwa sababu ajenda za nchi ni tofauti. Kwa kawaida mafunzo makini juu ya diplomasia ya uchumi huenda pamoja mafunzo juu ya ajenda mahsusi ya diplomasia ya uchumi inayoongoza nchi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi iliyotokana na diplomasia ya uchumi, Wizara imedai kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tarehe 17 Januari, 2017,

imeyataja mafanikio hayo kuwa ni kuishawishi Serikali ya Uganda kupitisha bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga; na kuishawishi Benki ya *Exim* ya China kuwa tayari kutoa mkopo wa kujenga Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa *(standard gauge).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa hiyo ya Wizara, baadaye zilitolewa taarifa kuwa Serikali imepata mkopo wa ujenzi wa reli hiyo kutoka Uturuki na siyo tena kutoka Benki ya *Exim* ya China. Aidha, kwa maneno ya Mkuu wa nchi ni kuwa fedha za ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge* ni fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haina tatizo na mafanikio hayo na mengineyo yaliyoelezwa na Wizara, pamoja na taarifa za kukinzana kuhusu fedha zitakazogharamia ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa. Kimsingi, huwa tunafarijika kila tunapoona jambo jema linatokea ndani ya nchi yetu.

Hata hivyo, ni ukweli ulio dhahiri kuwa mafanikio yaliyoelezwa, bado ni finyu mno ikilinganishwa na fursa nyingi za kiuwekezaji, kitalii na kibiashara ambazo Tanzania inazo kulingana na jiografia yake, raslimali na mahitaji ya watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, diplomasia ya uchumi iliyofanikiwa ni ile inayojibu mahitaji ya ndani ya nchi husika. Wakati Tanzania ikiwa na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, ikiwa ni pamoja na eneo kubwa linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji; na wakati zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wakiwa wamejiajiri kwenye kilimo duni cha jembe la mkono kisichotumia teknolojia wala mbinu za kisasa, bado mpaka sasa hakuna uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya kilimo. Sekta hii ndiyo inayoweza kuajiri Watanzania wengi na kuchangia sehemu kubwa ya pato la Taifa, yaani *GDP*. Kwa namna yoyote ile mafanikio ya Serikali katika diplomasia ya

uchumi yalipaswa yaonekane kwanza kwenye kuvutia uwekezaji na biashara kwenye sekta hii ya kilimo pengine kuliko kwenye sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikijinasibu kujenga uchumi wa viwanda, bado sehemu kubwa ya nchi hii haina viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya kilimo na mifugo *(agro-processing industries).* Sababu kuu ni ukosefu wa mitaji, teknolojia na miundombinu. Hata hivyo, mahitaji yote haya ya kusukuma uchumi wa viwanda yangeweza kupatikana ndani na nje ya mipaka yetu kama Serikali ingeweza kutekeleza kwa ufanisi Sera ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, tathmini yetu inaonesha kuwa yale ambayo Wizara imekuwa ikidai kuwa ni mafanikio ya juhudi zake kwa kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ya Diplomasia ya Uchumi," kumbe wakati mwingine huwa ni juhudi binafsi tu za nchi za nje au Makampuni ya Kimataifa ambayo hujileta yenyewe kwa msukumo wa maono *(vision)* waliyonayo na ajenda zao za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, taarifa za Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* zinaonyesha kuwa muitikio wa miaka ya hivi karibuni wa makampuni ya nje kuja kuwekeza nchini umechagizwa zaidi na fursa ya Sekta ya Madini na ugunduzi wa gesi. Hali hii inaashiria kuwa ukiondoa vivutio vya gesi, madini na uwindaji wa kitalii kwa kiasi fulani ambavyo vimekuwa vikiwavuta wawekezaji moja kwa moja, bado Serikali imekuwa haina ajenda wala umahiri wowote wa kuvutia uwekezaji kwenye Sekta nyingine zisizo na mvuto wa moja kwa moja kwa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo siri ya Serikali kushindwa kuvutia uwekezaji wa kuridhisha kwenye Sekta Kilimo na ya viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya kilimo na mifugo *(agro-processing indurstries).* Uwezo wa Wizara kutekeleza mikakati ya diplomasia ya uchumi umeishia kwenye kusubiria fursa zitufuate tu kuliko kuzitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** wataalamu wa diplomasia ya Uchumi hupenda kuzisitiza, napenda kunukuu: "*economic diplomacy is more than soliciting economic opportunities with your country's agenda than just waiting for foreign counterparts to advance their agenda through you."* Diplomasia ya Uchumi ni kuhusu zaidi kufukuzia fursa za kiuchumi ukiongozwa na ajenda ya nchi yako kuliko kusubiria tu nchi rafiki zikufuate zikiwa na ajenda zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kuwa nchi zote zilizofanikiwa kwenye diplomasia ya uchumi duniani kama Australia na India ni zile zilizojituma kufukuzia fursa kwenye nchi nyingine, zikiongozwa na ajenda mahsusi kwa maslahi ya raia wao. Siyo jambo la kujivunia hata kidogo kumwona Mwanadiplomasia wetu namba moja akifanya kazi ya kupokea Viongozi Wakuu wa nchi nyingine tu huku Serikali yetu ikiwa haijitumi vya kutosha kufukuzia fursa kwenye mataifa mengine*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji makini wa Sera ya Mambo ya Nje hususan Diplomasia ya Uchumi unaweza kuleta tija kubwa katika kuharakisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema: "Kwa jinsi tulivyoachwa nyuma, Watanzania tunapaswa kukimbia wakati wenzetu wakiwa wanatembea." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mataifa makubwa duniani, kama Australia, Marekani, China na hata India, yakizidi kupiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa kujiimarisha kwenye diplomasia ya uchumi, Tanzania yetu masikini lakini yenye fursa kubwa za utajiri, haina budi kuchukua hatua madhubuti na za haraka za kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na Sera ya Mambo ya Nje kwa ujumla, Kambi ya Upinzani kwa kujali maslahi ya mapana ya Tanzania yetu, inaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali itengeneze Agenda ya Taifa ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania yenye kuainisha malengo na vipaumbele vinavyopimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, Serikali itengeneze Agenda ya Taifa ya Diplomasia ya Uchumi yenye kuainisha malengo na vipaumbele vinavyopimika. Hapa Kambi ya Upinzani inashauri zaidi kuwa sekta ya kilimo, Nishati ya Umeme Vijijini na ile ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo *(agro-processing industries),* ndizo zipewe kipaumbele kikubwa katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kwa mitaji ya nje *(direct foreign investments)* na teknolojia kwa maendeleo ya sekta hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Agenda ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania isijikite tu kwenye Balozi, bali pia ibebe masuala ya kipaumbele ya kufanyiwa kazi kidiplomasia hadi kwenye Jumuiya za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa pendekezo hili ni mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania imekuwa ikishiriki kwenye *EAC, SADC* na jumuiya nyingine za kikanda bila hata kuwa na Sera ya Utengamano wala ajenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wizara ihakikishe kuwa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania kwenye nchi zote 35 duniani, zinakuwa na mipango mikakati ya diplomasia ya uchumi *(strategic plan)* uliojikita kwenye matokeo *(result-based)* na unaoweza kutekelezeka na kupimika ndani ya vipindi vifupi na vipindi virefu vya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mipango mikakati ya kila Ubalozi iunganishwe na kuwa na mpango kabambe mmoja wa Wizara. Huu ujikite zaidi kwenye kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa Balozi zote na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, mpango huu wa Wizara uweke malengo ya muda

mrefu na ya muda mfupi ya kuandaa wanadiplomasia waliobobea kwenye fani ya diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wizara ikishirikiana na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ifanye mapitio upya juu ya uhalisia wa lengo la kuongeza uwekezaji moja kwa moja wa kigeni *(Foreign Direct Investment - FDI)* nchini kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.5 za mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni tano, ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa Kambi ya Upinzani umebaini kuwa lengo lililowekwa na *TIC* ni dogo sana ikilinganishwa na fursa kubwa zilizopo za Tanzania kupata *FDI* kubwa zaidi kama Serikali itaacha mzaha kwenye kutekeleza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo msemo usemao: “Mafanikio ni kama maji ya bahari, tatizo ni kwamba baadhi yetu tunapokwenda kuyachota huwa tunakwenda na vijiko.” Lengo dogo la kufikia *FDI* ya dola bilioni tano mwaka 2020 linaweza kabisa likaifanya Tanzania kuendelea kufanya jitihada ndogo kwenye diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, lengo hilo dogo la *TIC* lipo mbali sana na ndoto ya Tanzania ya kutaka kuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Ukweli ni kwamba nchi zote zilizopo kwenye uchumi wa kati huwa zina sifa ya kupata *FDI* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema ikakumbukwa kuwa mwaka 2014, Tanzania ilipokea jumla ya wawekezaji wa mitaji ya moja kwa moja ya kigeni *(FDI)* ya thamani ya dola bilioni mbili za Kimarekani. Hii inaashiria kuwa Tanzania inaweza kabisa kupata zaidi ya dola bilioni tano za Kimarekani ifikapo mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa ipo miradi ya maendeleo ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambayo hugharamiwa na washirika ndani ya Jumuiya moja kwa moja na wadau mbalimbali

duniani hasa Umoja wa Ulaya. Gazeti la *The Citizen* la tarehe 17 Mei, 2017 ukurasa wa 15 liliripoti kuwa Jumuiya ya Afrika imekumbwa na tatizo uhaba wa fedha za kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo hugharamiwa na Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa suala la kuchangia miradi ya maendeleo lipo kwa mujibu mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, bado michango ya kifedha kwa baadhi ya nchi washirika ndani ya Jumuiya hiyo, imekuwa haitolewi kwa ukamilifu ikiwemo nchi yetu. Ieleweke kuwa Ibara ya 132(4) inaelekeza kuwa bajeti kwa ajili ya jumuiya zitachangiwa kwa usawa na nchi washirika ndani ya jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana wazi kuwa nchi wanachama zinaanza kugawanyika kuhusu utaratibu wa kuchangia miradi ya maendeleo ambapo nchi kama Burundi inaona kuwa haiwezi kuchangia sawa na nyingine kutokana na matatizo yake ya ndani. Hata hivyo, baadhi ya nchi kama Tanzania zimekuwa hazitoi fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati, hivyo kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kuwa kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ya jumuiya ni takriban dola milioni 101.6 ambapo kila nchi hutakiwa kuchangia kiasi cha dola milioni 8.3 za Kimarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu, 2017 ni nchi ya Kenya pekee ambayo imetoa mchango wake kwenye bajeti ya maendeleo kwa 100% ikifuatiwa na Uganda 90%, Rwanda 51%, Tanzania 35% *and we call ourselves big brother* na Burundi 0%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haishangai kuona Tanzania imetoa 35% ya bajeti ya miradi ya maendeleo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu hata kwenye miradi ya maendeleo ya ndani katika Wizara mbalimbali Serikali haiweki msisitizo kutoa fedha za miradi ya maendeleo. Ndiyo maana baadhi ya Wizara bajeti

ya miradi ya maendeleo ilitolewa kwa kiasi kidogo, mathalan Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika sekta ya kilimo ni 3% pekee fedha za maendeleo ndizo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Mei, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kuwa miradi ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inanufaisha pia nchi yetu kama moja ya nchi washirika ndani ya Jumuiya. Tanzania imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa Jumuiya wa Afrika kuwa moja ya nchi ambayo mara kwa mara imekuwa kikwazo cha maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa haiwi kikwazo kwa kazi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hasa kwenye miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu sababu za kutotoa fedha hizo za miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa iwapo Wizara hii, na hapa nakwenda kuhitimisha na Serikali hii kwa pamoja wataacha ujuaji na kuamua kufanya kazi kwa ushauri tunaoutoa, watafikiri tofauti, kupanga tofauti na hatimaye kutenda tofauti. *(Makofi)*

Ikiwa kila mtumishi wa Wizara hii ataachana na utendaji wa mazoea wa Serikali za CCM, *business as usual,* basi Tanzania kwa mara ya kwanza tutashuhudia Tanzania iliyo tofauti, yenye kupiga kasi kubwa ya kimaendeleo ambayo haijapata kutokea ndani ya historia na uhai wa Taifa hili. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu yote irekodiwe kwenye *Hansard* na yale ambayo sijayasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA PETER SIMON MSIGWA KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

**(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hotuba yangu ya pili nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Leo tunajadili bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 ya wizara hii, nikiwa sijaridhishwa hata kidogo na kiwango cha usikivu ulionyeshwa na serikali hii katika kutekeleza masuala mengi ya msingi, ambayo kambi ya upinzani iliyashauri mwaka jana kwa nia njema kabisa ya kulinyanyua Taifa!

**Mheshimiwa Spika,** ili Taifa letu liweze kupiga hatua kubwa sana kimaendeleo, ni muhimu sana viongozi wa serikali na wabunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wakazingatia ushauri huu aliowahi kuutoa mwanazuoni wa Korea ya Kusini, Jim Yong Kim; alisema, nanukuu:

***"No matter how good you think you are; as a leader, my goodness, the people around you will have all kinds of ideas for how you can get better. So for me, the most fundamental thing about leadership is to have the humility to continue to get feedback and to try to get better - because your job is to try to help everybody else get better",*** mwisho wa kunukuu.

***"Haijalishi unajiona bora kiasi gani kama Kiongozi, Ndugu yangu, watu walio karibu nawe bado watakuwa na kila aina ya mawazo ya jinsi ya kukufanya uwe bora. Kwa hiyo, kwangu Mimi, jambo la msingi kabisa kuliko yote katika uongozi ni kuwa na ustahimilivu wa kuendelea kupokea maoni na kujaribu kuwa bora zaidi – kwasababu kazi yako ni kujaribu kumsaidia kila mtu awe na maisha bora."***

**Mheshimiwa Spika,** ufike wakati sasa tutoke kwenye ***"hangover"*** (mawenge) ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015" ili tuweze kuunganisha fikra zetu kwa faida ya nchi yetu. Haki na upendo huinua Taifa. Tuna Tanzania ya kujenga na tuna vizazi vya kuturithi. Wakati wa kuendekeza ujuaji, ubaguzi, dharau na vijembe visivyo na msingi sasa ni kheri ukafikia kikomo.

**Mheshimiwa Spika**, bila kujali itikadi za vyama vyetu, namuomba sana Mwenyezi Mungu Baba Aliye Juu atujalie busara ya kusikilizana zaidi, kuheshimiana zaidi na kukubali kuunganisha fikra zetu kwa manufaa ya Taifa letu. Kama alivyotujalia pumzi hata tukaifikia siku hii ya leo, basi na atujalie pia baraka za kitaifa ili tuweze kuyaona machweo ya ndoto njema za Tanzania yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kuwashukuru watu wangu wa nguvu wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kuendelea kuniamini na kunipa jeuri ya kufanya kila lililo jema kwaajili yao na Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uzito wa kipekee, namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mhe. Freeman Mbowe (Mb), Mheshimiwa Riziki Shahari (Mb)- Naibu Waziri Kivuli pamoja na wabunge wenzangu wote wa kambi nzima ya upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Umoja wa UKAWA, kwa imani kubwa wanayoendelea kuwa nayo kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** nimkumbuke Kissa Msigwa - Mama Mchungaji huyu, Mke na Rafiki yangu kipenzi. Ndiye aliye nyuma ya mbwembwe zangu, ari na kasi kubwa niliyonayo katika kuutumikia umma wa Wana-Iringa na Watanzania wote bila kuchoka. Namshukuru sana Mama huyu na watoto wangu wote kwa kuendelea kuwa nami bega kwa bega bila kujali muda mwingi wanaonikosa nyumbani.

**Mheshimiwa Spika**, ni imani yangu kuwa hotuba hii imebeba maono na mwelekeo mpya juu ya namna bora zaidi ya kutimiza dira na dhima ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kwa maendeleo ya haraka ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Kauli mbiu ya hotuba hii ni ***Tufikiri Tofauti, Tupange Tofauti na Tutende Tofauti; Tanzania ya Tofauti inakuja.*** Ni imani yangu kuwa nitapewa usikivu wa kutosha kutoka kwa Bunge lako tukufu.

## 2.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA SERA YA DIPLOMASIA YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** nianze na dira kuu ya sera mpya ya mambo ya nje: ***"Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kwa mujibu wa dira hii, ndiyo inayopaswa kuwa mshawishi mkuu wa maslahi ya kiuchumi na maslahi mengine ya Tanzania kupitia ushirikiano na utengamano wetu na nchi, makampuni, taasisi na jumuiya mbalimbali za kimataifa na kikanda."***

**Mheshimiwa Spika,** ili kuifikia dira hii wizara inapaswa, pamoja na mambo mengine, kutumia mikakati ya diplomasia ya uchumi katika kuvutia fursa za kiuchumi kwa maslahi ya nchi yetu. Kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka jana, hizi ni zama mpya. ***Kama diplomasia ya kizamani ililenga zaidi kutafuta ukombozi, kulinda uhuru, mamlaka na amani ya nchi, basi diplomasia ya uchumi inalenga zaidi ustawi.***

**Mheshimiwa Spika,** diplomasia ya uchumi, pamoja na mambo mengine, inahusu kuvutia fursa za uwekezaji wa kigeni (foreign investments), utalii (tourism) na biashara huria (free trade) kwa kufanya ushawishi wenye kufungua masoko mapya ya kuuzia bidhaa za Kitanzania; kupunguza au kuondoa masharti ya kikodi; na kusaidia wafanyabiashara na wawekezaji wa Kitanzania kuzitumia kikamilifu fursa za kiuchumi zinazopatikana.

**Mheshimiwa Spika,** wakati hotuba yangu ya mwaka jana ilizungumzia jinsi serikali ya CCM ilivyoshindwa kabisa kutekeleza sera ya diplomasia ya uchumi kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita; mwaka mmoja wa serikali ya awamu tano madarakani nao uliendelea kudumisha udhaifu ule ule wa serikali za CCM ambao umekuwepo siku zote. Hakuna jitihada zozote za msingi zilizofanyika ili kujenga uwezo na ushawishi wa serikali katika diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** utafiti uliofanywa na kambi ya upinzani hivi karibuni umebaini kuwa kuna sababu kuu mbili zinazoifanya serikali ya Tanzania ifanye vibaya kwenye diplomasia ya uchumi:

**Mheshimiwa Spika,** kwanza, ukiondoa sera ya mambo ya nje inayotoa tamko la jumla tu kwamba ***"diplomasia ya uchumi ndio kipaumbele kikuu cha sera ya mambo ya nje***"; Tanzania haina ajenda ya taifa juu ya diplomasia ya uchumi wala mipango mikakati inayopimika (strategic plans) ambayo ingebeba vipaumbele mahsusi (specific priorities) juu ya nini hasa tunakitafuta kwenye kila taifa tunaloshirikiana nalo kwa maslahi yetu ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** ili tuendelee ni lazima serikali hii ikubali kufikiri tofauti, kupanga tofauti na kutenda tofauti. Ni lazima serikali hii ikubali kusikia na kujifunza kutoka kwenye ***"akili kubwa"*** – kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani na kutoka kwenye mataifa yaliyofanikiwa sana kwenye medani za kimataifa. Leo nawapeleka kidogo Australia!

**Mheshimiwa Spika,** Australia ni moja ya mataifa yenye uchumi mkubwa sana duniani. Sababu kuu ya kufanikiwa kwa taifa hili ni kutekeleza kwa umahiri na weledi mkubwa diplomasia ya uchumi. Mathalan, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana (2016) thamani ya biashara ya nje ambayo Australia inafanya na nchi mbalimbali duniani ilikuwa ni sawa na asilimia 41 ya pato lote la taifa (GDP) la taifa hilo; na hii ni takwimu ambayo haijawahi kuporomoka tangu mwaka 1,900.

**Mheshimiwa Spika,** akizungumzia mafanikio ya nchi yake kwenye diplomasia ya uchumi, Mwanadiplomasia mahiri na waziri wa 38 wa Australia – Julie Bishop – alisema kuwa nchi yake imefanikiwa katika diplomasia ya uchumi kwasababu ya kuwa na mipango mikakati inayotekelezeka na yenye malengo na vipaumbele mahsusi juu ya diplomasia gani ifanyike kwenye kila nchi kati ya nchi zote 95 zenye ubalozi wa Australia duniani. Mpango mkakati wa kila ubalozi unatoa muongozo wa jinsi gani wanadiplomasia wa Australia watachochea ushirikiano wa kibiashara, kiuchumi na kiuwekezaji kwa niaba ya taifa lao kwenye nchi walizopo**.**

**Mheshimiwa Spika,** mbali ya Australia, jirani zetu wa Kenya nao wana mipango mikakati iliyo bora ya kutekeleza diplomasia ya uchumi kwenye balozi zao. Mfano mzuri ni mpango mkakati wa ubalozi wa Kenya mjini Cairo Misri ambao umeainisha vipaumbele mahsusi na kueleza kinaga-ubaga nini hasa Kenya inalenga kukipata kwa ushirikiano wake na Misri. Hapa ndipo udhaifu wa kwanza wa Tanzania ulipo. Serikali ya CCM haina mipango bora inayoweza kutekelezeka na kupimika.

**Mheshimiwa Spika**, sababu ya pili ya nchi yetu kutopata mafanikio ya kuridhisha ni uhaba wa wanadiplomasia wenye weledi na umahiri kwenye diplomasia ya uchumi. Hatua ya serikali kuteua mabalozi wa nchi za nje kwa kuzingatia zaidi u-CCM wao badala ya utalaam, uzoefu na umahiri wao kwenye diplomasia ya uchumi itaendelea kuikwamisha nchi kwa miaka mingi zaidi ikiwa serikali haitabadilika.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka jana Kambi ya Upinzani tulieleza jinsi Wizara ilivyoshindwa kwa muda mrefu kutoa mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa idadi ya kutosha ya maofisa wake. Tulisema, wakati Tanzania ikiwa na ofisi za ubalozi kwenye nchi 35 duniani, hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2015 ni watumishi 32 tu ndio waliokuwa wamehitimu mafunzo ya muda mfupi ya diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** cha kusikitisha zaidi ni kuwa hata baada ya kambi ya upinzani kueleza mapungufu hayo, bado wizara haikuchukua hatua madhubuti za kumaliza tatizo hili. Sehemu ya Taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Januari 17 mwaka huu, pamoja na mambo mengine, ilisema, nanukuu:

"***Wizara imejiwekea mikakati mbalimbali katika kuhakikisha inatekeleza ipasavyo diplomasia ya uchumi. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutafuta fursa mbalimbali za mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa watumishi wa wizara katika nchi marafiki; kutafuta fursa za ufadhili wa masomo za muda mfupi na muda mrefu kutoka nchi mbalimbali; kushirikisha maafisa katika makongamano na mikutano mbalimbali ya biashara na uwekezaji ili kuwajengea uwezo."*** mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hiyo ya Wizara inathibitisha jinsi serikali isivyokuwa na umakini na inavyofanya mzaha na diplomasia ya uchumi, hasa ukitilia maanani ufafanuzi ufuatao;

- Maelezo ya Wizara yanathibitisha kuwa seriakali haijajipanga kabisa kufundisha watumishi yake yenyewe na badala yake inategemea kuokoteza fursa za kupeleka watumishi wake wakafundishwe diplomasia ya uchumi kwenye nchi rafiki kwa kadri zitakavyopatikana.

- Yanathibitisha kuwa Wizara haioni hata umuhimu wa kupanga bajeti ya kugharamia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ya diplomasia ya uchumi na badala yake itatafuta ufadhili. Kama ufadhili usipopatikana basi nchi itaendelea kupoteza fursa nyingi za kiuchumi zilizopo duniani kwasababu tu ya kuchelewa kuwa na wataalam wenye ujuzi wa diplomasia ya uchumi.

- Maelezo hayo ya wizara yanathibitisha kuwa kumbe Wizara inafanya ***"mzaha kazini"*** maana hupeleka

watumishi mbumbu kwenye makongamano na mikutano nyeti ya biashara na uwekezaji ili tu wakajifunze nini maana ya diplomasia ya uchumi, wakati mataifa mengine hupeleka wanadiplomasia wake waliobobea ambao sio tu hunadi maslahi ya kiuchumi ya nchi zao bali pia ndio na hujenga msingi wa kuvutia fursa za kiuwekezaji na kibiashara kwa nchi zao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla maelezo hayo, wizara nzima inatia shaka juu ya weledi ilionao kwenye diplomasia ya uchumi. Ni hatari kutegemea elimu ya nje pekee katika kuwapa mafunzo watumishi wa wizara wakati ajenda za nchi ni tofauti; mafunzo makini juu ya diplomasia ya uchumi huenda sanjari na kufundisha ajenda mahsusi ya nchi husika.

## 3.0 MIRADI ILIYOTOKANA NA DIPLOMASIA YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** wizara imedai kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tarehe 17 Januari 2017, imeyataja mafanikio hayo kuwa ni kuishawishi serikali ya Uganda kupitisha Bomba la Mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga; na kuishawishi Benki ya Exim ya China kuwa tayari kutoa mkopo wa kujenga Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge). Pamoja na taarifa hiyo ya Wizara, baadae zilitolewa taarifa kuwa serikali imepata mkopo wa ujenzi wa reli hiyo kutoka Uturuki na sio tena kutoka Benki ya Exim ya China, aidha kwa maneno ya Mkuu wa nchi ni kuwa fedha za ujenzi wa reli kwa kiwango cha standard gauge ni fedha zetu za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kambi ya upinzani haina tatizo na mafanikio haya na mengineyo yaliyoelezwa na wizara pamoja na taarifa za kukinza kuhusu fedha zitakazogharamia ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Kimsingi, huwa tunafarijika kila tunapoona jambo jema linatokea ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, ni ukweli ulio dhahiri kuwa mafanikio yaliyoelezwa, bado ni finyu mno ikilinganishwa na

fursa nyingi za kiuwekezaji, kitalii na kibiashara ambazo Tanzania inazo kulingana na jiografia yake, raslimali na mahitaji ya watu wake.

**Mheshimiwa Spika, 'diplomasia ya uchumi iliyofanikiwa ni ile inayojibu mahitaji ya ndani ya nchi husika'**. Wakati Tanzania ikiwa na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, ikiwa ni pamoja na eneo kubwa linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji; na wakati zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wakiwa wamejiajiri kwenye kilimo duni cha jembe la mkono kisichotumia teknolojia wala mbinu za kisasa...bado mpaka sasa hakuna uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye sekta ya kilimo!

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi ya kilimo. Na sekta hii ndiyo inayoweza kuajiri Watanzania wengi na kuchangia sehemu kubwa ya pato la taifa (GDP). Kwa namna yoyote ile mafanikio ya serikali katika diplomasia ya uchumi yalipaswa yaonekane kwanza kwenye kuvutia uwekezaji na biashara kwenye sekta hii pengine kuliko sekta nyingine yoyote ile.

**Mheshimiwa Spika,** wakati serikali ikijinasibu kujenga "uchumi wa viwanda", bado sehemu kubwa ya nchi haina viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya kilimo na mifugo (***Agro-processing industries***). Sababu kuu ni ukosefu wa mitaji, teknolojia, na miundombinu. Hata hivyo, mahitaji yote haya ya kusukuma uchumi wa viwanda yangeweza kupatikana ndani na nje ya mipaka ya nchi kama serikali ingeweza kutekeleza kwa ufanisi sera ya diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, tathmini yetu inaonyesha kuwa yale ambayo wizara imekuwa ikidai kuwa ni ***mafanikio ya juhudi zake za kutekeleza sera ya mambo ya nje na diplomasia ya uchumi"***, kumbe wakati mwingine huwa ni juhudi binafsi tu za nchi za nje au makampuni ya kimataifa ambayo hujileta yenyewe kwa msukumo wa maono (***vision***) na ajenda zao za kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano, taarifa za Kituo cha Uwekezaji (TIC) zinaonyesha kuwa mwitikio wa miaka ya hivi karibuni wa makampuni ya nje kuja kuwekeza nchini umechagizwa zaidi na sekta ya madini na ugunduzi wa gesi. Hali hii inaashiria kuwa ukiondoa vivutio vya gesi, madini na uwindaji wa kitalii kwa kiasi fulani, ambavyo vimekuwa vikiwavuta wawekezaji moja kwa moja, bado serikali imekuwa haina ajenda wala umahiri wowote wa kuvutia uwekezaji kwenye sekta nyingine zisizo na mvuto wa moja kwa moja kwa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** hii ndiyo siri ya serikali kushindwa kuvutia uwekezaji wa kuridhisha kwenye sekta kilimo na ya viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya kilimo na mifugo (***agro-processing indurstries***). Uwezo wa wizara kutekeleza mikakati ya diplomasia ya uchumi umeishia kwenye kusubiria fursa zitufuate tu kuliko kuzitafuta.

**Mheshimiwa Spika, economic diplomacy is more of soliciting economic opportunities with your country's agenda than just waiting for foreign counterparts to advance their agenda through you!** Kwamba, diplomasia ya uchumi inahusu zaidi kufukuzia fursa za kiuchumi ukiongozwa na ajenda ya nchi yako kuliko kusubiria tu nchi rafiki zikufuate zikiwa na ajenda zao.

**Mheshimiwa Spika,** uzoefu unaonyesha kuwa nchi zote zilizofanikiwa kwenye diplomasia ya uchumi duniani kama Australia na India ni zile zilizojituma kufukuzia fursa kwenye nchi nyingine, zikiongozwa na ajenda mahsusi kwa maslahi ya raia wao. Si jambo la kujivunia hata kidogo kumuona Mwanadiplomasia wetu namba moja (Rais) akifanya kazi ya kupokea viongozi wakuu wa nchi nyingine tu huku serikali yetu ikiwa haijitumi vya kutosha kufukuzia fursa kwenye mataifa mengine.

## 4.0 MAPENDEKEZO YA KUONGEZA UFANISI KWENYE UTEKELEZAJI WA SERA YA MAMBO YA NJE

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji makini wa sera ya mambo ya nje hususan diplomasia ya uchumi, unaweza

kuleta tija kubwa katika kuharakisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema: **"Kwa jinsi tulivyoachwa nyuma, Watanzania tunapaswa kukimbia wakati wenzetu wakiwa wanatembea".** Wakati mataifa makubwa duniani, kama Australia, Marekani, China na hata India, yakizidi kupiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa kujiimarisha kwenye diplomasia ya uchumi; Tanzania yetu maskini lakini yenye fursa kubwa za utajiri, haina budi kuchukua hatua madhubuti na za haraka za kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa weledi na umahiri wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na sera ya mambo ya nje kwa ujumla, Kambi ya Upinzani kwa kujali maslahi ya mapana ya Tanzania yetu, inaishauri serikali ifanye yafuatayo;

**Mheshimiwa Spika**, kwanza, serikali itengeneze Agenda ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania yenye kuanisha malengo na vipaumbele vinavyopimika. Hapa Kambi ya Upinzani inashauri zaidi kuwa sekta ya kilimo, nishati ya umeme vijijini na ile ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo (Agro-processing indurstries), ndizo zipewe kipaumbele kikubwa katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kwa mitaji ya nje (direct foreign investments) na teknolojia kwa maendeleo ya sekta hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Agenda ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania isijikite tu kwenye balozi, bali pia ibebe masuala ya kipaumbele ya kufanyiwa kazi kidiplomasia hadi kwenye jumuiya za kikanda, ikiwemo jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC). Hapa umuhimu wa pendekezo hili unazidi kuwa mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania imekuwa ikishiriki kwenye EAC, SADC na jumuiya nyingine za kikanda bila hata kuwa na sera ya utengamano.

**Mheshimiwa Spika,** pili, wizara ihakikishe kuwa ubalozi wa Tanzania kwenye zote 35 duniani unakuwa na mpango mkakati wa diplomasia ya uchumi ***(strategic plan)*** uliojikita kwenye matokeo ***(result-based)*** na unaoweza kutekelezeka

na kupimika ndani ya vipindi vifupi na vipindi virefu vya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** tatu, mipango mikakati ya kila ubalozi iunganishwe na kuwa na mpango kabambe mmoja wa Wizara. Huu ujikite zaidi kwenye kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa balozi zote na nchi nzima kwa ujumla. Pamoja na mambo mengine mpango huu wa wizara uweke malengo ya muda mrefu na ya muda mfupi ya kuandaa wanadiplomasia waliobobea kwenye fani ya diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** tatu, wizara ikishirikiana na Kituo cha Uwekezaji (TIC) ifanye mapitio upya juu ya uhalisia wa lengo la kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni "foreign direct investment (FDI)" nchini kutoka Dola za Kimarekani Bilioni 1.5 kwa mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Kimarekani Bilioni 5, ifikapo mwaka 2020. Utafiti wa kambi ya upinzani umebaini kuwa lengo lililowekwa na TIC ni dogo sana ikilinganishwa na fursa kubwa zilizopo za Tanzania kupata FDI kubwa zaidi kama serikali itaacha mzaha kwenye kutekeleza diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** upo msemo usemao ***"mafanikio ni kama bahari, tatizo letu baadhi tunapokwenda kuyachota huwa tunakwenda na vijiko".*** Lengo dogo la kufikia FDI ya Dola Bilioni 5 mwaka 2020 linaweza kabisa likaifanya Tanzania kuendelea kufanya jitihada ndogo kwenye diplomasia ya uchumi. Aidha, lengo hilo dogo la TIC lipo mbali sana na ndoto ya Tanzania ya kutaka kuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kwani nchi zote zilizo kwenye uchumi wa kati zina sifa ya kupata FDI kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** ni vema ikakumbukwa kuwa Tanzania mwaka 2014, nchi yetu ilishapokea jumla ya uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja ya kigeni (FDI) ya thamani ya Dola Bilioni 2 za Kimarekani. Hii inaashiria kuwa Tanzania inaweza kabisa kupata zaidi ya Dola Bilioni 5 za Kimarekani ifikapo mwaka 2020.

## 5.0 USHIRIKIANO NA UKUZAJI WA MAHUSIANO YA KIDIPLOMASIA NA MATAIFA MENGINE

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu ilijijengea heshima kubwa katika medani za kimataifa hasa kwenye masuala ya kupigania uhuru wa nchi nyingine barani Afrika, pamoja na kutetea nchi ambazo zilikuwa zinaonewa na mataifa mengine duniani.

**Mheshimiwa Spika,** Ushirikiano wa kimataifa kwa nchi inayoendelea kama Tanzania ni jambo la msingi sana kwani kuna mambo mengi ambayo tunahitaji kujifunza kutoka kwa mataifa mengine ili kuweza kuasili mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, kiuchumi na kiutandawazi yanayoendelea kutokea kila siku duniani.

**Mheshimiwa Spika,**wakatia akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb) alisema kwamba; Licha ya umuhimu wa kuwa na ushirikiano wa kidiplomasia na mataifa mengine;serikali ya awamu ya tano imeonekana kwenda na dhana hiyo kwa kudhibiti safari za nje kwa kisingizio cha kubana matumizi. Aliitahadharisha Serikali kwamba; kudhibiti safari za nje ni kuliingiza taifa kwenye giza nene kwani safari hizo zilikuwa ni lango la fursa za biashara ya kimatafa (international trade) ambayo ndiyo msingi wa diplomasia ya ki-uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** ushirikiano wa kimataifa unaimarishwa pale ambapo wakuu wa nchi mbalimbali wanapokutana kujadili masuala mbalimbali kuhusu mustakabali wa nchi zao na namna ya kusaidiana kukabiliana na changamoto mbalimbali. Ni jambo la kustaajabisha kuona Rais wa nchi yetu akiwa na mwamko mdogo wa kushiriki mikutano ya kimataifa kwa ajili ya kukuza ushirikano na mataifa mengine. Kitendo cha Rais kushindwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN General Assembly) mwaka jana kimeiweka Tanzania nyuma katika uhusiano wa kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kutambua kuwa Rais amekuwa akituma wawakilishi katika mikutano ya kimataifa, lakini vipo vikao au mikutano ya kimkakati (strategic meetings) ambayo ni lazima Rais wa nchi kushiriki.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Rais kuacha kukwepa kuhudhuria mikutano ya kimataifa na ya kikanda ambayo ni muhimu kwa ajili ya kujenga mustakabali wa diplomasia ya uchumi pamoja na uhusiano wa kimataifa kwa ujumla kama ambavyo umekuwa ni utamaduni wa taifa letu. Aidha, washauri wa Rais hasa wa masuala ya kimataifa wamshauri Rais juu ya umuhimu wa ushiriki wake katika vikao na mikutano hiyo pamoja na kuzingatia itifaki za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** kuna udhaifu mkubwa sana katika Serikali hii wa kutozingatia itifaki za kimataifa. Haingii akilini Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anakuja nchini halafu anapokelewa na Waziri wa Mambo ya nje wakati Rais yupo; lakini wakati huo huo Rais anafanya kikao na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China. Inaweza kuonekana kama ni kawaida tu Rais kutompokea Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; na inaweza kuonekana jambo la kawaida pia Rais kufanya kikao na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China lakini katika jicho la kidiplomasia kuna makosa makubwa sana ya kiitifaki yanayofanywa na Ofisi ya Rais.

**Mheshimiwa Spika,** uhusiano wa kimataifa unaweza kuathiriwa na namna sisi kama taifa tunavyowatendea raia wa nchi nyingine wanaoishi au kufanya kazi katika nchi yetu. Mataifa mengine huwa yanajali sana hali za raia wao wanaoishi au kufanya kazi katika mataifa mengine. Hivyo, mataifa hayo huwa yako tayari hata kupigana vita kwa ajili ya raia wao wanaonyanyaswa au kutendewa visivyo katika nchi nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha hivi karibuni cha Rais wetu kuagiza pasi ya kusafiria ya mkandarasi kutoka India ambaye anajenga mradi wa maji wa Ngapa huko Lindi

kutokana na makosa aliyoyafanya katika mradi huo unaweza kuingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia kwa sababu pasi ya kusafiria ni mali ya taifa ambalo limetoa pasi hiyo. Na katika pasi hiyo kuna tamko la Rais wa nchi husika linaloomba raia huyo apewe ulinzi na msaada wowote atakaohitaji katika nchi atakayokuwa ameingia kuishi au kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa utamaduni duniani ni kuwa; pasi ya kusafiria hutolewa na Rais wa nchi husika kwenda kwa mamlaka ya nchi ambayo mtu anasafiri kwa ajili kupata msaada wowote anaohitaji kulingana na malengo ya safari yake na taratibu za nchi aliyopo. Hata Sheria yetu inayosimamia utoaji wa pasi na nyaraka nyingine za kusafiri kifungu cha nne kinatamka kuwa pasi inatolewa na Rais kwa ajili ya kumtambulisha Mtanzania katika mamlaka ya nchi nyingine na kupatiwa msaada na usaidizi wowote atakaohitaji kwa mujibu wa taratibu za nchi husika. Hivyo, kuagiza pasi hiyo kushikiliwa ni kuidhalilisha mamlaka iliyotoa pasi hiyo kwa maana ya Rais wa nchi husika jambo ambalo linaiingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** agizo la Rais la kushikilia *passport* ya mkandarasi huyo tayari limeripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa ambavyo kwa vyovyote vile vinasomwa na watu mbalimbali duniani wakiwemo wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** serikali ina vyombo vya ulinzi na usalama mpaka mipakani, kama mwekezaji au mkandarasi kutoka nje amepewa maelekezo ya kumaliza mradi kwa muda flani, ni vema akapewa nafasi ya kufanya hivyo bila kuchukua pasi yake ya kusafiria. Mambo yote hayo yanafanyika kwa mujibu wa mikataba ambayo serikali imeingia na wawekezaji au wakandarasi na hivyo ni vema mikataba ikazingatiwa na au maelekezo/makubaliano mengine kuliko kuanza kuchukua pasi za kusafiria za mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika,** athari za maamuzi au amri za Rais zinaweza zisionekane leo lakini kwa utafiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kuwa agizo la Rais la kuamuru pasi ya raia mwingine kuchukuliwa liliripotiwa katika vyombo vya habari vingi duniani pamoja na nchi ya India yenyewe. Jambo hili si tu linatia doa nchi yetu katika masuala ya uhusiano wa kimataifa lakini pia linaweza kuleta athari katika sekta ya uwekezaji.

## 6.0 MIRADI YA MAENDELEO YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa ipo miradi ya maendeleo ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambayo hugharamiwa na washirika ndani ya Jumuiya pamoja na wadau mbalimbali duniani hasa Umoja wa Ulaya. Gazeti la *The Citizen* la tarehe 17 Mei 2017 ukurasa wa 15 liliripoti kuwa Jumuiya ya Afrika imekumbwa na tatizo ukosefu wa fedha za kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo hugharamiwa na Jumuiya hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa suala la kuchangia miradi ya maendeleo lipo kwa mujibu mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki bado michango ya kifedha za baadhi ya washirika ndani ya Jumuiya imekuwa haitolewi kwa ukamilifu ikiwemo nchi yetu. Ieleweke kuwa ibara ya 132(4) inaelekeza kuwa bajeti kwa ajili ya Jumuiya zitachangiwa kwa usawa na nchi washirika ndani ya Jumuiya.

**Mheshimiwa Spika**, imeonekana wazi kuwa nchi wanachama zinaanza kugawanyika kuhusu utaratibu wa kuchangia miradi ya maendeleo ambapo nchi kama Burundi inaona kuwa haiwezi kuchangia sawa na zingine washirika kutokana na matatizo yake ya ndani. Hata hivyo baadhi ya nchi kama Tanzania imekuwa haitoi fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati hivyo kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ikumbukwe kuwa 40% bajeti ya miradi ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inagharamiwa na nchi washirika huku 60% ikigharamiwa na nchi washirika.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa inaonesha kuwa kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ya Jumuiya ni takribani dola milioni 101.6 ambapo kila nchi hutakiwa kuchangia kiasi cha dola milioni 8.3. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu ni nchi ya Kenya pekee ambayo imetoa mchango wake kwenye bajeti ya maendeleo kwa 100% ikifuatiwa na Uganda 90%, Rwanda 51%, Tanzania 35% na Burundi 0%.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haijashangaa kuona Tanzani imetoa 35% ya bajeti ya miradi ya maendeleo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu hata kwenye miradi ya maendeleo ya ndanikatika Wizara mbalimbali serikali haikuweka msisitizo kutoa fedha za miradi ya maendeleo, ndiyo maana baadhi ya Wizara bajeti ya miradi ya maendeleo imetolewa kwa kiasi kidogo, mathalani Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika sekta ya Kilimo ni 3% pekee fedha za maendeleo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Mei 2017.

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kuwa miradi ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inanufaisha pia nchi yetu kama moja ya nchi washirika ndani ya Jumuiya. Tanzani imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa Umajumui wa Afrika kuwa moja ya nchi ambayo mara kadhaa imekuwa kikwazo cha maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa haiwi kikwazo kwa kazi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hasa kwenye miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu sababu za kutotoa fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## 7.0 UHUSIANO NA MAJIRANI ZETU

**Mheshimiwa Spika,** mahusiano na jirani ni kitu kikubwa Sana, na ndio maana kuna msemo unasema jirani yako ni zaidi ya ndugu yako na mara zote huwezi kuchagua jirani bali unachagua rafiki. Hivyo basi hata kama jirani yako sio wa chaguo lako ni lazima uishi nae vizuri tu na ndio utu , imani na utamaduni wetu wa asili.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa kutoa bashrafu hiyo kutokana na taarifa zilizochapishwa kwenye gazeti linalotolewa kila siku nchini Kenya Daily Nation, toleo la tarehe 14 Mei, 2017 lilimnukuu Kiongozi wa wabunge katika Bunge la Kenya Mhe. Aden Duale akitoa shutuma kwamba Tanzania inapanga kuingilia mchakato wa uchaguzi wa nchi hiyo, kwa kuweka kituo cha majumuisho ya kura za Urais kwa jumuiko la vyama vya Upinzani nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** shutuma hizi sio za kuzipuuzia kwa urahisi tu kwani zilitolewa ndani ya Bunge hilo la Kenya na hivyo zina athari za moja kwa moja katika masuala ya kidiplomasia ndani ya Jumuiya. Tumeshuhudia hivi karibuni Rais wa Kenya akishindwa kuhudhuria vikao vya Jumuiya mara kadhaa na kumtuma Naibu Rais wan chi hiyo jambo ambalo linapelekea wananchi wengi kujiuliza ni nini hasa kinachomfanya Rais Kenyata kushindwa kuhudhuria vikao vinavyofanyika Tanzania kwa mara ya pili sasa?

**Mheshimiwa Spika,** tukirejea katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Kifungu cha 6 (d), Kifungu cha 7 (2) ambapo vifungu hivi vinasisitiza misingi ya utawala bora unaozingatia misingi ya kidemokrasia, utawala wa sheria,uwazi na uwajibikaji n.k ambapo nchi wanachama wanatakiwa kufuata misingi hii. Endapo Tanzania tutaanza kuingilia chaguzi hizi basi tujue dhahiri tutakuwa miongoni mwa wachochezi wanaohatarisha amani za nchi za wenzetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani kabisa machafuko yale yaliyotokea nchini Kenya mwaka 2007 na kwa namna yoyote hatuwezi kuona hali ile ikijirudia. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulizungumzia jambo hili kwani kuendelea kukaa kimya kuna maanisha kuwa Msemaji aliyetoa shutuma hizi ndani ya Bunge la Kenya ni za kweli.

## 8.0 MSIMAMO WA TANZANIA JUU YA MATUKIO MBALIMBALI DUNIANI

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imekuwa na historia iliyotukuka duniani, ya kuwa mstari wa mbele kupinga aina zote za uonevu, unyonyaji na utumwa hususan ubeberu na

ukoloni. Kutokana na tunu yake ya kujali utu na usawa miongoni mwa binadamu wote, Tanzania ya enzi za Mwalimu Nyerere, ilifikia hatua ya kujitoa kupigana vita vya ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika, ili kuhakikisha kwamba ubeberu na ukoloni katika nchi hizo unatokomezwa na uhuru wa kweli unapatika.

**Mheshimiwa Spika,** itakumbuka kwamba Tanzania ndiyo iliyokuwa muasisi wa nchi za wa mstari wa mbele chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere katika miaka ya 1960 kwa lengo la kupinga ubaguzi wa rangi na utawala wa wazungu wachache katika nchi za kusini mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ilienda mbele zaidi hadi kufikia hatua ya kuvunja mahusiano yake ya kidiplomasia na mataifa mengine yaliyokuwa na tabia za ubaguzi wa rangi, unyonyaji, ubeberu na ukoloni dhidi ya mataifa mengine. Tanzania ilipinga pia utawala wa kidikteta miongoni mwa nchi za Afrika, kwa kuwa udikteta ulikuwa na tabia zote za unyonyaji, ubaguzi, uonevu na ukiukwaji wa haki za binadamu ,mambo ambayo Watanzania hawakuamini katika hayo na ndio maana Tanzania kwa wakati huo, haikumuunga mkono Mobutu Seseko wa iliyokuwa Zaire – sasa Kongo DRC, haikumuunga mkono Muamar Gadafi wa Libya na pia ilimng’oa madarakani dikteta wa Uganda Idd Amin Dadah.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Tanzania bado inatekeleza sera na msimamo wake wa kidiplomasia wa kutofungamana na upande wowote kwenye migogoro ya kiitikadi na misimamo kadhaa ya mataifa mbalimbali duniani..

## 8.1 Msimamo wa Tanzani kuhusu Morocco na Mataifa Mengine

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Oktoba, 2016 nchi yetu ilipokea ugeni kutoka Morocco ambapo mfalme wa nchi hiyo akiambatana na watu takribani 150 alitutembelea. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Morocco

sio sehemu ya Umoja wa Afrika kwa sasa kutokana na mgogoro wake na Sahara ya Magharibi.

**Mheshimiwa Spika**, 1971 vuguvugu la POLISARIO lilianzishwa na wanafunzi wa vyuo vikuu wenye asili ya watu wa Sahrawi ambao ni jamii ya watu wanaoishi Sahara Magharibi waliokuwa wanapigania uhuru wa Jimbo lao kuwa nchi. Baadae Sahara Magharibi ikatambuliwa na Umoja wa Mataifa huku nchi ya Morocco ikipinga na ikiendelea kuikalia sehemu hiyo kimabavu hadi leo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa taarifa zilizotolewa na Waziri wa Mambo ya Nje na kunukuliwa na vyombo vya habari nchini ni kuwa pamoja na uhusiano wa Tanzania na Morocco bado kama taifa hatujayumba kwenye msimamo wetu wa kuitaka Morocco kuiacha huru Sahara Magharibi kwa sababu zama za ukoloni zimeshapitwa na wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa serikali inayumba kwenye msimamo wake dhidi ya Morocco kwa sababu mazingira ya miaka ya 1970 ni yale yale ambapo mpaka sasa Morocco bado inaikalia kimabavu Saharra Magharibi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa uhusiano wa Morocco na Tanzania ni mwendelezo wa Morocco kutaka kurudi kuwa mwanachama wa Umoja wa Afrika huku ikiendelea kuikalia Sahara Magharibi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu undani wa uhusiano wa Tanzania na Morocco na taarifa ya kina ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya nchi hizo mbili.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa sasa nchi yetu inayumba kwenye diplomasia kwa sababu imeshindwa kuwatetea wanyonge wa Sahara Magharibi huku ikiikumbatia Morocco. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha serikali kuwa tarehe 03 Mei, 1967 Jimbo la Biafra la nchini Nigeria lilitangaza kujitenga na Nigeria ya Kaskazini ambapo wananchi wa Jimbo hilo waliona kuwa ni vema wakajitenga na kuunda taifa lao kutokana na vifo na mateso waliyokuwa wanakumbana nayo.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 13 Aprili, 1968 Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kulitambua Jimbo hilo kama nchi huru. Pamoja na mjadala mkali uliokuwepo wakati huo juu ya msimamo wa serikali lakini angalau wakati serikali ilikuwa na msimamo thabiti ya kutetea wanyonge. Ni rai ya Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kwa serikali kuhakikisha kuwa ile misingi mizuri iliyokuwepo inaenziwa na sio kuyumba kulingana na maslahi ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu juu ya msimamo wetu kama nchi kuhusu mgogoro uliopo Syria, Mgogoro kati ya India na Jimbo la Kashmiri, Mgogoro unaoashiria vita kati ya Marekani na washirika wake dhidi ya Koreah ya Kaskazini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua urafiki kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Kikomunisti cha China. Ieleweke kuwa mbali na Morocco, Taifa la China lipo kwenye mgogoro na Jimbo la Tibet na Taiwan kwa muda mrefu na China ikipewa lawama kuwa inazikalia sehemu hizo kimabavu. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoja msimamo wa serikali kuhusu mgogoro wa China na sehemu hizo ambayo imekuwa ya muda mrefu.

### 8.2 Brexit na Umoja wa Ulaya

**Mheshimiwa Spika**, mwaka uliopita haukuwa mzuri kwa Umoja wa Ulaya baada ya Taifa kubwa la Uingereza ndani ya Umoja huo kuamua kujitoa katika Umoja huo kufuatia kura ya maoni ya wananchi wa nchi hiyo maarufu kama Brexit.

**Mheshimiwa Spika**, Sakata la Brexit kwa vyovyote vile litaathiri masuala ya diplomasia duniani kwa sababu bado Umoja wa Ulaya una uhusiano wa karibu na nyingi za kiafrika Tanzania ikiwemo. Aidha, baada ya kura ya maoni na kuanza kupeleka rasmi maombi ya kujitoa katika Umoja wa Ulaya Taifa la Uingereza imeanza kwa kasi kujenga na kuboresha mahusiano ya kidiplomasia kati yake na mataifa mbalimbali duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya tathmini ya kina juu ya Brexit na Umoja wa Ulaya ili kuona ni wapi tutasimama kama nchi hasa kwenye masuala ya diplomasia ya uchumi kwa sababu kwa vyovyote sakata hilo litaathiri baadhi ya masuala ya kidiplomasia. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Tanzania imekataa kusaini mkataba wa EPA ambao unapigiwa chapuo na Umoja wa Ulaya na baadhi ya nchi washirika wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** msimamo wa Tanzania kutosaini mkataba wa EPA unaweza kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na Taifa la Uingereza baada ya Brexit. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwa serikali kufanya tathmini ya kina na kuweka msimamo wake kuhusu mahusiano haya ambayo yanaenda kuwa na mabadiliko makubwa.

## 9.0 UONEVU WANAOFANYIWA WATANZANIA NJE YA NCHI-WATANZANIA KUFUKUZWA MSUMBIJI

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni kumeanza kushamiri kwa tabia ya baadhi ya nchi kuwafukuza wananchi wa nchi nyingine kwa kisingizio cha kunyang'anywa ajira za wazawa. Tanzania imekuwa miongoni mwa waathirika wakubwa katika kadhia hii. Kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi la tarehe 16 Februari 2016 ,watanzania wapatao 180 walifukuzwa nchini Msumbiji.

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania hawa walipoteza mali, fedha, marafiki na waliathirika sana kiuchumi, kisaikoloji n.k. Watanzania hawa walitoa malalalamiko yao ambayo kwa sehemu kubwa yalilwaenga askari wa Msumbiji ambao walilalamikiwa kuwapora wakati wa operesheni hiyo ya kamatakamata. Wengine walilazimika kuacha wazi sehemu zao za biashara na kukimbia kwa kuhofia maisha yao. Watanzania waliokamatwa waliwekwa mahabusu bila kufuata taratibu za kisheria. Wengi walikaa mahabusu kwa siku kadhaa na kisha kupelekwa eneo la mpaka wa Kilambo mkoani Mtwara ambapo ni mpaka wa Tanzania na Msumbiji na kutelekezwa huko bila kujali utu wala mahusiano ya ujirani

mwema ambao umetengenezwa na Waasisi wa Mataifa haya kwa miaka mingi.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na madhila hayo yaliyowatokea Watanzania wenzetu; Mheshimiwa Rais alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari mnamo tarehe 05 Machi 2017, akiwa kwenye ziara Mkoani Mtwara aliwataka wananchi hao kuacha kukuza suala la Watanzania waliofukuzwa nchini Msumbiji ambao aliwaita wahamiaji haramuna alisisitiza kuwa serikali haiwezi kuwatetea watu waishio katika nchi nyingine bila kufuata sheria. Pamoja na hayo Mheshiwa waziri alitoa maelezo kuhusiana na kufukuzwa kwa Watanzania hao nchini Msumbiji na alieleza kuwa madhila yaliyowapata Watanzania wenzetu yanaweza kuendelea ***(Operation fukuza watanzania***) kwani mji uliokumbwa na tukio hilo wa Monte Puez uliopo Jimbo la Cabo Delgado kuna idadi ya Watanzania wanaokadiriwa kuwa takribani 3000.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu yafuatayo:

Je, Mheshimiwa Rais alipewa habari za uhakika kuhusiana na Watanzania walofukuzwa nchini Msumbiji?Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza swali hili kwa sababu wapo Watanzania waliofukuzwa na walikuwa na vibali halali za kufanya kazi nchini humo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni nini hasa wajibu wa Balozi katika kusimamia usalama wa Watanzania na mali zao wanapokuwa nje ya nchi kwa majukumu mbalimbali hasa tukizingatia nchi yetu inajipambanua katika kusimamia sera mpya ya Diaspora kama ilivyo katika tovuti ya Wizara?

## 10.0 MAUAJI YA WATANZANIA NCHINI OMAN

**Mheshimiwa Spika,** siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya unyanyasaji na mauaji ya watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi hususani nchini Oman. Matukio

mengi ya unyanyasaji yameripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari na pia kwenye ngazi za familia za wahusika, lakini kutokana na hali ya umasikini wa familia nyingi zilizokumbwa na madhila haya hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wahusika ambao ni raia wa Oman.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 14 Machi, 2017 Msichana wa Kitanzania mkazi wa Dar es salaam ambaye alikuwa anafanya kazi za ndani mtaa wa Bilad Ban Bu Alli nchini Oman aliuawa kwa kutupwa toka ghorofani jambo lililompelekea umauti. Hili ni moja tu ya matukio ya ukatili na ya kutisha wanayofanyiwa Watanzania hasa wanawake wanaofanya kazi za majumbani nje ya nchi hususani katika nchi za Arabuni na India kama Kambi ya Upinzani Bungeni ilivyoelezea katika hotuba yake ya bajeti kupitia Wizara hii mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi inataka kufahamu ni kwanini mambo haya yamekuwa yakizungumziwa lakini serikali haichukui hatua madhubuti? Ni kwa nini taarifa rasmi kuhusu mauaji ya Mtanzania huyu aliyeuawa kinyama haijatolewa na kulaaani matendo haya ya kinyama wanaofanyiwa Watanzania waishio Oman na maeneo mengine ?Je, serikali ina mikakati gani ya kuwatambua mawakala wote wanaojihusisha na kuwatafutia kazi za ndani Watanzania huko ughaibuni ili matatizo yanapotokea iwe rahisi kuwabaini wahusika?

## 11.0 WATANZANIA WALIOFUNGWA NCHINI CHINA

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania waliofungwa katika magereza mbali mbali Nchini China wanapata taabu na mateso kinyume na haki za binadamu na mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Vienna wa mwaka 1969 .Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kila nchi ina utaratibu wake wa ndani wa kisheria wa kushughulikia mambo yake ya ndani lakini sheria hizo hazipaswi kukiuka huo wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na haki za wafungwa.

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania waliofungwa nchini China wamekuwa wakipata mateso makubwa sana

ambayo ni kinyume kabisa na haki za binadamu na udhalilishaji mkubwa wa utu wa mwanadamu. Mpaka sasa Watanzania waliofungwa nchini China katika magereza mbalimbali wanakadiriwa kuwa takribani wafungwa 330.

**Mheshimiwa Spika**, Magereza yaliyoyalalamikiwa kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ni pamoja na YINGDE PRISON - GUANZIHOU WANDONG PROVINCE RPRC. (People republic of China) ambalo lina umbali wa karibu kilometer 180 kutoka Kaskazini mwa mji wa Gucughazou. Gereza hili linawafungwa takribani elfu nane wengi wao wakiwa ni mataifa kutoka Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, Wafungwa hao wamelalamika kufungwa kwa muda mrefu na baadae wanatumika kama watumwa. Katika magereza hayo kifungo kikubwa huwa sio zaidi ya miaka sita lakini wengi hufungwa mpaka miaka thelathini ili tuu kupata nguvu kazi ya shughuli mbalimbali za kizalishaji. Sababu kubwa zinazotolewa ni kukosekana kwa wasimamizi wa kisheria kwa Watanzania hao. Mfano wa *baadhi* ya Watanzania waliofungwa muda mrefu katika gereza la YINGDE ni pamoja na Rajab Salim Mwanyenza na Mohamed Bakari Mkemi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba nchi nyingi za Mashariki ya Mbali, hutetewa na sheria zao pale ambao panatokea kutofautiana kati yao na watu wa Mataifa mengine. Hivyo Wazawa za nchi hizo wana haki zaidi mbele ya vyombo vya dola kuliko watu wa mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa inawezekana kabisa Watanzania hao wamejikuta katika magereza hayo kwa sababu mbalimbali lakini ni muhimu kama nchi kuonyesha kuwa pamoja na makosa yao inathamini uraia wao.Wajibu mkubwa wa serikali ni kuhakikisha haki na usalama wa raia wake inakuwa ni kipaumbele cha kwanza. Pamoja na serikali kuwatambua kuwa wako magerezeni ni kuwatembelea, kuwasikiliza na kuhakikisha kuwa adhabu zao zinatekelezwa kama zilivyotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inafuatilia kwa karibu hukumu zinazohusiana na Watanzania walio kwenye mataifa wanayoiwakilisha nchi yetu na pia kutoa tamko pale inapobidi kwa nia njema ya kutetea haki za raia wake nje ya nchi.

## 12.0 JINA LA MWALIMU NYERERE NA HISTORIA INAYOPASWA KUENDELEZWA

**Mheshimiwa Spika,** ni takribani miaka 18 sasa tangu Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipotangulia mbele za haki. Pamoja na kuwa Mwalimu hayupo nasi kimwili bado tunatambua mawazo yake na mchango wake mkubwa hasa katika kupigania uhuru wa bara la Afrika na mchango mkubwa wa kisiasa katika nchi za Kikomunist.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na wadau wengine mbalimbali ambao wameendelea kumuenzi Mwalimu na kutambua mchango wake. Tutakumbuka mchango mkubwa wa Mwalimu hasa katika elimu na uandishi wa vitabu. Mwalimu aliwahi kutafsiri vitabu vya Mashairi vilivyoandikwa na Shakespear ikiwemo kitabu kilichoitwa "***Julius Caesar"*** and kingine ni ***"The Marchant of venice".***

**Mheshimiwa Spika,**huu ni mchango mkubwa wa Mwalimu katika kukuza lugha ya Kiswahili ulimwenguni.Pamoja na hilo Mwalimu ameandika vitabu na Machapisho mbalimbali yakiwemo Ujamaa -essays on socialism. Uhuru na Umoja (Freedom and unity), Crusade of liberation, Man and development, Freedom and development, Women freedom: Women are eagles not chickens, Uongozi na hatma ya Tanzania, Tujisahihishe, Freedom and a new world economic order n.k.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa tunashida kubwa katika masuala ya kiuongozi. Kutokana na matatizo hayo Tanzania inaanza kukosa uhalali wa kuwa nchi ambayo ni mfano bora

kwa mataifa mengine barani Afrika kama ilivyokuwa kwa utawala wa Mwalimu Nyerere. Rejea mbalimbali za kauli za Mwalimu Nyerere zimeanza kuwa mwiba kwa baadhi ya viongozi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika kitabu maarufu cha Uongozi na hatma ya Tanzania kilichopigwa marufuku kuchapishwa hapa nchini baada ya Mwalimu Nyerere kustaafu, mpaka pale alipoamua kuchapisha kitabu hicho nchini Zimbabwe ni ushahidi tosha kwamba tulianza kupanda mbegu ya kuporomosha misingi ya utawala bora na kupoteza mvuto kwa mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya nusu ya machapisho ya Mwalimu aliyoyaandika baada ya kustaafu yalijikita katika masuala ya uhuru na haki kwa raia, uongozi bora na misimamo mbalimbali ya taifa hili dhidi ya mataifa mengine. Kwa sasa mambo haya yote yamepigwa teke. Na ndio maana wananchi wetu wanateseka, kubaguliwa na hata kuuawa katika mataifa mengine lakini serikali ya sasa imekaa kimya kabisa na haina namna ya kujipambanua kusimamia haki wala kuizingumzia demokrasia nje ya mipaka yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuchukua hatua za makusudi katika kutengeneza tovuti maalum kwa hifadhi ya kumbukumbu za Mwalimu Nyerere tofauti na ilivyo sasa ambapo kazi kubwa ya kuendeleza jina la Hayati Baba wa Taifa katika medani za Kimataifa inayofanywa zaidi na taasisi binafsi. Badala ya serikali kudhani kuendelea kutumia majina ya Mwalimu Nyerere kwenye majengo na barabara ndio njia pekee katika kuenzi basi ni vyema sasa serikali ichukue wajibu wa kutengeneza tovuti maalumu kwa ajili ya maarifa na urithi wa elimu aliyotuachia katika kumuenzi na kuyaishi yale aliyoacha hasa katika kutafakari manufaa ya mahusiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine.

## 13.0 KUKAMATWA KWA MAGARI YA MIZIGO YANAYOFANYA BIASHARA KATI YA TANZANIA, ZAMBIA NA CONGO

**Mheshimiwa Spika,** kwa takribani miezi mitatu sasa magari zaidi ya 500 yenye namba za usajili kutoka Tanzania yamekamatwa nchini Zambia na mpakani mwa Congo kwa madai kuwa magari hayo yanafanya biashara kwa njia ambazo sio halali. Magari haya yamekamatwa katika maeneo ya Nakonde, Mkushi na Kasumbalesa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na madai hayo yaliyotolewa na serikali ya Zambia kwa wafanyabishara kutoka Tanzania ambao walikuwa wakisafirisha mizigo hiyo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchini Congo, wafanyabiashara hao waliwasilisha nyaraka mbalimbali za kufanya biashara pamoja na zile za kutimiza masharti yaani (movement sheets na nyingine)na zikafanyiwa ukaguzi lakini mpaka leo magari na mizigo yao inashikiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** wafanyabiashara hawa walichukua hatua zaidi ya kupeleka malalamiko yao ubalozini lakini jitihada hizo hazikuzaa matunda kwa kuwa ubalozi wa Tanzania nchini Zambia haujapewa ushirikiano wowote kutoka ndani ya serikali ya Zambia**.** Mpaka sasa hata ubalozi wa Zambia nchini haujatoa mrejesho wowote hata baada ya kufikishiwa suala hili.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na magari haya kushikiliwa yakiwa na mzigo mpaka sasa Wafanyabiashara hao wamepata hasara ya takribani dola 5,000,000 kwani kwa safari moja tu ya nchini ni dola 10,000.Hivyo wafanyabiashaa hawa wamekosa safari za kwenda na kurudi na hivyo kupoteza fedha nyingi na serikali kukosa kodi. Serikali itambue kuwa kwa kadiri magari hayo yanavyozidi kukaa katika ardhi ya Zambia faini inazidi kujilimbikiza kwani kwa siku inagharimu dola 40 mpaka 90. Familia nyingi nchini ziko katika wakati mgumu kwani madereva wa malori hayo wapatao 500 na wasaidizi wao 500 wako katika hali ngumu kiuchumi kwani hutegemea kazi hii ya kusafirisha mizigo ili wapate

kipato.Pamoja na hayo maisha ya madereva hawa yapo hatarini kw kuwa wanalazimika kulala nje ili kulinda mizigo yao.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo hili linajulikana kwani Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi ya kulifikisha kwa Mheshimiwa Rais. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua yafuatayo:

- Je, Mheshimiwa Rais alichukua hatua gani baada ya kufikishiwa habari hii na Mheshimiwa Waziri ikiwa tatizo hili limedumu kwa takribani miezi mitatu sasa

- Je, hali ya mahusiano kati ya Tanzania na Zambia yakoje kwa sasa?Hii ni kutokana na hali ya sintofahau ya serikali ya Zambia kushikilia magari haya bila kutoa kauli yoyote

- Je, Serikali inatoa kauli gani pale ambapo ubalozi wa nchi nyingine ndani ya nchi yetu wanaombwa msaada lakini hawatoi ushirikiano au pale ambapo ubalozi wa nchi yetu ndani ya ardhi ya nchi nyingine kunyimwa ushirikiano hasa katika masuala muhimu ya kulinda haki, heshima na utu wa raia yake.

## 14.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kambi ya upinzani inaamini kuwa iwapo Wizara hii na serikali hii kwa pamoja wataacha ujuaji na kuamua kuufanyia kazi ushauri tulioutoa; Watafikiri tofauti, kupanga tofauti na hatimaye kutenda tofauti; Na ikiwa kila mtumishi wa Wizara hii ataachana na utendaji wa mazoea wa serikali za CCM (business as usual);

Basi Tanzania, kwa mara ya kwanza, tutashuhudia Tanzania iliyo tofauti, yenye kupiga kasi kubwa ya kimaendeleo ambayo haijapata kutokea ndani ya historia ya uhai wa Taifa hili.

**Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania,**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mchungaji Peter Simon Msigwa (Mbunge)
**Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Mamboya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**29 MEI 2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia, namuita Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, dakika tano, Mheshimiwa Doto Biteko kwa dakika tano, jiandae Mheshimiwa Haji Khatib, dakika tano. Dakika tano, bajeti hii inakwisha saa kumi Serikali inaanza kujibu. *(Makofi)*

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kabisa Waziri wetu na Naibu wake ambao kama mnajua wamebobea pia katika nyanja za Kimataifa. Kwa hiyo, tunapowauliza habari za diplomasia ya uchumi, Wahaya tunasema, usimuulize mganga wa kienyeji kondoo kapita wapi? Kwa sababu anaelewa anachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongezeni kabisa kwamba hapa hatua tuliyopiga siyo haba na kazi kubwa ambayo inafanyika katika uwanja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kiasi cha kwamba sasa hili bomba lililokuwa linaenda Kenya tayari limeshaingia Tanzania, tunamshukuru sana. Hili ni jambo kubwa sana, siyo jambo la kuchukulia hivi hivi, linataka diplomisia ya kiuchumi ambayo inafanyika nyuma ya pazia, wanasema ni *lobbying.* Huwezi kupiga kelele ukafanya mapinduzi makubwa kama hayo. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba nipongeze sana juhudi ambazo zinaendelea pia kupanua wigo wa nchi rafiki, nchi ambazo zimepiga hatua kama Uturuki, nimeiona ni nchi ambayo naifahamu sana, nimeifanyia kazi kule na imepiga

hatua. Kwa hiyo, wakija kutusaidia, nalo siyo jambo dogo la kubeza, tunawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa nina dakika tano mbali ya pongezi, naomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama, nami unitoe dukuduku kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tuna tatizo la mipaka ya nchi hii ambayo haina mikataba *(treaty).* Nchi hii mwaka 1979 ilipigana vita Uganda kwa sababu ya kutokuwa na mpaka ambao una mkataba wa Kimataifa. Ninaomba nijue kabisa unachukua hatua gani kukamilisha jambo hili?

Jamani ndugu zangu naomba niwaambie, Rais Museveni akiondoka madarakani Uganda, msishangae tukienda pia kupigania huu mpaka. Kwa sababu ule mpaka ni *one degree South of the Equator* na ukifuata *protocol* hiyo, Tanzania itapoteza ardhi kubwa sana. Kwa hiyo, ni jambo ambalo lina utata, naomba nijue kama Mheshimiwa Waziri analifanyiaje kazi? Hii inaendelea kwenye mipaka sehemu kadhaa... *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Dakika tano zimekwisha?

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa mchangiaji taarifa kuhusu hiyo kauli yake kwamba mipaka yetu ya nchi haifahamiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1963 wakati *OAU* inaanzishwa, ule mkataba wa kuanzisha *OAU* ulitamka kwa wazi kabisa kwamba mipaka ya nchi zote za Afrika wanachama wa *OAU* kama ilivyotengenezwa wakati wa

Ukoloni, itakuwa ndiyo mipaka inayotambuliwa na nchi wanachama wa *OAU* na ndiyo mipaka inayotambuliwa mpaka leo na Jumuiya ya Kimataifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lissu, ameshakuelewa. Mheshimiwa Tibaijuka endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Lissu utafikiria na ungeamini kwamba anajua anachokiongea. Naweza kusema kwamba mimi kama mtaalam wa sekta, huyu hajui anachokiongelea sasa hivi Mheshimiwa Lissu. Kwa hiyo, siwezi kupokea taarifa ambayo haina *knowledge.* Ni lazima mpaka uwe na *treaty*. Hili tamko la *African Union* ni *aspiration* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nayakataa, naomba niendelee, nitakuja kumwelewesha zaidi Mheshimiwa Lissu baadaye nimpe habari anayotakiwa kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama atueleze ni jinsi sasa Tanzania tutakavyojipambanua katika Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo Mwalimu Nyerere na Amir Jamal walileta heshima za nchi hii. Shirika la *UNCTAD* sikuliona hapa katika orodha ya watu unaowasiliana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Rais wetu amekazana tusiibiwe madini, lakini kama huna mashirika haya *including South Center* kule Geneva, taasisi ambayo ilianzishwa na Mwalimu Nyerere kupigania haki za mambo ambayo tulikuwa tumeonewa, tukaweza kufutiwa madeni. Sasa nataka kujua mkakati ulionao Mheshimiwa Waziri kuhusu *UNCTAD* kutusaidia kuondokana na hii kadhia ya mikataba mibovu ambapo tumekuwa tumeibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kwenda na *International Diplomacy* sisi ni Taifa change, hatutaweza kufika, Rais wetu amejidadavua kama Mwalimu Nyerere, anapigania haki ambazo tulikuwa tumepokonywa. Sasa ninyi mnamsaidiaje kuhakikisha kwamba hatutatengwa? Kwasababu pia inabidi twende kimkakati *(strategically),* tusije tukajikuta tunaingia katika hatari ya kutengwa. Ni jambo ambalo nadhani ni diplomasia ya kiuchumi ambayo nilifikiria kwamba Mheshimiwa Mchungaji Msigwa angekuwa anaifahamu, lakini sikusikia akiizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa dakika tano, nilikuwa nataka kusema kwamba Afrika Mashariki, sasa hivi Kenya wameridhia Mkataba wa *EPA (Economic Partnership Agreement),* napenda kusikia Waziri anajitayarishaje sasa kuhakikisha kwamba zile athari zinazoweza kutokana na hali kwamba nchi moja imeshasaini na sisi bado, ni ipi? Sisi ni nchi inayoendelea, tuko *protected* na *World Trade Organization,* lakini ni vizuri kwa Wizara ya Mambo ya Nje kuwa wamejipanga katika hili kwamba athari zitapoanza kuonekana sisi tutalindaje maslahi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa dakika hizi tano, yangu ndio hayo. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Doto, naomba Mheshimiwa Haji Khatib, ajiandae Mheshimiwa Lema.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na dunia kwa kuniamsha salama siku ya leo nikiwa na afya na kuweza kufunga funga ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Vilevile niwatakie Ramadhan Mubarak waislamu wote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla baada ya kuhoji kwa muda mrefu na kutaka wananchi wa Kisiwa cha Pemba waweze kufikishiwa elimu

ya Mtangamano wa Soko la Afrika Mashariki. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Waziri, niseme kwamba elimu ya mtangamano ya Afrika Mashariki haikuwafikia walengwa. Hii ni kutokana na kwamba wakati wa maandalizi Wabunge wa Pemba hawakushirikishwa, hasa mimi ambaye muda wote wakati nikiwa kwenye Kamati nimekuwa nikihoji ni lini wananchi wa Kisiwa cha Pemba hasa kule Kaskazini watafikishiwa elimu hii ambayo itaweza kuwasaidia na kuweza kujua wajibu wao na haki katika Soko la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kisiwa cha Pemba, hasa Kaskazini Pemba, wananchi asilimia kubwa ni wavuvi. Wavuvi hawa kila mwaka, inapofika mwezi wa kumi hadi mwezi wa tatu wamekuwa wakisafiri kwenda nchini Kenya kufanya dago. Ni wazi kwamba wanakuwa wakipata matatizo na wananchi wangu wamewahi kufungwa nchini Kenya miezi sita na faini ya shilingi 20,000 juu. Kwa hiyo, hii ni kutokana na kwamba wananchi hawa hawajui wajibu na haki zao katika soko hili la Afrika Mashariki. Ndiyo maana nikasema kwamba wananchi wa Kisiwa cha Pemba hasa wale walengwa hawakufikiwa na elimu hii ya mtangamano wa soko la Afrika Mashariki ambayo ni muhimu kwa wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Desemba, 2015/2016 wapiga kura wa Jimbo langu wapatao 130 walifungwa kwa kuonewa. Hii yote ni kutokana na kwamba hawajui wajibu wao na ndiyo maana nikasema walengwa hawakufikiwa na elimu hii. Naomba nishauri kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mara nyingine Wizara itaandaa utaratibu wa kwenda kutoa elimu ya mtangamano wa soko la Afrika Mashariki, basi ibadilishe maneno, badala ya kusema Wizara inaenda kufanya semina, basi maneno yasemwe kwamba tunaenda kutoa mafunzo. Hii itasaidia wale walengwa hasa kuweza kufikiwa na elimu

iliyokusudiwa. Kwa kuwa Pemba ina sehemu kuu mbili, naomba na ninamshauri Mheshimiwa Waziri kwamba elimu hii igawanywe katika sehemu kuu mbili; katika Kisiwa cha Pemba kuna sehemu ya Kaskazini na Kusini, kwa hiyo, ni vyema katika taaluma hii au uelewa huu ugawanywe katika sehemu mbili ili taaluma hii iweze kuwafikia kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niseme kwamba katika taaluma hiyo hiyo ya Soko la Afrika Mashariki, yaani mtangamano ni vyema Wizara itapanga utaratibu na kuhakikisha kwamba Wabunge kutoka Pemba wote wanashirikishwa wakati wa maandalizi katika hoja hiyo ambayo itakuwa imepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, ili kuondoa matatizo ambayo wavuvi wetu ambao wamekuwa wakiyapata hadi kufugwa jela nchini Kenya, ni vyema Serikali hizi mbili...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema, ajiandae Mheshimiwa Mwanjelwa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba tu Wizara ifuatilie sana ushauri alioutoa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Wizara *sensitive* kama Wizara ya Mambo ya Nje kwa sababu dunia ya leo imekuwa kijiji. Katika mambo yanayohusu biashara na uchumi wa kidiplomasia kati ya mataifa na mataifa, *engagement* ya Wizara ya Mambo ya Nje ni muhimu sana kwa ajili ya kutoa ushauri ni mambo gani yanatakiwa kufanyika? Hatua ya kulinda rasilimali za nchi hii ni mtu mwendawazimu anayeweza asipongeze; lakini namna gani unalinda rasilimali za nchi hii, inaweza ikaligharimu sana hili Taifa na kuliingiza kwenye *consequences* nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Taifa hili wote tunafahamu kwamba nchi hii ina mgogoro na *Acacia*

*Mining,* mgogoro huo kwa sura ya kwanza unajenga hisia na sifa za kisiasa ndani ya nchi, lakini sura ya pili ya mgogoro huu unakwenda kabisa ku-*demoralize spirit* ya *investors* walioko nje kuja katika Taifa hili kufanya *investment. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu *Acacia,* ukiangalia ardhi kwenye Wizara ya Mheshimiwa Lukuvi, imekuwa ni sifa kunyang'anya watu ardhi na imekuwa ni sifa kunyang'anya wawekezaji ardhi, jambo hili mbele ya safari litalifanya Taifa hili liende likawe kama Zimbabwe. Wakati Mugabe anaanza sera hii ya kunyang'anya watu mashamba, kuwakandamiza *investors* wa nje, alipigiwa makofi na wananchi wake kama ambavyo leo tunapigiwa makofi, lakini leo ninavyoongea kwenye Bunge hili, Zimbabwe hawana noti yao, hawana fedha yao, ni Taifa ambalo limepoteza hata *identity.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ni muhimu sana mkamshauri Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala la *Acacia Mining,* linaonekana linapongezwa na kila mtu, lakini *consequences* zake; leo tuna taarifa kwamba *Acacia* wanakwenda Mahakamani London. *Concequences* zake Taifa hili litakuja kuingia kwenye gharama kubwa kama lilivyoingia kwenye ile minofu ya samaki na meli kule Dar es Salaam. Kwa hiyo, ni muhimu tukajenga mahusiano. Siasa na biashara ni vitu vinavyofanana. Mwanasiasa imara, mwanasiasa makini ni mwanasiasa atakayejua maana ya uchumi. Hawa wananchi wanaoshangilia leo, baada ya miezi miwili, mitatu watakosa chakula; wakishakosa chakula itakuwa rahisi kuingia barabarani kuliko wangeingia barabarani kudai mikutano ya hadhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashangaa mnafanya nini? Leo uchumi umeyumba. Ukienda hapo Kenya, tumemwona Uhuru Kenyatta amekwenda kwenye mkutano wa *G7 Summit.* Uhuru anakwenda ku-*present paper* kuhusu Taifa lake. Leo *Peugeot* wameweka *plant* yao kule Kenya, kiwanda cha magari kinakuja Kenya. Unajiuliza, hivi kweli Wizara ya Mambo ya Nje inafanya nini? Ukienda kwenye Ubalozi, Mabalozi wanalia. Kama mishahara yao haifiki kwa

wakati, wanawezaje wakafanya hiyo *connectivity* ya kupata wawekezaji kuja huku? Kitakachoondoa wawekezaji, hata hii bajeti mnayopitisha, mimi mwenyewe ningekuwa ni mwekezaji, nasikia mambo mnayoyafanya kwa hizi *multinational companies,* ningevuta subira kwanza nione hali inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni shahidi kwamba Wazungu wanapokuja kufanya *investments* za mabilioni, wanaangalia pia *future* ya nchi hiyo kisiasa. Leo nchi hii masuala ya kidemokrasia yamepigwa marufuku, leo nchi hii mikutano ya hadhara imepigwa marufuku. Maana yake, kwa *investor* yeyote ambaye yuko *serious* anataka kuja kufanya *investment* ya hela nyingi atasema Taifa lile hawana *political stability.* Maana yake ni nini? Maana yake hawatakuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lema. Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, ajiandae Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote naomba niwatakie Waislam wote nchini na duniani kote Ramadhan Kareem. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais, Jemedari wetu kwa tendo lake la kihistoria na la kizalendo kabisa juu ya suala zima la mchanga wa dhahabu unaojulikana kama makinikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mikataba mibovu na kukosa uzalendo ndivyo vilivyotufikisha hapa tulipo, wala siyo siri. Pamoja na hayo, hii ni vita yetu sote Watanzania, kama Mheshimiwa Lema alivyozungumza, Mama Mheshimiwa Profesa Tibaijuka naye amezungumza masuala ya *UNCTAD,* lakini lazima tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu. Hii vita ni yetu sote kwa vizazi

na vizazi vijavyo, kwa sababu vita hii aliyoanzisha Mheshimiwa Rais ni vita ya uhuru wa nidhamu na uchumi katika masuala mazima ya kidiplomasia ya uchumi. Nina uhakika hata Mheshimiwa Waziri husika naye ataliweka hili jambo kidiplomasia zaidi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa dakika tano ni mdogo. Sasa kama mtu ana taarifa, andikianeni vi-*note* hapo. Endelea Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hakuna upande utakaopewa taarifa *as of now. (Kicheko)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kulinda muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kuzungumzia kwa uharaka sana ni suala zima la *commercial attaches* wetu katika Balozi. Nimekuwa nikisema hili kwa muda mrefu sana, kuwa Mabalozi wetu na *commercial attaches* wetu kwa diplomasia ya kiuchumi ambayo imeanza tangu mwaka 2001, tunahitaji Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atueleze *performance targets* zao kama wanapewa ama hawapewi kwa maana ya kwamba, je, wanapewa *marbles?* Vilevile *mid reviews* zinafanyika ama hazifanyiki? Tunaomba hilo tuweze kuelezwa kama wanafanya kazi kimkakati, basi tunahitaji wawe kimasoko zaidi na matokeo chanya tuweze kuyaona. Vinginevyo ikishindikana nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 18 mpaka 50 amezungumzia *conference diplomacy,* tunampongeza, matokeo chanya tumeyaona, sihitaji kwenda kwa urefu na mapana ni viongozi gani ambao wameweza wakijadiliana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la *shuttle diplomacy.* Mimi natoka katika Mkoa wa Mbeya, kuna Ziwa Nyasa ambalo mgogoro wake ni wa muda mrefu sana. Hii *shuttle diplomacy* kama imeshindikana, *worse to worse* basi tuingie katika *sanctions* kama ambavyo iko kule katika nchi ya Burundi. *Shuttle diplomacy* naona haifanyi kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakaa, naomba niipongeze Serikali kwa kufungua Balozi mbalimbali pamoja na Ubalozi wa Israel. Nimekuwa nikilia kwa muda mrefu sana lakini nikasema pia wengine kule sisi ni Taifa teule, ndiko tunakokwenda kuhiji na pia kama nchi mengi tunajifunza kutoka kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ni mfupi, naunga mkono hoja, nakushukuru. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Mbilinyi hayupo, basi nitampangia. Subiri Mheshimiwa Lissu, tunakwenda na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud.

**MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa dakika hizi chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Muendelee kushika uzi huo huo wa utekelezaji wa majukumu yenu kama mlivyopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni dakika tano, naomba nichangie kitu kimoja, Wizara hii ni nyeti sana, ni Wizara ambayo inaonesha uso wetu nje ya nchi. Ikiwa leo Bunge linaamua kuiwekea siku moja ya kuchangia ni dhahiri kwamba Wabunge wengi hawataweza kutoa mchango wao wa kutosha wa kuweza kuboresha ofisi zetu kwa Watendaji walioko nje ya nchi. *(Makofi)*

Hivyo, naiomba ofisi hii iendelee kufikiria zaidi jinsi ya kuipatia nafasi Wizara hii ipate michango mingi ili iweze kuboresha zaidi na kuonesha sura nzuri nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo muhimu yanayotakiwa kufanywa nje ya nchi kwa sasa ni pamoja na kuboresha majengo yetu. Majengo mengi ya Wizara hii nje ya nchi hayapo katika hali nzuri. Kweli tuna uhaba wa fedha, lakini bado utumike utaratibu mwingine wowote utakaowezekana kuhakikisha tunaonesha sura nzuri nje ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao hawajafika, sisi wengine tumeona, nchi mfano ya Msumbiji, hali ya Msumbiji siyo nzuri. Ukiangalia na sisi tabia hii tuliyoipata sijui tumerithi wapi? Tabia ya kwamba mtu nyumba yako ikichakaa unahama, ni tabia gani? Nyumba ikichakaa hurekebishwa na baadaye uendelee kuishi ndani ya nyumba hiyo. Balozi amehama kwa kuwa nyumba imechakaa, amepangishiwa nje. Tunapoteza fedha nyingi sana kwa kupangisha nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi naishukuru Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutumia fedha katika kipindi hiki kifupi kwa ajili ya pango la Balozi kutengeneza ile nyumba ya Balozi kule Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naiomba Serikali na Wizara hii waendelee kuweka kipaumbele kuhakikisha jengo la ghorofa tisa nchini Msumbiji linamalizika haraka kwa kuwa hii ni njia moja itakayotukomboa na kuhakikisha kwamba tunafanya kazi nzuri, tunaboresha nyumba zetu na wafanyakazi wetu wanaishi katika mazingira mazuri. Ni kweli, nchi nyingi tulizo na Ubalozi hatuna majengo mazuri, lakini kama Wizara na Serikali itatoa kipaumbele kutoa fedha za kutosha, nina uhakika Watendaji katika Wizara hii wanaweza kufanya kazi nzuri sana na ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba niachie nafasi wengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa muda huu mfupi niliopewa nitakuwa na jambo moja tu la kulielezea, nalo ni hali halisi ya balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na takribani wiki mbili zimepita tulipata fursa ya kutembelea Balozi mbalimbali ikiwemo Sweden, *South Africa* na Maputo. Mimi binafsi nilipata kutembelea Ubalozi wa Maputo, kwa hiyo, saa hizi nitaelezea hali halisi ambayo tumeiona kwenye Ubalozi wetu na mradi ambao unaendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mchango mkubwa ambao Taifa letu liliutoa kwa nchi ya Msumbiji, Serikali hiyo ilitupa jengo la Ubalozi, nyumba ya Balozi na uwanja ambao uko mkabala na jengo hili la ghorofa tisa. Mwaka 2012 Serikali iliamua kufanya matengenezo ya Ubalozi huu kwa sababu hili jengo limeanza kutumika toka mwaka 1975. Sasa kwa kuwa mradi huu ulikuwa *viable* tukapitisha kuwa jengo hili lifanyiwe ukarabati. Mradi huu umechukua muda mrefu sana, sasa hivi ni takriban miaka mitano na imeisababishia Serikali hasara kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tunatumia dola za Kimarekani 240,000 kila mwaka kuhakikisha tunalipia nyumba ya Balozi na watumishi kwa ajili ya kuendesha shughuli za Ubalozi nchini Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, *you know this is not reflecting well on our part.* Haiwezekani tukawa tumepewa jengo, tumepewa kiwanja, tumepewa nyumba ya Balozi na sisi tunaendelea kupoteza pesa hizi kila mwaka kulipia pango.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, wewe umekuwa ni mwanadiplomasia mzuri, nakuomba, hizi pesa ambazo zinaombwa kuhakikisha tunamaliza jengo hili zipelekwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tuko Msumbiji tuliweza kuonana na Mkandarasi akasema anadai dola za Kimarekani 888,000. Akipewa pesa hizi, ataweza kukamilisha jengo hili *within two months. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulinda heshima ambayo nchi ya Msumbiji ilitupa Tanzania, tuhakikishe tunaendeleza hata kile kiwanja ambacho kiko pale. Kama Serikali inashindwa kujenga kiwanja hiki, basi iwashirikishe Shirika la Nyumba waweze kwenda ku-*develop* lile eneo kwa sababu *demand* ya *real estate* Mjini Maputo ni kubwa sana. Tukimaliza ghorofa hili tuna uwezo wa kuiingizia Serikali shilingi milioni 600 kwa mwaka ambayo itatusaidia sisi ku-*service* ule Ubalozi wetu na kusaidia balozi mbalimbali ambazo zinazunguka Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe ule Ubalozi wa Msumbiji unatengenezwa kwa wakati, *image* yetu pale haionekani vizuri. Nina uhakika miezi miwili ijayo tutaweza kufungua Ubalozi huu ili uweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namuita Mheshimiwa Mahawe. Mheshimiwa Ester Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa namshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kuthubutu kuthubutu kuanza kushughulika na masuala haya ya mchanga wa dhahabu, makinikia kwa lugha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tunalalamika sana kwamba kuna mikataba mibovu tumeingia, tunapata hasara, hatulindi rasilimali za nchi. Leo Mheshimiwa Rais amethubutu kufanya hiki, ninashangaa

kuna watu wanabeza hiki kinachoendelea. Ni ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatua kubwa sana ambayo Rais ameifikia, sisi kama wananchi wa Tanzania bila kujali itikadi zetu za vyama, ni lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa hatua hii. Hata kama kungekuwa na *concequences* zozote ambazo nchi inakwenda kuzipata kwa hili ambalo Rais amelifanya, ni lazima tukubaliane kama nchi kwamba hili ni letu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wale wanaoanza kutoa lawama bado mapema, tayari Wizara ya Nishati na Madini inakuja, tusubiri, tuache nafasi ya Wizara nyingine kuendelea kuchangia kuhusu hili suala zima la mchanga wa dhahabu. Kwa hiyo, naomba tuwe na kumbukumbu kwamba tuliilaumu sana Serikali kwamba haichukui hatua, sasa Mheshimiwa Rais amechukua hatua. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hatua hizi zikiendelea kuchukuliwa, uchumi wetu unakwenda kutengemaa na hatimaye maisha mazuri yaliyoahidiwa yanakuwa ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia, dakika tano.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, sikitiko langu ni sawasawa na Wajumbe waliopita. Tatizo la bajeti, Bunge tunapitisha lakini mwisho wa siku pesa haziendi kwa wakati kwenye kasma ambayo sisi tumeipelekea. Sasa Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujibu hoja yako jioni, ninaomba utuambie safari hii utafanya nini kuhakikisha fedha hizo zinafika kwa wakati hasa zikasaidie kazi za Balozini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunazungumzia uchumi wa kidiplomasia. Sisi kama Kambi, Mbunge wetu ameelezea vizuri sana ni jinsi gani inabidi tujikite kwenye uchumi wa kidiplomasia. Na mimi nazidi kusisitiza kwamba bila kuwa na uchumi wa kidiplomasia hatuwezi kufanya vizuri kwenye zama hizi za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunafahamu biashara nyingi sana zinaendelea, lakini kundi kubwa la wanawake ambao ndio wajasiriamali wakubwa, sijaona kama Wizara imefanya juhudi za makusudi kuweza kutambulisha fursa hizo za kijasiriamali kwa wanawake wa Tanzania kwa ujumla wake. Kuna maonesho mbalimbali yanafanyika, likiwemo Jua Kali na mengineyo, sijaona kama Wizara imetangaza hata kwa kutumia Televisheni ya Taifa kuwaeleza wanawake wa Tanzania kuzijua hizo fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni ya muhimu sana. Tunajua kwamba Mabalozi wanalipwa mishahara kule waliko. Wanatumia juhudi gani kuitangaza Tanzania hasa katika maeneo ya kiutalii pamoja na mambo mengine ambayo watu wetu wanaweza wakanufaika na hizo nchi. Nadhani ifike wakati tupeleke wataalam na kama wapo, wapewe onyo kali wasipofanya kazi zao na wajibu wao wa kuitangaza nchi katika hizo nchi wanazokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tuna tatizo katika Wizara hii. Balozi mmoja, kwa mfano Balozi wa Msumbiji, anasimamia na Balozi nyingine zinazomzunguka. Ni kweli tunabana bajeti, lakini mwisho wa siku ufanisi unakuwa mdogo kwa sababu hakuna pesa zinazokwenda mahali pale. Kwa hiyo, nashauri bado ninafikiri tuna wasomi wengi katika Taifa hili, ninaomba wapewe nafasi za Ubalozi katika hizo nchi badala ya kutegemea Balozi mmoja kusimamia Balozi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie Chuo cha Diplomasia, Kurasini. Chuo kile ni cha muhimu sana na wote tunajua kwa nini kilianzishwa. Hivi tunavyoongea kile

chuo wenzetu wa Msumbiji walijitoa, lakini pia hatuna pesa ya kukiendeleza kile chuo. Mapato yanayotumwa kwenye kile chuo ni madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja tunaomba atuambie, tunasimamiaje chuo kile ili kiendelee kutoa Wanadiplomasia makini katika Taifa letu la Tanzania? Tunataka kujua kwa nini wenzetu wa Msumbiji walijitoa na wengineo? Basi watuachie tubadilishe matumizi ya chuo kile kiweze kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki na lile jengo letu la *AICC* pale Arusha. Nataka kujua linasaidiaje? Kwa sababu ninaamini pesa zinazopelekwa bado ni ndogo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa haraka haraka, napenda kukushukuru. Naishukuru Wizara na Watendaji wote kwa ujumla kwa mawasilisho ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nateta na mwenzangu hapa, nikawa najiuliza kuna kila sababu sisi kama Bunge kwa nafasi yetu Kikatiba kuna mambo bila kujali itikadi lazima tuwe kitu kimoja kwa maslahi ya Taifa. Sasa hata kama uzalendo wako ni wa mashaka, kwenye suala hili la mchanga mimi matarajio yangu kuna mambo tunaweza tukabishana kwa kutafuta kiki na kadhalika, lakini kwenye masuala kama haya ya mchanga wa dhahabu *my dear friends, brothers and sisters* hili jambo ushauri wangu, nawaomba tuwe kitu kimoja, tuwe nyuma ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuwape *mileage,* mtu anazungumza eti atashitakiwa kwenye Mahakama za

Kimataifa, si zipo! Kazi yake ni nini? Tutaenda, tutakutana huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge kuna mambo hebu tuweni kitu kimoja; tunaweza kujijengea huko nje kwa wananchi, ni aibu kubwa sana *especially* kwa jambo hili. Jambo hili hata mtu ambaye ni *layman* analiona kwamba ni jambo la thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna Tume nyingine ambayo inafiti ni namna gani tumeibiwa sisi na kuhujumiwa kiuchumi katika suala la mchanga. Sitarajii kwamba suala hili tuwe *against* kwa mipango mizuri hii ya Serikali, kwa sababu tunalia maji, tunalia dawa, sasa tunalia majengo. Juzi tumesema zahanati hazijakamilika, tunalia hapa majengo huko Ubalozini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo kama haya tushirikiane kuunga mkono jitihada hizi. Nami ningetegemea hata ambao ni Wanasheria nguli wa nchi hii, sasa wajipange kwamba kama Serikali itapelekwa kwenye hizo mahakama wao watakuwa msitari wa mbele kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba wanatetea maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuna mambo hebu sisi tuwe *united*, tuwe kitu kimoja. Tusipinge tu *simply because* itikadi zipo tofauti. Haya ni mambo yanagusa maisha yetu, ni mambo yanagusa maisha ya vizazi vyetu. Kama kuna makosa yalifanyika, hatuwezi kukaa macho tukasema sasa tuache tuendelee tu kukosea, hiyo haiwezekani kwa sababu kulifanyika makosa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dakika pia ni chache, ningependa kuzungumzia pia umuhimu wa Wizara kuhakikisha kwamba inapeleka Maafisa katika Balozi zetu. Maafisa wapo wachache, kuna baadhi ya Balozi unakuta Balozi yupo mmoja, hana Afisa wa kumsaidia kufanya kazi na Balozi huyu ni mgeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lissu, dakika tano.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi nimepinga sera za uwekezaji za Chama cha Mapinduzi kabla sijawa CHADEMA, kabla sijaja Bungeni toka mwaka 1999. Yaliyofanyika na Mheshimiwa Rais Magufuli juzi ni ya hovyo, nitayapinga kama ambavyo nimepinga sera zote ambazo zimetufikisha leo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa kifupi. Hoja iko hivi, kwa haya ambayo yametendeka, sahauni kabisa diplomasia ya kiuchumi. Suala siyo *Acacia* watafanya nini? Suala ni kwamba watu wote tunaohusiana nao kiuchumi, Wachina ambao ndio *the biggest investors in the world today* na ndiyo *biggest proponents* wa *free trade* na *globalization today.* Fikiria Wachina watafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria *EU* watafanya nini? *United States,* ile *North America Economic Group* itafanya nini? Japan, *all the major economic blocks of this world* fikiria zitafanya nini kwa sababu ya kitendo kimoja tu cha kunyang'anya michanga ya dhahabu kwa hoja ambazo, kwa wanaojua; sizungumzii wasiojua, washangiliaji hawa, kwa wanaojua, ni hoja za kijinga. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Sasa…

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa sasa hivi nilishasema. Endelea Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kwamba leo hii kiuchumi dunia hii ni *multipolar,* mwanadiplomasia wetu ataelewa nikisema *multipolar* wengine wote hawa ni wapiga debe tu. Leo hii… *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu tumia lugha za Kibunge. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna kitu kinaitwa *Silk Road Economic Belt*, kuna kitu kinaitwa *The 21st Century Maritime Silk Road, these are the biggest economic initiatives in today's world economy. We are not a member!* Kenya ni *member* wa *21st Century Maritime Silk Road* yaani Kenya ya leo ndiyo marafiki wakubwa wa kiuchumi wa China kuliko sisi ambao tumekuwa marafiki wa China wa miaka yote, kwa sababu tunazungumza *economic diplomacy, we don't know nothing about the economic diplomacy.* Ndiyo maana tunafanya haya tunayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, ni mwanadiplomasia, anafahamu haya, asikubali hizi kelele, nchi yetu sasa hivi ina hali mbaya kidiplomasia kwa sababu tumefanya kitu ambacho kisheria ni makosa kwa mujibu wa sheria zetu, kwa mujibu wa mikataba ni makosa, kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa ni makosa na gharama tutakayolipa ninyi Wabunge mnaopiga kelele, gharama tutakayolipa ni kubwa kuliko huo mchanga wa *Acacia. We will become an economic busket case* kama Zimbabwe. Tusishabikie maamuzi ya kijinga kwa sababu tu yamefanywa na Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, kaa chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina taarifa, ninaenda kwenye utaratibu. Ninaheshimu sana uamuzi wako kwamba michango inapotolewa tusije kwenye taarifa.

Mimi naenda kwenye utaratibu na ninarudi kwenye Kanuni ya 64(1)(g) kwamba Mbunge anapochangia humu ndani hatatumia lugha ambayo ni ya kuudhi na inadhalilisha pia watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Lissu angeweza kuchangia hoja zake, lakini ukimsikiliza mchango wake toka ameanza, anatumia lugha ambazo siyo za Kibunge, ni za kuudhi na udhalilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba utuongoze, Mheshimiwa Tundu Lissu afute hizo lugha zake ama achangie kwa kutumia lugha za Kibunge na siyo hizo lugha ambazo zinakatazwa kwa mujibu wa kanuni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lissu ni kweli kwa hii Kanuni yetu ya 64, umetumia maneno ya kidhihaka, mikataba ya kijinga na nini, naomba uyafute uendelee na shughuli yako.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba tumefanya maamuzi ya hovyo sana. Kama kuna lugha ambayo imekera watu kwa yale niliyoyasema, nawaomba msamaha, yafutwe. Ndiyo nasema hoja ni kwamba *we are making a terrible mistake...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, futa tu hilo neno lako.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Nimefuta, lakini sikuambiwa nifute yapi...

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hayo ambayo yamewakera, nimeyafuta, naomba nimalizie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, kazi za Mawaziri ni kumshauri Rais. *Our economic diplomacy and our economic development is on the brink* kwa sababu tumeharibu mahusiano. Kwa hili tu, tumeharibu mahusiano ya kiuchumi kila mahali. Siyo na *Acacia.* Suala siyo kupelekwa mahakamani tu, suala ni kwamba mwekezaji gani atakayetaka kubakisha hela zake hapa? Mwekezaji gani atakayetaka kuleta hela zake hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema siyo Wamarekani na Wazungu tu, fikiria na Wachina ambao ndiyo wawekezaji wakubwa wa dunia hii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shonza, jiandae Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini vilevile nawapongeza kwa dhati Serikali ya Awamu ya Tano kwa jitihada kubwa ambazo imezifanya katika kukuza diplomasia ya kiuchumi na hatimaye kufanikisha kufungua Balozi sita ambazo ni Balozi mahususi kwa ajili ya kukuza biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja; nimeshangazwa sana na uchangiaji wa baadhi ya Wabunge humu ndani. Walipinga ndani ya Bunge hili wakisema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi Rais wake ni dhaifu. Leo hii tumempata Rais ambaye ni mchapakazi, tumempata Rais ambaye anasimamia maslahi ya umma, maslahi ya Watanzania masikini, wamegeuka na kusema kwamba anafanya maamuzi ambayo ni ya hovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwanza nichukue nafasi kuweza kuwakumbusha, wanasema ukiwa mwongo usiwe msahaulifu. Ni wewe mwenyewe kaka yangu Mheshimiwa Lissu ulisimama na kusema kwamba CCM imempa fomu ya kugombea Urais fisadi Lowassa, lakini ni wewe mwenyewe ambaye ulizunguka kumnadi Lowassa katika nchi hii. Sasa naomba niulize swali, je, kuna maamuzi ya hovyo kama hayo kusema mtu ni fisadi na baadaye mzunguke kuanza kumnadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Lema alisema kwamba ni heshima kwa Mungu kumzomea na kumpiga mawe mtu kama Lowassa, lakini wewe ndio ulizunguka nchi nzima kumnadi. Jamani mnapoongea maneno, msiwe wepesi kusahau. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme jambo moja, hawa watu wameshazoea sana kila kitu kinachofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi wamekuwa wakikipinga.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, kaa chini *please!*

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu ambacho Serikali hii inafanya wao wamekuwa ni wapondaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijashangaa kuona hawa wenzetu wawili wanaponda jitihada za Mheshimiwa Rais Magufuli, kwa sababu hawa kila kitu kinachofanywa wao wamekuwa ni wapondaji; wamejipa vyeo vya kuwa mtoto wa kambo kwamba kila kitu lazima wao walalamike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inahitaji Rais kama Magufuli. Hata kama, hatuwezi kuona kwamba tunakuza diplomasia ya kiuchumi wakati tunaendelea kuibiwa. Kwa hiyo, huu utaratibu wa kuendelea kutetea wezi, tumeshauzoea, ninyi wenzetu kazi yenu kutetea wezi na ndiyo maana mko tayari kwamba Taifa hili liendelee kuibiwa dhahabu eti kwa sababu tu tunakuza diplomasia ya kiuchumi. Hilo jambo haliwezi kukubalika na tunaomba tumpe nafasi kama Rais aweze kutimiza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba mngekuja kushauri, lakini ninyi mmekuwa watu wa kulalamika. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba Mheshimiwa Rais aendelee kuchapa kazi, huu ni wakati wetu

wa sisi kuchapa kazi na hawa wenzetu waliojipa vyeo vya watoto wa kambo tuwaache waendelee kulalamika, hapa kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa niweze kuzungumzia suala la uhaba wa Maafisa katika Balozi zetu. Balozi zetu zinakabiliwa na uhaba mkubwa sana wa Maafisa... *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haji Khatib, baadaye Mheshimiwa Nsanzugwanko, mtagawana na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunirudishia dakika zangu tano kwa vile umetumia busara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pale ambapo nilibakiza. Nilisema ili kumaliza matatizo ambayo wavuvi wetu wamekuwa wakiyapata kule nchini Kenya, basi ni vyema Serikali hizi mbili zikarudi kwenye mkataba ambao Serikali hizi mbili Mawaziri wetu wa Mambo ya Nje walikubaliana na kusaini. Kwa hiyo, ninao hapa naomba Watendaji wachukue ili wampatie Mheshimiwa Waziri ili jambo hili liweze kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, mimi nikiwa mmoja ambaye niliteuliwa kwenda nchini Afrika Kusini, Pretoria, tulipofika Ubalozi tulipatiwa taarifa ya majengo nane ambayo tulienda kuyakagua. Katika jengo moja ambalo tulilikagua na kupewa taarifa yake ni jengo ambalo linamilikiwa na SMZ yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jengo hili kunataka umakini mkubwa sana. Katika Serikali ya SMZ kuna chombo cha kutunga sheria kama vile Bunge la Jamhuri ya Muungano

na katika Baraza la Wawakilishi ziko Kamati za Kisekta ambazo zimekuwa zikizungukia miradi na kuona miradi ambayo inamilikiwa na SMZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri atutoe wasiwasi hapa wakati wa ku-*wind up:* Je, kuna utaratibu wowote au kuna makubaliano yoyote ya jengo hili ambalo linamilikiwa na SMZ ambalo sasa hivi linataka kuingizwa katika Jamhuri ya Muungano? Je, endapo litakuwa hivyo, hakuna maneno yoyote? Hakuna malalamiko yoyote ambayo yanaweza kuleta shida huko mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la pili ambalo tulienda kulikagua ni jengo la *Tanzania House* ambayo ni Ofisi ya Ubalozi. Jengo hili unapoliangalia katika sura ya mbele utaliona ni zima, lakini ukweli ni kwamba jengo hili limeshafanya *crack* au nyufa. Jengo hili utashangaa kwamba nyumba ya Balozi na Maofisa ziko vizuri, ziko salama, lakini unapokuja katika jengo la Ofisi ya Ubalozi maisha ya Maafisa Ubalozi wetu tunayaweka rehani. Tusiombe litokee tetemeko la aina yoyote. Endapo kutatokea tetemeko la aina yoyote, basi tunaweza kupoteza Maafisa Ubalozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jengo ambalo linakaliwa na Afisa Ubalozi wetu ambaye anaitwa Rose Jairo. Jengo hili kwa bahati mbaya sana na hali halisi ya nchi ya Afrika ya Kusini na usalama wa nchi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko, dakika hizo hizo utagawana na nguguyo Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nitakuwa na mambo machache sana. Mheshimiwa Waziri Balozi Mahiga wewe ni Waziri

mzoefu nina uhakika yote yaliyosemwa utatuonyesha njia, namna ya kutoka hapa tulikofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili; katika hotuba yote hii, Mheshimiwa Balozi Mahiga hujaweka hata sentensi moja kuhusu wakimbizi *(refugees).* Katika Mkoa wa Kigoma tumekuwa na wakimbizi tangu miaka ya 1960 na nilidhani kupitia diplomasia yetu hii ya mahusiano na majirani zetu, ni wakati muafaka sasa kwamba wakimbizi hawa wangerudi kwao. Wewe unajua, Mkoa wa Kigoma una raia zaidi ya nusu milioni wanaotokea katika Jamhuri ya Congo, Burundi na Rwanda. Leo *DRC* mambo siyo mabaya sana Kusini mwa *DRC,* watu wao hawa wangeweza kwenda kuhifadhiwa katika *DRC* na makambi yakawa ndani ya *DRC,* hivyo hivyo kwa Burundi na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa sababu muda wenyewe ni mdogo, nizungumzie juu ya huu mpango kabambe wa *UN.* Naomba unisikilize. Mpango kabambe wa *UN* wa kusaidia maeneo yaliyoathirika na ujio wa wakimbizi *(Refugee Hosting Area Program).* Wewe na Wizara yako na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mna uwezo mkubwa mkakaa na hawa *UNHCR* mkaja na program ya kusaidia maeneo ambayo tumekaa na wakimbizi kwa miaka zaidi ya 60 *in this country.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana muda wenyewe ni mdogo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini kwamba mtatoa majibu yanayofaa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi. Moja ni suala la Ubalozi

huko tuliko kwenye viwanja vyetu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, viwanja maeneo mazuri Nairobi; ukienda nyumba yetu pale London; ukienda Sweden; kote ninaamini tukiweka uwekezaji tutapata fedha za kuendesha Balozi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa suala la kufungua Ubalozi na watu wa *Israel* na tumeona faida zake, sasa tumeanza kupata watu wanakuja kutalii kutoka Israel. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, mimi kama mwanasiasa, ukiona mtu ambaye ni adui yako umefanya jambo akakusifia, ujue liko tatizo. Ukiona umefanya jambo adui yako akasema umekosea, maana yake umepatia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Taifa. Nami naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyofanya. Niwambie Waheshimiwa Wabunge, naomba niwambie duniani kote, *extractive industry* inaenda kubadilika na atakayekuwa kwenye historia amebadilisha *extractive industry* ni Mheshimiwa Rais Magufuli. Leo duniani kote, kwenye kila mgodi mambo yatabadilika kwa sababu sasa ilikuwa ni vitu vinatengenezwa, mnaambiwa kuna tatizo, lakini sasa amefungua mlango. Nina hakika kila ambako kuna *extractive industry,* mambo yatabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwambieni Watanzania tusiogope. Kwenye hili lazima kama nchi tuwe nyuma ya Mheshimiwa Rais, tumuunge mkono aendelee. Ninayo hakika wawekezaji watakuja mezani. Wakati fulani ili watu waje mezani lazima na pa kuanzia. Kama ni suala la ku-*negotiate,* ume-*negotiate* toka mwaka 1999, hatujapata vya kutosha. Nadhani umefika wakati, hii ndiyo ilikuwa njia ya kuleta haya mabadiliko ambayo nina hakika tutayapata kama Taifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, huu siyo wakati wa kutupiana maneno...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Ni wakati wa kufikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kutumikia Watanzania hasa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu tukufu itoe ajira kwa Balozi zetu hasa wachumi, kwani inavyoonesha kwenye Balozi zetu wachumi ni wachache mno, hii itapelekea kukuza na kuitangaza nchi yetu kiuchumi katika mataifa ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vijana wengi wanaomaliza Chuo cha Diplomasia lakini wanakaa kwa muda mrefu bila kupata ajira, ni ushauri wangu vijana hawa Serikali iwachukue kwa mkataba wa muda wakati huo huo wakiendelea kupata uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu, kuna hawa wageni kutoka nje na wamekaa kwa muda mrefu na kuwekeza hapa nchini na wakati huo wanasaidia misaada mbalimbali. Mfano kujenga shule, kujenga zahanati na kujenga hosteli kwa njia ya kusaidia wananchi wanaoishi maeneo yanayowazunguka. Pamoja na hayo wafadhili hawa kwa sasa wamezuka na wanataka kurudi makwao, sababu ya kurudi kwao wanasema kwa sasa wamezeeka na pia kodi ya makazi ya kuishi nchini ni kubwa

hivyo labda Serikali iwasaidie kupunguza *fee* hiyo au kuondoa kabisa kwa sababu bado wanaendelea kusaidia jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali watu hawa wangepewa uraia wa Tanzania ili waweze kusaidia jamii yetu, ukizingatia watu hawa wamechoka na wamezeeka.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu, uzidi kumpa afya na nguvu na umzidishie umri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira za nje na ushirikiano wa kimataifa kwa Afrika na Afrika Mashariki ni kubwa nchini lakini kuna tatizo katika ushirikiano huu, nafasi za ajira zimekuwa zinatangazwa muda mwingine kwa kufichwa, wananchi wanakuja kushtuka watoto wa wakubwa ndiyo wameajiriwa kimataifa huku watoto wa maskini hawapati fursa hizi. Je, kupitia tatizo hili ni ubaguzi huu kati ya watoto wa maskini na matajiri, Serikali imejipanga vipi kuondoa ubaguzi na urasimu wa ajira za kimataifa? Usawa uko wapi, ni lini watoto wa maskini watafarijika katika Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uchakavu wa Balozi Nje ya nchi, Balozi zina hali mbaya, tunapoteza fursa za uwekezaji, Balozi zinadaiwa mapango ya nyumba za ofisi na nyumba za watumishi ziko hovyo. Kwa bajeti hii moja kwa moja haioneshi kwamba inaweza kumaliza changamoto hizi katika Balozi zetu za Zimbabwe, Mozambique, Botswana na *South Africa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa Serikali kusaidia wanafunzi waliopo masomoni katika nchi korofi, hivi karibuni yamejitokeza matatizo kwa wanafunzi wanaosoma nchi za nje, huko waliko kuna ubaguzi, vita, mitafaruku na wafanyakazi wa ndani kuuwawa nchi za nje, kutokana na matatizo hayo Serikali hii ya CCM haijawahi

kusaidia moja kwa moja. Mfano tatizo la unyanyasaji na usafirishaji wa wafanyakazi wa ndani nchi za nje. Je, nini mkakati wa Serikali kupitia bajeti hii ihakikishe inasimamia waajiri wanaonyanyasa Watanzania wenzetu inaonekana nchi haiko katika mstari wa kusaidia/kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali/utawala huu utaacha ukandamizaji wa demokrasia nchini ili sasa hawa wawekezaji na ushirikiano wa nchi jirani na nchi za Ulaya ili waone kwamba kama watawekeza basi watakuwa katika nchi salama, lakini kadri siku zinavyoenda wawekezaji wanapungua? Je, hamuoni kuwa tunapoteza uchumi?

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza kwa uwasilishaji wote mzuri. Naishauri Serikali kupeleka fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kukidhi matumizi ya balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kukarabati au kujenga ofisi zake za balozi nchi husika ili kuondokana na upangaji aghali. Naishauri pia Serikali kufuatilia urasimu unafanywa na Mabalozi kuhusu wawekezaji wanaotaka kuwekeza Tanzania, wafungue milango ya Tanzania ya uwekezaji badala ya kuwapa masharti makubwa ambayo yanawakatisha tamaa wawekezaji.

Pia niishauri Serikali kufuatilia balozi zetu katika utendaji kwani vimekuwepo vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu kwa watu wetu wanaokwenda nje hali balozi zikishindwa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri pia Serikali kuangalia juu ya mipaka, mfano mpaka wa Tanzania na Malawi ambao una utata mpaka sasa hivi.

**MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa kuweka kipaumbele kutekeleza miradi ya ujenzi wa ofisi za balozi zetu nchi za nje ili kupunguza gharama za kukodisha nyumba kwa watendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kuibana Wizara ya Fedha ili ikamilishe fedha za ujenzi wa ofisi ikiwa pamoja na ukarabati wa jengo la Msumbiji ambalo endapo litamalizika basi litakuwa na tija na ukombozi mkubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna utata wa fedha zilizopelekwa Msumbuji na fedha iliyotolewa na Wizara ya Fedha. Je, shilingi milioni 900 ndiyo iliyotolewa au bado ipo fedha iliyobaki Wizarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu uliotumika Msumbiji wa kukarabati jengo la Balozi kwa kutumia fedha za pango ambazo zilikuwa zipangishiwe nyumba ya Balozi kufanyiwa ukarabati ni jambo jema sana, sehemu nyingine ifanyiwe ukarabati.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Wizara hii, hata hivyo nina ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya wakimbizi katika Mkoa wa Kigoma tangu tupate uhuru, Mkoa wetu wa Kigoma umekuwa ndiyo makazi ya wakimbizi watokao DRC, Burundi, Rwanda. Ni vizuri sasa Serikali yetu ikaanza mkakati wa kuwarejesha wakimbizi hawa kwao, kwa kiwango kikubwa DRC ipo salama katika maeneo mengi, kwa nini raia wao waliopo Nyarugusu mkoani Kigoma wasirejeshwe kwao na/ au kulindwa katika nchi yao? Kwa nini makambi haya yasifunguliwe ndani ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za wakimbizi ni nyingi sana ikiwa ni pamoja na usalama wa wanavijiji wetu, kusambaziwa maradhi mengi ikiwemo maradhi hatari ya Ebora na mengine mengi, Kigoma sasa inahitaji utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Kimataifa kusaidia maeneo yaliyoathirika na ujio wa wakimbizi katika Mkoa wa Kigoma, lazima Serikali sasa ibuni na ije na mkakati wa namna bora wa kusaidia wananchi wa Kigoma ambao

wamehifadhi wakimbizi tangu enzi ya Uhuru miaka ya 1960. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kusaidiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kaeni pamoja ili mjenge programu ya aina hii; "*Refugees Host Area Program*" Mheshimiwa Waziri *do something on Kigoma.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na nchi yetu kuwa na mahusianao na nchi mbalimbali duniani kuna kila sababu ya kuboresha maeneo muhimu ili kudumisha mahusiano makubwa na yenye manufaa kwa nchi yetu ikiwemo yafuatayo:-

Kwanza, kuunganisha soko la ndani ya nchi yetu na masoko ya nje kwa kufanya uboreshaji wa mazao yanayozalishwa nchini, kuyapandisha thamani ili yaweze kutumika nchi nyingine ambazo tuna uhusiano mzuri na nchi yetu, kupata manufaa kwa kupitia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kupeleka wanadiplomasia wenye uwezo. Kutokana na mazingira halisi ya nchi yetu ni vema wanadiplomasia nafasi zao zikawa na faida kwa nchi yetu, kwa kutumia uwezo wao kuchukua mambo ya nchi nyingine na kuyaleta nchini kwetu yalete manufaa. Kuwa na utaratibu wa kuunganisha Watanzania wanaoishi nchi za nje kulingana na kauli mbiu ya Awamu ya Tano, kauli mbiu ni viwanda ni vema Wizara hii ya mambo ya nje kuangalia ni jinsi gani watasaidia Taifa kuendana na kauli mbiu ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni namna gani Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi kubeba ajenda ya utalii ili Taifa letu liweze kunufaika na watalii, endapo kama Wizara itaweza kutangaza na kubeba ajenda ya utalii ili kupata fedha za kigeni pamoja na kujenga uhusiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Watanzania wanaoajiriwa nje ya nchi husussan kazi za ndani, wamekuwa

wakiuawa na kuteswa na kunyanyaswa ni vema Wizara ikawa na mipango endelevu ya kumaliza na kufuatilia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi ni mdogo sana, Wizara ni vema pamoja na Mabalozi waweze kuangalia kwa ukaribu wanafunzi wote na kuwapa misaada ambayo inaweza kuwa ndani ya uwezo wao.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar, hii itasaidia kuwa na jengo la ofisi ambalo lipo chini ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uraia wa nchi mbili *(diaspora)* ni jambo la siku nyigi lakini bado halijafanikiwa. Ofisi yako ukurasa wa 112 na113 ndiyo kwanza inasimamia usajili, ina maana fursa hii ya kuinua uchumi wetu wa Tanzania bado?

Kuhusu diplomasia ya kiuchumi hususan kwenda katika uchumi wa viwanda, hii vita ni kubwa na bado nchi yetu hatujajipanga, sababu elimu bado kutolewa kwa mabalozi wetu, Balozi anakwenda nchi za nje lakini haielewi Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Tunaomba elimu itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashairiki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ishughulikie suala la Watanzania wanaonyanyaswa katika nchi za nje hasa huko Uarabuni. Kuna mabinti wengi wanateswa na hata wengine wanauawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi hawana uelewa wa Wizara, hivyo kukosa fursa. Hivyo naiomba Wizara

kutoa elimu kwa wananchi wa Tanzania kazi ya Wizara hii. Pia majengo mengi ya Balozi ni chakavu, naiomba Serikali ikarabati majengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la diaspora bado halina nguvu, ninaiomba Serikali ilichukulie kwa umuhimu kwani inachangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kuwapa fursa mbalimbali za uchumi kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti ya Wizara huchelewa, naiomba Wizara kuhakikisha bajeti inatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi nchini ni wajasiriamali, mfano akina mama wana viwanda vidogo vidogo kama vile vya kushona vikapu, kutengeneza vinyago, vyungu na vitu vingine, ninaiomba Wizara iwakumbuke akina mama ili waweze kuuza bidhaa zao nje ya nchi na waweze kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe kipaumbele katika kulipa michango ya nchi yetu kwenye Taasisi za Kimataifa ili kuepusha kukwamisha uendeshaji wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kurudia masikitiko yangu niliyoyatoa katika Mkutano wa Bajeti ya mwaka jana kuhusu muda mchache unaotengwa kujadili hoja ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa Bunge lako Tukufu ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo si haki kulinyima muda wa kutosha kujadili suala hili muhimu la Muungano. Ifike muda uongozi wa Bunge ubadili utaratibu uliozoeleka wa kutenga muda mchache wa kujadili Wizara za Muungano, zikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Wizara ya Muungano, (Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu kusikiliza na kusikia yaliyosemwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu hali ya utendaji ya Wizara hii na hali ya Balozi zetu nje ya nchi. Hivi ni kweli Serikali haioni umuhimu wa kuwa na majengo mazuri yenye hadhi kuwakilisha taswira ya nchi yetu? Ni aibu kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri husika aisome kwa makini hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na ayafanyie kazi yaliyomo kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona Wizara na Serikali kwa ujumla kuendelea kufanya kazi kwa mazoea. Bado Wizara hii haiainishi mkakati madhubuti wa kutekeleza Sera yetu ya Mambo ya Nje hasa kuhusiana na diplomasia ya kiuchumi. Hotuba ya Waziri haina taarifa yoyote kuonesha mkakati wa kuhakikisha nchi yetu inapata wawakilishi nje ya nchi na watendaji kwenye Wizara husika wenye sifa na walioandaliwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa Wizara yetu ya Mambo ya Nje wanatakiwa kuandaliwa katika maeneo mahsusi ya maeneo *(regional specialization),* kisha watendaji hawa walioandaliwa ipasavyo ndio wapande ngazi Wizarani na hatamae kuwa wawakilishi (mabalozi) wetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni mazoea, kwa Serikali kuteua mabalozi wa kutoka nje ya Wizara. Hii inakatisha tamaa watendaji wa Wizara lakini pia inadhalilisha fani ya mambo ya nje *(foreign service). Foreign service* ni *profession* kama zilivyo *professions* nyingine. Wahusika hupata mafunzo na kukidhi vigezo maalum.

Mheshimiwa mwenyekiti, wengi wamesema kuhusu Chuo chetu cha Diplomasia - Kurasini. Chuo hiki kitendewe haki, kipewe hadhi stahiki kwa kuhakikisha kinawezeshwa kujenga mazingira ya kufundisha maafisa wetu na vijana wetu kwa ujumla. Wizara ikisaidie Chuo kuwa na walimu mahiri na wenye maslahi mazuri.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia Wizara hii. Pia nawatakia Watanzania Ramadhani Kareem. Naunga mkono hotuba/ maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia kwa kuipongeza Wizara kwa kupata hati safi za ukaguzi wa mahesabu kasoro Ofisi moja tu ya Ubalozi wa Tanzania nje ya nchi. Ni vema wakati Waziri akifanya *winding up* aitaje ofisi hiyo ni ya Ubalozi wa Tanzania iliyo katika nchi gani na hatua gani zimechukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kutaka Serikali yetu kusaidia Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nchi za nje *(diasporas)* kupata haki na stahili zao, kuondoa manyanyaso kwa Watanzania lakini pia wabaki na *passport* zao katika baadhi ya nchi ambazo Watanzania wananyang'anywa *passport* zao na Serikali za nchi hizo. Kwa ufahamu wangu *passport* ni *document* halali inayotakiwa kumilikiwa na raia wa nchi husika. Je, inakuwaje katika baadhi ya nchi duniani Watanzania wakiajiriwa wanaporwa *passport* zao na Serikali za nchi hizo wanazofanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu demokrasia na haki za binadamu, kufuatia uchaguzi wa Zanzibar wa tarehe 25 Oktoba, 2015 ambapo matokeo yake yalibatilishwa kimazingaombwe hali iliyopelekea uchaguzi ule kurudiwa na Chama cha CUF na vyama vingine vya mageuzi kuususia na kuleta sintofahamu kwa wananchi, taarifa za *International Observers* nazo ziliweka wazi kuwa mshindi katika Uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba, 2015 alikuwa ni mgombea wa chama cha CUF, Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sakata hili imepelekea Taasisi ya *MCC* (USA) imefunga ofisi zake na kusitisha kutoa shilingi trilioni 1.06. Je, fedha hizi shilingi trilioni 1.06 sawa na US$ milioni 472.8 zingeendesha miradi mingapi ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Waziri aeleze kuna mikakati gani ya kufanya mazungumzo ya kutatua jambo hili ili *MCC* irudishe ofisi dar es Salaam na tuweze kurejeshewa shilingi trilioni 1.06 ambayo ni sawa na US$ milioni 472.8.

(ii) Je, hatutafanya makosa ya kuwekewa vikwazo vya kiuchumi kimataifa kwa kukandamiza demokrasia? Naomba Waziri afafanue.

(iii) Serikali ianzishe utaratibu Watanzania wanaoishi nje na kufanya kazi *(diasporas)* waruhusiwe kupiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu kama zinavyofanya nchi nyingine duniani.

(iv) Kuna nchi tulizopewa viwanja, majengo na rasilimali nyingine na tumeshindwa kuvijenga (Oman na Mozambique) lakini pia katika ofisi 35 baadhi ya majengo yamechakaa sana, zifanyiwe ukarabati.

(v) Mabaharia wa Tanzania waliosomea katika Chuo cha Bandari - Temeke Dar es Salaam wanasumbuliwa kuwa vyeti vyao havitambuliki kimataifa. Serikali ichukue hatua zinazostahili ili vyeti vya chuo hiki vitambulike kimataifa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue furasa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu akiongoza wataalam wa Wizara kwa kazi nzuri sana wanayofanya kusimamia sera na wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iangalie namna ya kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa na hasa fursa za uwekezaji ndani ya nchi yetu

lakini pia fursa za Watanzania kuwekeza katika nchi za Afrika Mashariki na nchi zingine.

Leo hii Watanzania wakihitaji msaada wa kupata taarifa mbalimbali za fursa hizo za kibiashara nje za Afrika Mashariki au zingine ni ngumu kupata. Wizara iboreshe Kitengo cha Uchumi Wizarani na kuwezesha Balozi zetu zote katika Kitengo cha Uchumi ili waweze kutusaidia kufanya biashara kirahisi na kujua utaratibu wa sheria na kanuni. Nipongeze Kitengo cha *Protocal* kwa msaada mkubwa wanaotupa sisi Watanzania tukisafiri.

(ii) Wizara ihamasishe Watanzania kutumia fursa mbalimbali zilizopo kibiashara.

(iii) Wizara ya Mambo ya Nje ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Elimu kuboresha mitaala ya elimu na kusaidia kupata vifaa na nyenzo za kufundishia masomo ya mahusiano ya kimataifa katika vyuo vyetu. Hali ni mbaya sana na wanaohitimu hawana viwango vya kufanya kazi waliosomea.

(iv) Wizara iangalie namna ya kuwatambua *diasporas* wetu hasa kwa wale waliokuwa Watanzania na sasa wamechukua uraia wa nchi nyingine *(Persons of Tanzanian Origin)* kwani wengi wao wamechukua uraia wa nchi nyingine kutokana na mazingira yao ya kupata huduma za kijamii kama afya, elimu, ajira na fursa zingine ambazo wasingezipata bila uraia wa huko. Nchi yetu haina utaratibu wa kisheria wa kuwa na uraia wa nchi mbili hivyo Watanzania hao walilazimika kuchukua uraia wa huko.

Pia Wizara ingeangalia utaratibu wa kisheria wapate kitambulisho kitakachowapa fursa ya kuwa watu wenye asili ya Kitanzania na waweze kuishi nchini na kuwekeza hapa kama Watanzania wengine ila wakose fursa ya kupata ajira ya Serikali, kuwa afisa au shughuli yoyote katika masuala ya ulinzi na usalama, kuchagua au kuchaguliwa (kupiga kura au kupigiwa kura).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itafanya hao waliokuwa Watanzania kuwa na fursa ya kuwekeza nyumbani (Tanzania) kwa urahisi sana. Nchi nyingi zimefanya hivyo na kuongeza mapato ya nchi kwa kuwapa haki hao waliokuwa Watanzania. Leo hii hawaruhusiwi kumiliki ardhi na wakitaka kuwekeza wanatakiwa kufuata utaratibu sawa na mtu asiye raia *(non Tanzanian).*

(v) Wizara hii iangalie namna ya kuwapatia Wabunge mafunzo mbalimbali hasa kuhusu itifaki kama walivyokuwa wanafanya miaka ya nyuma. Mafunzo haya yatolewe kwa Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano, Baraza la Wawakilishi na Wabunge wa *EALA*.

(vi) Kwa Wabunge wa *EALA*, muda huu ambapo bado hawajaanza kazi rasmi, wangepewa mafunzo maalum ya kuijua Afrika Mashariki, mikataba mbalimbali, nchi yetu inatarajia wafanye nini katika uwakilishi wao huko *EALA* pamoja na mambo mengine ambayo Wizara inaona ni muhimu wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kupongeza Wizara na timu nzima ya wataalam pamoja na Balozi wetu wote.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mchungaji Peter Msigwa kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni weledi na busara. Aidha, nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa jitihada kubwa anazozifanya katika kuleta mabadiliko ya kiutendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine duniani ni sharti uendane na utii wa Serikali yetu kwenye mikataba ya kimataifa. Mwaka 2016 Bunge la Kumi na Moja katika mikutano mbalimbali pamoja na mambo mengine lilipitisha Sheria ya Huduma ya Habari (*Media Services Act of 2016)* na Sheria ya Upatikanaji wa Habari *(The Access to Information Act*, 2016). Serikali ilieleza hapa Bungeni

kwamba utungwaji wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa au wengine wanaita *The Access to Information Act* kuwa utoaji wa taarifa siyo tena jambo la hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizo mbili hazikidhi matarajio ya wananchi na zimesheheni maneno matamu lakini yakiwa hayatekelezeki. Kinyume na matarajio ya wengi, sheria hazioneshi kwamba kutakuwa mwarubaini wa ukiritimba wa mamlaka za Serikali katika kutoa taarifa. Hii ni kwa kuwa zimepingana na dhana ya haki ya kupata taarifa na zimezika haki ya kikatiba ya raia kupata taarifa. Badala ya kusaidia wananchi kupata habari, sheria hizo zilizotungwa zitatumika kama kichaka cha kuficha udhaifu wa viongozi wasio waadilifu na zinaweza zikatumika hata kufungia baadhi ya vyombo vya habari. Hii ni kwa sababu ndani ya sheria hizo kumewekwa vifungu vinavyompa mamlaka mwenye taarifa kutotoa taarifa alizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(3) cha Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa kimetaja mambo ya Usalama wa Taifa yasiyopaswa kutolewa kuwa ni taarifa ya nchi au Serikali ya kigeni inayohusiana na Usalama wa Taifa na uhusiano wa mambo ya nje au shughuli za mambo ya nje yakiwemo masuala ya kisayansi na teknolojia yanayohusiana na Usalama wa Taifa, mathalani, taarifa juu ya ununuzi wa rada; udhaifu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU); uuzaji wa hati fungani za Serikali kwa benki ya Stanbic na unyonyaji kwenye mikataba ya madini na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu wa TAKUKURU uliripotiwa na mtandao mashuhuri wa *WikiLeaks.* Ulimnukuu aliyekuwa Balozi wa Marekani nchini, Michael Retzer akisema, Edward Hoseah ambaye kipindi hicho alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU alizuiwa na bosi wake, Rais Jakaya Kikwete, kuwashtaki vigogo wa wizi wa fedha za *EPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzaji wa hati fungani uliibuliwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Makosa Makubwa ya Ufisadi ya Uingereza *(SFO).* Kiasi cha shilingi trilioni 1.3 zimedaiwa kupotea katika sakata hilo. Kifungu cha 5(3) cha

sheria kimetaja taarifa ambazo hazipaswi kutolewa ni upelelezi unaofanywa na vyombo vya uchunguzi, faragha binafsi na taarifa za Usalama wa Taifa lakini nani asiyejua udhaifu wa vyombo vya uchunguzi? Vingi vinatuhumiwa kubebana kwa njia ya upendeleo au rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria mpya ya Upatikanaji wa Taarifa imerejesha kwa mlango wa nyuma sheria katili ya magazeti *(Newspaper Act* ya mwaka 1976) na ndivyo ilivyotarajiwa pia kwenye mikataba. Taifa hili limenyonywa kwa miaka mingi na limekumbwa na migogoro lukuki inayotokana na kuwapo mikataba iliyofungwa kinyemela na watendaji wa Serikali. Wengi walitarajia kuwa mikataba hiyo ingekuwa wazi angalau kwa Bunge, mambo mengi yangekuwa tofauti na yalivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu, Ibara ya 19; Ibara ya 19 ya Mkataba wa Haki za Kijamii na Kisiasa wa mwaka 1966 *(ICCPR),* Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu wa 1981 na kifungu cha 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 kinatoa uhuru wa maoni bila kikwazo cha aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kilio hiki cha Wabunge na wananchi hakijasikilizwa na hivyo kinaishia kuipaka matope Jamhuri ya Muungano mbele ya macho ya kimataifa. Baada ya Serikali na Bunge kutunga sheria hizi zinazoratibu shughuli za waandishi wa habari nchini, je, Wizara haioni kuwa sheria hizo zinaharibu taswira ya nchi yetu kimataifa?

Je, Serikali haioni haja ya kuwahusisha wadau wa habari ili kuanza kufanyia kazi malalamiko yao na hatimaye kuleta muswada ili sheria hizo zifanyiwe marekebisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ubalozi wetu kule Washington DC kumepatikana taarifa kuwa kumelipwa kiasi cha dola za Marekani milioni 1.05 (karibu shilingi bilioni 2.4), kwa mwanamke aliyepelekwa nchini humo kuwa mtumishi wa nyumbani wa Afisa wetu wa Ubalozi, Dkt. Allan Mzengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vimenukuu taarifa kutoka Ubalozi wa Tanzania mjini Washington DC zinasema, Serikali ililipa kiasi hicho cha fedha kwa makosa binafsi yaliyofanywa na Dkt. Allan Mzengi na alituhumiwa kumsafirisha kinyume cha sheria hadi nchini Marekani Bi. Zipora Mazengo. Dkt. Mzengi alishtakiwa kumfanyisha kazi kwa saa 15 kila siku na kushindwa kumrejesha nchini kwa miaka minne hata pale alipofiwa na ndugu yake Bi. Zipora Mazengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya sheria za Marekani, upelekaji mtu yeyote (mwanamke au mwanaume) kutoka eneo moja hadi lingine kwa shabaha ya kumtumikisha linakuwa ni kosa baya sana nchini humo la usafirishaji haramu wa binadamu *(human trafficking offence).* Aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Bi. Mwanaidi Maajar ananukuliwa akieleza wasiwasi wa kuharibika uhusiano kati ya nchi hizi mbili wakati akiwasiliana na Sanze Salula, aliyekuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua ya Balozi Maajar kwa Salula yenye Kumb. Na. WEPC.179/53 ya tarehe 4 Februari, 2011 ilinakiliwa pia kwa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi Philemon Luhanjo na aliyekuwa Katibu wa Rais Prosper Mbena. Alisema ingawa kwa sasa Serikali ya Marekani imeonyesha karidhika kutokana na Mawakili wa Bi. Zipora kupunguza deni na Dkt. Mzengi kukubali kuanza kulipa kwa awamu, suala hili litabaki kuwa tete kutokana na hatua ya Mawakili wa Bi. Zipora kupinga utaratibu wa kulipa. Balozi Maajar anasema Mawakili hao wameanza tena kampeni za kuichafua Tanzania katika *Congress,* pamoja na kuishinikiza tena Serikali ya Marekani ili nayo iishinikize Serikali yetu kulipwa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiandika kwa njia ya tahadhari, Balozi Maajar alieleza Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Watu ya Marekani ina kipengele kinachoipa mamlaka *Congress* kuiamuru Serikali kusimamisha misaada kwa nchi ambayo imethibitika kuvunja sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo ya Waziri kama fedha hizo zimeshalipwa zote ili kuiondolea nchi yetu aibu katika nyanja za kimataifa na kuyumbisha uhusiano kati ya Tanzania na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba maelezo ya Waziri kuwa ni hatua gani za kinidhamu alizochukuliwa Dkt. Mzengi kutokana na kosa alilolifanya ambalo limeiaibisha Tanzania mbele ya nchi wahisani? Tatu, Serikali inachukua tahadhari gani ili kuzuia kosa kama hili lililofanywa na Dkt. Mzengi lisijirudie tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Waziri na Naibu, pia watendaji wote katika Wizara kwa kazi nzuri na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia kuhusu makazi ya wakimbizi. Serikali ilipokea wakimbizi kutoka Burundi na kufufua makambi ya Katumba na Mishamo (Mpanda) na Ulyankulu (Tabora) na mwaka 2009 walianza kupewa uraia, lakini kwa sasa bado watu wachache hawajapata uraia. Wito kwa Serikali ni kuwataka Umoja wa Mataifa kufadhili maeneo hayo katika huduma za jamii mfano afya, elimu, barabara na uchumi kwa kuwa maeneo hayo yalikuwa yanafadhiliwa na *UN.* Hivyo ni muhimu nchi ambazo zimeathirika kwa namna moja au nyingine na kupokea wakimbizi basi *UN* izisaidie kama wanavyofanya kwa nchi zingine.

Tunaomba kauli ya Waziri ni lini Serikali itaibana *UN* kufadhili makazi ya Katumba (Mpanda - Katavi) kwani kwa sasa wametoa *ambulance* moja na kukarabati Kituo cha Afya Katumba, kituo ambacho bado hakitoshi kabisa kwa wananchi zaidi ya 60,000 waliopo Katumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu huduma za Konseli Miji ya Biashara. Tunajua kwa Serikali imefungua Balozi

nchi ambazo tunafanya nazo biashara lakini mfano China Ubalozi upo Beijing, lakini Mji wa Biashara ni Guangzhou ambao upo mbali sana toka Beijing. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na huduma za konseli kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nizungumzie suala zima la kuimarisha amani. Tunazidi kutoa wito kwa Wizara kuongeza juhudi za kuimarisha amani kwa nchi jirani za Burundi, Kongo, Rwanda na Uganda ili kupunguza kuingia kwa wakimbizi ambao wanaathari nyingi katika jamii yetu kiutamauni, kiuchumi, ujambazi, wizi wa nyara na silaha haramu. Hivyo, Tume zilizoundwa ziendelee kuimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna nyanja nne za ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Changamoto zilizopo katika maeneo mawili tunazikabili vipi na tunajiandaa vipi kwa maeneo ambayo bado kuingia katika ushirikiano? Vilevile Serikali iendeleze kushirikisha Wabunge wa *EAC* kama nchi katika kujenga hoja na kusimamia vema maslahi ya nchi. Nawasilisha.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanyia nchi yetu. Naomba nichangie kwa kifupi kama ifuatavyo:-

(i) Mabalozi wote wa Tanzania wawe chachu ya maendeleo ya nchi yetu hasa kwenye sekta ya viwanda na biashara ili tutimize azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Tanzania ya viwanda. Waweze ku-*connect* fursa za kiuchumi ili tupate malighafi ya viwanda vyetu kwa urahisi, lakini zaidi tupate soko la uhakika la nje la bidhaa za viwanda.

(ii) Mabalozi wetu waiuze Tanzania katika sekta ya utalii. Tanzania haifananishwi na nchi yoyote ya Kiafrika, tukiacha *South Africa,* kwa kuwa na mbuga nzuri za Ngorongoro, Serengeti, Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Wanyama wazuri wawe kivutio cha watalii wengi kuja Tanzania ili tuinue uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kuandaa hotuba ya Wizara ya makadirio ya Bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Ubalozi zimekuwa na changamoto kubwa ya majengo. Ofisi za Balozi zimepanga ofisi, makazi ya mabalozi na makazi ya maafisa ubalozi. Hakuna eneo, Serikali inamiliki majengo ya balozi zake kwa asilimia mia moja kama tunavyoona baadhi ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwezi Serikali inatumia fedha nyingi kulipia kodi. Ikumbukwe kwamba mara nyingi Serikali huchelewesha kupeleka fedha katika Balozi hizi, hivyo kuleta fedheha sana kwa Ofisi za Balozi zilizopo ughaibuni. Nashauri Serikali ikaweke bajeti ili Ofisi zetu za Ubalozi zijenge Ofisi zetu huko nje ya nchi ambako Balozi zetu zinawakilisha. Ni vizuri kodi za pango zikalimbikizwa ili ziweze kujenga majengo badala ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Balozi za nchi yetu zilipewa viwanja tangu miaka ya 1980. Nashauri Serikali iweke mkakati wa muda mrefu na mfupi ili kujipanga na kuanza kuendeleza viwanja hivyo. Kama upo uwezekano wa kuviendeleza viwanja hivyo kupitia mikopo ya benki, *mortgage finance, higher purchase system* na njia nyingine ni budi Serikali ikaona jambo hili na kutekeleza mapema ili majengo hayo yaendelezwe. Tukiacha kuendeleza tunaweza kunyang'anywa, kwani viwanja vingi vipo katika maeneo maalum *(Diplomatic Quarters).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa wafanyakazi nalo ni tatizo kubwa. Ofisi nyingi za Ubalozi zina maafisa wachache sana. Hivi sasa tuna dhana ya diplomasia ya kiuchumi, ni budi Serikali ikaona umuhimu wa kuweka

wataalam mbalimbali katika Ofisi za Ubalozi kama wachumi, wanasheria, wenye utaalam wa utalii, Maafisa Uhamiaji ili kuendana na kasi ya diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wageni wengi wafikao katika shughuli za uwekezaji na shughuli nyingine za kibiashara hukosa taarifa za kutosha kutoka taasisi na Wizara. Nashauri suala la matangazo kwa njia mbalimbali zitumike na hasa njia za mitandao ya kijamii kama *facebook*, *twitter, websites* na nyingine nyingi ambao zitaleta tija ili kufanya nchi yetu itambulike zaidi Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza mara kadhaa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, lakini bado nahisi hakuna uelewa wa pamoja kuhusu suala hili na hasa kuhusu umuhimu wake katika suala zima la *FDI*. Nashauri Wizara i-*take lead* hata kwa kuishauri mamlaka kuu kuhusu nafasi ya suala hili hasa katika dhana nzima ya kuelekea uchumi wa viwanda ambao kwa hakika tunategemea pia wawekezaji kutoka nje ambao wangependa kuhakikishiwa masuala muhimu kama *Avoidance of Double Taxation* na hili la *Promotion and Protection of Investments.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kutenga fedha za kukarabati majengo, upo umuhimu wa kutafuta mbinu mpya hata kwa utaratibu wa *PPP,* kadri taratibu zinavyoelekeza ili tujenge kwenye viwanja ambavyo viko maeneo ambayo ni *prime*, lakini pia hata kimahusiano, viwanja kama pale Maputo, tumepewa zaidi ya miaka 30 iliyopita, hatujaweza kujenga. Nchi husika pamoja na mengine mengi inaweza kuona kuwa hatujali au hatuthamini mchango wao wa sisi kupewa viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *posting (downsizing* ni sawa na *downgrading*); ninafahamu kwamba kuna maafisa wamerejeshwa, lakini hatujapeleka Maafisa Balozini. Kuna

nchi Balozi yupo peke yake bila maafisa, suala ambalo linaathiri sana utendaji. Nchi kama China, Belgium *(EU),* France, Italy, Uganda, Sweden, Ujerumani na kadhalika, kimajukumu Balozi kukosa Afisa inadumaza jitihada zote za kuelekea uchumi wa viwanda.

Mhashimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wamekua vituoni, hivyo nina imani wanapata *feeling* ni kwa namna gani utendaji wa kazi unakuwa mgumu kwa Mabalozi wasiokuwa na Maafisa. Kuna dhana kuwa *posting* ni kama *privilege,* ninashauri kama suala hili liko juu ya uwezo wa Wizara, kwa uzoefu wao Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu waieleze mamlaka kuna athari za Mabalozi kutokuwa na Maafisa vituoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Mabalozi ambao kitaalam na kitaaluma siyo wanadiplomasia, tunajaribu kufikiria Balozi wa aina hiyo awe hana Afisa, atafanya kazi katika mazingira gani? Hata nchi husika zinapata shahada kuwa ni kama tunapunguza mahusianao kwa ku-*down size staff.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Honorary Consul* Lubumbashi limezungumzwa sana kutokana na umuhimu wa *DRC Congo* katika uchumi wetu lakini pia halina gharama za kifedha. Je, limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la malalamiko kuhusu unyanyasaji wa *house girls* Arabuni limejitokeza mara kadhaa na hata Kamati yetu imelijadili kwa kukutana na baadhi ya wadau na Waheshimiwa Wabunge wenye familia zao Arabuni na hususan Oman.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni vizuri Wizara ikashinikiza ipasavyo na Wizara ya Kazi na Ajira ili kuwepo utaratibu ambao utaondoa ukakasi unaoanza kujitokeza kiasi kwamba suala hili linaweza kuathiri mahusiano yetu na nchi hizo. Uganda wamefanikiwa sana katika suala hili, wapo wanaotaka wasichana wazuiwe kwenda kufanya kazi

Arabuni, lakini kwa upande mwingine watu wanataka fursa kufanya kazi nje. Wafilipino wamefanikiwa katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Serikali ikiweka utaratibu mzuri, jambo hili ni la manufaa kwa Taifa kiuchumi, lakini pia kimahusiano. Ni matarajio kuwa baada ya michango ya Wabunge Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho atasema lolote hasa kushauri wanaofanya kazi ya uwakala wa kupeleka wafanyakazi wa ndani Arabuni kuwasiliana pia na Balozi zetu kwa taarifa tu. Kimsingi suala limejadiliwa sana katika *social media* na kwa hisia kali sana, ni muhimu Serikali/Wizara kulisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba mtumishi wa umma anafanya kazi sehemu yoyote ndani ya Serikali. Hata hivyo ni faida zaidi kuwatumia watumishi pale ambapo wanakuwa na tija zaidi. Kwa mfano, maafisa waliorejea hasa watu wa uchumi ambao wamejengewa uwezo kwa kufanya kazi nje, baadhi yao wamepata mafunzo kuhusu diplomasia ya uchumi. Ni matarajio kuwa kuelekea uchumi wa viwanda, maafisa hao kwa uzoefu na taaluma yao wangeweza kuwa msaada mkubwa kwa Wizara. Hata hivyo, waliporejea wamehamishiwa Wizara, bado ninashawishika kuamini kuwa ilikuwa ni tija kuwa-*retain* watumishi hao kwa kuangalia pia waliingiaje Wizarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliokuwepo enzi Mheshimiwa Jakaya Kikwete akiwa Waziri wa Wizara hii watakumbuka alivyotoa wazo la Wizara kupata maafisa wa fani ya uchumi. *Good enough* wamekaa na kupikwa katika nyanja hii hapo Wizarani na Balozini, lakini ghafla kumeingia uoga kwa kuwahamishia kwenye Wizara nyingine, sijui uoga huu unasababishwa na kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uteuzi wa baadhi ya Wakurugenzi kuwa Mabalozi nje ya nchi, waliopo wanakaimu, nashauri Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na kuwa uteuzi ni suala la mamlaka kuu, ipo nafasi ya kushauri ili Wizara kupata watendaji ambao siyo makaimu kwa nia ya kuleta ufanisi zaidi.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda wangu ambao haukutosha, nimeona nimalizie kwa maandishi. Ili kumaliza tatizo la wavuvi wetu na hata wengine kufikia kufungwa jela nchini Kenya, ni vema Serikali zetu mbili yaani Kenya na Tanzania zikarudi kwenye mkataba uliosainiwa na Mawaziri wa Mambo ya Nje, nchi hizi mbili Tanzania na Kenya Desemba 17, 1975.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *copy* ya Mkataba pamoja na kwamba nilikuambatanishia Mheshimiwa Waziri na barua niliyomwandikia hapa nilipo *copy* ninayo. Akiitaka nitampatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wao wote wa Wizara hii kwa kutayarisha hotuba hii kwa ufanisi na kuweza kuwakilisha kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii, napenda kugusia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia ni chuo chenye walimu hodari katika Idara zake zote. Ni walimu wanaofanya kazi kwa bidii na kizalendo. Napenda kuchukua nafasi hii kupongeza walimu hao na kuwataka waendelee na juhudi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya chuo hicho hayaendani na jina la kidiplomasia. Miundombinu ni mibovu kidogo, hivyo naiomba Wizara iboreshe miundombinu hii ili chuo kiwe bora zaidi Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha. Neno Kimataifa ni neno lenye hadhi. Unaposema Kituo cha Kimataifa ni lazima uwe katika nafasi fulani ambayo ni kubwa ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Mikutano cha Arusha bado kinahitaji marekebisho ili nacho kiwe cha Kimataifa. Serikali inajitahidi kuanzisha miradi ambapo ni jambo zuri sana, lakini bado jengo haliko safi upande wa vyoo; hakuna vyoo vya watu mashuhuri *(VIP),* vyoo vilivyopo ni kama vya shule za *primary/secondary*. Hivyo naomba Wizara nayo irekebishe suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu uvumi wa udhalilishaji wa Watanzania katika nchi za Kiarabu. Kumekuwa na uvumi usiokuwa na uhakika katika mitandao na vyombo vya habari zinazoeleza juu ya uteswaji wa Watanzania huko Arabuni. Hili ni jambo linalotia wasiwasi sana katika jamii ya Watanzania. Hivyo namuomba Mheshimiwa Waziri akija kutoa majumuisho atueleze na atoe tamko la Serikali juu ya jambo hili ili liwaweke Watanzania katika utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kuipongeza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ushauri uliotolewa kwa Serikali. Mchango wangu uko katika Shirika la *AICC* ambalo inamilikiwa au liko chini ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *AICC* ni Shirika la Muungano ambalo kwa kipindi cha miaka 39 toka kuanzishwa kwake limefanikiwa kufanya uwekezaji wa kutosha kwa upande mmoja tu wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ambayo tayari imeshaelekezwa, bado *AICC* inatarajia kutekeleza miradi mipya kama vile ujenzi wa Taasisi ya Kimataifa eneo la Lakilaki (Arumeru), hospitali ya kisasa, maonesho, shughuli za mikutano na burudani. Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha *Kilimanjaro International Convention Centre (KICC), Convention Centers'* katika Miji ya Mwanza, Mtwara na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji unalenga kutengeneza ajira na hivyo kunyanyua shughuli za kiuchumi kwa maeneo husika. Hivyo basi, ni kwa namna gani Zanzibar inafaidika na uwekezaji unaofanywa na Shirika la *AICC?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema Zanzibar ni sehemu ya Shirika la *AICC,* je, ni kwa nini Shirika bado halijafikiria kufanya uwekezaji katika visiwa vya Zanzibar wakati uchumi wa visiwa hivi unayumba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na Zanzibar kuwa na uchumi usioridhisha, lakini Zanzibar ina mazingira mazuri ya kuvutia biashara ya utalii, biashara ambayo shirika ndiyo kiini cha shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Kumi katika Mkutano wa Sita cha tarehe 10/02/2017, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje alijibu swali la msingi Na.110 lililohusu gawio la Zanzibar. Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kuwa gawio linapelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu hayo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alinyanyuka na akasema kwamba *AICC* haijawahi kupata gawio na kwamba *Joint Finance Commission* na Ofisi ya Msajili wa Hazina wameunda

kikosi kazi ili kusaidia kituo kupata faida na kuleta gawio Serikalini kuanzia mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha yanakizana na yale ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na kwa hiyo, yamelenga kuwadanganya Wazanzibari kuhusiana na mapato ya *AICC*. Mbali na hayo, majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha pia yanakinzana na taarifa ya Msajili wa Hazina, lakini pia na taarifa ya Shirika wenyewe la *AICC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *AICC* inasema, nanukuu; "*AICC* kwa kipindi kirefu imekuwa ikijiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali na imekuwa ikichangia ruzuku ya Serikali na imekuwa ikichangia Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia maelekezo ya Msajili wa Hazina."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mgongano huu wa taarifa zinazohusu faida zinazotokana na Shirika la *AICC* kati ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Shirika la *AICC,* binafsi ninaomba maelezo ya kina na yanayojitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu. Jioni saa 10.00 Serikali mtaanza kujibu moja kwa moja ili tumalize kwa muda ambao umepangwa.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza na Mwanasheria Mkuu, dakika tano.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipatia hii fursa na mimi nichangie. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mimi kupata fursa kipindi hiki lakini niwapongeze sana Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa hotuba yao nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwatakia heri ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Waislamu wote wa Tanzania wanaofunga. Mwenyezi Mungu atubariki, mnapokuwa mnashiriki toba hii mshiriki na sisi waovu wengi mtuombee pia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Magufuli kwa hatua aliyochukua kuhusiana na mchanga. Unajua Katiba yetu, Ibara ya 27 imeeleza vizuri wajibu wetu kama Serikali kuhusu matumizi ya maliasili tulizonazo na hii ni maliasili. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote kwenye hili tushirikiane na Serikali kuhakikisha kwamba tunalinda maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili hakuna sababu ya kulaumiana, ni mapema sana kuilaumu Serikali kwa hatua ilizochukua. Zimeundwa Kamati mbili, hii ya kwanza na Kamati nyingine ya sheria ambayo inaangalia pia na mikataba. Kati yetu hakuna hata aliyewahi kuona mikataba hii au aliye na hii mikataba. Kwa hiyo, naomba tutambue kwamba sisi ni familia moja, tunayoyasema leo yatakuja kuturudia, hatuwezi tukaanza kuilaumu Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tunapochangia tuchangie kwa hekima, kwa heshima na kwa nidhamu kubwa kwa maslahi ya Taifa letu na kwa viongozi wa Taifa hili na kwa lugha ya Kibunge. Tunazo kanuni

zinazotuongoza, mimi sioni hii ina maslahi gani kwa watu, kwa sababu tusichangie kana kwamba tunachochea watu wengine watuchukulie hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge waiunge mkono Serikali kwenye suala hili. Ni suala ambalo lilipaswa lituunganishe sisi kama watu wamoja kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. Hii baadhi yetu mnayoshabikia kwamba tukishtakiwa, hakitashtakiwa Chama cha Mapinduzi kama ni *liability* itakuwa ni ya Serikali nzima. Hapa hawachagui kwamba ni huyu au ni yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia, naomba tuendelee kuipatia Serikali ushirikiano, Wizara inafanya vizuri, wawekezaji kwa kweli wataendelea kuja. Nimerudi asubuhi hii kutoka Uganda kusaini mkataba ule wa bomba la mafuta na ninyi wenyewe mmeona Waziri wa Viwanda na Biashara amewasilisha hapa bajeti yake wiki moja iliyopita na mwitikio umekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tunapochangia, tusichangie kwa kuogopesha watu kwamba mambo ni mabaya sana. Kila kilichofanyika kwenye hatua hii ya michanga ni halali kisheria na kimikataba. Kwa hiyo, tutakapokamilisha ile ripoti ya Kamati ya Sheria tutaona tufanye nini kwa sababu Sheria ya Madini inatoa fursa ya ku-*review* mikataba ile kila baada ya miaka mitano. Sasa mnawezaje ku-*review* kama hamko *well informed*? Yaliyotokea sasa kwenye taarifa hii yanatusaidia sisi kuwafuata wenzetu na kuwaambia jamani hiki ndicho tulichoona, turekebishe hapa, sasa kosa lake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema, kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii ya kipekee, kama wenzangu walionitangulia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake madhubuti na makini unaoendelea kugusa si tu Watanzania, bali mfano wa kuigwa katika nchi za Bara la Afrika na Dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza sana na kipekee Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa uongozi wake makini na kuhakikisha tunapata ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara anayoiongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake ndani ya Bunge hili. Aidha, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika na kwa namna wanavyoongoza Bunge hili. Pia nampongeza Mheshimiwa Andrew John Chenge, wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kwa namna mnavyoweza kuonesha uwezo wenu mkubwa wa kuliongoza Bunge hili katika kipindi hiki. Pia nawashukuru sana Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa, nawaombea kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao hapa Bungeni na kwenye majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru wananchi wenzangu na wanawake wote wa Mkoa wa Njombe na kwa kipekee Jumuiya ya Wanawake Tanzania, Mkoa wa Njombe kwa imani kubwa waliyonipa na wanayoendelea kuonesha kwangu.

Nitaendelea kuwa nao karibu na kushirikiana nao kuleta maendeleo makubwa zaidi na naahidi kuwa sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana familia yangu, ikiongozwa na mume wangu mpendwa Dkt. George Yesse Mrikariya, kwa uvumilivu wao kwangu na kwa namna inavyonisaidia na kuniunga mkono katika majukumu yangu. Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, viongozi, watendaji, wasaidizi wangu, Mabalozi, Wakurugenzi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushauri na msaada wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na ni dhahiri kwamba michango yao itatusaidia sana katika kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi na utendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kwa kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani na zitakazobakia Mheshimiwa Waziri ataendelea kuzijibu. Kambi ya Upinzani ilikuwa inataka kujua juu ya mpango mkakati wa Wizara na kama Wizara ina Mpango Mkakati wowote kuhusu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mipango ya maendeleo ya Serikali ambayo inaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2020-2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hususan Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 mpaka 2020/2021, unaojikita kwenye uchumi wa viwanda ambao utaiwezesha nchi yetu kufika katika uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mipango hiyo imekuwa ikiendana na mipango ya maendeleo ya Kikanda

na Kimataifa kama vile Mpango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa 2013/2014 - 2017/2018; Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC); Regional Indicative Strategic Development Plan (RISDP)* wa 2005-2020; Agenda 2063 na Umoja wa Afrika pamoja na Mpango wa Maendeleo Endelevu wa 2030 wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mipango hii, Wizara imekuwa ikivutia uwekezaji, biashara na utalii na misaada kutoka nchi mbalimbali kupitia makongamano ya biashara ya uwekezaji na kushawishi wawekezaji wakubwa kuja kuwekeza nchini na kutangaza fursa zilizopo nchini kwenye sekta mbalimbali ikiwemo utalii, kilimo, madini, nishati na kadhalika. Ninyi wenyewe mmekwishakuona wawekezaji mbalimbali wamekuja Mikoa kama ya Pwani, Singida na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia ilikuwa inataka tueleze kinaga ubaga hadi sasa kupitia diplomasia ya uchumi inavyoweza kujitangazia fursa zilizopo nchini kupitia Balozi zake kwa lengo la kuvutia uwekezaji wa kigeni, kuimarisha uhusiano wa kibiashara na mataifa mengine sambamba na kukuza sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema ikaeleweka kuwa Sera ya Mambo ya Nje ni mwendelezo wa sera zote iliyojiwekea Serikali katika kujiletea maendeleo. Hivyo utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje unahusisha Wizara, taasisi zote za umma na sekta binafsi pamoja na wadau wengine ikiwemo Bunge hili. Maneno haya yalisemwa pia mwaka jana tukimweleza Waziri Kivuli wa Wizara hii lakini naona swali limajirudia vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa la Wizara yangu limekuwa siku zote ni kusimamia, kuratibu na kurahisisha utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje inayojikita kwenye diplomasia ya uchumi. Ni ukweli ulio wazi kuwa Wizara yangu hulifanikisha jukumu hili kwa kushirikiana na Wizara na taasisi zote pamoja na sekta binafsi. Hii inatokana

na kuwa Wizara hii inahusika na masuala mtambuka ya Wizara tofauti kama vile kilimo, utalii, biashara, madini, elimu, afya na sekta nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa zilizopo nchini zinatangazwa na Balozi zetu ikiwa ni sehemu ya majukumu yao ya ubalozi. Balozi hizi huhudhuria makongamano ya uchumi, biashara, kilimo, elimu na kushiriki katika mialiko ya sekta hizo, hivyo, kupata fursa nzuri ya kuzitangaza fursa zilizopo nchini sambamba na kuweza kuvutia uwekezaji wa kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majukumu ya Wizara na Sera yetu ya Mambo ya Nje pamoja na vipaumbele vya Taifa letu, Wizara iliandaa Kitabu Maalum (*Ambassadors Handbook* 2008) kinachoainisha majukumu ya msingi ya Balozi mbalimbali katika maeneo wanayowakilisha nchi yetu. Lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba Balozi hizi zinadumu kwenye malengo ya Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo kwenye diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia waliuliza swali kwamba ni kigezo gani wanatumia kuwateua Mabalozi na kwa nini inaonekana kwamba uteuzi wa Mabalozi hao unazingatia zaidi u-CCM na itikadi ya chama hicho badala ya kuzingatia zaidi utaalam, uzoefu, umahiri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe kuwa suala la uteuzi wa Mabalozi liko kwenye mamlaka ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushauriana na viongozi wengine mbalimbali ikiwemo Wizara. Uteuzi wa Mabalozi tangu na baada ya Uhuru umehusisha watumishi wa Wizara ya Mambo ya Nje na kutoka Wizara na taasisi nyingine za Serikali na sekta binafsi kwa kuzingatia taaluma, uzoefu, weledi na uchapakazi wao. Ni busara hizo Marais wote watano wamekuwa wanateua Mabalozi kutoka kada za Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, wasaidizi, viongozi wa Kitaifa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa hatutendi haki kama tutahitimisha kwa kusema kuwa viongozi wote hawa hawana sifa za kuwa Mabalozi baada ya kulitumikia Taifa kwenye nyadhifa mbalimbali muhimu kama hizo. Aidha, uteuzi umekuwa unazingatia matakwa ya eneo la uwakilishi kwa mfano utaona kabisa Mabalozi kutoka kada ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama wanapelekwa sehemu zile zenye hitajio la aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa na kada yeyote ndani na nje ya Wizara hufanyika hapa nchini kwa kutumia vyombo vyetu vya nje na ndani kwa kulipiwa na Serikali yenyewe au nafasi hizo kutolewa na nchi na mashirika wahisani. Ni kwa msingi huo Wizara yangu inatumia kikamilifu fursa zote zinazojitokeza nje na ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo Kambi ya Upinzani pia waliuliza kwamba Wizara kwa muda mrefu sasa imeshindwa kutoa mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa maafisa wake badala yake kutegemea ufadhili kutoka nje na marafiki. Naona hii ni dhana potofu na tulikwishaizungumzia katika bajeti ya mwaka jana na nilifikiri labda pengine Waziri Kivuli ameelewa lakini naona niendelee kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Chuo chake cha Diplomasia kilichopo Kurasini imekuwa ikitoa mafunzo ya Diplomasia ya Uchumi mara kwa mara kwa watumishi wa Wizara yangu na wadau wengine ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi duniani. Kwa Maafisa wa Mambo ya Nje ni lazima kujiunga na chuo hicho kama mojawapo ya sharti ya kupandishwa cheo. Aidha, Wizara pia imekuwa ikiwapeleka maafisa wake kuongeza ujuzi zaidi ya Diplomasia ya Uchumi kwenye nchi za China, Japan, Misri, Afrika Kusini, Uswis, Marekani, Urusi pamoja na nchi zingine kupitia bajeti yake na ufadhili wa nchi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafuta fursa za mafunzo nje ya nchi ni moja ya utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya

Uchumi kwenye eneo la elimu. Aidha, chuo kimeandaa kozi fupi na ndefu za diplomasia ya uchumi kwa Waheshimiwa Wabunge na tayari chuo kimepeleka ombi kwa Wabunge Wateule wa Bunge la Afrika Mashariki walioteuliwa hivi karibuni ili nao waweze kushiriki katika kozi hiyo. Itakuwa ni upotofu kusema kwamba Wizara haijajipanga na haijatekeleza maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuweka kumbukumbu sawa kwa takwimu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 watumishi 77 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na wa kati na watumishi 14 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Umahiri kupitia fedha za ndani na za wafadhili. Hivyo basi, mafunzo haya hayategemei ufadhili kutoka nchi marafiki peke yake kwa kuwa Wizara imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya mafunzo haya kila mwaka na ukiangalia katika kila kitengo kuna bajeti ambayo inaonesha kwamba kuna mafunzo ya ndani na mafunzo ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii amesema hapa kwamba kwa miaka ya nyuma tumefundisha tu watu 32. Nataka niweke taarifa sawa, ile ilikuwa ni mwaka 2015/2016 ndiyo walikuwa wamefundishwa watu 32. Ili uweze kuelewa ni lazima ijue kwamba idadi ya watumishi ndani ya Wizara ile wapo wangapi na wangapi wanafundishwa kwanza, lazima waende kwa mpango. Huwezi ukapeleka wote 300 wakaenda shule wakati pengine hitajio ni watu 12, kwa hiyo, ni mipango mikakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Kambi ya Upinzani wameulizia ilikuwa ni kwamba Wizara imechukua hatua gani katika kuvutia wawekezaji wakubwa kwenye sekta kilimo ambao asilimia 75 ya Watanzania wameajiriwa kwenye kilimo duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, Wizara yangu ndiyo inayosimamia na kuratibu masuala ya mahusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani na

mashirika ya Kimataifa. Kwa hiyo, tuna jukumu la kuratibu Wizara na taasisi nyingine kwenye masuala haya. Wizara imekuwa inatangaza fursa za uwekezaji na kuvutia wawekezaji kwenye sekta zote na siyo kilimo peke yake. Lazima ieleweke hiyo kwanza, mahitaji ni mengi ni lazima tuyashughulikie kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kupitia ushiriki wa Mikutano ya Kimataifa, ziara za viongozi, makongamano ya kibiashara na uwekezaji, mikutano ya Tume ya Pamoja ya Kudumu pamoja na shughuli za kila siku za Mabalozi na Wizara yangu kwa ujumla huvutia wawekezaji kwenye miradi mikubwa ya kilimo katika kukuza sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mkutano wa Jukwaa la Kiuchumi la Dunia kwa nchi za Afrika uliofanyika Dar es Salaam Mei, 2010, Tanzania ilichaguliwa kutumia Ushoroba wa Kati (*Central Corridor)* kuanzia *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)* katika kuendeleza sekta ya kilimo. Ushoroba huu ulishindanishwa na nchi nyingine za Kiafrika na ukaibuka kuwa mshindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *SAGCOT,* Tanzania imefanikiwa kuvutia makampuni makubwa kuja kuwekeza kwenye sekta ya kilimo nchini. Kwa sasa *SAGCOT* inaratibu miradi mbalimbali ya makampuni yasiyopungua 100. Miongoni mwa hayo, makampuni 80 yameshafanya uwekezaji na mengine yanaendelea kuwekeza. Makampuni 36 yameandika barua ya kukusudia kuwekeza na makampuni 20 yamefanya ubia wa kimkakati kwenye kuzalisha mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uwekezaji unaokadiriwa kuwa wa thamani ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.2 umefanyika. Kwa mfano, mradi wa Shamba la Chai Iringa na Njombe *(Unilever)*; mradi wa uzalishaji wa mchele Kilombero *Plantantion* (Morogoro); mradi wa kununua mbolea kwa wingi na kuifungasha hapa hapa nchini chini ya kampuni ya *YARA;* mradi wa maziwa

*Asas Dairies (*Iringa); mradi wa mbegu za viazi, Mtanga *Food Limited* (Iringa na Njombe) na mradi wa chakula cha kuku na uuzaji wa vifaranga, *Silverland Tanzania Ltd* (Iringa) ambapo mimi nashangaa na yeye anatoka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo inatarajia kuwaondoa kwenye umaskini wakulima wengi. Mpaka sasa zaidi ya Dola za Marekani 250,000,000 zinaendelea kuwekezwa kwenye uzalishaji wa mahindi, chai, viazi, soya, nyanya pamoja na huduma zingine za pembejeo. Haya ni matunda ya uratibu wa Wizara yangu katika kuvutia wawekezaji. Utasema kwamba akili ndogo inaongoza kubwa au kubwa inaongoza ndogo, ipi ni kubwa na ipi ni ndogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano kati ya Tanzania na Mashirika ya Kimataifa kama vile *FAO, IFAD, WFP* pamoja na nchi marafiki imefanikisha misaada katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini. Kwa mfano, *IFAD* imetoa msaada wa Dola za Marekani milioni 10 na mkopo wenye masharti nafuu na jumla ya Dola za Marekani milioni 56.6 kwa ajili ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashangaa nimechukua muda mrefu, Waziri wangu amenituma niongelee hilo tu na yeye atasema machache, mengine tutayajibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada gani zinafanywa na Wizara katika kuchangamkia fursa za uchumi badala ya kusubiri nchi rafiki ambazo zenyewe zina ajenda zao. Wizara imeendelea kutafuta fursa za uchumi kwa kushirikiana na Wizara na taasisi zote za Serikali pamoja na sekta binafsi kupitia makongamano ya biashara na uwekezaji, mikutano ya kimataifa, Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano na mikutano ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fursa zilizopo nchini zinatangazwa na Balozi zetu ikiwa ni sehemu mojawapo ya majukumu yake. Balozi hizo huudhuria makongamano, biashara, kilimo, elimu na kushiriki kwenye mialiko ya sekta

hizo kwenye maeneo ya uwakilishi na hivyo kupata muda mrefu wa kuzingatia fursa zilizopo nchini sambamba na kuvutia uwekezaji wa kigeni. Hivyo, siyo kweli kwamba Wizara haichangamkii fursa za kiuchumi na badala yake kusubiri nchi rafiki zije. Huu ni mkakati, unaweza ukawaita wakaja na mkazungumza, mkamaliza mikakati yenu, lakini vilevile ukawafuata na tumefanya hivyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mengine yajibu kwa maandishi. Tunaendelea na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuhitimisha mjadala wa hoja yangu kwa kutoa shukrani za pekee kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu kwa mchango wenu wa maneno na maandishi. Pia naamini kabisa kwamba Wizara yangu itaendelea kutegemea mawazo ya ujumla ya Bunge hili katika kutekeleza sera na mipango yake ya kuendeleza uhusiano na nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wangu ambaye amemaliza kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza. Pia natoa shukrani za pekee kwa wafanyakazi Wizarani kwangu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, viongozi na wafanyakazi wote ambao tumeshirikiana katika kuandaa hotuba hii na kujibu maswali ambayo yamejitokeza ndani ya Bunge hili Tukufu ambapo jumla ya Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 30 wamechangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu hoja zote zilizowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu, moja baada ya nyingine lakini kutokana na uchache wa muda hoja zote nitazijibu kwa maandishi kama yatakavyowafikieni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea pale alipoishia Naibu wangu. Je, Serikali haioni kuwa kutosafiri mara kwa mara kwa Mheshimiwa Rais nje ya nchi katika ziara rasmi au kushiriki Mikutano ya Kimataifa kwa kuzingatia kubana matumizi kunadhoofisha ushirikiano na ukuaji wa mahusiano ya kidiplomasia na mataifa mengine? Inapotokea kiongozi anasafiri kutafuta fursa na kujenga mahusiano ya nchi na Mashirika ya Kimataifa panakuwepo na kubezwa sana kwa safari hizi pamoja na maelezo mazuri sana ambayo yamekuwa yanatolewa mara kwa mara na Wizara yangu na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, inapotokea safari ya kwenda nje na kiongozi akaamua kutuma msaidizi wake kumwakilisha kwenye safari hizo kiongozi huyo anatuhumiwa kwamba anadhoofisha mahusiano. Hapo Wizara yangu inajiuliza, ni lipi jema hasa? Ukisafiri unaitwa mtalii na usiposafari unaua mahusiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kama Mwanadiplomasia namba moja anatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Kwa miaka mingi Tanzania inaheshimika katika medani ya kimataifa. Heshima hiyo imechangiwa sio tu kwa safari za viongozi na Serikali bali kwa kazi nzuri wanazofanya ndani ya nchi, Afrika Mashariki na Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu hii ya Tano, Tanzania imeshatembelewa na viongozi wengi wa Mataifa makubwa yaliyoendelea na yale yanayoendelea na ambao walioambatana nao, ujumbe mkubwa wa wafanyabiashara hao, wamekuja na kufanya mazungumzo yenye tija kabisa kwa nchi yetu. Lazima ifahamike kwamba watu wanaokuja kututembelea wanaridhika kabisa na mazungumzo baada ya wao kuja kututembelea hapa na yameleta tija kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine ni kwa nini michago ya kifedha ya baadhi ya washirika ndani ya Jumuiya

ya Afrika Mashariki imekuwa haitolewi kwa ukamilifu? Jibu, michango yote ya Tanzania ndani ya Jumuiya hiyo imeshalipwa na hatudaiwi hata senti moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa za Gazeti la nchi ya Kenya la *Daily Nation* la tarehe 14 Mei, 2017 lilimnukuu Kiongozi wa Bunge katika Bunge la Kenya akitoa shutma kuwa Tanzania inapanga kuingilia mchakato wa uchaguzi wa nchi hiyo. Je, Serikali haioni kuwa taarifa hiyo itaathiri mahusiano kati yetu na nchi ya Kenya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa hotuba yangu nilisema moja ya malengo ya Sera ya Mambo ya Nchi za Nje ya Tanzania ni kutoingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine. Tanzania imekuwa nchi inayofuata na kuheshimu misingi ya demokrasia, utawala bora, ujirani mwema na uhuru wa nchi nyingine hasa majirani zetu. Tanzania inaheshimu maamuzi ya nchi nyingine ya kujiamulia mambo yao wenyewe na kuchagua viongozi wanaowataka kama ambavyo sisi tumefanya kwa awamu zote tano tangu ya Mwalimu Nyerere hadi ya sasa ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kusuluhisha migogoro kwenye Bara la Afrika na hasa nchi zinazotuzunguka ikiwemo Jamhuri ya Kenya mwaka 2007 ilipoingia kwenye machafuko ya kisiasa baada ya uchaguzi. Ni kwa misingi hiyo, Wizara inapenda kuweka bayana kuwa Tanzania haijaingilia na haitakaa iingilie masuala ya ndani ya nchi nyingine. Ni vema waandishi wa habari wakaandika habari za kweli na kuacha kuzichonganisha nchi majirani na ndugu kama vile sisi na ndugu zetu Wakenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni upi msimamo wa Tanzania kuhusu nchi za Morocco na Sahara Magharibi. Tanzania ni mojawapo wa NchiWwanachama wa Umoja wa Afrika waliounga mkono ombi la Morocco kurejea katika Umoja wa Afrika ikiamini suluhu ya mgogoro uliopo wa Sahrawi ya Magharibi utazungumzwa. Nifafanue kwamba

katika sera yetu ya kutofungamana na nchi yoyote tumeamua kuwa na mahusiano na Morocco kwa sababu Morocco ikiwa ni nchi ya tano yenye uchumi mkubwa katika Afrika tutakuwa tunajinyima fursa ya kufanya biashara na uwekezaji na nchi hii. Kuisusa siyo suluhu ya mgogoro wa Sahrawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa kwamba ili kuisaidia Sahrawi, misingi yetu inayojulikana ya kulinda uhuru na heshima wa watu na makundi, suluhu inaweza kupatikana kwa mazungumzo. Baada ya miaka karibu 40 bila kupata suluhu tunaamini kwamba suluhu kati ya Morocco na Sahrawi itapatikana kwa mazungumzo ndani ya Umoja wa Nchi za Kiafrika ambapo Morocco imerudi na Tanzania itashiriki kikamilifu katika mijadala hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kueleza msimamo wa nchi kuhusu mgogoro uliopo Syria, mgogoro kati ya India na Pakstan juu ya Kashmir pamoja na mgogoro kati ya nchi ya Marekani na washiriki wake dhidi ya nchi za Korea Kaskazini. Kwa misingi ile ile kwamba sisi hatufungamani na nchi zozote na suala hili la India na Pakstan ni la zaidi ya miaka 50 na wala halizungumzwi hata katika Umoja wa Mataifa. Nadhani hili ni suala ambalo nchi hizo mbili zinaweza kulizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Syria itakumbukwa kwamba katika mageuzi ya Mashariki ya Kati yaliyoanzia Tunisia yakaenda Libya yakaikumba Misri yalifika Syria pale yakakwama. Sasa hivi ushindani kati ya upinzani na Serikali na vikundi mbalimbali vya upinzani imepelekea mataifa makubwa kuchukua nafasi tofauti zinazokingana. Katika hili, Tanzania inapendekeza kwamba suluhu ipatikane kwa mazungumzo. Kwa kuzingatia siasa yetu ya kutofungamana na upande wowote, sisi hatuwezi kuingilia mvutano huo wa ndani ya Syria na makundi yale ambayo yanaunga vikundi hivyo yakiongozwa na mataifa makubwa ya duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kugusia suala lingine ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Profesa Anna

Kajumulo Tibaijuka. Anasema mpaka baina ya Tanzania na Uganda haupo vizuri na Serikali imejipangaje kuliweka vizuri suala hili ili pawe na maelewano na mkataba kwenye mpaka huu pamoja na mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwakumbusheni kwamba mipaka ya nchi za Kiafrika inatokana na maamuzi ya nchi za Kiafrika kwamba isibadilike na sisi nia yetu siyo kubadilisha mpaka huo lakini kuna wakati ambapo ni lazima tujaribu kufanya marekebisho kwa sababu wananchi wa pande zote mbili wanaoishi katika nchi hizi mara kwa mara wamekuwa hawaoni mstari ambao unatenganisha nchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baina yetu na Uganda tumeshafanya kikao huko Bukoba kuzungumzia suala hili ambapo katika pande mbili za mpaka kuna Waganda na Watanzania ambao wamevuka mpaka. Majadiliano haya yaliingia pia katika Tume ya Pamoja ya mazungumzo kati ya Uganda na Tanzania na tutaendelea kuyazungumza tena na tumepanga ndani ya mwezi ujao wa Juni tutaendelea kuzungumza. Nia siyo kubadilisha mpaka lakini ni kuwasaidia wananchi wa pande zote mbili kuelewa mpaka ulipo na kuleta tija zaidi katika ushirikiano na udugu wa nchi hizo. Nadhani hili linaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kumhakikishia Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwamba katika hotuba yangu nimeeleza kwamba Tanzania inachukua kila fursa ya majukwaa ya kimataifa kuzungumzia masuala ya uchumi. Kati ya majukwaa muhimu ya Umoja wa Mataifa ni Jukwaa la *UNCTAD*. Tumekuwa tukishiriki kikamilifu tangu mwaka 1964 na mazungumzo yanayoendelea pale ni ya tija kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ambayo yanajitokeza sasa tutaendelea kuyaweka katika ajenda ya *UNCTAD*. *UNCTAD* itaendelea kuwa ni chombo muhimu cha nchi zinazoendelea na hasa pale inapokuwa kati ya mahusiano ya sisi tunaoendelea na nchi za nje. Kama vile ilivyo *WTO (World Trade Organization),* Jukwaa la *UNCTAD* ni muhimu kwa Tanzania. Kama alivyogusia Mheshimiwa kwa

kuleta ajenda zetu pale masuala mengi ya mahusiano ya kibiashara na uwekezaji yanaweza kutatuliwa kwa kutumia chombo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *EPA,* napenda ifahamike kwamba huu ni mkataba ambao Ulaya walitaka nchi za Afrika Mashariki kwa umoja wao waweke saini lakini baada ya uchambuzi tumeona kwamba kuna upungufu katika mkataba huo. Tatizo linalokuja ni kwamba katika nchi za Afrika Mashariki, nchi tano zinaendelea kufanya biashara na Ulaya na kupeleka bidhaa bila vikwazo lakini nchi moja ambayo ni Kenya yenye uchumi wa wastani, Ulaya walisema ifikapo Oktoba mwaka jana wao hawatanufaika na kile kipengele cha kuondolewa ushuru kama sisi wengine. Wakasema Kenya haiwezi kuendelea lakini sisi wote kwa pamoja lazima tuweke saini ili kuinusuru Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaiambia Kenya kwamba itakuwa vigumu kwa sisi kama mkataba huu ulivyo kwa sasa. Kuna haja ya kuchambua zaidi lakini tunaiambia Jumuiya ya Ulaya kwamba ivute subira na isiiwekee vikwazo Kenya kwa sababu Kenya ikisaini peke yake makubaliano hayakubaliki, hata ikisaini Kenya peke yake haikubaliki mpaka Kenya isaini pamoja na wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye mkutano wa juzi wa nchi za Afrika Mashariki tumeamua kwamba kwa Umoja wetu wa Afrika Mashariki na Mwenyekiti wetu mpya Yoweri Museveni ataongoza ujumbe maalum kwenda Brussels mwezi ujao na kuiambia Jumuiya ya Ulaya kwamba wasubiri wasiweke vikwazo kwa Kenya mpaka hapo tutakapokubaliana sisi wanachama wa Jumuiya kutazama upya masuala ambayo yanatukera. Ndiyo maana Bunge hili Tukufu lilitoa ushauri ambao unaheshimika kabisa kwa Serikali yetu na kwa Mheshimiwa Rais kwamba tusiweke saini mkataba ule kwa sababu una upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maamuzi ya juzi, Museveni atakwenda kufanya mambo matatu. La kwanza ni kuiambia Jumuiya ya Ulaya kwamba vuteni subira,

msiiwekee vikwazo au msiifungie biashara Kenya. La pili, chini ya Uenyekiti wa *President* Museveni sisi Wanajumuiya ya Afrika Mashariki tutakaa tena kutazama upya kipengele kwa kipengele mahali ambapo panahitaji marekebisho na Ulaya watusubiri tukubaliane kwa sababu nchi moja hata ikisaini, haina tija, haina nguvu mpaka wote tusaini mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kwamba endapo hiyo itashindikana kuna kipengele katika Mkataba wa *East Africa* ambacho kinaruhusu kitu kinaitwa *variable-geometry. Variable-geometry* ni kwamba ninyi wanachama mnamruhusu mwenzenu aendelee kuweka saini mkataba ninyi wengine mkiwa bado mnajipanga. Hata hivyo, dhamira ya nchi za Afrika Mashariki ni kwamba tuweke mkataba huu kwa pamoja na mpaka tufike kwenye *variable-geometry* itakuwa baada ya kwamba tumeshindwa kuwaambia Ulaya kwamba wavute subira ili tuweze kurekebisha mapatano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndani ya mwezi ujao ni matarajio yetu kwamba Umoja wa Ulaya hautaiwekea Kenya vipingamizi vya biashara. Sisi tutaendelea kutazama mkataba ule na pale ambapo Kenya inaona umuhimu wa kuendelea sisi tutaridhia kwamba mwenzetu aendelee kwa kutumia kipengele kinachoitwa *variable-geometry* huku tukiendelea kuzungumza ili hatimaye sisi wote tuweze kuweka mkataba huo kwa pamoja. Nadhani hilo linaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengine Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq ameshauri Serikali iwe na majengo yake kwenye Ofisi za Balozi nje ya nchi ili kupunguza gharama za kulipia kodi za pango. Aidha, Wizara iwe na mkakati wa muda mrefu na mfupi, kuendeleza viwanja ambavyo Serikali imepewa nje ya nchi kupitia Balozi zetu na kutumia utaratibu wa mikopo ya benki ya *hire purchase* na *mortgage finance* ili iweze kuviendeleza viwanja hivyo kwa kujenga majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuendeleza na kukarabati majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozini na imekuwa ikitekeleza jukumu hilo kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo zinazopangwa katika kila kipindi cha mwaka wa fedha. Mpango wa Wizara wa miaka 15 wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Ubalozini ulianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali kwenye Balozi zetu kama vile kufanikisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania New Delhi India; ununuzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Washington DC – Marekani; ununuzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania New York – Marekani; ununuzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi, Ubalozi wa Tanzania Paris – Ufaransa; ukarabati wa makazi ya Ubalozi wa Tanzania Nairobi – Kenya na ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Tokyo – Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara itakamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa tisa la Ofisi na Makazi lililopo Ubalozi wa Tanzania Maputo – Msumbiji; ukarabati wa makazi ya Balozi na nyumba za watumishi zilizoko Ubalozi wa Tanzania Stockholm - Sweden na ukarabati wa Jengo la Ofisi na makazi ya Balozi yaliyoko Khartoum - Sudan. Hivi sasa Wizara inaandaa mpango mwingine wa miaka 15 wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi na Makazi ya watumishi Ubalozini utakaoanza kutekelezwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya miradi itakayotekelezwa ni ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya watumishi kwenye Balozi za Tanzania Harare – Zimbabwe; Kampala – Uganda; Beijing - China, Pretoria – Afrika Kusini na Cairo – Misri. Vilevile ukarabati wa nyumba za Ubalozi zilizoko kwenye Ubalozi wa Tanzania Lilongwe – Malawi na Kinshasa – DRC; ukarabati wa jengo la zamani la Ofisi ya Ubalozi ulioko Washington – DC; ukarabati wa miundombinu

ya Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini na ujenzi wa makazi ya Balozi, Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa – Ethiopia na Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kutekeleza mpango huu ni kuendelea kutumia bajeti ya maendeleo ya Serikali, kuishirikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile Taasisi ya Miradi ya Maendeleo ya Miundombinu (*UTT-PID)* na kwa kutumia utaratibu wa karadha katika kutoa mikopo ya kutekeleza miradi ya maendeleo Ubalozini kwenye nchi za uwakilishi ambapo utaratibu huo unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuwaonyesha kwamba tuna mkakati na kutoa mifano halisi ingawa ombi letu ni kwamba Bunge hili Tukufu litusaidie kupitisha maombi yetu ili tuweze kuanza kutekeleza haraka. Hii pia inajibu hoja kwamba tunachelewa kupeleka pesa kwenye Balozi zetu, kama Hazina ikitupatia pesa kwa wakati tutajitahidi kupeleka pesa hizo ili zikafanye kazi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine linahusu upungufu wa wafanyakazi kwenye Ofisi za Balozi ambapo hakuna wataalam mbalimbali kama Wachumi, Wanasheria, wataalam wa utalii na Maafisa Uhamiaji ili kufanikisha Diplomasia ya Uchumi. Wizara imerejesha kiasi kikubwa cha watumishi waliomaliza muda wao katika Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tupo katika hatua ya kurejesha waliobaki ili kutekeleza hatua ya pili ya kupeleka watumishi nje kulingana na mahitaji. Tuko katikati ya mchakato huo, hatuwezi kupeleka watu kabla ya hatujarudisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara zina tovuti na mtandao wa kijamii ambao una taarifa muhimu kuhusu huduma zinazotolewa na Wizara au taasisi husika zikiwemo taarifa za uwekezaji. Aidha, taarifa hizo zinapatikana kwa upana katika tovuti zinazohusika na taarifa zaidi kuhusu kazi zinazoendelea katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cosato Chumi ameuliza na kwa kweli ametoa ushauri, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine isimamie suala la makubaliano ya kutoza kodi mara mbili baina ya nchi yetu na nchi nyingine yaani *double taxation* na kulinda wawekezaji wa nje nchini (*protection of investment).* Wizara inapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutalifanyia kazi pendekezo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia anashauri Wizara ijenge majengo yake yenyewe katika viwanja, nadhani hilo nimeshalijibu. Kuhusu upungufu wa wafanyakazi, hilo pia nimeshatoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa, ni lini Wizara itapeleka Balozi wa Heshima Lubumbashi, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo. Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na wawakilisha kamili wa Ubalozi wenye makazi katika nchi mbalimbali duniani na Konseli kuu katika maeneo ya kimkakati. Kutokana na mwingiliano mkubwa wa biashara baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na Mashariki mwa Congo, Wizara imeanza utaratibu wa kupata Mwakilishi wa Heshima ambaye atakidhi mahitaji ya Watanzania wanaoishi Mashariki mwa Congo pamoja na wafanyabiashara watokao Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa Serikali imefungua Balozi sita mpya ambazo nilizitaja, lakini tutaendelea pia kutazama maeneo mengine ambayo ni muhimu na hasa kwa vile Mabalozi wanasimamia nchi nyingi na kuna umuhimu wa kuwa na Konseli Jenerali na hilo katika mwaka ujao tutalipa kipaumbele, siyo tu katika *DRC* lakini kuna nchi nyingine ambazo tumeona umuhimu wa kuwa na Konseli Jenerali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa kuhusu kunyanyaswa kwa Watanzania wanaokwenda kufanya kazi katika nchi za Uarabuni hususan Oman. Wameomba kupata taarifa juu ya kifo cha Mtanzania huyu anayesemekana kuwa

aliuawa nchini humo. Aidha, wameshauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Kazi na Ajira ili kuwepo na utaratibu ambao utaondoa unyanyasaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 Machi, 2017, Wizara ilipokea taarifa kutoka Ubalozi wetu nchini Oman kuhusu kifo cha kutatanisha cha Mtanzania Bi. Husna Issa Abdallah, mwenye umri wa miaka 28 aliyekuwa akifanya kazi za ndani. Taarifa hiyo imeeleza sababu za kifo hicho kwamba marehemu alijirusha na kuanguka kutoka ghorofa ya kwanza ya nyumba ya mwajiri wake huku mwajiri na familia yake wakiwa wameketi sebuleni. Aidha, taarifa ya Serikali ya Oman imeeleza kuwa kifo hicho kimetokana na yeye mwenyewe kujiua kwa kujirusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea taarifa hiyo, Ubalozi ulichukua hatua ya kuwasiliana na ndugu wa marehemu ili kupanga mipango ya kusafirisha mwili. Aidha, Ubalozi ulisaidia kushughulikia *documentation* zote zinazohusiana na usafirishaji wa mwili wa marehemu. Kwa upande wake, aliyekuwa mwajiri wa marehemu alijitolea kulipa gharama zote za kusafirisha mwili hadi kijijini kwao na pia kugharamia gharama za mazishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ilipokea barua kwa mtu aliyejitambulisha kuwa ni ndugu wa marehemu kudai kuwa yeye ana nyaraka zinazoonyesha taarifa tofauti na ile tuliyonayo. Tulimwandikia barua ya kuomba nakala ya *document* hizo ili tuweze kufuatilia kupitia Ubalozi wetu mpaka sasa hatujapata jibu kutoka kwa ndugu huyu wa marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kupata suluhu ya kudumu kuhusu changamoto zinazowakuta Watanzania wanaokwenda kufanya kazi nje ya Mashariki ya Kati, Wizara inaendelea kusisitiza Watanzania wanaoenda kufanya kazi nje ya nchi hususani katika eneo la Mashariki ya Kati, wafuate taratibu zilizowekwa na Wakala wa Ajira Tanzania *(TaESA)* kwa kutumia mawakala waliosajiliwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa baadhi ya watumishi wanaotoka Balozini wamekuwa wakipelekwa na Serikali katika Ofisi mbalimbali ili kupata ujuzi katika sekta hizo lakini pia ili kupeleka ujuzi walionao. Suala hili pia limezungumzwa kwa kirefu katika hotuba yangu na lipo kwenye kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Haji Khatib, ili kumaliza tatizo la kukamatwa na kufungwa kwa wavuvi wetu nchini Kenya, ni vema Serikali ya Tanzania na Kenya ikarudi kwenye mkataba uliosainiwa na Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi hizi mbili mwaka 1975. Wizara kwa kutumia mahusiano yake mazuri na nchi rafiki imeingia makubaliano na Serikali na Wizara hii itahakikisha kwamba tunazungumza tena na kutazama mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kule Pemba tukitoa mafunzo na semina, suala hili tulilipokea na tunaahidi kwamba tutaendelea kulifanyia kazi na hasa katika kuzingatia mahusiano ya biashara na usafiri kati ya wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Tanzania na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa pia kwamba Wizara ifanye maboresho katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha, hususani upande wa vyoo vya watu mashuhuri (*VIP)* na vyoo vingine vya kawaida. Tunachukua ushauri huo. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe maelezo juu ya uvumi kuhusu unyanyasaji wa Watanzania katika nchi nyingine ambazo tuna uhusiano nao. Majibu ni yaleyale tuhakikishe kwamba tunatoa elimu kwa vijana wetu ili wanapokwenda huko waweze kuwa wamepewa kibali na wanasimamiwa na *agency* ambazo zimewekwa za kupeleka watu kufanya kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, anasema kuwe na sera

moja ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazotumia Ziwa Victoria juu ya uvuvi na forodha. Kwa utaratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, sheria inayoweza kutumiwa na nchi zote za Jumuiya hujadiliwa kwa pamoja na nchi wanachama zikachukua vipengele vinavyovitaka katika kila nchi. Hivyo, Sheria ya Uvuvi ya Tanzania ikirekebishwa haitakuwa kigezo cha kutumika katika nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa namna gani Zanzibar inanufaika na uwekezaji unaofanywa na Shirika la *AICC* kule Arusha. Ni kweli *AICC* ni Shirika la Muungano kwa kuwa liko chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo ni Wizara ya Muungano. Uwekezaji unaofanywa na *AICC* unanufaisha wananchi pande zote za Muungano. Hii ni kutokana na ukweli kuwa gawio linalopatikana linawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango ambayo yenyewe ina mamlaka ya kutoa gawio Zanzibar kulingana na utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, alishauri Serikali ipeleke ...

**MWENYEKITI:** Dakika moja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati Balozini. Nadhani hili tumeshalizungumza na itategemea uhusiano wetu baada ya ninyi kutusaidia katika kuidhinisha pesa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala kadhaa ambayo yameulizwa hapa, mengi tutayajibu kwa maandishi na tunatoa heshima ya pekee kwa mchango huu. Masuala mengi ni ya kuchangia kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri toa hoja tu, hiyo utakuja kuisema baadaye, toa hoja tu umalize.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Sawa, itakuja baadaye.

**MWENYEKITI:** Toa hoja tu, sema naomba kutoa hoja basi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani huu ndiyo mwisho, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kif.1001-*Administration and HR Mngt........*Sh.11,204,167,000/=

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina tayari, ninalo jina la Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Mwanjelwa, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Richard Mbogo, itategemea na muda wetu unavyokwenda. Tunaanza na Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana pamoja na mwaka huu kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani tumezungumza sana kuhusu diplomasia ya uchumi na niseme mapema kabisa nakusudia kutoa shilingi kama sitapata majibu ya kuridhisha na sina uhakika sana kama Naibu Waziri amesoma na kuielewa hotuba yetu ambayo kimsingi tumeandika kwa kutoa ushauri kama Taifa la pamoja badala yake amekuja na kutoa kejeli na vijembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Wizara iniambie, ni nini ajenda ya diplomasia ya kiuchumi kimataifa na mkakati uliopangwa. Kwa mfano, *SADC* tunataka nini na tuna-*implement* vipi diplomasia ya uchumi, East Africa, Asia, Ulaya na Amerika tunataka nini. Mwaka jana tuliuliza swali hili na hatujajibiwa, mwaka huu nilitegemea Wizara itakuja na *strategic plan, document* ambayo itatuonyesha kwamba tuna mipango ya kutekeleza diplomasia ya kiuchumi badala yake Waziri Mdogo amekuja na majibu ya jumla jumla, nina mashaka sana kama ameelewa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate majibu vinginevyo nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, Mheshimiwa Waziri jibu mwenyewe maana wewe ndiyo mtaalam.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge na ambalo alilirudia kwenye hotuba yake nililijibu kabisa kwenye hotuba yangu ya awali kwa kuonyesha kwanza maana ya *economic diplomacy*, pili kuonyesha maana ya *economic diplomacy* ya viwanda na nikaainisha mkakati wa kutekeleza hii *economic diplomacy*. Hiyo ipo kwenye hotuba lakini pia iko kwenye kitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kumrejesha katika hotuba hiyo kwani tumefafanua kwa kirefu kuhusu *economic diplomacy* na uhusiano wetu na Jumuiya za Kanda, Afrika ya Mashariki na *SADC*. Tumeainisha pia kile ambacho nimekieleza hapa hapa tena, uhusiano wetu na Ulaya utakuwaje baada ya mazungumzo katika suala la *EPA*. Tumeeleza kwa kirefu jinsi Tanzania itakavyoshiriki katika majukwaa ya kimataifa katika kuzungumza na kuleta ajenda ya *economic diplomacy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba hotuba ya Mheshimiwa iliyoandikwa mapema kwa hivyo haikuzingatia yale niliyosema katika hotuba yangu. Pia katika ufafanuzi uliotolewa na Naibu Waziri amefafanua kwa kirefu kabisa maana ya mkakati wa *economic diplomacy* na ajenda ambayo tutakuwa nayo ikijumlisha uandalizi na maandalizi ya maafisa wetu. Kila kitu kimo katika hotuba zetu na katika majibu ambayo yametolewa humu. Tuko tayari kukaa na kuzungumza kwa kirefu zaidi lakini hakitakuwa tofauti na vyote vinazingatia ajenda, mkakati wa kutekeleza siasa ya viwanda na *diplomacy*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri umejibu vizuri sana, Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi kwa sababu majibu ya Mheshimiwa Waziri ni majibu ya ujumla tena na hii inaonesha bado kama Taifa hatujawa *serious* kabisa na diplomasia ya kiuchumi. Mheshimiwa Waziri anatoa majibu ya ujumla ambayo hata haelezi kwenye kitabu chake ni wapi amezungumzia diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Usalama, Nje na Mambo ya Ulinzi na katika kipindi cha wiki mbili nimebahatika kutembelea Ubalozi wa South Africa pamoja na Ubalozi wa Kenya, haya mambo mnayoyazungumza mnazungumza siasa hayako kwenye *ground.* Kama kweli hii nchi tunataka tuwe na

uchumi wa kukua haya majibu mnayatoa kisiasa na hamko *serious* kwenye diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hao wanaosema wamewa-*train* haya masuala ambayo Naibu Waziri anani-*challenge,* mimi nimeyatoa kwenye randama ya Wizara. Randama ya Wizara imesema Wizara imejiwekea mikakati mbalimbali katika kuhakikisha inatekeleza ipasavyo diplomasia ya uchumi, mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutafuta fursa mbalimbali...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa umejieleza vizuri sana na hoja yako inafahamika toa shilingi, toa hoja tuendelee.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*, nitakuja kujibu, natoa shilingi na naomba Wabunge hata upande huo kwa sababu uchumi ni wa wote mniunge mkono Wizara iji-*commit* katika ku-*implement* diplomasia ya kiuchumi, haya wanayoyatoa hapa hayako duniani, nimejaribu kutoa na mifano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Watakaochangia ni Mheshimwa Riziki, Mheshimiwa Alberto, Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Adadi, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa *AG,* mimi nakupenda *AG* maeneo yote umo, sheria umo na uchumi umo safi sana. Huku mmekwisha, nani bado, Mheshimiwa Ali Khamis.

**MHE. MASOUD A. SALIM:** Masoud hujamwandika.

**MWENYEKITI:** Kuandika wote si kupewa wote.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Kubenea umemwacha.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Kubenea. Mheshimiwa umetaka nafasi umepewa, huna maneno?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Msigwa, Serikali ilianzisha Kituo cha Biashara cha Kimataifa (London), ikaanzisha Kituo cha Biashara cha Kimataifa (Dubai) na sasa vituo hivyo imevifunga, maafisa wake wamerudi Tanzania, kazi ambayo ilikuwa inafanywa na vituo vile vya biashara vya kimataifa sasa hivi haifanyiki vizuri. Kwa msingi huo, diplomasia ya uchumi haifanyiki vizuri duniani na wafanyakazi wale hawakulipwa posho zao na mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, hoja ya Mheshimiwa Msigwa ya kutaka kujenga diplomasia ya uchumi ni muhimu ikaungwa mkono na Bunge hili ili Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili kwamba Wizara yake iko tayari kuuhakikishia ulimwengu kwamba Tanzania ya viwanda, ya kibiashara ya kimataifa itapatikana. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Alberto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina wasiwasi kwamba bado hatujaweka nia katika eneo hili kwa sababu tunachofanya hivi sasa ni kuwaita watu kuja kuchota rasilimali zetu, basi. Wamekuja Morocco, Vietnam, India, Thailand, Marekani wanaondoka na rasilimali zetu, sisi tunafanya nini kwa wao? Hiyo ndiyo diplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa tunawaita waje wa-*damp* uchumi na mambo yao kwetu. Nchi ndogo ya Mauritius inawekeza India, ni *the second biggest investor* ndani ya India. Nataka Serikali yangu iniambie sisi tumewekeza wapi, tumewekeza China, Morocco au Vietnam, ni kwamba tunataka kuwaleta wao lakini sisi hatufaidiki kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwamba bado hatujaifanya kabisa ni kuwaleta wao waje kwetu sisi hatufaidiki kwao wao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja hii ya diplomasia ya uchumi wala siyo ya Mheshimiwa Msigwa na asitake kuaminisha kwamba hoja hii ni yake kwa sababu Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ya kuimarisha diplomasia yetu katika nyanja za kiuchumi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, naomba kumpeleka Mheshimiwa Msigwa ukurasa wa 40, ibara za 76 na 77 na ukurasa wa 47, ibara za 88 na 89 inazungumzwa mikakati mbalimbali ya kuimarisha mahusiano yetu na nchi nyingine katika nyanja za kiuchumi na ndiyo maana Tanzania imekuwa siyo kwamba ina-*host* tu makongamano...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hoja aliyoitoa Mheshimiwa Msigwa kwa sababu Wizara ya Mambo ya Nje mimi nikiwa Balozi wamekuwa wakitoa maagizo mara kwa mara namna ya kutekeleza diplomasia ya uchumi na sisi Mabalozi ambao tumekuwa nje tumejitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuleta wawekezaji hapa. Tumeleta wawekezaji mbalimbali na huko nje tumehudhuria makongamano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri kwamba Mheshimiwa Msigwa na yuko kwenye Kamati yangu angeomba hela ziongezwe zaidi kwa ajili ya ku-*implement* ajenda hii. Kwa hiyo, kama hoja ni kuongeza hela, hiyo ni hoja ya msingi lakini hoja ya *implementation* ya diplomasia ya uchumi inatekelezwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ali Khamis.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Nami naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Msigwa kwamba ni hoja ambayo ina *value.* Leo hii Rais wa Ufaransa na Rais wa Urusi wanakutana kujadili masuala ya uchumi wa kidiplomasia na zinaoneshwa *statistics* kwamba Ufaransa imeweza kuwekeza Urusi kwa *Euro* bilioni 780, yaani nchi ya Ufaransa iwekeza katika nchi ya Urusi. Kwa hiyo, tunachozungumzia hapa siyo kuleta wawekezaji, tunazungumzia sisi tumewekeza nini kwao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakija wawekezaji hapa wanachukua mali zetu wanaondoka nazo sisi tunafaidika nini kutoka kwao? Hiki ndio kitu muhimu tunachokitaka. Kwa hiyo, Waziri atuambie ni mkakati gani umewekwa wa sisi kuweza kuwekeza katika hizo nchi ambazo tuna mahusiano nazo ili Taifa hili liweze kunyanyuka kiuchumi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Nseme tu kwamba dhamira ya Serikali kutekeleza diplomasia ya uchumi na hasa Awamu ya Tano inathibitishwa na hivi karibuni Mheshimiwa Rais kuamua kufungua ofisi mpya za kibalozi zipatazo sita. Hiyo inatosha kumshawishi Mheshimiwa Msigwa kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kutekeleza diplomasia ya kiuchumi. Kama alivyosema Mheshimiwa Adadi, kinachohitajika ni kuongeza nguvu ya rasilimali fedha na raslimaliwatu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na huyu aliyemalizia ndiyo naanzia kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kusema hapa hapa, nia iende na vitendo, dhamira iko moyoni mwako siye tunaionaje? Hatuoni namna gani Serikali imetuwekea mipango mahsusi ambayo ni *measurable* (inayopimika) kwa vigezo vilivyo wazi, kwamba sisi kuanzia hapa *trade officers* kwenye Balozi ni hawa, wamesoma *field* hizi na tunatarajia baada ya mwaka watafanya hivi. Balozi hizo Maalum tuambieni vigezo gani vilitumika na nini *specifically* tunatarajia kutoka kwenye hizo zinazoitwa Balozi Mpya. Tunataka *strategic and measurable measures* ambazo zinatambulika, zinaonekana, ni *tangible. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, suala hili ni suala mahsusi, tusifanye mchezo. Tunasema haya kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu, tunapata nini na tume-*review* vipi *economic diplomacy* yetu toka ilipoanzishwa 2001 mpaka sasa kuona matatizo na mbinu mpya tunazokwenda nazo. *First and foremost* lazima tupeleke *qualified diplomat's* nje ambao kweli wamesomea *field's* ambazo tunataka kuzipata. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza kuna tatizo hapa naliona na nitamwomba Mheshimiwa Rais ajaze nafasi ya Wizara ya Nishati na Madini haraka ili baadhi ya Wabunge wanaofikiri hiyo nafasi iko wazi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, nenda kwenye hoja yako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu moja. Alichosema Mheshimiwa Msigwa amekisema kwenye hotuba yake lakini asubuhi mimi nimesema, hiyo *sense* ya uchumi wa kidiplomasia iko wapi kwenye Taifa ambalo

kwanza lenyewe haliheshimu demokrasia. Ni *investors* gani mnakwenda kumwalika kuja kufanya *investment* katika Taifa ambalo haliamini katika uhuru wa maoni, haliamini katika utaratibu wa kisiasa, mtu yeyote atakuwa na mashaka ya kufanya *investment.* Kwa hiyo, huu uchumi wa kidiplomasia lazima uende sambamba na siasa safi na uongozi bora...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachozungumza Mheshimiwa Msigwa nafikiri ni kushindwa kutambua jitihada mbalimbali ambazo zimefanywa na Serikali katika kutekeleza uchumi wa kidiplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kuhesabu leo mambo ambayo yameshafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi, nafikiri Mheshimiwa Msigwa hatakuwa na haja ya kushikilia shilingi. Ni wiki hii tu au wiki iliyopita *AG* na Waziri wa Sheria wametoka Uganda ku-*sign* mkataba wa bomba la mafuta ambalo lilikuwa na ushindani mkubwa sana. Huo ni mfano mmojawapo tu wa kuonesha nchi yetu ilivyoimarisha diplomasia ya kiuchumi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana kabisa na Mheshimiwa Msigwa. Pia mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiria kwamba Serikali ilifaa iseme kuwa kuna tatizo, tunalikubali, tunalifanyia kazi. Ilikuwa ni kauli tu ya kiungwana mara moja imalizike tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri tuchukulie pale Sweden katika *economic diplomacy.* Balozi wetu aliyeko pale Sweden amesha-*present credentials* (hati za utambulisho) katika zile nchi ndogo ndogo lakini yeye binafsi tulipokwenda ana malalamiko kwamba hapa bado Serikali haijakaa vizuri kuandaa mazingira yaliyo mazuri kuweka hii diplomasia ya kiuchumi kwa kupeleka watu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshangaa, kwa nini Serikali isikubali ikatoa tu kauli ya mara moja kwamba suala hili ni zuri, jambo jema, tunalichukua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kuhusu hoja ya Mheshimiwa Msigwa, ningeomba msiwatie hofu Watanzania kwamba sisi hatuna diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema suala la diplomasia ya kiuchumi ni mtambuka. Sisi tuko kwenye *FOCAC,* sisi tuna-*sit* na India, kwenye *Continental Free Trade Area* sisi tumo, tuko kwenye *SADC* na *industrialization*. Kwenye hotuba yangu nimesema kwamba *through SADC efforts* ndiyo tunaweza kujenga sekta ya sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie suala la wafanyakazi waliokuwa na London na Dubai, kwa sababu ya *resource* ndogo tumeamua kutambua maeneo yenye tija, ndiyo tupeleke watu. Tanzania hatuna uwezo wa kusambaza

wataalam wa biashara duniani kote, wa London na Dubai nimewarudisha, tumetambua maeneo ya kuanza nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ngoja niwaambie, watu msilinganishe, Mauritius kuna kitu kinaitwa *bitter honey,* kama hamjui mkakati huo huwezi kulinganisha Mauritius na Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *Attorney General.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ni kweli kwamba Serikali imepiga hatua sana kwenye diplomasia ya kiuchumi na iko mifano mingi. Moja, alivyokuja Rais wa Uganda hapa tumeona bomba la mafuta limesainiwa, linakuja na fursa nyingi. Amekuja mfalme wa Morocco tumepata uwanja wa mpira wa kisasa na Msikiti mkubwa wa kisasa pale Dar es Salaam. Amekuja Rais wa Uturuki tumepata ufadhili kwa ajili ya kujenga reli ile ya kati. Amekuja Rais wa *World Bank* tumepata ufadhili kwa ajili ya ujenzi wa *fly overs* Dar es Salaam na mifano mingi tu ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ni kwamba kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameitaja mikakati yote. Ile ambayo hakuitaja, ni siri hawezi akaisema. Mimi ninayeshiriki kuandika mikataba naona manufaa mengi sana yanayoletwa na diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwamba siyo Serikali ndiyo inayokwenda kuwekeza kwenye hizo nchi...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muacheni basi awapeni maneno!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** ...hizo sasa ni fursa za wananchi wenyewe, wafanyabiashara waende wakawekeze kule. Ndiyo maana kila wanapokuja hapa hao viongozi wafanyabiashara wanashiriki kupata fursa hizo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa, mjadala ni mzuri na mjadala wote una lengo la kujenga Taifa letu. Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mtoa hoja ametoa hoja ambayo anajua kabisa inamfurahisha kila mmoja kuisema, lakini kubwa hapa nilivyomsikiliza kwa makini anauliza kuna mkakati gani wa Tanzania katika diplomasia ya uchumi duniani. Sasa nikiangalia hii hotuba ya Waziri yote imejaa mikakati, maana mikakati ya diplomasia ya kiuchumi ni mipango ya mahusiano yenye faida. Ni *simple* tu, ni mipango ya mahusiano yenye faida. Sasa kila jambo lililozungumzwa hapa kila ukurasa lina faida yake kiuchumi kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme tu hapa kama ni *detailed strategy* huwezi ukaziandika humu kwa sababu ni siri. Kwani Marekani mikakati yake ya kiuchumi inaweka wazi yote? Kwa hiyo na sisi tuna mikakati yetu, tunajua tutahusiana na Morocco kwa lipi, kwa sababu ipi

na kwa misingi ipi. Tunajua tunahusiana kikanda ukienda *SADC, East African Community* tunahusiana kwa mikakati kivipi. Haiwezi ikawa mikakati yote tuiweke hapa, tuainishe humu, sasa sisi ni Taifa au kijiwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa, nia yake ni njema sana, hebu arudie kusoma hotuba ya Waziri ataiona mikakati iko humu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Msigwa kabla hujasimama, ukifungua ukurasa wa 30, Waziri anasema tumekutana na Morocco, Zambia, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Ethiopia kutekeleza diplomasia ya uchumi. Kwa hiyo, hoja yako ni *very valid,* umenielewa na Serikali imejibu kama anavyosema Mheshimiwa Simbachawene, kuna *marketing intelligence,* watu wakishaanza kuona vitu kama hivyo wanaweza kuja kuvidandia bila utaratibu.

Pia Mheshimiwa Waziri amekuwa *so candid,* amekuambia yuko tayari kukaa na wewe, mkashauriana zaidi ukamweleza, sababu ukitaka kwenda kupiga kura, mimi nakueleza, utapiga kura lakini haitakuwa na maana kwenye Taifa kama hoja ambayo unataka kuijenga. Waziri yuko tayari kukutana na wewe na upande wowote ule ili kusaidiana na kupeana mikakati ya kutupeleka mbele. Hii ndiyo *plea* ya Waziri, Mheshimiwa Msigwa, karibu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ushauri wako mzuri...

**MWENYEKITI:** Subiri, samahani. Mheshimiwa Waziri una lolote la kusema kabla hatujampa Mheshimiwa Msigwa au waliyokusemea Mawaziri yanatosha? Kama una nyongeza, jiongeze kidogo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongeze tu kidogo. Kitabu hiki kimejaa mikakati, hotuba yangu

imejaa mikakati, ajenda ya diplomasia ya uchumi na hasa diplomasia ya uchumi wa viwanda imekuwa ndiyo kauli mbiu ya hotuba yangu leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali, daima kuna nafasi ya kuboresha, daima ni vizuri tuwe wazi tupokee mawazo kama ulivyosema katika hotuba yako, tupeane mawazo kuboresha, lakini siyo sahihi kusema hakuna ajenda iliyowekwa kwenye mjadala huu wa mkakati wa diplomasia ya uchumi. Tuko tayari kupata mawazo na daima kutakuwa na nafasi ya kuboresha. Hiki ni kitu endelevu na uendelevu unatokana na kuchangia mawazo tofauti na tutayasikiliza. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mawazo yako mazuri lakini nasikitika kwamba sijayapokea kwa sababu ndiyo maana tuko hapa tulete mawazo mbadala, tuwe kwenye *chamber,* tu-*dialogue,* mawazo mazuri Serikali ichukue, pale tunapokosea tuambiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu, nimetoa mifano mizuri, bahati mbaya wengine asubuhi hawakuwepo kama Mheshimiwa Simbachawene wala hajasoma hotuba yangu, *I think it is one of the best speech* ambayo niliiandika leo. Nimetoa mifano ya nchi kama Australia, mkakati walionao katika nchi 95, nini wanataka katika nchi yao hiyo katika masuala ya diplomasia ya uchumi. Hamuwezi kuniambia nyie mna mkakati hapa na *resources* ndogo tulizonazo. Huwezi kuwa na Ubalozi Zimbabwe, Mozambique, South Africa na kila kona wakati *resources* ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Mabalozi hao hao, hawana ma-*attachés* wa *trade* na uchumi. Juzi tulikuwa Kenya pale, unamuuliza maskini Mheshimiwa Pindi Chana ndiyo Balozi, amekaa pale, namuuliza yupo nani? Anasema yeye Balozi, huyu wa *visa,* anakuwepo Mwambata wa Jeshi, yupo Usalama wa Taifa na *cashier,* biashara

imekwisha. Nawauliza akija mtu hapa aulize anataka ku-*invest* Tanzania nani mtaalam, anasema tunajiongeza wenyewe. Mheshimiwa Pindi Chana si tulikuwa naye mwanasiasa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza hapa siyo nani anapata *credit,* hapa sio tunatafuta *credit* nani mshindi, *we are talking about the nation and the future of this country; you guys* hamko *serious* na uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnazungumzia masuala ya kwamba mtu wa Morocco alikuja kutuletea Msikiti hapa na uwanja wa mpira ambao ni msaada, huo ni uchumi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, muda wako umekwisha. Mimi nakuomba...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano hazijaisha.

**MWENYEKITI:** *No, no, no,* muda huu napanga mimi sio wewe.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Siyo wewe Mheshimiwa?

**MWENYEKITI:** *No, no, no,* unapoanza mwanzoni dakika tano safari hii naamua mimi Waziri anasema muda gani, wewe muda gani kwenye hoja, Kanuni iko *very clear.*

Mheshimiwa Msigwa, mimi nakuomba, umekuja na hoja ya msingi sana na umeeleza vitu *very pertinent* kwa Serikali na Waziri ame-*open up* kwako, amekwambia hivi na yeye yuko tayari, hii hotuba yako ameipokea na yuko tayari kukusikiliza mengine umweleze kuisaidia nchi iende mbele na mimi nakuomba kwamba mrudishie hela yake twende na shughuli zingine.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namrudishia hela yake atoe *commitment* mwakani tutakapokuja hapa tunataka tuwe na *strategic plan,* wana mpango gani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado. Lazima waje hapa waseme wana mpango gani wa *economic diplomacy.* Wizara haina mpango huo, kama hawajafanya *commitment* sitoi shilingi ili Watanzania waone kwa sababu huu ni utani, wanafanya utani.

**MWENYEKITI:** *No, no, no,* Mheshimiwa Msigwa kaa kwanza. Hoja yako ni ya msingi na Serikali, Waziri Mkuu na sisi tumesikia. Sisi wote tutasaidiana kuhakikisha Serikali inafanikisha yote ambayo yamechangiwa ndani ya Bunge. Nakushukuru kwa kurudisha shilingi. Tunaendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba *commitment* ya Serikali lakini kwa sababu hawana *plan,* hawana mipango yoyote...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, hebu kaa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi mimi sijarudisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, umetamka hapa narudisha shilingi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hajasema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu subiri, wewe ni Mwanasheria uliyebobea, sidhani kama Mahakamani pale Hakimu akisimama na wewe unasema, huyu anasema, subiri basi.

Mheshimiwa Msigwa, umetamka umerudisha shilingi unataka *commitment.* Mheshimiwa Msigwa, unataka twende kupiga kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya toa hoja.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali na Wizara hii haijaonesha *commitment* na inaonekana haijui diplomasia ya uchumi, mimi nang'ang'ania shilingi, Bunge lipige kura.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa tunaenda kwenye kuhitimisha hoja lakini masikio yetu wote yamemsikia Mheshimiwa Msigwa amerudisha shilingi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuhitimishe hoja hiyo lakini kesho itabidi tuje na *Hansard* tuone ambacho...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Kiti kinampa *benefit of doubt,* mimi nampa *benefit of doubt,* tutapiga kura kwa mujibu wa Kanuni afunge hoja yake lakini hoja yako ilikuwa ni nzuri, unaipigia kura kama vile sasa unaleta kitu kama vile, *anyway.* Waheshimiwa tujiandae na kupiga kura pande zote mbili.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Biashara imekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Inline* na hiyo diplomasia na kiuchumi kuelekea kwenye viwanda na utalii, kwenye

mchango wangu asubuhi nilizungumzia sana suala la *diplomats* wetu hususan *commercial attachés* waweze kupewa *performance targets.* Nilitaka Mheshimiwa Waziri anihakikishie, je, *diplomats* wetu nchi za nje watapewa hizi *performance targets* au itakuwa ni *business as usual?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge wazo lako ni zuri na hata baada ya kulizungumza asubuhi tulilizungumza zaidi. Ulichosema ni sehemu ya utekelezaji wa Wizara yetu katika kuwaandaa watumishi wetu ili waweze kuendelea kufanya kazi ya diplomasia ya uchumi kikamilifu. Nakubaliana kabisa na wewe kwamba hilo linawezekana na imekuwa ni sehemu ya kupima wafanyakazi wetu na siyo hiyo tu kuwapima wafanyakazi lakini kuendelea kuwapa dira ya kutenda kazi katika fani ya diplomasia ya uchumi. Hilo ni wazo zuri, linakubalika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaridhisha, ina maana ametambua umuhimu wa kuonesha *deliverables* kwa ajili ya hawa *diplomat's* wetu ambao wako nchi za nje. Kwa hiyo, tunasubiri utekelezaji wa hapa kazi tu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru. Ili kutekeleza diplomasia ya uchumi na hususan kuelekea uchumi wa viwanda ni wazi kwamba Balozi zetu zinahitaji kuwa na watumishi wa kutosha lakini *as of now,* karibu Balozi 15, Mabalozi wanafanya kazi peke yao bila maafisa wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, anaweza

kutuhakikishiaje kwamba kuelekea kutekeleza uchumi wa diplomasia na kupata *foreign direct investment* Balozi hizo zitapelekewa watendaji *especially* maafisa wa mambo ya nje vinginevyo nitashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Cosato Chumi kuhusu suala alilouliza kwamba kuna Balozi 15 hazina Maafisa wa Mambo ya Nje. Labda tu nimpe taarifa kwamba, maafisa wale ambao walikuwa Ubalozini kwa muda mrefu tulikuwa na mpango mkakati wa kuwarudisha na tumewarudisha. Sasa hivi Wizara inajipanga kwa bajeti hii tumeweka hela ambayo itawapeleka wale ambao wanatakiwa kwenda ku-*replace* zile nafasi ambazo tumewarudisha. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Chumi kwamba watakwenda kwa sababu iko katika mpango.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini hayajaniridhisha kwa sababu zifuatazo. Amekiri kwamba waliokuwa wamekaa muda mrefu wamerejeshwa na kama nilivyosema katika Balozi nyingine, Mabalozi tulionao sio *career diplomat*. Sasa asipokuwa *career diplomat* inampa ugumu sana wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa nchi tatu tu, China Balozi yupo peke yake ni nchi ambayo tunaitegemea kuvutia wawekezaji lakini na mahusiano mbalimbali na masuala mazima ya misaada. Mfano wa pili, nchi kama Ubelgiji ambako ni Makao Makuu ya *EU*, Balozi pale anatakiwa kuhudhuria vikao na vingine kuwatuma maafisa wake. Bahati nzuri Waziri amekaa kwenye fani hii, nchi kama Ujerumani Balozi anawakilisha karibu nchi tisa, sasa unapo-*downsize* ki-diplomasia maana yake una-*downgrade* mahusiano hata mwenzako anaweza kuona

kwamba labda wewe hutaki tena kuhusiana kama ilivyokuwa *especially* kwa nchi marafiki kama China. Kwa sababu hiyo inaonesha labda kama tunakosa *seriousness* katika hili.

**MWENYEKITI:** Hoja yako imeeleweka, umeshatoa shilingi, toa hoja sasa watu wakuunge mkono.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mniunge mkono tuimarishe diplomasia kiuchumi. Ahsante.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Shonza, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Lissu, Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Ndugulile. Tuanze na hawa jamani muda wenyewe mnauona unavyokwenda leo si mnajua mwisho saa 12, haya Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, nitazungumza kwa kifupi sana. Huwezi ukazungumzia diplomasia ya kiuchumi halafu kwenye Balozi 15 huna mtu wa uchumi, huna *economic attachés,* haiwezekani na hayo ndiyo ambayo yamezungumzwa tangu asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *just* kuonesha tu kwamba hatuna *any serious diplomatic initiatives* kwenye masuala haya, jiulize, nilisema asubuhi China ndiyo *the leading investor in the world today,* nani ni Balozi wetu China, ana ufahamu gani wa masuala ya Kichina? *Does he speak Chinese? Is he an expert on China? Does he know Chinese history?* Balozi wa Marekani China amesomea *PhD on Chinese*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa Lissu. Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja na mkakati kwamba nchi yetu sasa hivi inatakiwa kujielekeza katika diplomasia ya uchumi ni jambo ambalo linapaswa kupewa kipaumbele na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri katika mchango wake na katika majibu yake ya hapa karibuni amesema kwamba wamewarudisha nyumbani baadhi ya *economic* na *trade attachés* waliokuwepo. Swali langu ambalo nataka nipate majibu, waliorudishwa walikuwa ni wangapi na katika bajeti hii tunatarajia kuwapeleka wangapi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa haya, unajua ulikuwa unaleta kitu kingine kabisa. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupeleka Maafisa Ubalozini na kurudisha lina gharama nyingi sana. Tulikuwa na maafisa wengi sana nje ambao walikaa muda mrefu sana, wengine walifikia miaka 10, sasa hivi Serikali na Wizara imerudisha wote wale. Naamini kwenye bajeti hii ambayo ipo sasa hivi Wizara ina mpango wa kupeleka maafisa wengine. Msisitizo ambao tumeuweka mpaka kwenye Kamati mnafahamu kwamba wawapeleke maafisa biashara *(trade attachés)* na ndiyo naamini kwamba mkakati ambao upo sasa hivi ni kupeleka hao watu. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba Wizara imejipanga na itatekeleza hilo suala la kuhakikisha kwamba inapeleka Maafisa Ubalozi hasa *trade attachés* katika Balozi zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema kwamba tusizungumze kana kwamba nchi ipo vibaya na niwaeleze kwa moja dogo la sisi na China. *FOCAC* inaendelea, wasioifahamu *FOCAC,* lakini Mheshimiwa Kairuki ambaye ni Balozi wetu, tangu aondoke ameshaniletea *delegation* nne za watu toka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Jumamosi kwenye vyombo vya habari Dar es Salaam amekuja mwekezaji ambaye yeye anamiliki asilimia 65 ya viwanda vyote vya saruji duniani amemleta Kairuki, mnataka alete nini? Kwa hiyo, twende taratibu, tunafanya kazi tukiwa hapa, tunafanya kazi tukiwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesaini mkataba wa mihogo tani milioni 2, ulikuwa umeshindikana chini ya Kairuki umewezekana. Wamekuja watu wanataka kujenga majumba hapa, amewaleta Kairuki mnataka afanye nini? Siyo lazima ujenge Kichina na Wachina wamesema katika Afrika nchi nne walizozichagua ni pamoja na Tanzania. Viongozi wangu wanafanya kazi, Mheshimiwa Rais anafanya kazi siyo lazima wote tuhame twende China, tuonyeshe mapenzi na Wachina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami niseme wazi kwamba kwenye mchango wangu asubuhi nilitaka pia nizungumzie suala hili la upungufu wa maafisa katika Balozi zetu. Hata hivyo, nishukuru sana kwa *commitment* ambayo Serikali imeitoa. Kwa hiyo, nimwombe sana kaka yangu Mheshimiwa Chumi aweze kukubaliana na *commitment* ambayo Serikali imeitoa. Niiombe pia Serikali kwamba hii *commitment* ambayo leo imeitoa hapa basi iweze kutekelezwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Chumi ni ya msingi sana na Serikali inatakiwa iitilie maanani. Haiwezekani nchi kama China tukose maafisa kwa sababu tu kwamba walikaa muda mrefu wamerudishwa basi tungepeleka wengine. Mimi nafahamu pale Mambo ya Nje kuna maofisa wengi sana, wengi walikuwa Italy na wengine walikuwa Marekani kwenye Umoja

wa Mataifa. Kwa hiyo, *strategically,* naomba Mheshimiwa Waziri akubaliane kabisa na watoe *commitment* wapeleke maofisa haraka iwezekanavyo kwa sababu wapo nawafahamu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Chumi kwamba jambo hili ni muhimu na Wizara inatambua hivyo na tunatoa *commitment* kwamba hawa watu watakwenda kwa sababu ipo katika *plan*. Tunachoomba tu sasa Waheshimiwa Wabunge waiunge mkono hoja hii ili kusudi tuweze kupata hiyo bajeti na kuwapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Chumi funga hoja yako.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii wote wameshakaa na ku-*serve* Ubalozini, wanajua magumu ya kufanya kazi bila kuwa na watumishi. Nawaomba na kuwasihi kwa uzoefu wao wa kukaa Ubalozini na umuhimu wa kuwa na watendaji, basi jambo hili liharakishwe kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawarudishia shilingi ili wakalitekeleze kwa haraka na kwa ufanisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja yangu ni kwamba wananchi wengi wamekuwa wakisikia na kuona kwenye vyombo vya habari mikataba na makubaliano mbalimbali yakisainiwa pale Ikulu

na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zote ambazo anazifanya kwa ajili ya kupata miradi na mikataba mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kwamba bomba la gesi sasa linajengwa lakini kuna miradi mingine inayogusa Wizara zingine, kwa mfano afya, elimu, kilimo na mambo mengine. Tungependa wananchi wawe wanapata mrejesho lakini ufuatiliaji wake na mrejesho hatuupati. Je, Waziri yupo tayari kutengeneza au kuunda kitengo maalum kwa ajili ya kushughulikia mikataba hii na kutoa mrejesho kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tupo tayari kutoa mrejesho, lakini kwa taarifa tu ni kwamba katika Wizara yetu tuna kitengo maalum ambacho kinashughulikia masuala ya sheria na kitengo kile ndiyo ambacho kina-*coordinate* mikataba na makubaliano yote ambayo tunayaweka. Wakati tulipofanya mkutano na Mabalozi walipokuja tulikubaliana kwa pamoja na kumwomba Katibu Mkuu Kiongozi kwamba wanapokwenda Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali katika vikao vyao sisi kama Wizara tutakuwa tunawasilisha yale makubaliano tuliyokwisha kuyafanya ili kufanyia *follow-up,* lakini tunapokea pia ushauri wa Mheshimiwa Martha Mlata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini kila ambavyo wananchi wanaelezwa

mikataba inaposainiwa, tunaomba basi wananchi wawe wanaelezwa kama tulivyoona bomba la gesi na mambo mengine yawekwe hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nataka waendelee kutekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa, tunaingia kwenye *guillotine,* Katibu.

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mngnt*...............Sh.11,204,167,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*...........Sh.952,705,000/=
Kif.1003 – *Foreign Affairs Office Zanzibar*..........................Sh.494,965,000/=
Kif.1004 – *Policy and Planning* ........... Sh. 880,125,000/=
Kif.1005 – *International Cooperation* ...........Sh.638,721,000/=
Kif.1006 – *Europe and America* ............ Sh.540,956,000/=
Kif.1007 – *Asia and Australia* ................ Sh.459,995,000/=
Kif.1008 - *Africa* ............................... Sh.985,003,000/=
Kif.1009 – *Regional Cooperation*........... Sh.553,683,000/=
Kif.1010 - *Protocol*..............................Sh.10,286,406,000/=
Kif.1011 – *Legal Service*.................... Sh.1,084,396,000/=
Kif.1012–*Government Comm. Unit*..............Sh.299,433,000/=
Kif.1013 – *Middle East Division* ..................Sh.455,453,000/=
Kif.1014 – *Internal Audit Unit*................. Sh.323,548,000/=
Kif.1015 – *Procurement Unit*.................. Sh.362,179,000/=
Kif.1016 – *Information and Comm. Technology*.........................Sh.280,460,000/=
Kif.1017–*Diaspora Engagement and Opportunity*.............................Sh.291,922,000/=
Kif.1018–*Economic Infra and Social Supp Servs Div*........................Sh.519,394,000/=
Kif.1019–*Political, Defence and Security Affairs*.................................Sh.477,173,000/=
Kif.1020 – *Trade, Investment an Productiv Sector Div*......................................Sh.473,672,000/=

Kif.2001–*Embassy of Tanzania –*
*Addis Ababa*..............................Sh.2,564,267,000/=
Kif.2002 – *Embassy of Tanzania – Berlin*.......Sh.3,553,384,000/=
Kif.2003–*Embassy of Tanzania – Cairo*.......Sh.1,458,674,000/=
Kif. 2004 – *Embassy of Tanzania –*
*Kinshasa*....................................Sh.1,793,337,000/=
Kif.2005–*High Commission of*
*Tanzania – Abuja*..........................Sh.3,639,813,000/=
Kif.2006 – *High Commission of*
*Tanzania – London*....................Sh.3,378,052,000/=
Kif.2007 – *High Commission of*
*Tanzania – Lusaka*.....................Sh.1,054,375,000/=
Kif.2008–*High Commission of*
*Tanzania – Maputo*......................Sh.2,267,264,000/=
Kif. 2009 – *Embassy of Tanzania –*
*Moscow* ....................................Sh.2,860,199,000/=
Kif. 2010 – *High Commission of Tanzania*
*– New Delhi*...............................Sh.2,391,800,000/=
Kif.2011 – *Permanent Mission to the UN*
*– New York*.................................Sh.4,975,909,000/=
Kif. 2012 – *High Commission of*
*Tanzania – Ottawa*....................Sh.2,557,883,000/=
Kif. 2013 – *Embassy of Tanzania – Paris*......Sh.3,305,443,000/=
Kif. 2014 – *Embassy of Tanzania – Beijing*.....Sh.3,329,670,000/=
Kif.2015 – *Embassy of Tanzania – Rome*.......Sh.3,866,099,000/=
Kif. 2016 – *Embassy of*
*Tanzania – Stockholm*................Sh.3,492,900,000/=
Kif. 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo*......Sh.2,610,988,000/=
Kif. 2018 – *Embassy of Tanzania*
*– Washington*...............................Sh.4,320,092,000/=
Kif. 2019 – *Embassy of Tanzania – Brussels*.....Sh.2,332,046,000/=
Kif. 2020 – *Permanent Mission to*
*The UN – Geneva*.....................Sh.6,401,296,000/=
Kif. 2021 – *High Commission of*
*Tanzania – Kampala*................Sh.1,944,470,000/=
Kif.2022 – *High Commission of*
*Tanzania – Harare*....................Sh.1,585,548,000/=
Kif.2023 –.*High Commission*
*of Tanzania – Nairobi*...................Sh.3,441,393,000/=
Kif. 2024 – *Embassy of Tanzania – Riyadh*.....Sh.2,283,299,000/=

Kif.2025 – *High Commission of Tanzania – Pretoria*..................Sh.2,856,785,000/=
Kif.2026 – *Embassy of Tanzania – Kigali*.......Sh.1,700,063,000/=
Kif. 2027 – *Embassy of Tanzania – Abu Dhabi*...........................Sh.3,247,047,000/=
Kif.2028 – Embassy of Tanzania – Bujumbura................Sh.1,641,493,000/=
Kif.2029–*Embassy of Tanzania – Muscat*.......................................Sh.1,514,450,000/=
Kif. 2030 – *High Commission of Tanzania – Lilongwe*.................Sh.1,098,114,000/=
Kif. 2031 – *Embassy of Tanzania – Brasilia* ..................Sh.3,441,406,000/=
Kif. 2032 – *High Commission of Tanzania – Kuala Lumpa*............Sh.2,067,695,000/=
Kif.2033 – *Embassy of Tanzania – The Hague*................Sh.2,579,305,000/=
Kif. 2034 – *Embassy of Tanzania – Moron* ...Sh.1,528,051,000/=
Kif. 2035 – *Embassy of Tanzania – Kuwait*....................Sh.1,212,115,000/=
Kif. 2036 – *High Commission of Tanzania – Algiers* .....................Sh.2,290,981,000/=
Kif. 2037 – *High Commission of Tanzania – Ankara*.......................Sh.2,588,740,000/=
Kif. 2038 – *Embassy of Tanzania – Khartoum*...............................Sh.2,360,755,000/=
Kif. 2039 – *Embassy of Tanzania – Seoul*.......Sh.3,618,223,000/=
Kif. 2040 – *Embassy of Tanzania- Tel Aviv*........................Sh.2,810,114,000/=
Kif. 2041 – *Embassy of Tanzania Doha*........Sh.3,317.525,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kif. 1004 – *Policy and Planning*................ Sh.8,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae, mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono na sasa tunaingia kwenye hatua ya kuhoji kuhusu Bunge kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio na Matumizi ya Serikali ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKTI:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, wamefanya kazi nzuri na tuna hakika mikakati waliyoileta itatupeleka mbele. Mheshimiwa Waziri wala usiwe na hofu, lete tu mipango yako itapitishwa na Bunge hili litakusaidia. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.52 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 30 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*